# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

### Kikao cha Ishirini na Tisa – Tarehe 14 Mei, 2020

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa, tukae.

Katibu!

**NDG. PAMELA PALLANGYO - KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani Na:-

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

**MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO - K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2019/2020 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Sikudhani Yassin Chikambo kwa niaba ya Mwenyekiti. Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, hayupo, tunaendelea.

## MASWALI NA MAJIBU

*(Maswali yafuatayo yameulizwa na kujibiwa kwa njia ya mtandao)*

Na. 268

### Kuongeza Ajira Kinondoni

**MHE. MAULID S. MTULIA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza ajira katika Wilaya ya Kinondoni ?

**WAZIRI MKUU** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maulid Said Mtulia, Mbunge wa Kinondoni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutatua changamoto ya nafasi za ajira kwa vijana, Serikali imekuja na mikakati ifuatayo:-

(i) Kuwajengea ujuzi kupitia mafunzo ya ufundi stadi kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kujiajiri kupitia programu mbalimbali za ukuzaji ujuzi zilizo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Programu hizo ni uanagenzi *(apprenticeship),* mafunzo ya uzoefu wa kazi *(internship)* na kutambua na kurasimisha ujuzi uliopatikana nje ya mfumo rasmi *(RPL);*

(ii) Uwezeshaji kiuchumi wa vikundi vya vijana kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana *(YDF)* na asilimia 10 ya mapato ya ndani ya Serikali za Mitaa katika kuwezesha vijana ili waweze kujiajiri ambapo asilimia nne ni vijana, asilimia nne

ni wanawake hata vijana wanawake na asilimia mbili kwa vijana wenye ulemavu;

(iii) Kuandaa Miongozo ya kufundisha masuala ya ujasiriamali kuanzia ngazi ya Shule za Msingi hadi Vyuo vya Elimu ya Juu. Mafunzo haya yanalenga kuwawezesha vijana kuibua miradi na kuitekeleza kwa lengo la kujiajiri na kuweza kuajiri vijana wengine; na

(iv) Kutenga maeneo maalum ya uzalishaji mali kwa vikundi vya vijana katika ngazi ya Halmashauri.

Na. 269

**Uhaba wa Walimu Nchini**

**MHE. RASHID A. SHANGAZI** aliuliza:-

Sekta ya elimu nchini inakabiliwa na uhaba wa walimu.

Je, Serikali imeweka mkakati gani wa kuziba pengo hilo la uhaba wa Walimu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mbunge wa Mlalo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzia mwaka wa fedha 2015/2016 hadi Machi 2020, Serikali imeajiri Walimu 18,181 katika sekta ya elimu. Idadi hiyo inahusisha Walimu wa shule za msingi 10,666, Walimu wa shule za sekondari 7,218 na mafundi sanifu maabara 297. Serikali itaendelea kuajiri Walimu katika sekta ya elimu kwa kadri ya upatikanaji wa rasilimali fedha.

Na. 270

**Sekondari Zinazofundisha TEHAMA Nchini**

**MHE. TUNZA I. MALAPO** aliuliza:-

Je, ni Shule ngapi za Sekondari zinazofundisha somo la TEHAMA nchini?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, shule za sekondari zinazofundisha somo la TEHAMA nchini ni 188 ambapo 47 ni za Serikali na 141 ni shule binafsi. Serikali inaendelea kuandaa mazingira wezeshi na kuimarisha eneo la rasilimali watu kwa kuongeza Walimu waliosomea somo la TEHAMA na kuziwezesha shule za sekondari kuwa na vifaa vya kisasa vya TEHAMA kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ili kuziwezesha shule nyingi kufundisha somo la TEHAMA.

Na. 271

**Kata za Manispaa ya Bukoba Kupatiwa Umeme wa REA**

**MHE. BERNADETHA K. MUSHASHU** aliuliza:-

Manispaa ya Bukoba ina Kata na vijiji vingi; katika Kata hizo ni *Green Belt* na wakazi wake ni wakulima na wavuvi, maeneo haya hayakupatiwa umeme wa *REA*:-

Je, ni lini vijiji hivyo vya *Green Belt* vitapatiwa umeme wa *REA*?

**WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bernadetha Kasabago Mushashu, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Shirika la Umeme *(TANESCO)* inaendelea kutekeleza miradi ya kusambaza umeme katika maeneo ya miji, majiji, manispaa na vijiji miji ikiwa ni mpango endelevu wa kuunganisha umeme na kuongeza idadi ya wateja. Maeneo ya Bukoba Mjini yasiyofikiwa na miundombinu ya umeme yataendelea kusambaziwa umeme katika kipindi cha mwaka 2019/2020 na baadhi yake katika kipindi kinachoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hatua nyingine Serikali imebuni Mradi wa *Peri Urban* utakaosambaza umeme katika maeneo yaliyopo pembezoni mwa miji (vijiji Miji – *Peri Urban*). Upembuzi wa awali umekamilika kwa nchi nzima ikiwemo Mkoa wa Kagera na utekelezaji wa mradi unatarajia kuanza mwezi Julai, 2020. Maeneo aliyotaja Mheshimiwa Mbunge ni kati ya maeneo yatakayopendekezwa kusambaziwa umeme huo.

Na. 272

**Umeme wa REA – Momba**

**MHE. DAVID E. SILINDE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itamaliza kusambaza umeme wa *REA* katika Jimbo la Momba kwa maeneo ambayo hayajafikiwa na umeme mpaka sasa?

**WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mbunge wa Momba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Momba ina jumla ya vijiji 72. Kati ya vijiji hivyo vijiji 37 vimepatiwa umeme kupitia miradi ya *TANESCO, REA* awamu ya pili na katika *REA* awamu ya tatu inayoendelea. Vijiji 35 ambavyo havina umeme vitapata umeme kupitia mzunguko wa pili unaotarajia kuanza mwezi Julai, 2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi za mradi wa kupeleka umeme kwenye vijiji 35 vilivyosalia katika Halmashauri ya Momba zitajumuisha ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 33 yenye urefu wa kilomita 197.6. Ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 0.4 yenye urefu wa kilomita 126, pamoja na ufungaji wa transfoma 36 za *KVA* 50 na 100 na kuwaunganishia huduma ya umeme wateja wa awali 1,427. Gharama za mradi ni shilingi bilioni 2.65 na utakamilika mwezi Juni, 2021.

Na. 274

**Ujenzi wa Barabara ya Tabora Mpaka Mhulidade**

**MHE. ALMAS A. MAIGE** aliuliza:-

Barabara ya Tabora mpaka Mambali, Bukene na Ishihimulwa, Shitage mpaka Mhulidade ni muhimu na inaunganisha Mikoa ya Tabora na Shinyanga:-

Je, ni lini barabara hiyo itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami kama ilivyoainishwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2015?

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Almas Athuman Maige, Mbunge wa Tabora Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara anazozungumzia Mheshimiwa Mbunge ni barabara ya Tabora – Mambali -

Bukene – Itobo – Kagongwa (kilomita 168) na Mambali - Bukumbi – Muhulidede – Shitage - Tulole (kilomita 74.7) ambazo zinahudumiwa na Wakala wa Barabara *(TANROADS)* Mikoa ya Tabora na Shinyanga. Kati ya barabara hizo, sehemu ya Bukumbi – Muhulidede (kilomita 24.7) na Muhulidede – Shitage – Tulole (kilomita 21) ni barabara za Wilaya zilizokasimiwa *TANROADS.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa Barabara ya Tabora — Mambali — Bukene — Itobo (kilomita 114) na Nzega — Itobo — Kagongwa (kilomita 54) ili kuzijenga kwa kiwango cha lami inaendelea na inatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2020. Baada ya kazi ya usanifu wa kina kukamilika, Serikali itatafuta fedha ili kuzijenga barabara hizi kwa awamu.

Aidha, katika mwaka wa fedha 2020/2021 jumla ya shilingi milioni 1,000 zimetengwa na Serikali ili kuanza ujenzi wa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu sehemu ya barabara ya Mambali – Bukumbi -Muhulidede — Shitage — Tulole (kilomita 41.5) iliyoko katika Mkoa wa Shinyanga zitaendelea kufanyiwa matengenezo mbalimbali ili ziweze kupitika majira yote ya mwaka.

Na. 275

## Matumizi Kwa Wanaomiliki Silaha Kisheria

**MHE. KHATIBU SAID HAJI** aliuliza:-

Serikali hutoa vibali vya kumiliki silaha kisheria kwa raia wake kwa ajili ya kujilinda:-

Je, ni wakati gani na matukio gani ya hatari ambayo mmiliki wa silaha anapotumia silaha au hata kuua hatakuwa na hatia?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Khatib Said Haji, Mbunge wa Konde, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, silaha itatumiwa na mmiliki wakati wowote kwa matumizi halali yanayozingatia matakwa ya sheria. Aidha, mmiliki wa silaha anaweza kuitumia silaha yake katika hali ya kujihami yeye mwenyewe, kumhami mtu mwingine ama mali dhidi ya hatari/tukio ambalo linaweza kuleta madhara/athari kubwa dhidi ya maisha au mali.

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi ya silaha yanayosababisha kifo hayakubaliki kisheria kwani mmiliki wa silaha anao wajibu wa kutumia silaha kwa usahihi bila kuleta madhara kwa wengine. Hata hivyo, yapo mazingira ambayo mmiliki wa silaha wakati akijilinda ama kumlinda mtu mwingine ama mali yanaweza kusababisha kifo ambapo katika mazingira hayo Mahakama inaweza kumuona/kupima uwiano wa nguvu iliyotumika ya matumizi ya silaha dhidi ya hatari/tishio.

Na. 276

**Kilimo cha Mpunga – Mpanda**

**MHE. RICHARD P. MBOGO** aliuliza:-

Kata ya Itenka, Ibindi, Kakese na Mwamkulu Wilaya ya Mpanda zinalima kwa wingi zao la mpunga:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kufanya wananchi wa maeneo hayo kuwa na kilimo cha mara mbili kila mwaka?

**WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Richard Philip Mbogo, Mbunge wa Jimbo la Nsimbo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Kata za Itenka, Ibindi, Kakese na Mwamkulu Wilaya ya Mpanda zinalima kwa wingi zao la mpunga. Serikali imejenga Mradi wa Umwagiliaji wa Mwamkulu ambapo utekelezaji wake ulifanyika chini ya Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa *(BRN).* Aidha, mradi huo umekamilika na umeanza kutumika toka mwezi Februari, 2018 na Serikali inaendelea kutafuta fedha ili kuboresha zaidi miundombinu ya umwagiliaji wa mradi huo ili kuwezesha mradi huo kutumika kwa ufanisi na manufaa kwa wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mabadiliko ya tabia ya nchi, Serikali ina mpango wa kujenga Bwawa la Katuma ili kuwezesha Mto Katuma uwe na maji ya kutosha hasa kipindi cha kiangazi. Aidha, Ujenzi wa miradi hiyo ya umwagiliaji kwenye maeneo hayo utawezesha wakulima waweze kulima zaidi ya mara moja kwa msimu na hivyo kuongeza uzalishaji wa mazao kwa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Kata za Itenka, Ibindi na Kakese, tayari Serikali ilishapeleka wataalam waliowezesha uundaji wa Chama cha Wamwagiliaji kinachoitwa KAMBUI. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kujenga Mradi huo mkubwa wa Umwagiliaji utakaohusisha ujenzi wa banio, mifereji na Bwawa la Dirifu ambapo maeneo yote ya ujenzi wa bwawa la Katuma kwenye Mto Katuma na Bwawa la Dirifu kwenye Mto Mpanda tayari yameshaainishwa.

**NAIBU SPIKA:** Katibu!

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge nimuite sasa Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mheshimiwa Luhaga Mpina.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba kutokana na taarifa iliyowasishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Kwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge Kilimo, Mifugo na Maji iliyochambua bajeti ya wizara ya Mifugo na Uvuvi Kifungu cha 99 Mifugo na Kifungu cha 64 Uvuvi; Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kujadili mapitio ya utekelezaji wa mpango wa bajeti wa mwaka 2019/2020. Aidha naliomba pia Bunge lako Tukufu likubali kupisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi katika mwaka wa 2020/2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote tunamshukuru Mwenyeki kwa kutuweza kusimamia kusimama mbele ya Bunge hili Tukufu kuwasilisha hotuba yangu hii siku leo. Aidha kwa heshima na unyenyekevu mkubwa namshukuru sana Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini kushika wadhifa huu.

Mheshimimiwa Naibu Spika, pia nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuingoza nchi yetu kwa uhodari na umahili mkubwa kwa takribani miaka mitano sasa tangu aingie madarakani. Katika kipindi hicho tumeshuhudia maendeleo makubwa ya kiuchumi na kijamii, umahili na uhodari wake katika kuiongoza nchi umegusa na kusisimua Taasisi za Kimataifa Afrika na Dunia. Pia amekuwa kiongozi wa mfano na gumzo kila kona Mungu ambariki sana Rais wetu aendeleze mapambano ya kutafuta maendeleo ya kweli kwa Watanzania Afrika na Dunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa hatua alizozichukua katika mapambano haya ya janga la ugonjwa wa *(COVID 19)* unaoambukizwa na virusi vya corona, Rais wetu ametuondolea hofu watanzania na kuweka msimamo usioyumba katika kukabiliana na janga hili jambo linalowezesha watanzania kuendelea na shughuli zao za kiuchumi huku wakichukua tahathali za ugonjwa huu *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Ally Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa Mbunge wa Rungwa na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna wanavyomsaidia sana Mheshimiwa Rais kuiongoza nchi yetu vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukupongeza wewe binafsi, Mheshimiwa Spika na Wenyeviti ambao mmetuongoza vizuri sana katika kuhakikisha kwamba majukumu ya Serikali yanatekelezwa. Aidha naipongeza Kamati ya Kudumu ya Bunge, Kilimo, Mifugo na Maji inayoongozwa na Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mgimwa - Mbunge wa Mufindi Kaskazini na Makamu wake Mheshimiwa Christine Gabriel Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum Morogoro na Wabunge wote wa Kamati kwa ushirikiano wao mkubwa maelezo na ushauri mzuri walioutoa wakati wa kupitia taarifa ya utekelezaji wa mpango wa bajeti ya Wizara ya mwaka 2019/2020 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha katika mwaka 2020/2021. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imepokea kwa masikitiko makubwa taarifa za vifo cha Mheshimiwa Balozi. Dkt. Augustine Philip Mahiga, Mbunge wa Kuteuliwa na Waziri wa Katiba na Sheria; Mheshimiwa. Ajali Rashid Akbar, Mbunge wa Newala Vijijini; na Askofu Dkt. Getrude Pangalile Rwakatare, Mbunge wa Viti Maalum Morogoro; na Mheshimiwa. Richard Mganga Ndassa, Mbunge wa Sumve; naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa salaam za pole kwa familia ya marehemu, ndugu na wananchi ambao walikuwa wakiwatumikia Wabunge hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nichukue nafasi hii kumshukuru Naibu Waziri wangu wa Mifugo na Uvuvi Mheshimiwa Abdallah Hamis Ulega, Mbunge wa Jimbo la Mkuranga kwa jinsi alivyonisaidia katika kuiongoza wizara hii hakika wananchi wa Mkuranga wamepata mwakilishi

makini ndani ya Bunge na Serikali naamini kwamba wataendelea kumuunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nawashukuru Makatibu Wakuu Dkt. Rashid Tamatamah (Uvuvi) na Katibu Mkuu Profesa Elisante Ole Gabriel (Mifugo) kwa kuwa kiungo kikubwa cha watumishi na kwakuwezesha kutekeleza majukumu ya Wizara kwa ufanisi. Aidha, ninawashukuru kwa dhati na kuwapongeza watumishi wote wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa mara nyingine tena niwapongeze na kuwashukuru sana wananchi wangu wa Jimbo la Kisesa ninaloliwakilisha kwa kunichagua kwa ushirikiano wote walioendelea kunipa katika kipindi hiki cha uwakilishi wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji mpango wa bajeti mwaka 2019/2020, mpango wa bajeti wa mwaka 2020/ 2021 ambao umeanishwa katika mapato na matumizi yameanishwa katika ile Ibara ya 20 mpaka ya 27, makusanyo na maduhuli, katika mwaka wa 2019/2020 Wizara kupitia Fungu la 99 ilitarajia kukusanya shilingi bilioni 50, hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2020 Wizara imeweza kukusanya shilingi kupitia hili Fungu la 99 Mifugo imekusanya bilioni 38.5 ambayo sawa na asilimia 77 ya lengo lengo lote la kukusanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika 2019/2020 Fungu la 99 ilitengewa jumla ya shilingi bilioni 28.77 hadi kufikia tarehe 30 Aprili jumla ya shilingi bilioni 22.14 zilikuwa zimetolewa ambazo ni sawa na asilimia 79.96 ya bajeti ya bajeti yote. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 12.78 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni 9.3 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi ya maendeleo, katika mwaka wa 2019/2020 Wizara kupitia Fungu la 99 ilitengewa jumla ya shilingi bilioni 3 kwa ajili ya matumizi ya maendeleo, hadi kufikia tarehe 30 Aprili 2020 kiasi cha shilingi milioni 328.8 sawa na asilimia 10.9 kilipokelewa kutoka Wizara ya Fedha na Mipango.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo linalofuata ni Sera, Sheria Kanuni, Wizara imeendelea kupitia Sheria za Sekta ya Mifugo kwa ajili ya kuboresha mazingira na kuwezesha ukuaji wa Sekta ya Mifugo, ambapo marekebisho ya Sheria na ustawi wa ambao Sheria mbalimbali zimefanyiwa marekebisho. Wizara imeandaa kanuni 11 chini ya Sheria ya magonjwa ya wanayama sura ya 156 kiambatisho cha nne (4) na Kanuni na Sheria zingine zilizotajwa katika eneo hilo. Katika mwaka 2020 Wizara itaendelea kuratibu na kuboresha Sheria, Kanuni na Taratibu kuu ili kuweza kuhusu ubora wa bidhaa za mifugo pembejeo na huduma za Kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uhimilishaji, Wizara imehimilisha jumla ya ng'ombe 76,612 kutoka katika Mikoa 21 ya Tanzania Bara na kati ya mifugo hao ng'ombe 4,668 wamehilishwa bure na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, biashara ya mifugo na mazao yake, udhibiti wa biashara ya mifugo na mazao yake, katika operesheni Nzagamba kulikuwa na ukwepaji mkubwa kabla ya operesheni Nzagamba kulikuwa na ukwepaji mkubwa wa kulipa maduhuli ya biashara ya mifugo na mazao yake; uingizaji holela ya mazao ya mifugo na uuzwaji wa bidhaa za mifugo zisizokidhi viwango.

Katika mwaka 2019/2020 Wizara imeendelea kutekeleza opereseheni zagamba ili kudhibiti utoroshaji wa mifugo na mazao ndani na nje ya nchi kupitia operesheni hizo hadi kufikia tarehe 30 Aprili 2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio makubwa yameweza kupatikana ambapo jumla ya shilingi bilioni 5.5 zimekwishakusanywa kupitia doria hii, lakini jumla ng'ombe 362,661;mbuzi 676,715 walikaguliwa ambapo mifugo 3,393 ilikamatwa ikiwa inatoroshwa kwenda nje ya nchi. Pia jumla ya lita za maziwa 5,621 na kilo 303.69 za nyama na bidhaa zake, trei 112 zilikamatwa zikiwa zinaingizwa nchini kinyume cha Sheria, udhibiti huu umesaidia na kuhamasisha ujenzi wa viwanda vipya vingi ambavyo vinaendelea kujengwa hapa nchini kwetu sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu machinjio ya Dodoma ilipokabidhiwa kwa kampuni ya *TMCL* mwaka 2008 utendaji wake umekuwa siyo wa kuridhisha. Aidha majengo, miundombinu na machinjio, mitambo na vifaa vimechakaa bila ukarabati wowote, kuongezeka kwa madeni na kutengeneza hasara kila mwaka na haijawahi kutoa gawio kwa Serikali, pia usimamizi dhaifu na ubadhilifu wa fedha umepelekea Serikali kupata hasara ya shilingi bilioni 42.28 kwa kipindi cha miaka 11 kutokana na udhaifu huo wa uendeshaji na uchakavu wa machinjio hiyo Wizara ya Mazingira inayosimamia ubora wa wanyama iliifutia machinjio ithibati ya kuuza nyama katika Nchi Falme za Kiarabu. Kwa kuwa Serikali ilifanya jitihada nyingi sana kunusuru machinjio hii bila mafanikio yoyote mnamo tarehe 27 Desemba 2019 Wizara ilirejesha machinjio hayo serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na uamuzi huo kumekuwepo na mafanikio makubwa ambapo ndani ya muda wa miezi minne tu uchinjaji wa mifugo umeongezeka kutoka wastani wa ng'ombe 41 na kufikia wastani wa ng'ombe 125 kwa siku. Pia makusanyo ya mapato yameongeza kutoka wastani wa milioni 39.8 hadi shilingi milioni 90.2 kwa mwezi. Katika kipindi cha miezi minne Wizara imeweza kulipia gharama ya uendeshaji ikiwemo kulipa kishahara ya watumishi; kupata faida kubwa na sehemu ya fedha hizo kwa mara ya kwanza tumeweza kutoa gawio la Serikalini la bilioni 70. Hali hii ni mara ya kwanza kwa Serikali kupata gawio kutoka katika machinjio hiyo. Aidha kampuni ya *NICOL* na *NARCO* wamekubaliana kuvunja kampuni ya *TMSL* bila kwenda Mahakamani, pia Serikali imeendelea na ukarabati wa kuboresha ili kuweza kupata ithibaki ya kuuza nyama katika Falme za Kiarabu*. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2020/2021 Wizara itaendelea kuimarisha machinjio ya Dodoma kwa kuweka usimamizi wa machinjio hiyo chini ya Taasisi ya *RITA* na *NARCO.*

Mheshimiwa Naibu Spika, malisho na maji, ustawi wa mifugo, utatuzi wa migogoro baina ya wafugaji na watumiai

wengine wa ardhi. Katika kutatua migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi Mheshimiwa Rais John Pombe Joseph Magufuli aliamua kuunda timu ya Mawaziri nane iliyoongozwa na William Vangimembe Lukuvi Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo na Makaazi Mbunge wa Isimani ili kupata ufumbuzi wa migogoro ya ardhi katika maeneo ya wafugaji, wakulima na watumiaji wengine wa ardhi. Timu hiyo ilizunguka nchi nzima kwenda kwenye maeneo yenye migogoro kwa kutumia ndege maalum ya kijeshi ambapo baadaye Mheshimiwa Rais alitoa maagizo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kurasimisha Vijiji 920 ambavyo vina migogoro na matumizi ya ardhi hifadhi na mashamba, *Ranchi* na mapori ya akiba, na vyanzo vya maji visiondolewe katika maeneo yake. Lakini Mheshimiwa Rais pia aliagiza kufutwa kwa jumla mapori tengefu 12 yenye hekta 707,659.94 yamefutwa na misitu saba yenye ukubwa wa hekta 46,247 na yenye yamefutwa, lakini pia akaagiza hifadhi ya misitu 14 na mashamba 16 yasiyoendelezwa yamegwe na kugawiwa wananchi, hali hii imeleta unafuu mkubwa sana kwa wananchi wenye migogoro ya ardhi. Hivi sasa Wizara nane za Kisekta ziko zinaendelea kutekeleza maagizo ya Mheshimiwa Rais*. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2019/2020 Wizara yangu ilifanya ziara katika halmashauri 152 kwa lengo la kukutana kusikiliza na kutatua changamoto zinazowakabili wafugaji; ziara hiyo ilipokewa kwa vilio kwa baadhi ya maeneo ambao yana migogoro sugu baina na wafugaji na watuamiji wengine wa ardhi. Naomba nitoe maelezo kwa muhtasari kuhusu migogoro hiyo kama ilivyoainishwa wakati wa ziara:-

Mheshimiwa Naibu Spika, migogoro kati ya wakulima na wafugaji, wafugaji wanaingiza mifugo yao katika mashamba ya wakulima na kuharibu mazao yao, lakini wafugaji huvamia vyanzo vya maji na kuwapiga na kuwaumiza wakulima na kukataa kuwalipa fidia. Lakini wakulima kuvamia na kufanya shughuli za kilimo katika

maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya kulishia mifugo yao, wakulima kuziba njia mifugo na kwenda katika malisho maji, josho mnada, kukata mapanga mifugo, kushikilia mifugo kwa muda mrefu. Lakini pia baadhi wa watendaji wa Serikali kulalamikiwa kwakutokutenda haki kwa kufaya upendeleo yanapotokea malalamiko ya wakulima na wafugaji.

(i) Migogoro kati ya mamlaka za hifadhi na mashamba ya Serikali malalamiko yalikuwa ni mengi ambapo wafugaji kuvamia na kuingiza mifugo yao ndani ya maeneo ya hifadhi na mashamba ya Serikali na kusababisha uharifu mkubwa wa mazingira na kueneza magonjwa baina ya mifugo na wanyamapori;

(ii) Kutanua mipaka ya hifadhi na kujumuisha maeneo ya malisho kwenye hifadhi, hifadhi kutokuwa na alama na mipaka inayoonekana hali inayolepekea mifugo kukamatwa hata ikiwa nje ya hifadhi;

(iii) Maeneo ya malisho kubadilishwa matumiz bila kuzingatia mahitaji, uwazishwaji wa *WMA* na kukatazwa matumizi ya mseto katika maeneo hao kumechangia kupungua kwa maeneo ya malisho nchini,

(iv) Mifugo kushikiliwa kwa muda mrefu bila kupatiwa huduma muhimu kama maji, malisho, chanjo, matibabu ambapo kumepelekea mifugo mingi kufa ikiwa imeshilikiwa;

(v) Wafugaji wanaposhinda kesi Mahakamani hawarudishiwi mifugo na pengine kurudishiwa mifugo pungufu;

(vi) Baadhi ya Maaskari wa hifadhi wamekuwa wakiwapiga risasi mifugo ili kuwakomoa wafugaji na kupoteza ushahidi, mifugo kuuzwa kiholela wakati ikiwa imeshikiliwa;

(vii) Ukamataji holela wa mifugo usioshirikisha viongozi wa Vijiji na wamiliki wa mifugo umepelekea kutofautiana kwa idadi ya mifugo iliyokamatwa na inayofikishwa Mahakamani, wanyamapori wakali, simba, chui na tembo wamekuwa

wakishambulia mifugo bila kupata msahada fidia yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya mamlaka za Miji zimekuwa zikilazimisha wafugaji kuhamisha mifugo yao bila kuzingatia haki zao za umiliki wa ardhi, na mwisho wafugaji kulalamika kutozwa faini kubwa kinyume cha Sheria ya mifugo na mifugo yao inapokamatwa katika maeneo yasiyoruhusiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kutatua migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi, migogoro mkubwa 11 kati ya 17 imekwishakutatuliwa, migogoro iliyotatuliwa imeainishwa katika maeneo mbalimbali. Pia Wizara imemega hekta 29.4 kutoka katika mashamba ya Ranchi na kuwapatia wananchi. Serikali pia imewezesha kupimwa kwa hekta 108,427.49 zimepimwa za Halmashauri ii kupunguza matatizo ya wafugaji. Lakini pia Serikali imeamua kuwapangisha wafugaji katika hekta 778,470 ili kuweza kupunguza hii kero ya ukosefu wa malisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara pia imeweza kuhakikisha kwamba maeneo ambayo hayapimwa nayo yamepimwa na kwa sasa malalamiko haya yote katika mwaka huu wa 2020/2021 Wizara itaendelea kutenga na kupima zaidi ya hekta 1,500,000 ili kuweza kumaliza hili tatizo la malisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, magonjwa, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2019 hadi Aprili, 2020 jumla ya matukio 537 ya magonjwa mbalimbali ya mifugo yalitolewa katika maeneo mbalimbali. Ikilinganishwa na matukio 1,025 yaliyotolewa taarifa katika mwaka 2018/2019 nchini. Ambapo mifugo iliyopatwa na magonjwa imepungua kwa asilimia 29, mifugo iliyokufa imepungua kwa asilimia 37.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kuchukua hatua mahususi ya kukabiliana na magonjwa 13 ya kimkakati kwa kuzingatia sera, sheria, kanuni na haki ya ustawi wa wanyama.

Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya michovyo milioni 211 ya uogeshaji imefanyika katika mwaka 2019/2020 ikilinganishwa na michovyo milioni 101 iliyofanyika katika katika mwaka 2018. Tumeweza kukarabati majosho 542 ambayo yalikuwa hayafanyi kazi na sasa yanafanya kazi na tumejenga majosho mapya 85. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo mengine yametolewa ufafanuzi katika hilo eneo la utafiti. Wizara imeandaa Agenda ya Utafiti ya Kitaifa ya Mifugo ya Miaka Mitano *(Livestock Research agenda 2020 - 2025)* iliyozinduliwa tarehe 16 Novemba, 2011. Lengo la Ajenda hii ni kutekeleza vipaumbele vya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza ajenda hii kwa ufanisi Wizara imeandaa *Livestock Research Regulations 2020,* pia imeandaa Kanzidata za Mifugo Nchini *(The National Livestock Research Database).* Matokeo makubwa hapa yameonekana kwa kuanzishwa kwa tafiti hizi na mpaka sasa tumeweza kuibua jumla ya tafiti 433 zilizokuwa zimefungiwa kwenye makabati na sasa hizo Tafiti kutoka kwenye Taasisi mbalimbali zimeweza kutumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia *TALIRI* kupitia utekelezaji wake, Mradi wa *MOET* sasa umeanza kufanya kazi na tayari viini tete 34 kwa ng'ombe wenye kulea mimba 34 na mpaka sasa hivi tayari zoezi limeshaanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, makusanyo ya maduhuli yameainishwa, maeneo ya vipaumbele yameainishwa. Katika kuhakikisha kwamba sheria inayosimamia Sekta ya Uvuvi inakidhi mahitaji yaliyomo kwa sasa. Wizara imeamua kuifumua kwa sasa Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya mwaka 2003 na kanuni zake za mwaka 2009 ambapo itazalisha sheria mpya ya Uvuvi na sheria mpya ya Ukuzaji viumbe maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, sheria imefanyiwa mapitio na marekebisho katika Kifungu cha 8 (40) na (47) ili kuwa na adhabu zinaendana na ukubwa wa makosa. Vile vile Wizara imefanya marekebisho ya baadhi ya Kanuni za Uvuvi ya Mwaka

2009 ili kuliwezesha Taifa kunufaika na rasilimali zake. Baadhi ya marekebisho yaliyofanywa katika sheria hiyo ni:-

(i) Kuruhusu matumizi ya taa za nguvu ya *solar* katika maeneo ya uvuvi katika Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika, Ziwa Nyasa na Bahari ya Hindi; (Makofi)

(ii) Kuruhusu matumizi ya nyavu za makila za kuunganishwa, kufikia ukomo wa macho 78 katika Ziwa Victoria; na Ziwa Tanganyika macho 144 katika uvuvi wa samaki aina ya sangara na migebuka;

(iii) Kuruhusu matumizi ya *ring net* ya uvuvi wa dagaa katika Ziwa Tanganyika kwa umbali wa mita 1,000 kutoka mwaloni, peninsula na kisiwa;

(iv) Kuruhusu nyavu za makila zenye ukubwa wa macho inchi 1.5 kwa ajili ya uvuvi wa samaki aina ya vitui na matula katika Ziwa Nyasa; *(Makofi)*

(v) Kuweka mazingira ya kipimo kisichopungua sentimita mbili kwa samaki wabichi; na sentimita tatu kwa samaki waliokaushwa;

(vi) Kuruhusu msimu wa uvuvi wa samaki aina ya kambamiti katika kipindi cha kuanzia tarehe 1 Machi hadi tarehe 30 Septemba kwa ukanda wa Kaskazini na kuanzia tarehe 1 Aprili hadi tarehe 31 Agosti kila mwaka katika ukanda wa Kusini;

(vii) Kuruhusu uzito wa pweza kuanzia gramu 450 baada ya kuchakatwa;

(viii) Kuruhusu uvuvi wa kamba kochi aina ya pakupaku kuanzia gramu 250;

(ix) Kuruhusu kuvuliwa kwa samaki jamii ya perege wenye urefu wa kuanzia sentimita 20 katika Ziwa Rukwa, Ziwa Tanganyika, Ziwa Nyasa, Bwawa la Mtera na Bwawa la Nyumba ya Mungu;

(x) Kuruhusu samaki wasiochakatwa *bullet fish* waliotolewa matumbo tu kuuzwa katika masoko ya kikanda na Kimataifa;

(xi) Kuruhusu biashara ya mabondo chini ya urefu wa sentimita 12 au uzito wa gramu 13 kwa mabondo mabichi na urefu wa sentimita nane au uzito wa gramu nne kwa mabondo makavu; na

(xii) Kuweka miongozo ya usimamizi wa uvuvi katika maji madogo kwenye maziwa ya Eyasi, Manyara, Kitangiri, Rukwa, Singidani, Msoto, Burigi, Bwawa la Bahi na Mto Kilombero.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imesikia kilio cha wadau wa uvuvi na kufanya maboresho ya ada mbalimbali za leseni katika *loyality* ambako Waziri wa Fedha atakapokuja hapa ataainisha maeneo yote ya *loyality* ambayo yameweza kupunguzwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uvunaji wetu wa rasilimali unazidi kuongezeka na mpaka sasa hivi tayari tumeshavuna rasilimali yenye thamani ya shilingi bilioni 636.96 nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, uingizaji wa samaki kutoka nje ya nchi umepungua kwa asilimia 99.9 ambapo kutoka wastani wa bilioni 56 mpaka shilingi milioni 161 tu. Katika kipindi cha miaka mitatu, mapambano dhidi ya uvuvi haramu yameendelea vizuri sana na mafanikio makubwa sana tumeendelea kuyapata kutokana na haya mapambano ya uvuvi haramu ambayo tunayoendelea nayo. Hii ni pamoja na kuongezeka kwa samaki na kushuka kwa bei ya mazao ya uvuvi ambapo kwa sasa hivi tumeonyesha katika jedwali letu kwamba samaki wameongezeka kwa wingi katika makundi mbalimbali na soko letu la nje na lenyewe linazidi kuongezeka mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeandaa Mpango wa Biashara wa Shirika la Uvuvi Tanzania *(TAFICO).* Lengo la Mpango huu ni kutoa mwelekeo wa kibiashara wa Shirika hili

kwa kipindi cha miaka 10 ambapo itafanyika kupitia Serikali na Sekta Binafsi kwa njia ya ubia. Mpango huu umeainisha miradi mikubwa mitatu ambayo imeainishwa. Fedha kiasi cha shilingi bilioni 4.2 zimeshapatikana kwa kuanzia na tayari mipango imeanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Serikali imeendelea na mazungumzo na Mfuko wa Maendeleo wa Dunia *(IFAD)* ili kuwezesha kupatikana kwa Shilingi bilioni 68.8 kwa ajili ya ununuzi wa meli na kuanza kwa shirika hili. Wizara inaendelea kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa Bandari ya Uvuvi kupitia Mtaalam Mwelekezi ambaye ni Kampuni iliyotajwa na fedha zimeshaanza kulipwa. Ubora na usalama wa mazao umeainishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Dawati la Sekta Binafsi limeendelea kutekeleza majukumu yake vizuri. Katika uwezeshaji, Wizara imeendelea kuhamasisha ujenzi wa viwanda vya nyama ili kuzalisha nyama safi na salama kwa ajili ya soko la ndani na viwanda vilivyohamasika ni hiyo *Tan Choice* ambacho kipo asilimia 90, sasa kitaanza uzalishaji - *Elia Foods;* viwanda hivi vyote viwili vinategemewa kuanza uzalishaji mwezi wa sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tuna kiwanda cha Gereza la Karanga, ambacho uwekezaji wake ni shilingi bilioni 75; na bado tuna kiwanda kingine cha *ACE Leather* kwa ajili ya ngozi, shilingi bilioni 23 na chenyewe ujenzi wake uko hatua za mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, gawio la Serikali katika Taasisi za Wizara ya Mifugo na Uvuvi limeongezeka kutoka shilingi milioni 520 hadi shilingi bilioni 1.49. Mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli unaendelea vizuri katika malengo ya shilingi bilioni 82.3 na sasa tumefikia shilingi bilioni 62.9 sawa na asilimia 75.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho; kwa namna ya pekee ninampongeza na kumshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe

Joseph Magufuli, kwa namna anavyoliongoza Taifa letu na anavyotusimamia katika kutekeleza majukumu ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimewahi kukutana na kufanya kazi na viongozi wengi ndani na nje ya nchi, lakini Mheshimiwa Rais wewe ni Kiongozi na Mwalimu bora, nakushukuru sana. Umenikabidhi majukumu ambayo ninayatekeleza kikamilifu katika Wizara yangu na kuhakikisha kuwa ahadi ulizozitoa kwa Watanzania wakati unaomba kura mwaka 2015 zimetimia na kuhakikisha kuwa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015 - 2020 imetekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nichukue nafasi hii kuwapongeza wafugaji na wavuvi wote nchini kwa kazi nzuri wanazozifanya za kutunza, kuzalisha na kulinda rasilimali za Taifa. Kazi wanazozifanya ni nzuri na za heshima na kwamba Wizara yangu itaendelea kusimamia na kuunga mkono juhudi zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nawashukuru wafanyabiashara na wawekezaji na wadau wote katika Sekta za Mifugo na Uvuvi kwa dhamira hiyo njema ya kuendeleza sekta.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nirejee tena kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Abdallah Hamis Ulega, Mbunge wa Jimbo la Mkuranga, Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi kwa msaada wake katika kusimamia kazi za Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, napenda pia nitoe shukrani zangu za dhati kwa Katibu, Mkuu Uvuvi, Dkt. Rashid Tamatamah; na Katibu Mkuu, Profesa Elisante Gabriel; Wakurugenzi pamoja na watendaji wote wa Wizara na Taasisi kwa kazi nzuri sana wanazofanya. Nimefurahi sana kufanya kazi na ninyi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimwa Waziri omba fedha.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia.

**NAIBU SPIKA:** Omba fedha.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimefurahi sana kufanya kazi na ninyi na nawapongeza kwa kukubali mabadiliko na kukubali kuchapa kazi usiku na mchana kwa kauli mbiu ya masaa ni namba tu kwa manufaa ya Taifa letu, tunalojivunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwandishi wa Kitabu cha "*How Successful People lead.*" *John Maxwell* aliwahi kusema: "*Nobody achieves anything greater by giving the minimum*. *No teams wins championship without making sacrifices and giving their best*." Namwomba Mungu aendelee kuwabariki katika utumishi wenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wangu watakumbuka kuwa walinichagua nikiwa bado kijana mdogo, hadi sasa zijawahi kuwaangusha...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri omba fedha.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** ...jembe lipo shambani, muda ukifika niwahisheni tena. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuomba fedha. Sekta ya Mifugo Wizara inaomba kutumia jumla ya shilingi 32,096,197,000 kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya Sekta ya Mifugo. Kati ya fedha hizo, shilingi 27,034,826,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 5,061,371,000 ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Mgawanyo wake ni kama hivyo nilivyoouonyesha hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu la 64 – Uvuvi; katika mwaka 2020/2021, Wizara inaomba jumla ya shilingi 34,721,321,000 kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya Sekta ya Uvuvi. Kati ya fedha hizo, shilingi 21,662,107,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 13,059,214,000 ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo katika mgawanyiko huo niliouanisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge wote.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

## HOTUBA YA WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI MHESHIMIWA LUHAGA JOELSON MPINA (MB) KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI KWA MWAKA 2020/2021 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

### A. UTANGULIZI

***1. Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja kwamba, kutokana na taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge inayosimamia Kilimo, Mifugo na Maji iliyochambua Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Fungu 99 – Mifugo na Fungu 64 – Uvuvi) Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kujadili Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2019/2020. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

***2. Mheshimiwa Spika,*** Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha hotuba yangu siku ya leo. Aidha, kwa heshima na unyenyekevu mkubwa namshukuru sana **Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini kushika wadhifa huu. Pia, nampongeza Mheshimiwa

Rais kwa kuiongoza nchi yetu kwa uhodari na umahiri mkubwa kwa takriban miaka mitano (5) tangu aingie madarakani. Katika kipindi hicho tumeshuhudia maendeleo makubwa ya kiuchumi na kijamii, umahiri na uhodari wake katika kuiongoza nchi yetu umegusa na kusisimua Taasisi za Kimataifa, Afrika na Dunia pia amekuwa kiongozi wa mfano na gumzo kila kona Mungu ambariki Rais wetu ili aendeleze mapambano ya kutafuta maendeleo ya kweli ya Watanzania, Waafrika na Dunia.

***3. Mheshimiwa Spika,*** nampongeza Mheshimiwa Rais kwa hatua anazochukua katika kipindi hiki kigumu cha janga la ugonjwa wa *CORONA (COVID – 19)* unaoambukizwa na Virusi vya Corona, Rais wetu amewaondolea hofu watanzania na kuweka msimamo usioyumba katika kukabiliana na janga hili jambo lililowezesha watanzania kuendelea na shughuli zao za kiuchumi huku wakichukua tahadhari ya kujikinga na ugonjwa huo.

***4. Mheshimiwa Spika,*** nawapongeza Mheshimiwa **Samia Suluhu Hassan,** Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa **Dkt. Ally Mohamed Shein**, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Mheshimiwa **Kassim Majaliwa Majaliwa,** Mbunge wa Jimbo la Ruangwa na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna wanavyomsaidia Mhe. Rais kuiongoza vema nchi yetu kwa hekima na busara.

***5. Mheshimiwa Spika,*** aidha, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza, Mheshimiwa **Kassim Majaliwa Majaliwa,** Mbunge wa Jimbo la Ruangwa na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwasilisha hotuba yake iliyotoa mwelekeo wa utendaji wa sekta zote katika Serikali. Pia, namshukuru na kumpongeza **Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango (Mb**) Waziri wa Fedha na Mipango, kwa wasilisho lake la Mpango wa Bajeti ambao umefafanua vizuri mipango na mikakati ya Serikali katika mwaka wa fedha 2020/2021 wenye lengo la kuimarisha na kuboresha huduma za kiuchumi na kijamii nchini.

***6. Mheshimiwa Spika,*** napenda pia kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa kuliongoza vizuri Bunge letu Tukufu. Uongozi wenu bora umewezesha Bunge la **11** kutekeleza majukumu yake kikamilifu kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo.

***7. Mheshimiwa Spika,*** naomba kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji chini ya Mwenyekiti wake **Mhe. Mahamoud Hassan Mgimwa**, Mbunge wa Mufindi Kaskazini na Makamu wake **Mhe. Dkt. Christine Gabriel Ishengoma**, Mbunge wa Viti Maalum wa Mkoa wa Morogoro kwa ushirikiano, maelekezo na ushauri mzuri walioutoa wakati wa kupitia Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2019/2020 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Aidha, napenda kuwapongeza Mhe. Justine Monko, Mbunge wa Singida Kaskazini, Mhe. Miraji Mtaturu, Mbunge wa Singida Mashiriki, Mhe. Dkt. John Daniel Pallangyo, Mbunge wa Arumeru Mashariki kwa kuchaguliwa na kisha kuapishwa na Bunge lako Tukufu ili wawatumikie wananchi waliowachagua.

***8. Mheshimiwa Spika,*** Wizara ilipokea kwa masikitiko makubwa taarifa za vifo vya **Mhe. Balozi. Dkt. Augustine Philip Mahiga**, Mbunge wa Kuteuliwa na Waziri wa Sheria na Katiba; **Mhe. Ajali Rashid Akbar**, Mbunge wa Newala Vijijini; **Mhe. Askofu Dkt. Getrude Pangalile Rwakatare**, Mbunge wa Viti Maalum Morogoro; na **Mhe. Richard Mganga Ndassa**, Mbunge wa Sumve; Naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa salaam za pole kwa familia za marehemu, ndugu na wananchi ambao walikuwa wanatumikiwa na Wabunge hao. Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi, AMINA. Aidha, naomba nitumie fursa hii kuwapa pole Waheshimiwa Wabunge waliopata ajali mbalimbali na waliougua katika kipindi cha mwaka 2019/2020.

Napenda pia kuwapa pole wale waliopoteza ndugu zao na wapendwa wao kutokana na Ugonjwa wa *Corona (COVID – 19)(COVID – 19*), ninawaombea kila la kheri wale ambao wameambukizwa ugonjwa huo ili Mungu awape afya njema mapema iwezekanavyo. Tuendelee kuzingatia maelekezo ya

kitaalamu yanayotolewa na viongozi mbalimbali kwa ajili ya tahadhari huku tukiendelea kufanya kazi kwa bidii ili uchumi wetu usitetereke.

***9. Mheshimiwa Spika*,** ninaomba nichukue nafasi hii ya pekee kumpongeza Mhe. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb) kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Sheria na Katiba katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

***10. Mheshimiwa Spika*,** pia nichukue nafasi hii kumshukuru Naibu Waziri wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi **Mhe. Abdallah Hamis Ulega**, Mbunge wa Jimbo la Mkuranga kwa jinsi alivyonisaidia katika kuiongoza wizara hii hakika wananchi wa Mkuranga wamepata mwakilishi makini ndani ya Bunge na Serikali na ninaamini kwamba wataendelea kumuunga mkono, pia nawashukuru Makatibu Wakuu wa Wizara **Dkt. Rashid Adam Tamatamah** (Uvuvi) na Prof**. Elisante Ole Gabriel** (Mifugo) kwa kuwa kiungo kikubwa cha watumishi na kuwezesha kutekeleza majukumu ya wizara kwa ufanisi. Aidha, ninawashukuru kwa dhati na kuwapongeza watumishi wote wa Wizara yangu kwa kazi nzuri mnayofanya.

***11. Mheshimiwa Spika,*** naomba kwa mara nyingine tena niwapongeze na kuwashukuru wannachi wa Jimbo ninaloliwakilisha, yaani Jimbo la Kisesa, lililopo Mkoa wa Simiyu, kwa kunichagua na kwa ushirikiano wanaoendelea kunipa katika kuwawakilisha na kuwatumikia katika Bunge hili Tukufu.

## B. SEKTA YA MIFUGO (FUNGU 99) HALI HALISI YA SEKTA YA MIFUGO

***12. Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2019/2020 idadi ya mifugo hapa nchini inakadiriwa kuongezeka ikilinganishwa na mwaka 2018/2019 ambapo idadi ya ng'ombe imeongezeka kutoka **milioni 32.23** hadi **milioni 33.4,** mbuzi kutoka **milioni 20** hadi **milioni 21.29** na kondoo kutoka **milioni 5.5** hadi **milioni 5.65.** Aidha, kuku wameongezeka kutoka **milioni 79.1** hadi **milioni 83.28** ikiwa kuku wa asili wameongezeka kutoka **milioni 38.5** hadi **milioni 38.77**, kuku wa kisasa wameongezeka kutoka

**milioni 40.6** hadi **milioni 44.51**, nguruwe kutoka **milioni 2** hadi **milioni 2.14** na punda kutoka **636,997** hadi **657,389 (**Taarifa ya Uchambuzi wa Sekta ya Mifugo Tanzania 2016/2017 - 2031/2032**)**. Aidha, Sekta ya Mifugo katika mwaka 2019 ilikua kwa asilimia **5** na kuchangia asilimia **7.4** katika Pato la Taifa ikilinganishwa na kukua kwa asilimia **4.9** na kuchangia asilimia **7.2** katika Pato la Taifa mwaka 2018.

***13. Mheshimiwa Spika,*** uzalishaji wa maziwa umeongezeka kwa asilimia **12.1** kutoka lita **bilioni 2.7** mwaka 2018/2019 hadi kufikia lita **bilioni 3.0** mwaka 2019/2020 **(**Taarifa ya Uchambuzi wa Sekta ya Mifugo Tanzania 2016/2017 - 2031/2032**),** ambapo kati ya hizo, lita **bilioni 2.1** zilitokana na ng'ombe wa asili na lita **bilioni 0.9** zilitokana na ng'ombe wa kisasa (**Kiambatisho Na. 1**). Aidha, kati ya ng'ombe **milioni 33.4** waliopo nchini ng'ombe wa maziwa ni **milioni 1.95** (TLMP).

***14. Mheshimiwa Spika,*** usindikaji wa maziwa umeongezeka kutoka lita **milioni 70.9** mwaka 2018/2019 hadi lita **milioni 74.3** mwaka 2019/2020 sawa na ongezeko la asilimia **4.8**. Hadi sasa, kuna viwanda vya kusindika maziwa **99** kati ya hivyo, viwanda **91** vinafanya kazi na viwanda **8** havifanyi kazi kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo migogoro miongoni mwa wanaushirika na kushindwa katika ushindani wa kibiashara (**Kiambatisho Na. 2**)

***15. Mheshimiwa Spika,*** uzalishaji wa zao la nyama umeongezeka kutoka tani **690,629** mwaka 2018/2019 hadi tani **701,679.1** mwaka 2019/2020 sawa na ongezeko la asilimia **1.6 (Kiambatisho Na. 1)**. Kati ya hizo, tani **486,736.1** za nyama ya ng'ombe, tani **95,964.2 za** nyama ya mbuzi na kondoo, tani **80,601.3** za nyama ya kuku na tani **38,377.4** za nyama ya nguruwe. Aidha, ng'ombe walionenepeshwa wameongezeka kutoka ng'ombe **371,200** mwaka 2018/2019 hadi kufikia ng'ombe **512,256** mwaka 2019/2020 sawa na ongezeko la asilimia **38.**

***16. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020 uzalishaji wa mayai umeongezeka kutoka mayai **bilioni 3.58** mwaka 2018/2019 hadi mayai **bilioni 4.05** mwaka 2019/2020 sawa na

ongezeko la asilimia **13.3 (Kiambatisho Na. 1)**. Ongezeko hilo limesababishwa na kuongezeka kwa vituo vya kutotolesha vifaranga vya kuku.

***17. Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia tarehe 30 Aprili 2020 jumla ya kilo za ngozi **16,746,589.36** (ng'ombe - **14,449,075.49**, mbuzi - **1,775,298.5** na kondoo - **522,215.38)** zenye thamani ya shilingi **bilioni 23.9** zimezalishwa ikilinganishwa na kilo **16,012,800.71** (ng'ombe - **13,904,620.27**, mbuzi - **1,653,669.26** na kondoo - **454,511.17)** zenye thamani ya shilingi **bilioni 22.8** zilizozalishwa mwaka 2018/2019.

***18. Mheshimiwa Spika***, hadi kufikia tarehe 30 Machi, 2020 jumla ya vipande vya ngozi vyenye uzito wa Kilo **6,747,011** (ng'ombe – **5,948,791**, mbuzi/kondoo **114,904** na punda - **683,317**) vyenye thamani ya shilingi bilioni **12.90** viliuzwa nje ya nchi, katika nchi za Ghana, China, Pakistani, Indonesia, Ethiopia, Nigeria na Italy (**Kiambatisho Na. 3**) ikilinganishwa na kilo **5,384,735.79** (ng'ombe – **4,588,579.56**, mbuzi/kondoo **660,369.69** na punda - **114,800.00**) vyenye thamani ya shilingi bilioni **13.0** vilivyouzwa nje katika nchi za Nigeria, Ghana, Ethiopia, China, Italy, Kenya, India, Misri, Uturuki, Pakistani na Benin mwaka 2018/2019.

## 1.0 **UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2019/ 2020 NA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2020 /2021**

## 2.0 **Maeneo ya Kipaumbele katika Mwaka 2019/2020**

***19. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020 maeneo ya kipaumbele katika Mpango na Bajeti ya Wizara kupitia Idara Kuu ya Mifugo (Fungu 99) yatakayotekelezwa ni pamoja na:-

(i) Kuimarisha afya ya mifugo;

(ii) Kuwezesha upatikanaji endelevu wa rasilimali za vyakula vya mifugo na maji kwa ajili ya mifugo;

(iii) Kuboresha kosaafu ya mifugo ili kuongeza tija na uzalishaji:
(iv) Kuboresha biashara ya mifugo ndani na nje;

(v) Kuimarisha huduma za utafiti wa mifugo, huduma za ugani na mafunzo kwa wafugaji na maafisa ugani;

(vi) Kuanzisha na kuimarisha vikundi na vyama vya ushirika vya mazao ya mifugo;

(vii) Kusimamia na kuratibu shughuli za taasisi zilizo chini ya Wizara;

(viii) Kuboresha masuala ya rasilimali watu;

(ix) Kuboresha utekelezaji wa sera, sheria na kanuni katika sekta ya mifugo; na

(x) Kuimarisha uratibu na usimamizi wa wataalamu wa sekta ya mifugo.

## 3.0 **Makusanyo ya Maduhuli**

***20. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, Wizara kupitia Fungu 99 ilitarajia kukusanya kiasi cha shilingi **50,000,000,000.00**. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2020 kiasi cha shilingi **38,501,236,284.25** kimekusanywa sawa na asilimia **77** ya lengo la makusanyo kwa mwaka 2019/2020. Hata hivyo, makusanyo hayo ni sawa na asilimia **92.41** ya makusanyo yaliyolengwa kukusanywa ndani ya kipindi cha miezi kumi (10) ambayo ni shilingi **bilioni 41.66**. Makusanyo hayo hadi Aprili, 2020 (**38,501,236,284.25**) yameongezeka kwa shilingi **6,361,524,248.03** ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2018/2019 ambapo makusanyo yalifikia shilingi **32,139,712,036.22**

## 4.0 **Fedha Zilizoidhinishwa kwa Ajili ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo 2019/2020**

***21. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, Wizara kupitia Fungu 99 ilitengewa jumla ya shilingi **31,774,378,000.00.** Kati ya Fedha hizo, shilingi **28,774,378,000.00** ni fedha za Matumizi ya Kawaida na shilingi **3,000,000,000.00** ni fedha kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo.

## 5.0 **Matumizi ya Bajeti ya Kawaida**

***22. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, Fungu 99 lilitengewa jumla ya shilingi **28,774,378,000.00**. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2020, jumla ya shilingi **22,146,054,084.63** zilikuwa zimetolewa, ambazo ni sawa na asilimia **76.96** ya bajeti iliyotarajiwa kwa miezi kumi na miwili, ikiwa ni sawa na asilimia **92.36** ya kipindi cha miezi kumi (yaani hadi 30 Aprili, 2020). Kati ya hizo, shilingi **12,783,043,056.50** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Wizara (PE) na shilingi **9,363,011,028.13** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC).

## 6.0 **Matumizi ya Bajeti ya Maendeleo**

***23. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, Wizara kupitia Fungu 99 ilitengewa jumla ya shilingi **3,000,000,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo zikiwa ni fedha za ndani ili kutekeleza Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II). Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2020 kiasi cha shilingi **328,821,307.00** (sawa na asilimia **10.9**) kilipokelewa kutoka Wizara ya Fedha na Mipango

## 7.0 **Sera, Sheria na Kanuni Katika Sekta ya Mifugo**

### 7.1 ***Sera, Mikakati na Programu***

***24. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020 Wizara imeendelea kutoa elimu kuhusu Sera ya Taifa ya Mifugo ya mwaka 2006 na Mpango Kabambe wa Kuendeleza Sekta ya Mifugo Tanzania (Tanzania Livestock Master Plan - TLMP). Jumla ya wadau **7,835** walipata elimu hiyo kupitia Maonesho ya Sabasaba, Nanenane na Siku ya Chakula Duniani. Aidha, Wizara imesambaza nakala **150** za Sera ya Taifa ya Mifugo na nakala **120** za Fursa za Uwekezaji kwa wadau katika Sekta ya Mifugo. Vilevile, Wizara imeendelea kutekeleza Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili *(Agriculture Sector Development Programme – ASDP II)*.

***25. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/2021, Wizara itaendelea kutekeleza Programu ya Kuendeleza Sekta ya

Kilimo Awamu ya Pili *(Agriculture Sector Development Programme – ASDP II)* na kuandaa Mpango Mkakati wa Wizara kwa mwaka 2020/2021 hadi 2025/2026, kukamilisha tathmini ya Sera ya Taifa ya Mifugo ya mwaka 2006 na kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi ya mifugo, Wakala, Bodi na Taasisi zilizo chini ya Wizara.

***Sheria na* Kanuni**

***26. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kupitia Sheria za sekta ya mifugo kwa ajili ya kuboresha mazingira na kuwezesha ukuaji wa sekta ya mifugo ambapo marekebisho ya Sheria za Ustawi wa Wanyama SURA 154 na Sheria ya Magonjwa ya Mifugo SURA 156 yamefanyika kupitia *Written Laws Miscelleneous Amendments Act 2019, Act No.14 of 2019.* Aidha, marekebisho ya Sheria za Tasnia ya Maziwa SURA 262 na Sheria ya Tasnia ya Nyama SURA 412 yamefanyika kupitia *Written Laws Miscelleneous Amendments, Act 2020, Act No.1 of 2020*.

***27. Mheshimiwa Spika,*** *mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Nyanda za Malisho n*a Rasilimali za Vyakula vya Mifugo SURA 180 yaliyopo katika Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Written Laws Miscelleneous Amendments Act 2020) tayari yameshasomwa kwa mara ya kwanza katika kikao cha Bunge la Mwezi Januari, 2020.

***28. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeaandaa Kanuni mbalimbali chini ya Sheria ya Magonjwa ya Wanyama SURA 156 na kutangaza katika Gazeti la Serikali kwa ajili ya kuanza kutumika ili kutatua changamoto mbalimbali katika Sekta ya Mifugo (Kiambatisho Na.4), kanuni hizo ni:-

*(i) Animal Diseases (Acaricide Application and Management) Regulations, 2019 GN. No. 955;*

*(ii) Animal Diseases (Hatcharies and Breeding Flock Farms) Regulations, 2019 GN. No.956;*
*(iii) Animal Diseases (Artificial Breeding) Regulations, 2020 GN. No.118*

*(iv) Animal Diseases (Regional Veterinary Officers and District Veterinary Oficers) Notice, 2019 GN. No.66; na*

*(v) The Animal Diseases (Vaccines and Vaccination) Regulations, 2020 GN. Na. 180*

***29. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imefanya marekebisho ya tozo katika Kanuni za Magonjwa ya Wanyama (*Animal and Animal Products Movements Control) 2020* na kuwasilishwa Wizara ya Fedha na Mipango. Aidha, kanuni mbalimbali chini ya Sheria ya Veterinari SURA 319 zimeandaliwa na kutangazwa katika Gazeti la Serikali kwa ajili ya kuanza kutumika. Kanuni hizo ni:-

(i) *The Veterinary (Appointment of Veterinary Inspectors) Notice,2020 GN No.132;*

(ii) *The Veterinary (Cancellation of Veterinarians) Notice, 2020 GN No. 133; na*

(iii) *The Veterinary (Registration of Veterinarians and Veterinary Practise Facility (Amendment) Regulations, 2020 GN No. 134.*

***30. Mheshimiwa Spika,*** chini ya Sheria ya Tasnia ya Nyama SURA 412 kanuni mbalimbali zimeandaliwa na kutangazwa katika Gazeti la Serikali kwa ajili ya kuanza kutumika. Kanuni hizo ni:-

(i) *Meat Industry (Import and Export of Livestock, Meat and Meat Products) (Amendment), 2019 GN.No.538;*

(ii) *Meat Industry (Registration of Meat Industry Stakeholders) (Amendment), 2019 GN.No.677; na*

(iii) *Meat Industry (Inspection of Meat Industry Stakeholders Activities) 2019 GN.No.739*.

***31. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020 Wizara imeandaa Kanuni chini ya Sheria ya Tasnia ya Maziwa (SURA 262), Ustawi wa Wanyama (SURA 154) na Taasisi ya Utafiti wa

Mifugo Tanzania (SURA 434) ambazo zimepitiwa na kuwasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Kanuni hizo ni:-

(i) *The Dairy Industry (Registration of Dairy Industry Stakeholders) (Amendment) Regulations, 2020;*

(ii) *The Dairy Industry (Raw Milk Transportation) (Amendment)Regulations, 2020;*

(iii) *The Dairy Industry (Treatment and Disposal of Unfit Milk) (Amendment) Regulations, 2020;*

(iv) *The Dairy Industry (Duties and Powers of the Inspectors and Analysts) (Amendment)Regulations, 2020;*

(v) *The Dairy Industry (Raw Milk Grading and Minimum Quality and Safety Requirement) (Amendment)Regulations, 2020;*

(vi) *The Dairy Industry (Import and Export of Milk and Milk Products) (Amendment) Regulations, 2020*

(vii) *The Animal Welfare (Impounded Animal)Regulations, 2020*

(viii) *The Animal Welfare(Humane Slaughter and Killing of Animals) Regulations, 2020 and*

(ix) *Livestock Research Regulations, 2020*

***32. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/2021 Wizara itaendelea kuratibu na kuboresha Sheria, Kanuni na Taratibu kuhusu ubora wa bidhaa za mifugo, pembejeo na huduma za kisheria.

## 8.0 **Uzalishaji wa Mifugo wa Masoko**

### 8.1 ***Huduma ya Uhimilishaji***

***33. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na TAMISEMI pamoja na *Public Private Partnership for Artificial Insemination*

*Delivery* (PAID), *African Dairy Genetic Gain* (ADGG) pamoja na Kituo cha Taifa cha uhimilishaji (NAIC) imeandaa na kutekeleza Muundo wa Biashara ya Uhimilishaji (Dairy Business Model) na kufanya majaribio katika maeneo ya mfano (Pilot areas) ya Kawe na Mabwepande katika Manispaa ya Kinondoni; Chanika na Kinyerezi katika Manispaa ya Ilala Jijini Dar es Salaam. Aidha, lengo la *Dairy Business Model* ni kuzijengea uwezo Halmashauri na wafugaji kuweza kumudu gharama za uhimilishaji kibiashara pindi muda wa utekelezaji wa miradi ya PAID na ADGG utakapomaliza muda wake. Pia, jumla ya ng'ombe **76,612** wamehimilishwa katika Mikoa **21** ya Tanzania Bara (**Kiambatisho Na. 5a**).

***34. Mheshimiwa Spika,*** kati ya ng'ombe waliohimilishwa, ng'ombe **4,668** wamehimilishwa bure na Wizara kupitia kambi za uhimilishaji zilizoanzishwa katika Mikoa ya Dodoma, Simiyu, Katavi, Geita na Kagera (**Kiambatisho Na.5b**) ambapo kiwango cha ushikaji mimba *"conception rate"* ni asilimia **60.** Kambi za uhimilishaji zimechochea hamasa kubwa kwa wananchi kuhimilisha mifugo yao ili kuboresha mbari za mifugo. Aidha, Wizara inaendelea kufuatilia viwango vya ushikaji mimba kutoka kwenye mikoa husika.

***35. Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeandaa Kanuni za Uhimilishaji *Animal Diseases (Artificial Breeding) Regulations, 2020 GN. No.118* ambazo zimetoa bei elekezi ya kuhimilisha ng'ombe isiyozidi shilingi **10,000** kwa mpandisho mmoja bila kichocheo (Hormone) ikilinganishwa na gharama ya shilingi **25,000** kabla ya kanuni hiyo. Ili kuwezesha mafanikio na ufanisi wa kanuni hizi Wizara imetekeleza yafuatayo:-

(i) Wahimilishaji **37** katika Halmashauri **8** wamejengewa uwezo kwa vitendo kuhusu uhimilishaji.

(ii) Wataalam wa uhimilishaji waliopata mafunzo ya uhimilishaji kwa nadharia na vitendo wameongezeka kutoka **333** 2018/2019 hadi kufikia watalam **441** mwaka 2019/2020.

(iii) Lita **7,441.25** za kimiminika baridi cha Naitrojeni zilisambazwa kwenye Vituo vya Kanda vya Uhimilishaji.

***36. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/2021 Wizara itaendelea kuimarisha Kituo cha Taifa cha Uhimilishaji (NAIC), Vituo saba (**7**) vya Kanda vya Uhimilishaji na kuwezesha kambi za uhimilishaji kuhimilisha ng'ombe 100,000 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs).

### 8.2 *Uzalishaji na Usambazaji wa Mitamba*

***37. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020 jumla ya mitamba **18,255** ya maziwa imezalishwa kati ya hiyo mitamba **2,349** wametoka kwenye Mashamba ya Serikali (**Kiambatisho Na. 6**) na mitamba **15,906** kutoka kwa wafugaji binafsi ikilinganishwa na mitamba **619** iliyozalishwa na kuuzwa kutoka katika Mashamba ya Serikali na mitamba **14,460** kutoka kwa wafugaji binafsi mwaka 2018/2019.

***38. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/2021 Wizara itanunua mitamba **53** ya boran wazazi kwa ajili ya Shamba la Kuzalisha Mitamba Nangaramo (LMU) na madume matano (**5**) ya Friesian kwa ajili ya Shamba la Kuzalisha Mitamba Kitulo (LMU). Aidha, uhamasishaji wa wadau ili kuwekeza kwenye mashamba binafsi kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa mitamba unaendelea.

### 8.3 *Uzalishaji wa Kuku na Mayai*

***39. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, jumla ya vifaranga **70,323,000** vimezalishwa na kusambazwa nchini. Kati ya hivyo, vifaranga **60,463,872** ni wa nyama, vifaranga **7,860,000** ni wa kuku chotara hususan *Sasso* na *Kroiler* na vifaranga **1,999,128** ni wa kuku wa mayai ikilinganishwa na vifaranga **50,928,000** vilivyozalishwa mwaka 2018/2019. Aidha, Wizara ilitoa vibali vya kusafirisha nje ya nchi vifaranga vya kuku wazazi **850,000** wa nyama na mayai katika nchi za Kenya, Rwanda, Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Comoro, Malawi, Korea Kusini na Uturuki. Vilevile, Wizara imetoa vibali maalum vya kuingiza kuku wazazi **750,000** wa nyama na mayai kutoka Uholanzi, Ufaransa, Zambia na India ikilinganishwa na vifaranga wa kuku wazazi **556,616** vilivyoingizwa nchini mwaka 2018/2019.

***40. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, vituo vya kutotolesha vifaranga vimeongezeka kutoka vituo **19** mwaka 2018/2019 hadi kufikia vituo **26.** Vituo hivyo vipo katika mikoa ya Dar es Salaam (**7**), Iringa (**2**), Njombe (**1**), Pwani (**11**), Kilimanjaro (**2**), Arusha (**1**), Mbeya (**1**) na Mwanza (**1**). Aidha, mashamba ya kuku wazazi nchini yameongezeka kutoka **16** hadi **20** katika kipindi hicho yenye uwezo wa kutunza zaidi ya kuku wazazi **1,200,000** (**Kiambatisho Na. 7a** na **7b**).

***41. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020 Wizara kwa kushirikiana na Kampuni ya AKM Glitters imewezesha upatikanaji wa vifaranga **81,160** katika vikundi **151** kutoka Mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Pwani na Rukwa (**Kiambatisho Na. 8a na 8b**). Aidha, vikundi **27** vya wafugaji kuku na kaya **950** zimepatiwa vifaranga **8,500** katika Wilaya za Bagamoyo (**4,500**) na Sumbawanga (**4,000**). Pia, mtandao wa wanawake **400** wanaofuga kuku katika Wilaya ya Mkuranga wamepatiwa vifaranga **5,700**.

***42. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/2021 Wizara itaendelea kuratibu na kusimamia uzalishaji wa kuku, vifaranga na mayai. Vilevile, Wizara itaendelea kuhamasisha ulaji wa mayai ili kuongeza kiwango cha ulaji kwa mtu kwa mwaka.

8.4 ***Uzalishaji wa Nguruwe***

**43. Mheshimiwa Spika,** Wizara inaendelea kuhamisha sekta binafsi kuwekeza katika ufugaji na biashara ya nguruwe ambapo hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2020 jumla ya tani **38,377.4** za nyama ya nguruwe zimezalishwa ikilinganishwa na tani **37,773** zilizozalishwa mwaka 2018/2019 sawa na ongezeko la asilimia **1.6**. ongezeko hili limetokana na kuimarishwa kwa mashamba ya Serikali ya Ngerengere na Kitulo ili yaweze kuendelea kuzalisha mbegu bora za nguruwe. Aidha, Chama cha Wazalishaji Nguruwe nchini (Tanzania Piggery Farmers Association - TAPIFA) kimeendelea kuhamasisha wafugaji wa nguruwe kujiunga na chama ambapo mpaka mwezi Aprili 2020 jumla ya wanachama 220

wanaofuga nguruwe wanaofikia takriban **200,000**. Pamoja na mafanikio tajwa hapo juu, tasnia hii bado inakabiliwa na gharama kubwa ya vyakula, upatikanaji wa mbegu bora na uhaba wa machinjio na viwanda. Hivyo, Wizara kwa kushirikiana na TAPIFA inaendelea kukabiliana na changamoto kama ifuatavyo:-

(i) Kuagiza mbegu bora za nguruwe aina za *Camborough, Duroc, Peatrain, Large White* na *Topic* kutoka nchi za Zambia, Rwanda, Afrika ya Kusini na Ufaransa;

(ii) Kupunguza gharama za vyakula vya nguruwe kwa kusimika mitambo ya kisasa ya kuchanganya vyakula;

(iii) Kujenga machinjio ya kisasa ya nguruwe katika mkoa Dar es Salaam; na

(iv) Kuanza usindikaji wa nyama ya nguruwe katika Kiwanda cha *Happy Sausage* kilichopo Sakina Arusha.

***44. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/2021, Wizara itahimiza sekta binafsi kuzalisha na kusambaza mbegu bora za nguruwe kwa wafugaji ili kuongeza uzalishaji wa nguruwe na bidhaa zake. Aidha, Wizara itaendelea kuhamasisha uwekezaji katika uzalishaji, usindikaji na biashara ya nguruwe. Pia, Wizara itaendelea kuimarisha mashamba yake ya Ngerengere, Kitulo na Mabuki ili yaweze kuendelea kuzalisha mbegu bora za nguruwe. Vilevile, Wizara itaendelea kuimarisha Chama cha Wazalishaji Nguruwe nchini TAPIFA kwa lengo la kuboresha kosaafu za nguruwe.

## 9.0 **Haki Miliki za Waboreshaji Mbari za Wanyama**

***45. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, Wizara imeendelea na taratibu za kutunga Sheria ya Mbari za Mifugo ili kuanzisha Mfumo wa Kisheria wa Kulinda Haki za Wagunduzi wa Mbari mpya za Wanyama, hifadhi ya kosaafu zilizopo nchini na kusimamia ubora wa mbegu za mifugo. Uwepo wa mfumo huo utatoa hamasa kwa wadau wa sekta binafsi na ya umma kuwekeza kwenye ugunduzi wa mbari mpya za

wanyama, uzalishaji wa wanyama bora wa mbegu na kuzalisha mbari zenye tija zaidi katika uzalishaji wa mazao ya mifugo. Vile vile, mfumo huo unalenga kutoa na kulinda haki miliki kwa wagunduzi wa mbari mpya ili waweze kufaidika na uwekezaji wao. Aidha, Sheria hiyo itaanzisha utaratibu wa kuhifadhi na kuendeleza mbari zilizopo nchini pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa mbegu bora za wanyama.

***46. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020 Wizara imetambua wadau wanane (8) wa uboreshaji wa mbari za mifugo katika mikoa ya Manyara, Kilimanjaro, Mbeya, Tanga na Morogoro (**Kiambatisho Na. 9)**. Aidha, Wizara imetambua vyama vitatu (3) vya wadau wa uzalishaji wa mbari za mbuzi katika mikoa ya Kilimanjaro, Manyara na Morogoro. Kazi wanazofanya wadau hao ni pamoja na kuhifadhi (conservation) mbari za wanyama wa asili, kudumisha ubora wa mbegu za mifugo na kuzalisha mbari mpya za wanyama zenye tija katika uzalishaji wa maziwa, nyama na mayai. Pia, Wizara inaendelea kushirikiana nao katika hatua za kukamilisha uzalishaji mbari mpya.

***47. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/2021 Wizara itafanya tambuzi yakinifu (characterization) ya mbari za wanyama zilizopo nchini, kusajili na kutunza daftari la mbari za wanyama, wanyama wa mbegu na waboreshaji mbari katika mikoa mitatu (**3**).

## 10.0 **Biashara ya Mifugo na Mazao Yake**

### 10.1 ***Biashara ya Mifugo***

***48. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara imeendelea kuratibu biashara ya mifugo na mazao yake ndani na nje ya nchi. Katika mwaka 2019/2020 jumla ya ng'ombe **1,513**,926 mbuzi **1,733,463**, kondoo **299,157** na punda **198,000** wenye thamani ya shilingi **trilioni 1.06** waliuzwa katika minada mbalimbali hapa nchini ikilinganishwa na ng'ombe **2,006,816**, mbuzi **1,491,251**, kondoo **341,814** na punda **124,000** wenye thamani ya shilingi **trilioni 1.3** waliouzwa katika minada mbalimbali hapa nchini

mwaka 2018/2019. Sababu za kushuka kwa biashara hii ni pamoja na mwaka 2019/2020 kuwa na mvua nyingi hivyo kuathiri biashara ya mifugo katika minada. Aidha, hadi tarehe 30 Aprili, 2020 jumla ya Shilingi **5,217,369,393.2** zilikusanywa kama Maduhuli ya Serikali. Pia, Wizara imetoa mafunzo kwa watendaji **26** wa minada kuhusu Sheria na Kanuni za Uendeshaji wa Minada, ikiwa ni pamoja na matumizi ya PoS na taratibu za ukusanyaji na uwasilishaji wa maduhuli ya Serikali.

10.2 ***Udhibiti wa Biashara ya Mifugo na Mazao yake (Operesheni Nzagamba)***

***49. Mheshimiwa Spika, kabla ya Operesheni Nzagamba kulikuwa na*** ukwepaji mkubwa wa kulipa maduhuli ya Serikali yahusuyo biashara ya mifugo na mazao yake; uingizaji holela wa bidhaa mbalimbali kinyume cha Sheria, Kanuni na Taratibu; na uuzwaji wa bidhaa zisizokidhi viwango. Katika mwaka 2019/2020 Wizara imeendelea kutekeleza operesheni Nzagamba ili kudhibiti utoroshaji wa mifugo na mazao ndani na nje ya nchi na upotevu wa mapato katika maeneo matano ya kimkakati ambayo ni: - Nzega (Tabora), Lamadi (Simiyu), Babati (Manyara), Longido (Arusha) na Handeni (Tanga). Kupitia operesheni hiyo hadi kufikia 30 Aprili, 2020 mafanikio yafuatayo yamepatikana:-

**(i) Jumla ya** shilingi **5,516,568,128** zimekusanywa ikiwa ni tozo ya kusafirisha mifugo nje ya nchi shilingi **2,993,977,500;** tozo ya kusafirisha vyakula vya mifugo nje ya nchi shilingi **885,101,260;** vibali kusafirisha mifugo nchini shilingi **1,495,853,468;** na faini kwa makosa ya ukiukwaji wa Sheria, Kanuni na Taratibu katika biashara ya mifugo na mazao yake shilingi **141,635,900 (Kiambatisho Na. 10)**;

(ii) Jumla ya ngómbe **392,661,** mbuzi na kondoo **676,715** walikaguliwa ambapo jumla ya mifugo **3,363** (ngómbe, mbuzi na kondoo) iliyokuwa inatoroshwa kwenda nje ya nchi bila kulipiwa vibali na ushuru ilikamatwa na kutozwa faini yenye jumla ya shilingi **141,635,900**. Aidha, ng'ombe **44,791**, mbuzi na kondoo **220,033** waliuzwa nje ya nchi. Pia, ng'ombe

**354,906**, mbuzi na kondoo **243,435** walikatiwa vibali ndani ya nchi na jumla ya tani **56,986.48** za vyakula vya mifugo zilisafirishwa nje ya nchi;

(iii) Udhibiti wa utoroshaji wa mifugo na mazao yake nje ya nchi umesaidia kuhamasisha ujenzi wa viwanda vipya vya nyama, maziwa na ngozi;

(iv) Udhibiti wa uingizaji wa mazao mifugo ambapo jumla lita za maziwa **5,621.3,** kilo **303.69** za nyama na bidhaa zake, trei za Mayai **1,012** zilikamatwa zikiwa zimeingizwa nchini kinyume cha Sheria; na

(v)Kuhamasisha matumizi ya mizani katika minada na uanzishaji wa ushirika wa wafanyabiashara wa mifugo.

***50. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/2021 Wizara itajenga minada miwili ya upili; na mmoja wa mpakani; na kukarabati minada ya upili na mipakani na kuwezesha utekelezaji wa doria sita **(6**) za Mikakati ya Kudhibiti Upotevu wa Mapato yatokanayo na Biashara ya Mifugo na Mazao yake (Operesheni Nzagamba).

## 11.0 **Kodi, Ada na Tozo Katika Sekta ya Mifugo**

***51. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020 kutokana na malalamiko kutoka kwa wadau juu ya viwango vikubwa vya kodi, ada, ushuru na tozo Wizara imesikia kilio hicho na kufanya mapitio ya kanuni zake za tozo (*Animal and Animal Products Regulations*, 2007) ili kuondoa malalamiko na kukabiliana na hali ya sasa. Mabadiliko hayo yatabainishwa katika Hotuba ya Waziri wa Fedha atakapowasilisha Bungeni Bajeti ya Serikali.

***52. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2020/2021, Wizara itaendelea kutathmini kodi, tozo na ada mbalimbali zitakazoonekana kuwa kero kwa wazalishaji na wafayabiashara ya mifugo na mazao yake ili kuzifuta au kuzifanyia marekebisho.

12.0 **Zao la Ngozi**

***53. Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia tarehe 30 Aprili 2020 jumla ya kilo za ngozi **16,746,589.36** (ng'ombe **14,449,075.49**, mbuzi **1,775,298.5** na kondoo **522,215.38)** zenye thamani ya shilingi **bilioni 23.9** zimezalishwa ikilinganishwa na kilo **16,012,800.71** (ng'ombe **13,904,620.27**, mbuzi **1,653,669.26** na kondoo **454,511.17)** zenye thamani ya shilingi **bilioni 22.8** zilizozalishwa mwaka 2018/2019. Kilo za ngozi za ng'ombe 25,500 **z**enye thamani ya shilingi **milioni 14.4** na kilo za ngozi za mbuzi na kondoo **114,500** zenye thamani ya shilingi **milioni 202.7** zimesindikwa ikilinganishwa na kilo za ngozi ya ng'ombe **972,866.04 z**enye thamani ya shilingi **bilioni 2**, kilo za ngozi za mbuzi na kondoo **386,135** zenye thamani ya shilingi **milioni 867.9** na kilo **114,800** za punda zenye thamani ya shilingi **milioni 157.2** zilizosindikwa mwaka 2018/2019. Upungufu wa kilo zilizosindikwa umesababishwa na katazo la uingizaji wa ngozi zilizochakatwa kwa kutumia *chromine* na *sulphide* katika soko la Ulaya. Hivyo, Wizara inahamasisha wenye viwanda vya ngozi kubadilisha teknolojia ya usindikaji kutoka kwenye matumizi ya chromine na sulphide kwenda kwenye usindikaji unaozingatia usalama wa mazingira kwa kutumia teknolojia ya kutumia mimea aina ya mimosa (vegetable tanning).

***54. Mheshimiwa Spika***, Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine inaendelea kutekeleza Mkakati wa Kuendeleza Tasnia ya Ngozi (Leather Sector Development Strategy 2016 – 2020). Katika mwaka 2019/2020 mafanikio yaliyopatikana ni:-

(i) Kuanzisha kituo cha kutoa leseni na vibali vya kusafirisha ngozi nje ya nchi cha Dodoma na kuimarisha kituo cha Dar es Salaam. Hivyo, hadi Aprili 2020 jumla ya kampuni **17** zimepatiwa leseni za usajili wa maghala ya kuhifadhia ngozi (Premises License) na vibali vya kusafirisha ngozi nje ya nchi kwa lengo la kuwezesha biashara ya ngozi (**Kiambatisho Na. 11);**

(ii) Serikali imeweka mikakati madhubuti ya kampeni za uhimilishaji, uogeshaji mifugo, chanjo na upatikanaji wa maji na malisho, pia, uhamasishaji wa ujenzi wa machinjio za kisasa na viwanda vya kusindika mazao ya mifugo ambapo mikakati hii imesaidia upatikanaji wa ngozi bora kwa ajili ya uchakataji na usindikaji viwandani.

(iii) Visu maalum vya kuchunia ngozi za wanyama vimegawiwa kwa wachunaji wa ngozi wenye leseni katika Kanda za Mashariki, Kaskazini na Ziwa. Jitihada zinaendelea ili kugawa visu hivyo maalum katika kanda zote nane nchini.

(iv) Ili kuwezesha upatikanaji wa ngozi bora kulingana na mahitaji ya wachakataji na wasindikaji wa ngozi, wakaguzi wa ngozi **113** wameteuliwa na wachunaji ngozi **735** wamejengewa uwezo.

(v) Udhibiti wa utoroshaji na udanganyifu katika biashara ya ngozi kwa kutoza asilimia **80** ya usafirishaji wa ngozi ghafi na asilimia 10 ya usafirishaji wa ngozi zilizosindikwa kufikia hatua ya kati (wet blue) umeimarisha biashara ya ngozi nchini.

***55. Mheshimiwa Spika,*** hatua zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali zimechochea uwekezaji mkubwa katika tasnia ya ngozi, kwa mfano, ujenzi wa Kiwanda cha Ngozi cha Karanga Moshi wenye thamani ya shilingi **bilioni 75** umekamilika kwa asilimia **80** na ujenzi wa Kiwanda cha ACE Leather Morogoro wenye thamani ya Shilingi **bilioni 23** (Dola za Kimarekani **milioni 10)** umakamilika kwa asilima **90**. Pia, machinjio **30** zimejengwa na zinaendelea kujengwa katika maeneo mbalimbali nchini.

***56. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/2021 Wizara itaendelea kuwezesha utekelezaji wa Mpango Shirikishi wa Kuendeleza Tasnia ya Ngozi kwa kuvijengea uwezo vikundi vya wazalishaji wa bidhaa za ngozi katika mikoa ya Mwanza, Kagera, Geita, Simiyu, Mara na Shinyanga. Aidha, Wizara itaendelea kurasimisha wadau waliopo kwenye mnyororo wa thamani wa zao la ngozi ambao ni wakaguzi, waweka madaraja na wachunaji. Pia, Wizara itafanya mapitio ya Sheria ya Biashara ya Ngozi Na. 18 ya mwaka 2008 na kanuni

zake na kuhuisha Mkakati wa Kuendeleza Tasnia ya Ngozi wa 2016 hadi 2020.

## 13.0 **Machinjio ya Dodoma**

***57. Mheshimiwa Spika,*** tangu machinjio ya Dodoma ilipokabidhiwa kwa Kampuni ya TMCL mwaka 2008, utendaji wake umekuwa siyo wa kuridhisha. Aidha, majengo, miundombinu ya machinjio, mitambo na vifaa imechakaa bila ukarabati wowote; kuongezeka madeni; kutengeneza hasara kila mwaka na haijawahi kutoa gawio Serikalini. Pia, usimamizi dhaifu na ubadhilifu wa fedha umepelekea Serikali kupata hasara ya shilingi **bilioni 42.28** kwa kipindi cha miaka 11. Kutokana na udhaifu huo wa uendeshaji na uchakavu wa machinjio, Wizara ya Mazingira ya UAE inayosimamia ubora wa nyama iliifutia machinjio ithibati ya kuuza nyama katika nchi za Falme za Kiarabu (UAE).

Kwa kuwa Serikali ilifanya jitihada nyingi kunusuru machinjio hii bila mafanikio, mnamo tarehe 27 Desemba, 2019, Wizara ilirejesha Machinjio hiyo Serikalini. Kutokana na uamuzi huo, kumekuwepo na mafanikio makubwa ambapo ndani ya muda wa miezi minne, uchinjaji wa mifugo umeongezeka kutoka wastani wa ng'ombe **41** kufikia wastani wa ng'ombe **125** kwa siku. Pia, makusanyo ya mapato yameongezeka kutoka wastani wa shilingi **39,843,788** hadi shilingi **90,279,000** kwa mwezi. Katika kipindi cha miezi minne Wizara imeweza kulipia gharama za uendeshaji ikiwemo kulipa mishahara ya watumishi na kupata faida ambayo sehemu yake kiasi cha shilingi **milioni 70** kimetolewa kama gawio kwa Serikali. Hii ni mara ya kwanza kwa Serikali kupata gawio kutoka katika machinjio hiyo. Aidha, Kampuni ya NICOL na NARCO wamekubaliana kuvunja Kampuni ya TMCL bila kwenda Mahakamani. Pia, Serikali inaendelea na ukarabati ili kurejesha ithibati ya kuuza nyama nchi za UAE.

***58. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/2021, Wizara itaendelea kuimarisha machinjio ya Dodoma kwa kuweka usimamizi wa machinjio hiyo chini ya taasisi za LITA na NARCO.

## 14.0 **Rasilimali za Malisho, Vyakula na Maji kwa Mifugo**

### 14.1 ***Malisho, Vyakula na Maji kwa Mifugo***

***59. Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea kutekeleza Mkakati wa Upatikanaji wa Malisho na Maji pamoja na kukamilisha maandalizi ya miongozo ya usimamizi wa rasilimali hizo. Katika mwaka 2019/2020, Wizara imeendelea na hatua za awali kwa ajili ya ujenzi wa lambo katika Kijiji cha Chamakweza (Bagamoyo), Visima virefu katika Vijiji vya Mpapa (Manyoni) na Nsolanga-Ismani (Iringa) na ukarabati wa malambo katika Kijiji cha Kimana (Kiteto), Kijiji cha Narakauo (Simanjiro) na kijiji cha Kimokoa (Longido).

***60. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/2021, Wizara itachimba visima virefu vinne (**4**) katika Halmashauri za Tanganyika (Tanganyika) na Tunduru (Mkowela). Pia, itakarabati malambo **10** yaliyopo katika Halmashauri za Longido (Kemokoa), Simanjiro (Narakauo), Bukombe (Bukombe), Butiama (Bukabwa), Igunga (Igunga), Kiteto (Kimana), Kishapu (Mwalata), Chunya (Isewe), Kilindi (Lengusero) na Meatu (Isebanda). Pia, Wizara itaendelea kushirikiana na Wizara ya Maji ili miradi ya maji kwa ajili ya binadamu izingatie miundombinu ya maji kwa ajli ya mifugo, na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi ili uchimbaji wa mashimo kwa ajili ya malighafi ya ujenzi wa barabara yachimbwe kimkakati ili yaweze kutumika kama malambo baada ya miradi ya ujenzi kukamilika.

***61. Mheshimiwa Spika,*** katika kuboresha lishe na upatikanaji wa uhakika wa malisho kwa mifugo, Wizara inaendelea kutoa elimu kwa wafugaji na wadau wengine kuhusu uzalishaji na uhifadhi wa malisho. Katika mwaka 2019/2020, Jumla ya marobota **380,765** ya hei yamezalishwa kati ya hayo marobota **326,655** yamezalishwa katika mashamba ya Serikali (**Kiambatisho Na. 12)** na marobota **54,110** yamezalishwa kutoka mashamba ya Sekta Binafsi.

***62. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020 jumla ya tani **127.3** za mbegu bora za malisho na vipandikizi zimezalishwa

katika mashamba ya Serikali ikilinganishwa na tani **12.1** za mbegu za malisho zilizozalishwa katika mashamba ya Serikali mwaka 2018/2019. Ongezeko hili limetokana na uzalishaji wa tani **115.2** za vipandikizi zilizozalishwa kwa wingi kutokana na uwepo wa mvua za kutosha misimu ya vuli na masika na Serikali kuwekeza katika ununuzi wa vitendea kazi yakiwepo matrekta na *harrow* kwa ajli ya shamba la Serikali la mbegu za malisho lililopo Vikuge Kibaha, mkoani Pwani.

***63. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, viwanda vipya **11** vya kutengeneza vyakula vya mifugo vimeongezeka na kufanya viwanda vya vyakula vya mifugo kufikia **105** ikilinganishwa na viwanda **94** katika mwaka 2018/2019 (**Kiambatisho Na. 13)**. Aidha**,** katika kuhakikisha upatikanaji wa vyakula vya mifugo vyenye ubora na viwango stahiki unakuwepo, Wizara imeteua Wakaguzi **129** waliopo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa **109** na **20** ngazi za Mikoa. Pia, ukaguzi wa maeneo ya kuzalisha, kuhifadhi na kuuza vyakula vya mifugo umefanyika katika mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Iringa, Kilimanjaro, Morogoro, Mbeya, Mwanza, Njombe, Pwani, Ruvuma na Songwe. Jumla ya maeneo **11** ya kuzalisha vyakula, matano (**5)** ya kuhifadhi na **36** ya kuuzia vyakula vya mifugo yamekaguliwa na wadau wamepatiwa vyeti vya usajili baada ya kukidhi vigezo.

***64. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/2021, Wizara itaendelea kusimamia na kudhibiti ubora na usalama wa vyakula vya mifugo kwa kufanya ukaguzi katika maeneo **75** ya uzalishaji, uhifadhi na uuzaji wa vyakula vya mifugo ikiwa ni pamoja na kutoa mafunzo rejea kwa wakaguzi **159** wa vyakula vya mifugo na maeneo ya malisho. Pia, itaendelea kuimarisha mashamba ya Serikali ya kuzalisha mbegu za malisho na kuwezesha urasimishaji wa aina **10** za mbegu hizo.

15.0 **Ustawi wa Wanyama**

***65. Mheshimiwa Spika,*** kumekuwa na matukio ya ukamataji holela wa mifugo usiyozingatia ustawi na haki za wanyama ambazo ni chakula, maji, malazi, matibabu na uhuru wa kuonesha tabia za uasili. Ukamataji huo umekuwa ukifanywa

na Serikali za Vijiji, Halmashauri za Wilaya na Mamlaka za Hifadhi. Ukamataji huu umekuwa ukiambatana na utesaji wa wanyama ikiwemo mifugo kukatwa mapanga, mifugo kupewa sumu na kusababisha vifo pasipo kuzingatia Sheria ya Ustawi wa Wanyama Na. 19 ya mwaka 2008 (Animal Welfare Act No. 19/2008); Sheria ya Magonjwa ya Wanyama Na. 17 ya mwaka 2003 (Animal Diseases Act No. 17/2003) na Sheria ya Nyanda za Malisho Na. 10 ya mwaka 2010 (the Grazingland and Animal Feed Resources Act, No. 10/2010). Jumla ya mifugo **14,668,323 (**ngómbe **14,667,175,** mbuzi **718,** kondoo **248** na punda **182)** ilikamatwa kati ya mwaka 2017 na 2019 hususan kutoka mikoa ya Tabora, Mbeya, Dodoma, Geita na Rukwa (**Kiambatisho Na. 14**). Mikoa mingine ambayo kumekuwepo na matukio ya ukamataji wa mifugo kwenye hifadhi za maliasili ni pamoja na Katavi, Mara, Morogoro, Iringa, Simiyu, Tanga, Shinyanga, Manyara, Singida, Arusha, Kilimanjaro, Kigoma na Pwani.

***66. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/2021 Wizara itaendelea kuratibu na kusimamia haki na ustawi wa wanyama.

### 16.0 **Utatuzi wa Migogoro Baina ya Wafugaji na Watumiaji Wengine wa Ardhi**

***67. Mheshimiwa Spika,*** katika kutatua migogoro baina ya wafugaji, wakulima na watumiaji wengine wa ardhi, **Mhe. Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli** aliamua kuunda timu ya Mawaziri nane (8) iliyoongozwa na Mhe. William Vangimembe Lukuvi Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mbunge wa Isimani ili kupata ufumbuzi wa migogoro ya ardhi katika maeneo ya wafugaji, wakulima na watumiaji wengine wa ardhi (Kiambatisho Na. 15b-i). Timu hiyo ilizunguka nchi nzima kwenye maeneo yenye migogoro kwa kutumia ndege maalum ya kijeshi. Ambapo baadaye Mhe. Rais alitoa maagizo yafuatayo:

i. Kurasimisha vijiji 920 ambavyo vina migogoro ya matumizi ya ardhi na hifadhi, mashamba, ranchi, mapori ya akiba, na vyanzo vya maji visiondolewe katika maeneo vilipo;

ii. Kufuta baadhi ya maeneo ya hifadhi za misitu na maeneo tengefu na kuagiza yagawiwe kwa wananchi kwa ajili ya mifugo, kilimo na makazi. Jumla ya Mapori Tengefu **12** yenye jumla ya ekari **707,659.94** yamefutwa na misitu saba (**7**) yenye ukubwa wa ekari **46,247.56** imefutwa**.**

iii. Hifadhi za misitu 14 na mashamba **16** yasiyoendelezwa yamegwe na kugawiwa kwa wananchi kwa shughuli za mifugo, kilimo na makazi.

iv. Kuweka mwongozo wa matumizi kwa maeneo ya mita **500** katika maeneo ya kinga (*buffer zone*) na mita **60** katika hifadhi ya vyanzo vya maji ili ziendelee kutumiwa na wananchi kwa namna ambayo haitaathiri mazingira (**Kiambatisho Na. 15b-ii**).

***68. Mheshimiwa Spika***, hivi sasa Wizara nane (**8**) za kisekta ikiwemo Ofisi ya Rais TAMISEMI, Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Maji, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Katiba na Sheria (Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali) zinaendelea kutekeleza maagizo ya Mhe. Rais ambapo utekelezaji wake uko katika hatua mbalimbali.

***69. Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2019/2020 Wizara yangu ilifanya ziara katika Halmashauri 152 kwa lengo la kukutana, kusikiliza na kutatua changamoto zinazowakabili wafugaji. Ziara hizo zilipokelewa kwa vilio kwa baadhi ya maeneo ambayo yana migogoro sugu baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi. Naomba nitoe maelezo kwa muhtasari kuhusu migogoro hiyo kama ilivyowasilishwa wakati wa ziara:

i. Migogoro kati ya wakulima na wafugaji;

a. Wafugaji wanaingiza mifugo yao katika mashamba ya wakulima na kuharibu mazao;

b. Wafugaji kuvamia vyanzo vya maji, kuwapiga na kuwaumiza wakulima na kukataa kuwalipa fidia;

c. Wakulima kuvamia na kufanya shughuli za kilimo katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya kulishia mifugo;

d. Wakulima kuziba njia za mifugo za kwenda katika malisho, maji, josho na mnadani, kukata mapanga, kushikilia kwa muda mrefu mifugo; na

e. Baadhi ya watendaji wa Serikali kulalamikiwa kwa kutokutenda haki na kufanya upendeleo wanapoletewa malalamiko ya wakulima na wafugaji.

ii. Migogoro kati ya Mamlaka za uhifadhi, mashamba ya Serikali na wafugaji.

a. Wafugaji kuvamia na kuingiza mifugo ndani ya maeneo ya hifadhi na mashamba ya Serikali na kusababisha uharibifu mkubwa wa mazingira na kueneza magonjwa baina ya mifugo na wanyama pori;

b. Kutanua mipaka ya hifadhi na kujumuisha maeneo ya malisho kwenye hifadhi, hifadhi kutokuwa na alama na mipaka inayoonekana hali inayopelekea mifugo kukamtwa hata ikiwa nje ya hifadhi;

c. Maeneo ya malisho kubadilishiwa matumizi bila kuzingatia mahitaji, uanzishwaji wa WMA's na kukatazwa matumizi mseto katika maeneo hayo kumechangia kupungua kwa maeneo ya malisho nchini;

d. Mifugo kushikiliwa kwa muda mrefu bila kupatiwa huduma muhimu kama maji, malisho, chanjo na matibabu ambapo inapelekea mifugo mingi kufa ikiwa inashikiliwa;

e. Wafugaji wanaposhinda kesi mahakamani hawarudishiwi mifugo yao na pengine hurudishiwa mifugo pungufu kinyume na hukumu za mahakama;

f. Baadhi ya maaskari wa hifadhi wamekuwa wakipiga risasi mifugo ili kuwakomoa wafugaji na kupoteza ushahidi, mifugo kuuzwa kiholela wakati imeshikiliwa;

g. Ukamataji holela wa mifugo usioshirikisha uongozi wa vijiji na wamiliki wa mifugo umepelkewa kutofautiana kwa idadi ya mifugo inayokamatwa na inayofikishwa mahakamani;

h. Wanyama pori wakali kama Simba, Chui na Tembo wamekuwa wakishambulia mifugo bila kupata msaada au fidia yoyote;

i. Baadhi ya Mamlaka za Miji zimekuwa zikilazimisha wafugaji kuhamisha mifugo yao bila kuzingatia haki zao katika umiliki wa ardhi;

j Wafugaji kulalamikia kutozwa faini kubwa kinyume cha Sheria pale mifugo yao inapokamatwa katika maeneo yasiyoruhusiwa,

***70. Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliweza kutatua baadhi ya migogoro papo kwa papo, migogoro mingine inaendelea kufanyiwa kazi na baadhi ya migogoro hiyo imewasilishwa katika Wizara za kisekta na mamlaka husika kwa ajili ya utatuzi.

***71. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020 Wizara imeendelea kutatua Migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi katika maeneo ya Vilima vitatu (Babati), Hifadhi ya Ngorongoro (Ngorongoro), Mvuha (Morogoro vijijini); Ranchi ya Ruvu (Bagamoyo); Kwala (Kibaha); Gwata (Kisarawe); Mindutulieni (Chalinze); Mkiu, Njopeka, Kisegese, Chamgoi, Kifumangao, Mkuruwili na Mtongani (Mkuranga); Msaraza (Pangani), Katambuzi, Katera, Karukwanzi B, Ishaka Ibale na Nyakakoni (Kyerwa), Kahundwe (Karagwe), Ranchi ya Kongwa (Dodoma), Shamba la Kuzalisha Mitamba Hanga Ngadinda na Muhukulu Lilahi (Ruvuma) na Shamba la Kuzalisha Mitamba Mabuki (Mwanza). Aidha, migogoro mikubwa **11** kati ya **17 (**sawa na asilimia **64.7)** iliyodumu kwa muda mrefu imetatuliwa katika kipindi cha mwaka 2019/2020 katika Mikoa ya Pwani, Dodoma, Morogoro, Ruvuma, Mwanza na Geita. Migogoro iliyotatuliwa ni ya: Ranchi ya Ruvu, Ranchi ya Misenyi, Ranchi ya Kagoma, Kituo cha karantini Kwala, Ranchi ya Kongwa, Gwata Kisarawe, Ranchi ya Dakawa, Hifadhi ya Msitu wa

Kigosi ya Geita, Mamlaka ya Pori la Akiba la Mkungunero la Chemba, lililokuwa Shamba la Mifugo Hanga la Madaba na Shamba la Kuzalisha Mitamba Mabuki Misungwi.

***72. Mheshimiwa Spika***, Wizara katika jitihada za kupata suluhisho la migogoro kati ya watumiaji mbalimbali wa ardhi imetekeleza yafuatayo:-

(i) Imemega maeneo yenye ukubwa wa hekta **29,428.49**, katika mashamba na Ranchi za Taifa na kuwapatia wananchi maeneo hayo ili waweze kuendeleza shughuli za kilimo, ufugaji na makazi. Kati ya hekta hizo, hekta **1,800** kutoka katika shamba la Hanga Ngadinda (Ruvuma), hekta **2,208** kutoka Ranchi ya Ruvu, hekta **22,201.094** kutoka Ranchi ya Missenyi, hekta **80.4** kutoka shamba la Taasisi ya Utafiti wa Mifugo – Kongwa na hekta **3,139** kutoka Kituo cha Karantini cha Kwala (**Kiambatisho Na. 15a**).

(ii) Imefanya ziara katika Halmashauri **152** zenye mifugo ili kusikiliza, kutoa elimu na kutatua migogoro hiyo. Juhudi hizi zimesaidia kupunguza mauaji na kukatana mapanga na hivyo kurejesha amani na utulivu katika maeneo yenye migogoro. Aidha, Jumla ya migogoro **304** imetatuliwa kupitia ziara za viongozi wa Wizara.

(iii) Inafanya upimaji wa mashamba yote ya Serikali na kuweka mipaka na alama zinazoonekana ambapo hadi mwezi Aprili, 2020 jumla ya mashamba **8** yenye ukubwa wa hekta **23,066.94** yamepimwa na kuwekewa alama zinazoonekana. Mashamba hayo ni Hangangadinga (4,200), Mahukuru Lilahi (3,100), Chibe (2,054) Shishiyu (3,170), Mkwese (5,036), Kinyangiri (3,419.94), Nachingwea (1,497) na Kelema (590). Zoezi la upimaji linaendelea kwa mashamba yaliyobaki. Pia, Halmashauri za Wilaya zimeitikia wito wa kutenga maeneo kwa ajili ya malisho ambapo jumla ya hekta **2,818,687.17** zimetengwa na hekta **108,427.49** zimepimwa.

(iv) Imeunda timu ya watalam kwa ajili ya utatuzi wa migogoro ambayo inazunguka nchi nzima kutatua migogoro sugu. Timu hiyo inajumuisha wataalam kutoka Ofisi ya Rais – TAMISEMI,

Wizara za Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mambo ya Ndani; Usalama wa Taifa, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Chama cha Wafugaji. Toka kuzinduliwa kwa timu hiyo mwaka 2018 mafanikio makubwa yamepatikana ambapo jumla ya migogoro sugu **45** imetatuliwa na hivyo kuleta amani na utulivu kwa wananchi.

(v) Wizara inazifanyia mapitio Sheria ya Ustawi wa Wanyama Na. 19 ya mwaka 2008 (Animal Welfare Act No. 19); Sheria ya Magonjwa ya Wanyama Na. 17 ya mwaka 2003 (Animal Diseases Act No. 17) na Sheria ya Nyanda za Malisho Na. 10 ya mwaka 2010 (the Grazingland and Animal Feed Resources Act, No. 10) ili ziweze kutoa ulinzi wa kutosha wa ustawi endelevu wa mifugo. Pia, Wizara imetunga Kanuni za Ukamataji Mifugo (*The Animal Welfare (Impounded Animal) Regulations, 2020*) ambayo imeweka mwongozo wa namna ya kukamata wanyama, kuwatunza na kuwapa mahitaji muhimu ikiwemo malisho, dawa, chanjo na maji.

***73. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2020/2021 Wizara itaendelea kutoa elimu kuhusu ufugaji wa mifugo wenye tija, kudhibiti na kutatua migogoro kati ya wafugaji na watumiaji wengine wa rasilimali ardhi inayojitokeza katika maeneo mbalimbali nchini. Vilevile, Wizara itaendelea kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Wizara ya Katiba na Sheria ili kuhakikisha kuwa migogoro ya ardhi inazuiwa na kutatuliwa.

***74. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2019/2020, Wizara katika kuhakikisha wafugaji wanapata maeneo ya malisho imetenga na kuwapangisha wafugaji kwa muda wa mwaka mmoja mmoja jumla ya hekta **78,470.97** kutoka kwenye taasisi zake ikiwemo TALIRI (**2,501.03**), NARCO (**59,290**), Vituo vya Kupumzishia Mifugo (**13,679.94**) na Mashamba ya Kuzalisha Mitamba (**3,000**). Hadi sasa jumla ya ng'ombe **54,852** mbuzi na kondoo **11,578** wanachungwa katika maeneo ya Serikali (K**iambatisho Na. 15c)**.

***75. Mheshimiwa Spika***, Wizara kwa kushirikiana na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi imeandaa na

kutekeleza mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji kwa lengo la kupata ardhi kwa ajili ya matumizi mbalimbali ikiwa ni pamoja na maeneo ya malisho. Jumla ya vijiji **23** vimetenga hekta **29,786.0** katika Wilaya **8** za Kilindi (**2,109.98**), Handeni (**3,380.01**), Namtumbo (**11,076.8**), Songea (6,353.52), Nyasa (**198.78**), Mbinga (**1,493.66**), Ruangwa (**407.52**), Liwale (**1,216**) na Mpwapwa (**3,549.72**) na kufikia idadi ya vijiji **1,875** ukilinganisha na vijiji **1,852** mwaka 2018/2019 vilivyopimwa na kuandaliwa mipango ya matumizi ya ardhi. Hivyo, maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya malisho kwa sasa yamefikia hekta **2,818,687.17** ikilinganishwa na hekta **2,788,901.17** katika mwaka 2018/2019.

***76. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2020/2021 Wizara itaainisha, kutenga, kupima na kutangaza hekta **1,500,000** kwenye Gazeti la Serikali maeneo ya malisho yaliyotambuliwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya ufugaji endelevu. Aidha, itapima na kutenga vitalu katika eneo la Mwisa II Mkoani Kagera lenye ukubwa wa hekta **121,643.94** kwa ajili kuvimilikisha kwa wafugaji wazawa kwa utaratibu wa mikataba maalumu ili kuweza kufuga kisasa na kibiashara. Kazi ya upimaji na uwekeaji vigingi vya mpaka iko kweye hatua ya mwisho. Aidha, natumia fursa kuupongeza uongozi wa Mkoa wa Kagera ukiongozwa na Mkuu wa Mkoa Mhe. Brig. Jen. Michael Gaguti kwa ushirikiano mzuri katika kufanikisha zoezi hili muhimu ambalo sasa litatatua changamoto ya mgogoro wa wafugaji na watumiaji wengine wa Ardhi uliodumu kwa muda mrefu.

## 17.0 **Huduma ya Afya ya Mifugo**

### 17.1 ***Magonjwa ya Mifugo***

***77. Mheshimiwa Spika,*** Magonjwa mbalimbali ya mifugo yamekuwa kikwazo katika uzalishaji na biashara ya mifugo. Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kuchukua hatua mahsusi katika kukabiliana na magonjwa **13** ya kimkakati (**Kiambatisho Na. 16**) kwa kuzingatia Sera, Sheria, Kanuni na haki na ustawi wa wanyama katika utoaji wa tiba na kinga. Magonjwa hayo ni pamoja na:-

(i) magonjwa yaenezwayo na wadudu (Kupe na Mbungó) ambayo ni pamoja na Ndigana Kali, Ndigana Baridi, Mkojo Mwekundu na Moyo Maji yanayosababisha asilima **72** ya vifo vya mifugo.

(ii) Magonjwa ya mlipuko na kuvuka mipaka ambayo ni pamoja na Ugonjwa wa Miguu na Midomo, Homa ya Nguruwe, Mdondo, Homa ya Mapafu ya Ng'ombe (CBPP), Homa ya Mapafu ya Mbuzi (CCPP), Homa ya Bonde la Ufa, Mafua Makali ya Ndege, Sotoka ya Mbuzi na Kondoo, Kimeta, Kutupa Mimba, Mapele Ngozi na Kichaa cha Mbwa.

***78. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na wadau iliendelea kutekeleza mikakati ya kudhibiti magonjwa ya mifugo yaenezwayo na wadudu. Katika mwaka 2019/2020 mafanikio yafuatayo yamepatikana:-

(i) Wizara ilizindua kampeni ya pili ya kuogesha mifugo ambayo ilifanyika tarehe 29  Oktoba 2019 katika Wilaya ya Mlele Halmashauri ya Mpimbwe.

(ii) Jumla ya majosho **542** yamekarabatiwa na Wizara (**162**) na Halmashauri (**380**) na mapya **85** yamejengwa (**Kiambatisho Na. 17a**) na **(Kiambatisho Na. 17b)**.

(iii) Katika mwaka 2019/2020 Wizara ilinunua jumla ya lita **12,549.50** za dawa za kuogesha mifugo aina ya Paranex (Alphacypermethrin) na TikTik (Amitraz) zenye thamani ya Shilingi **440,714,750** ili kuendeleza zoezi la uogeshaji mifugo**.** Dawa hizi zilisambazwa kwenye majosho **1,738** katika Halmashauri **152** za Mikoa **25** ya Tanzania bara.

(iv) Kamati **1,036** za usimamizi na uendeshaji wa majosho zimeundwa, kati ya hizo **260** zimefungua akaunti benki (**Kiambatisho Na. 18**).

(v) Jumla ya michovyo **211,037,290** imefanyika ambapo michovyo **149,954,080** ya ng'ombe**, 45,477,778** ya mbuzi na kondoo **15,605,431**
(**Kiambatisho Na. 19).**

***79. Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliandaa kanuni na mwongozo wa uogeshaji ambao unatoa maelezo ya namna ya uogeshaji mifugo. Kanuni na mwongozo huo viliainisha majukumu mbalimbali ya wadau ikiwemo bei elekezi ya kuogesha mifugo ya shilingi **50** kwa ng'ombe na shilingi **10** kwa mbuzi au kondoo.

***80. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na wadau iliendelea kutekeleza mikakati ya kudhibiti magonjwa ya mifugo ya mlipuko na yanayovuka mipaka. Katika mwaka 2019/2020 mafanikio yafuatayo yamepatikana:-

(i) Utoaji wa chanjo umefanyika kwa mbuzi na kondoo **2,557,870** dhidi ya Ugonjwa wa Sotoka ya Mbuzi na Kondoo; ng'ombe **5,557,587** dhidi ya Ugonjwa wa Homa ya Mapafu ya Ng'ombe (CBPP); ng'ombe **1,036,769,** mbuzi **680,906** na kondoo **192,906** dhidi ya Ugonjwa wa Kimeta; ng'ombe **162,843** dhidi ya Ugonjwa wa Kutupa Mimba; mbwa **812,712** na paka **4,152** dhidi ya ugonjwa wa Kichaa cha Mbwa na Ngómbe **12,419** dhidi ya Ugonjwa wa Miguu na Midomo.

(ii) Maeneo Huru ya Magonjwa ya Mifugo (Disease Free Compartments) yenye ukubwa wa hekta **266,857** yameainishwa katika Ranchi za Taifa na vitalu vya watu binafsi kama maeneo yatakayo kuwa huru kwa Ugonjwa wa Miguu na Midomo. Aidha, sampuli **900** zimechukuliwa katika maeneo hayo na zinafanyiwa uchunguzi ili kubaini aina ya vinasaba (serotype) vya ugonjwa vilivyopo ili kuwezesha utengenezaji wa chanjo.

(iii) Jumla ya dozi **47,347,700** za Chanjo ya Matone ya Ugonjwa wa Mdondo (I2) zimezalishwa na kusambazwa kwenye Mikoa yote nchini ikilinganishwa na dozi **38,245,800** zilizozalishwa katika mwaka 2018/2019. Chanjo hiyo inastahimili hali ya joto hivyo inaweza kutumiwa na wafugaji wa kuku vijijini bila kuharibika.

***81. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2020/2021 Wizara itaendelea kutekeleza mikakati ya kudhibiti magonjwa ya mifugo kwa kununua dawa za ruzuku za kuogeshea mifugo

lita **19,700,** kukarabati majosho **125** na kujenga majosho mapya **20** ili kuwezesha kuongeza uogeshaji wa mifugo kutoka michovyo **milioni 211** hadi michovyo **milioni 405**. Pia, itaendelea kuzalisha chanjo za magonjwa 13 na kusimamia utekelezaji wa utoaji wa chanjo kwenye Halmasahuri zote nchini. Vilevile, katika udhibiti wa Ugonjwa wa Homa ya Nguruwe itahamasisha ufugaji bora wa nguruwe kwa kutengeneza mabanda bora, kutoa elimu na kupulizia dawa za kuua virusi kwenye mabanda.

17.2 ***Uzalishaji na Usambazaji wa Chanjo***

***82. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, Wizara imeandaa utaratibu wa manunuzi ya pamoja (bulk procurement) ya chanjo zote zinazohitajika na ambazo hazijaanza kuzalishwa hapa nchini ili kuongeza upatikanaji wa chanjo kulingana na kalenda ya chanjo, kulinda ubora wa chanjo na kupunguza gharama ya chanjo kwa wafugaji. Sambamba na mpango huo, Wizara imeandaa bei elekezi ya chanjo zote za magonjwa ya kipaumbele zinazozalishwa nchini na zitakazoagizwa kutoka nje ya nchi kuanzia ngazi ya uzalishaji, maduka yanayosambaza pamoja na bei atakayolipa mfugaji kwa kuzingatia Kanuni ya Chanjo na Uchanjaji ya mwaka 2020 GN.180 Animal Disease (Vaccine and Vaccination) Regulations, 2020 GN. No 180). Lengo la bei elekezi ni kuhakikisha kuwa kila mfugaji anachanja mifugo yake kwa kufuata Sheria ili kudhibiti magonjwa hayo kuanzia tarehe 01 Julai, 2020.

***83. Mheshimiwa Spika,*** **k**atika mwaka 2020/2021 Wizara itaendelea kutekeleza utaratibu na usimamizi wa bei elekezi za chanjo **13** za magonjwa ya kimkakati na ununuzi wa chanjo kwa pamoja (Bulk Procurement) kwa chanjo zote ambazo hazizalishwi nchini. Aidha jitihada hizi za serikali zitapelekea kupunguza gharama za chanjo kwa asilimia 60. Nitumie nafasi hii kutangaza bei elekezi ambazo wadau wote watapaswa kuzifuata na kuzizingatia (**Kiambatisho Na.20 na 21).**

## 18.0 **Kuimarisha Uchunguzi na Upatikanaji wa Taarifa za Magonjwa ya Mifugo**

***84. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020 Wizara kupitia Vituo vinane (**8**) vya Kanda vya Uchunguzi na Ufuatiliaji wa Magonjwa ya Mifugo kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa imeendelea kuimarisha ufuatiliaji wa magonjwa na utoaji wa taarifa za magonjwa ya mifugo. Jumla ya wataalam **108** kutoka Halmashauri **70** wamepatiwa mafunzo na vifaa vya kielektronic (smartphone) kwa ajili ya ufuatiliaji na utoaji wa taarifa za magonjwa ya mifugo kupitia Mfumo wa *Event Mobile Application* (EMAi).

***85. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha kuanzia Julai 2019 hadi Aprili 2020 jumla **ya** matukio **537** ya magonjwa mbalimbali ya mifugo yalitolewa taarifa katika maeneo mbalimbali yakilinganishwa na matukio **1,025** yaliyotolewa taarifa katika mwaka 2018/2019 nchini. Pia, katika matukio hayo mifugo **605,722** ikiwemo ngómbe **432,521**, mbuzi **140,180** na kondoo **32,021** ilipatwa na magonjwa na **221,733** kufa kutokana na magonjwa hayo. Mifugo iliyokufa kwa magonjwa ni ngómbe **198,010**, mbuzi **21,203** na kondoo **2,520** ambapo mifugo iliyopatwa na magonjwa imepungua kwa asilimia **29** ikiwa ni mifugo **853,180** (ngómbe **627,155**, mbuzi **185,038** na kondoo **40,987**). Aidha, mifugo iliyokufa imepungua kwa asilimia **37** ikilinganishwa na mifugo iliyokufa kwa magonjwa mwaka 2018/2019.

***86. Mheshimiwa Spika,*** **k**atika mwaka 2020/2021 Wizara itaendelea kuimarisha upatikanaji wa taarifa za magonjwa ya mifugo kwa kuwezesha kutoa mrejesho wa kitaalamu juu ya udhibiti wa magonjwa yanayoambukiza binadamu kutoka kwa wanyama na matumizi sahihi ya pembejeo za Wanyama katika Halmashauri **30** na kuwezesha uchanjaji wa wanyama **25,000,000** dhidi ya magonjwa ya kipaumbele **13**. Aidha, Wizara itaimarisha huduma za uchunguzi na matibabu kwa kujenga kliniki na maabara katika Mamlaka za Serikali za Mitaa **10**.

19.0 **Baraza la Veterinari Tanzania**

***87. Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia Baraza la Veterinari Tanzania (Veterinary Council of Tanzania – VCT) ina jukumu la kusimamia maadili ya wataalam wa afya ya wanyama na viwango vya huduma ya wanyama zinazotolewa na wataalam hao. Katika kipindi cha tarehe 1 Julai, 2019 hadi 30 Aprili, 2020, Wizara, kupitia Baraza la Veterinari Tanzania imetekeleza yafuatayo:-

(i) Vituo vya kutoa huduma ya afya ya wanyama **928** vimekaguliwa kati ya **1,900** vilivyotarajiwa kukaguliwa katika mikoa 17. Ukaguzi huu ulilenga kuhakikisha vituo vya afya ya wanyama vinatoa huduma stahiki na zinazokidhi matarajio ya wafugaji (**Kiambatisho Na. 22**);

(ii) Vituo 40 vya kutolea huduma ya afya ya wanyama vimefungwa kutokana na kukosa sifa (**Kiambatisho Na. 23**);

(iii) Watoa huduma sita (**6**) wasio na sifa waliokamatwa kwenye minada katika Mikoa ya Singida na Simiyu wakiuza dawa kinyume na taratibu na kuchukuliwa hatua za kisheria;

(iv) Madaktari wa mifugo **59** wamesajiliwa kati ya **60** waliotarajiwa kusajiliwa na vituo vya afya ya wanyama **250** vimesajiliwa kati ya **400** vilivyotarajiwa kusajiliwa;

(v) Wataalam wasaidizi **200** wameandikishwa kati **50**0 waliotarajiwa kuandikishwa na kuorodhesha, wasaidizi wa wataalam **305** wameorodheshwa kati ya **500** wanaotarajiwa kuorodheshwa;

(vi) Leseni 64 zimetolewa kwa wakaguzi wanyama, wataalam wa maabara na wahimilishaji kati ya leseni 200 zilizotarajiwa kutolewa;

(vii) Jumla ya maeneo ya kutolea huduma ya afya ya wanyama 1,730 yamesajiliwa, ikiwemo Hospitali moja (1) ya wanyama iliyopo SUA - Morogoro; Kliniki (18); maabara (2) na vituo vya afya ya wanyama (1,709) link https://

www.mifugouvuvi.go.tz/publicatio ns/39. (1) Vyuo viwili (**2**) vipya vimekaguliwa na kutambuliwa kuwa na sifa ya kutoa mafunzo ya Astashahada na Stashahada za afya na uzalishaji wa wanyama ambavyo ni Tanzania Research and Career Development Institute (TRACDI), kilichopo Nzughuni, Dodoma na (2) KARUCO kilichopo Kagera. Vyuo hivyo vitaanza kutoa mafunzo katika mwaka wa masomo 2020/2021.

(viii) Chuo cha Mahinya (Ruvuma) kimekaguliwa na kuelekezwa kukamilisha hatua zilizobakia za maandalizi kabla ya kutambuliwa.

***88. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020 Wizara kupitia Baraza la Veterinari Tanzania imeweka utaratibu kwa wahitimu wote wa shahada ya veterinari kupitia mafunzo kwa vitendo (internship) ya mwaka mmoja (1) na wale wa Stashahada ya afya na uzalishaji wa wanyama miezi sita (6) kama ilivyoelekezwa katika Sheria ya Veterinari (SURA 319). Lengo la mpango huu ni kuwajengea weledi na umahiri zaidi wahitimu wote wa Udaktari wa Wanyama na Stashahada ya Afya na Uzalishaji wa Wanyama katika kuwahudumia wafugaji. Utaratibu huu utaanza kutekelezwa katika mwaka 2020/2021.

***89. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2020/2021 Wizara kupitia Baraza la Veterinari Tanzania itaendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Veterinari (SURA 319) na Kanuni zake kwa kusajili madaktari wa mifugo **70;** vituo vya huduma ya afya ya wanyama **400;** kuorodhesha na kuandikisha wataalam wasaidizi **1,000;** na kutoa leseni kwa wakaguzi wa nyama, wahimilishaji na wataalam wa maabara za veterinari **200.** Aidha, Baraza litaendelea kusimamia maadili ya wataalam na viwango vya utoaji huduma ya mifugo kwa kufanya ukaguzi wa vituo vya kutoa huduma ya mifugo katika Halmashauri zote nchini na kusimamia mafunzo kwa vitendo na ya kujiendeleza kwa wataalam kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

## 20.0 **Utafiti, Mafunzo na Ugani**

### 20.1 ***Uratibu wa Utafiti na Mafunzo***

***90. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuratibu na kusimamia shughuli za Utafiti na Mafunzo ya Mifugo nchini kupitia Taasisi ya Utafiti wa Mifugo (TALIRI) na Wakala wa Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo (LITA). Aidha, Wizara, imeandaa Ajenda ya Kitaifa ya Utafiti wa Mifugo ya miaka mitano (Livestock Research agenda 2020 -2025) iliyozinduliwa tarehe 16 Novemba, 2019.Lengo la Ajenda hii ni kutekeleza vipaumbele vya Serikali, katika kutekeleza ajenda hii kwa ufanisi Wizara imeandaa kanuni za utafiti (Livestock Research Regulations 2020) na Kanzidata ya Watafiti wa Mifugo Nchini (National Livestock Research Database). Matokeo makubwa yanayotarajiwa ni pamoja na:-

(i) Kufungua makabati yaliyoficha tafiti zilizofanyika miaka iliyopita kuanzia mwaka 2010, kuziorodhesha na kuwezesha kuwafikia wadau ili kutatua changamoto za Sekta ya Mifugo. Katika mwaka wa fedha 2019/2020 jumla ya tafiti **279** zimeorodheshwa.

(ii) Kupanua wigo wa utafiti kwa kuzitambua na kuziorodhesha tafiti mbalimbali zinazofanywa na watafiti nchini ikijumuisha wanafunzi wa Shahada za Uzamili na Uzamivu.

(iii) Kuweka msingi wa kisheria katika kusimamia na kutoa wajibu na majukumu kwa watafiti kuzingatia vipaumbele vilivyowekwa na Serikali katika kufanya tafiti mbalimbali nchini.

(iv) Kuwezesha ukusanyaji wa tafiti zote za mifugo zinazofanyika kila mwaka na kuzisambaza kwa wadau, hali ambayo itawezesha wadau mbalimbali kupata taarifa za utafiti kwa urahisi na kwa wakati, pia, kwa upande wa Serikali itasaidia kutunga na kurekebisha sera, sheria, kanuni na miongozo.

(v) Kuimarisha ushirikiano na mahusiano ya taasisi za utafiti.

***91. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020 Wizara imeandaa Mpango Mkakati wa Uendelezaji na Uhifadhi wa Kosaafu na Uboreshaji wa Mbari za Mifugo (National Compact Strategies and Action Plan to Implement Global Plan of Action for Animal Genetic Resources in Tanzania). Utekelezaji wa mkakati huo utasaidia:-

(i) Kuweka miongozo ya kutambua kabila, koo na mbari za mifugo na kufanya uchambuzi yakinifu wa kosaafu (characterization) pamoja mifumo ya uzalishaji mifugo nchini;

(ii) Kukuza utumiaji endelevu wa kosaafu kwa kupitia teknolojia za kisasa na maarifa asilia;

(iii) Kutengeneza mfumo imara na wa uhakika wa Uhifadhi Kosaafu za Mifugo nchini; na

(iv) Kushawishi jamii za kimataifa katika kuimarisha uwezo wa Taasisi zetu zinazohusika na uendelezaji mbari.

***92. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020 Wizara ilifuatilia ajira za wahitimu (tracer study) wa Vyuo vya mafunzo ya Mifugo nchini katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2014 – 2019). Lengo la ufuatiliaji huo ilikuwa ni kutambua kiwango cha wahitimu walioajiriwa katika sekta za umma na binafsi ndani ya sekta ya mifugo na kuainisha changamoto. Aidha, ufuatiliaji huu umebainisha changamoto kubwa kuwa ni upungufu wa mafunzo ya ujasiriamali katika mitaala na ukosefu wa mitaji kwa wahitimu. Serikali inaendelea kuzitafutia ufumbuzi changamoto hizi ili kuwawezesha wahitimu wengi kujiajiri katika sekta ya mifugo kwa kuhakikisha vituo atamizi (incubation centres), mafunzo kazini (internship) na kupitia upya mitaala.

***93. Mheshimiwa Spika***, Wizara, imeandaa Mitaala mitatu (**3**) ya kozi fupi za umahiri katika Tasnia za maziwa, nyama na ngozi. Lengo la mitaala hii ni kuwezesha upatikanaji wa wataalam mahususi katika viwanda vya Uchakataji na Usindikaji wa mazao yatokanayo na mifugo. Walengwa wa mafunzo haya ni wataalamu wa mifugo na wajasiriamali

katika Mnyororo wa thamani wa Sekta ya Mifugo. Mafunzo haya yatatolewa katika Kampasi za LITA na hivyo kutatua tatizo la uhaba wa Wataalamu hawa wa umahiri.

***94. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/2021 Wizara itaendelea kuratibu na kusimamia utoaji wa mafunzo ya mifugo kwa vyuo vya Serikali na Binafsi vinavyotumia Mitaala ya Wizara iliyopitishwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE). Vyuo binafsi vya Mifugo vinavyotumia Mitaala ya Wizara ni pamoja na Igabiro (Muleba), Hagafilo (Njombe), Kilacha (Moshi), Visele (Mpwapwa), CANRE (Ubungo) na Kaole (Bagamoyo). Aidha, Wizara itaendelea kuwaandaa wakufunzi wa vyuo vya mifugo kutoa mafunzo kwa kutumia mfumo wa Weledi na Stadi Stahiki (yaani Competency-based Education and Training - CBET). Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Taasisi na vitengo itaanzisha kanzidata ya TEHAMA (ICT) ya Mafunzo na Ugani. Lengo ni kurahisisha upatikanaji wa taarifa za mafunzo na ugani.

20.2 ***Huduma za Ugani wa Mifugo***

***95. Mheshimiwa Spika*;** idadi ya watumishi wa ugani kwa sekta ya mifugo bado ni ndogo ikilinganishwa na mahitaji. Mahitaji ya wataalam wa Ugani wa mifugo kwa sasa ni Wagani **17,848** kwa mchanganuo ufuatao; ngazi ya Mkoa **52**, Halmashauri za Wilaya **1,643**; Kata **3,834** na vijiji **12,319**. Aidha, Wagani wa mifugo waliopo kwa sasa katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ni **3,795** na hivyo kuwa na upungufu wa Wagani **14,053** kwa kada za uzalishaji, afya ya mifugo na nyanda za malisho. Serikali itaendelea kuongeza idadi ya Maafisa Ugani kadiri ya upatikanaji wa fedha.

***96. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, Wizara imeendelea kutoa elimu ya mafunzo rejea na maarifa mapya kuhusu uzalishaji wa kibiashara kama ifuatavyo:-

(i) Wadau **8,158** katika Halmashauri **25** wakiwemo wafugaji **6,030** maafisa ugani **471,** wanafunzi wa shule za sekondari na msingi **1,433,** wakuu wa shule za sekondari na msingi **87** na watendaji wa kata na vijiji **137.** Hivyo, hili ni ongezeko la

asilimia 77.4 kutoka **1,840** katika mwaka 2018/2019 hadi kufikia **8,158** mwaka 2019/2020. Mafunzo hayo yametolewa katika Halmashauri za Mvomero, Sumbawanga Mji, Sumbawanga Vijijini, Nkasi, Kalambo, Mpanda, Chato, Tanganyika, Mpimbwe, Nsimbo, Mlele, Meatu, Songwe, Ileje, Tunduma Mji, Mbozi, Momba, Mkuranga, Mbeya Jiji, Mbeya Vijijini, Mbarali, Chunya, Kyela, Busokelo na Rungwe. Mafunzo hayo yalihusu ufugaji bora wa mifugo ya aina mbalimbali.

(ii) Wachunaji wa ngozi **735** na wataalam wa mifugo **94** wamejengewa uwezo kuhusu uchunaji bora wa ngozi unaozingatia mahitaji ya soko kutoka katika Mikoa nane (**8**) (**Kiambatisho Na. 24**).

(iii) Vyama hai **40** vya ushirika wa wafugaji vimeratibiwa katika Mikoa ya Manyara (**2**), Iringa (**2**), Simiyu (**1**), Tanga (**8**), Kilimanjaro (**6**), Arusha (**7**), Singida (**1**), Mbeya (**11**) na Morogoro (**2**).

(iv) Wafugaji na wadau **115,979** wamepatiwa elimu ya ufugaji bora wa kibiashara kupitia maonesho ya Saba Saba (**25,200)**, Nane Nane (**75,089)** na Siku ya Chakula Duniani (**15,670**).

(v) Machapisho mbalimbali kuhusu ufugaji bora vikiwemo vitabu **1,533;** vipeperushi **16,260**; majarida **500;** na mabango **150** yaliandaliwa na kusambazwa.

(vi) Jumla ya Wataalamu **117** walipata mafunzo ya kudhibiti kuenea kwa magonjwa yasiyokuwa na mipaka (Trans Boundary Animal Diseases – TADs) kwa ufadhili wa USAID.

(vii) Mashamba darasa **31** ya malisho yameanzishwa katika Halmashauri **13** za Ikungi, Itigi, Mkalama, Iramba, Singida Manispaa, Singida Vijijini, Manyoni, Monduli, Rungwe, Njombe vijijini, Mufindi, Kahama na Kishapu. Aidha, kwa sasa kuna jumla ya mashamba darasa **88** katika Halmashauri **37**.

***97. Mheshimiwa Spika,*** katika 2020/2021 Wizara itaendelea kutoa mafunzo rejea kwa wafugaji **181,000** katika Halmashauri **156** na Maafisa Ugani **200**, kuanzisha mashamba

darasa **50** katika Halmashauri **30** na kusambaza teknolojia za ufugaji bora kupitia maonesho ya Nane Nane, Saba Saba na Siku ya Chakula Duniani. Aidha, Wizara itaandaa na kusambaza machapisho ya ufugaji bora, kuratibu utoaji wa huduma za ugani nchini, kuhamasisha uanzishwaji wa vyama vya ushirika wa wafugaji na kuandaa makala mbalimbali.

## 21.0 **Taasisi Zilizo Chini ya Wizara**

### 21.1 ***Kampuni ya Ranchi za Taifa***

***98. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020 Wizara kupitia Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) imetekeleza majukumu yake ikiwa ni pamoja:

(i) Kutunza jumla ya ng'ombe **14,742**, mbuzi **2,920**, kondoo **2,889,** nguruwe **259** na farasi **31**.

(ii) Kuzalisha na kukuza ndama **4,781** ikilinganishwa na ndama **4,606** waliozalishwa na kukuzwa katika mwaka 2018/2019.

(iii) Kununua ng'ombe **2,283** wenye thamani ya shilingi **1,369,800,000** kutoka kwa wafugaji wa asili kwa ajili ya kunenepesha kwa kutumia vyakula vya ziada ili kuzalisha nyama bora na hivyo kuwa sehemu ya soko la uhakika kwa wafugaji nchini ikilinganishwa na ng'ombe **1,343** walionunuliwa katika mwaka 2018/2019.

(iv) Kuuza ng'ombe **4,998** wenye thamani ya shilingi **3,040,309,298** ikilinganishwa na ng'ombe **3,598** wenye thamani ya shilingi **2,572,000,000** waliouzwa katika mwaka 2018/2019. Kati ya ng'ombe hao waliouzwa, ng'ombe **2,283** walinunuliwa kutoka kwa wafugaji na kunenepeshwa na **2,715** walitoka kwenye ranchi.

(v) Jumla ya ekari **6,771** zimefyekwa vichaka kwa ajili ya kuruhusu ukuaji wa malisho. Pia, Kampuni itanunua vifaa vya kisasa kwa ajili uandaaji wa mashamba ya malisho na kuvyeka vichaka.

(vi) Kuweka mipaka ya kuonekana katika Ranchi za Missenyi, Ruvu na Uvinza.

(vii) Kumega eneo lenye ukubwa wa hekta. **24,435.912** kutoka katika Ranchi za Missenyi (**22,201.094**) na Ruvu (**2,234.818** ha) kwa ajili ya matumizi ya kilimo, mifugo na makazi katika vijiji.

(viii) Yapo maduka **7** ya nyama katika maeneo ya Bukoba, Dar es Salaam, Dodoma, Kongwa, Hai, Morogoro na Kalambo (Rukwa).

***99. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/2021 Kampuni ya NARCO imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kuzalisha ng'ombe **4,964**, mbuzi **1,937** kondoo **1,317** pamoja na kuzalisha na kuuza nyama tani **896**;

(ii) Kununua jumla ya ng'ombe **6,000** wenye thamani ya shilingi **3,600,000,000** na kuuza jumla ya ng'ombe 7,996 kwa thamani ya shilingi 6,272,870,000.

(iii) Kufyeka vichaka ekari **2,696** na kupima na kuweka alama za mipaka inayoonekana katika ranchi **11** za Kagoma, Mabale, Kitengule, Kikulula, Kongwa, Mzeri, West Kilimanjaro, Kalambo, Usangu, Mkata, Dakawa; na eneo la Mwisa II.

(iv) Kutoa ushauri wa kitaalamu kwa wafugaji **50**0 katika vijiji vinavyozunguka Ranchi za NARCO; na mafunzo kwa vitendo kwa wanachuo **290** kutoka katika Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo hapa nchini.

(v)Kufungua maduka mapya mawili (**2**) ya nyama katika Mikoa ya Mwanza na Arusha. Pia, itanunua magari mawili (**2**) yenye mfumo baridi (refrigerated trucks) kwa ajili ya kusafirisha nyama.

21.2 ***Bodi ya Nyama Tanzania***

***100. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, Bodi ya Nyama Tanzania imeendelea kuratibu, kusimamia na

kuendeleza tasnia ya nyama nchini ambapo mafanikio yafuatayo yamepatikana:-

(i) Vibali **86** vya kuuza nyama nje ya nchi vilitolewa. Aidha, jumla ya tani **692.36** za nyama (nyama ya ng'ombe **tani 142.18**, mbuzi **tani 36.07** na kondoo **tani 1.11**, punda na **tani 513**) zenye thamani ya shilingi **2,985,609,691** (Dola za Marekani **1,298,091.17**) ziliuzwa nje katika nchi za Dubai, Iraq, Omani, Comoro, Hongkong na Vietnam ikilinganishwa na kiasi cha tani **1,207.93** zenye thamani ya shilingi **5,207,057,286.21** zilizouzwa nje ya nchi katika mwaka 2018/2019.

(ii) Vibali **36** vimetolewa kuingiza nyama ndani ya nchi yenye jumla ya tani **243.65** (nyama ya ng'ombe tani 195.12, nguruwe tani 48.53) na thamani ya shilingi **4,066,632,530** (Dola za Marekani **1,768,101.10**) kutoka Kenya, Afrika Kusini, Ubelgiji na Uingereza ikilinganishwa na kiasi cha tani **516.63** zenye thamani ya Shilingi **4,970,240,959.00** (Dola za Marekani **2,160,974.33)** zilizoingizwa nchini mwaka 2018/2019.

(iii) Uingizaji wa mazao ya mifugo kutoka nje ya nchi umeshuka kwa asilimia **90**.

(iv) Wadau wa nyama **757** wametambuliwa na kusajiliwa katika mikoa **21** (**Kiambatisho Na. 25**). Jumla ya machinjio **31** zimekaguliwa. Kutokana na ukaguzi huo machinjio **8** zimefungwa kutokana na kushindwa kukidhi vigezo, machinjio hizo zipo katika mikoa tisa (9) (Kiambatisho Na. 26).

(v) Wadau wa nyama **706** wamepatiwa mafunzo juu ya uanzishaji vyama vya ushirika vya mifugo, uzalishaji wa nyama bora na salama, elimu ya biashara ya nyama, utambuzi na usajili wa mifugo na fursa za uwekezaji katika tasnia ya nyama nchini.

***101. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/2021 Wizara kupitia Bodi ya Nyama itaendelea kuhamasisha uboreshaji mifugo ili kuimarisha mnyororo wa thamani katika tasnia ya nyama unaokidhi mahitaji ya soko la ndani na nje ya nchi; kuendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza zaidi katika

ujenzi wa viwanda vya kuchakata na kusindika nyama ili kuziba pengo la mahitaji ya nyama nchini; kutoa mafunzo ya uzalishaji na uuzaji wa nyama kwa kuzingatia taratibu za usafi; kutambua na kusajili wadau wa tasnia ya nyama na vyama vyao.

21.3 ***Bodi ya Maziwa Tanzania***

***102. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Bodi ya Maziwa Tanzania imeendelea kusimamia biashara ya maziwa ndani na nje ya nchi ili kuimarisha uzalishaji na biashara ya maziwa na mazao yake. Katika mwaka 2019/2020 jumla ya lita bilioni 3 za maziwa zilizalishwa na vibali **443** vimetolewa ili kuingiza maziwa yenye ujazo wa lita **11,725,859.84** vikiwa na thamani (FOB value) ya Shilingi **15,199,487,699** kutoka nchi za Afrika Kusini; Uganda; Kenya; United Arab Emirates; Uholanzi; na Ireland ikilinganishwa na vibali **692** vilivyotolewa mwaka 2018/2019 kuingiza maziwa yenye ujazo wa lita **18,617,659.07** vikiwa na thamani (FOB value) ya Shilingi **26,224,025,033.80** sawa na upungufu wa asilimia **42.04.** Kupungua kwa kiasi cha maziwa kinachoingizwa nchini kumetokana na kuimarika kwa udhibiti wa uingizaji maziwa na mazao yake kutoka nje ya nchi kwa lengo la kulinda viwanda vya ndani, kuongezeka uzalishaji wa maziwa na kuimarika kwa viwanda vya ndani vya kusindika maziwa.

***103. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020 Bodi imeendelea kusimamia tasnia ya maziwa ambapo mafanikio yafuatayo yamepatikana:-

(i) Programu ya Unywaji Maziwa Shuleni imeratibiwa katika shule **49** za mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Njombe, Mbeya na Tanga zenye wanafunzi **33,115**.

(ii) Siku ya Unywaji Maziwa Shuleni imeadhimishwa kitaifa Mkoani Iringa tarehe 26 Septemba, 2019 ambapo jumla ya shule 10 zenye wanafunzi 3,400 zilishiriki na pakiti 600 za ujazo wa mililita 250 ziligawiwa kwa wanafunzi.

(iii) Wadau 16,000 wamehamishwa kuwekeza katika tasnia ya maziwa kupitia maonesho ya Saba Saba, Wiki ya unywaji Maziwa shuleni, Nane Nane na Bonanza la michezo.

(iv) ATM tatu (3) za maziwa zimezinduliwa katika mikoa ya Kilimanjaro na Arusha. Bodi ya Maziwa kwa kushirikiana na TAMPA imeingia makubaliano na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ili kudurufu mashine hizo na kusambazwa nchini baada ya kuthibitishwa ubora wake.

(v)Wiki ya maziwa itaadhimishwa kielekroniki kuanzia tarehe 28 Mei hadi tarehe 1 Juni, 2020 kwa kuzingatia tahadhari na kujikinga na ugonjwa wa COVID 19.

(vi)Wadau **250 wa** maeneo ya Arusha, Dar es Salaam, Mwanza, Morogoro, Mbeya, Tanga na Pwani wamesajiliwa ikilinganishwa na wadau **63** waliosajiliwa katika mwaka 2018/ 2019.

(vii) Ukaguzi umefanyika katika maeneo 160 ya kuzalisha, kusindika, kutunza na kuuza maziwa ikiwemo vioski (19), maduka (62), viwanda (17) na magari ya kusafirisha maziwa (62).

(viii) Wadau 283 wamepatiwa mafunzo, kati ya hao 126 kuhusu usindikaji maziwa; 135 uzalishaji maziwa na 22 Udhibiti wa Ubora wa Maziwa katika mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Mbeya, Mwanza, Morogoro na Pwani.

(ix) Vikundi 18 vyenye wanachama 3,182 vimejengewa uwezo katika maeneo ya Kiutawala; Kiufundi na Usimamizi wa Fedha kutoka katika Mikoa ya Iringa (6); Njombe (4); Mbeya (3); Songwe (1); Morogoro (1); Pwani (1); Mwanza (1); na Dar es Salaam (1).

(x) Vituo 10 vya kukusanyia maziwa vimejengwa kwa kushirikiana na sekta binafsi katika mikoa ya Ruvuma (6), Pwani (2) na Dar es Salaam (2).

(xi)Kusimamia upatikanaji wa mkopo kutoka Benki ya Maendeleo ya Kilimo wenye thamani ya shilingi 241,742,000 kwa wafugaji 46 wa vyama vya CHAWAMU na UWAMWA vilivyopo Mkoani Tanga kwa ajili ya kununua mitamba 76 na ujenzi wa mabanda bora 25.

***104. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/2021 Wizara kupitia Bodi ya Maziwa Tanzania itaendelea kuimarisha na kujenga vituo **50** vya kukusanyia maziwa vyenye uwezo wa **lita 135,000** kwa siku katika maeneo yanayozalisha maziwa kwa wingi; kuhamasisha ujenzi wa mabanda bora ya ng'ombe wa maziwa; uwekezaji katika viwanda vya kusindika maziwa na mazao yake; uhamasishaji wa uundaji wa ushirika wa wafugaji wa ng'ombe wa maziwa na kuwaunganisha wafugaji hao na taasisi za kifedha ili kupata mitaji na kufuga kwa tija. Aidha, Bodi itaendelea kuhamasisha unywaji wa maziwa kupitia wiki ya maziwa; unywaji wa maziwa shuleni na Bonanza la michezo.

### 21.4 ***Wakala wa Maabara ya Veterinari***

***105. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020 Wizara kupitia Wakala wa Maabara ya Veterinari Tanzania (TVLA) imepata mafanikio yafuatayo:-

(i) Idadi ya chanjo za mifugo zinazozalishwa imeongezeka kutoka chanjo nne (**4**) mwaka 2018/19 kufikia chanjo sita (**6**) mwaka 2019/2020;

(ii) Jumla ya dozi **49,008,325** za chanjo za mifugo zimezalishwa na kusambazwa nchini ambapo Halmashauri **40** dozi **1,287,000**, wasambazaji wa pembejeo za mifugo na wachanjaji binafsi dozi **47,721,325** (**Kiambatisho Na. 27**);

(iii) Ujenzi wa jengo jipya litakalotumika katika utengenezaji wa chanjo za bakteria umekamilika kwa asilimia **75**;

(iv) Uchunguzi na utambuzi wa magonjwa ya mifugo katika sampuli 13,587 umefanyika ambapo magonjwa muhimu yaliyotambuliwa ni pamoja na Kichaa cha Mbwa, Kimeta,

Ugonjwa wa Kutupa Mimba, Nagana, Ndigana Kali, Ndigana Baridi na Homa ya Mapafu ya Ng'ombe;

(v) Uchambuzi wa ubora wa vyakula vya mifugo katika sampuli **1,260** umefanyika ambapo sampuli **46** sawa na asilimia **6** zilibainika kuwa na upungufu wa nishati na protini;

(vi) Kituo kipya cha Wakala kimeanzishwa katika Mji wa Sumbawanga kwa ajili ya kuhudumia Kanda ya Nyanda za Juu Kusini Magharibi;

(vii) Miradi ya kutokomeza ugonjwa wa malale inatekelezwa katika vijiji vya Emboreet, Loibor siret na Kimotorok katika Wilaya ya Simanjiro ambapo jumla ya mbung'o **5,000** na sampuli **770** za damu za ng'ombe zilikusanywa kwa lengo la kuangalia maambukizi ya ndorobo. Pia, utafiti unaendelea ili kubaini kemikali bora ya kufukuzia/kuvutia mbung'o na jamii ya inzi wasumbufu wa mifugo katika vijiji vya Mwangudo, Sungu, Makao na Mbushi katika Wilaya ya Meatu;

(viii) Utafiti katika maeneo ya utengenezaji wa chanjo ya Homa ya Mapafu ya Mbuzi (CCPP), uimarishaji wa ufugaji wa kuku wa kienyeji, udhibiti wa ndorobo na uimarishaji wa uwezo wa kudhibiti viini vya magonjwa unaendelea. Utafiti huo umepata ufadhili wenye thamani ya shilingi **1,635,094,800** kutoka International Atomic Energy Agency (IAEA), Biotechnology and Biological Sciences Research Council (BBSRC), BIOINNOVATE na COSTECH.

(ix) Jumla ya sampuli **82** za dawa za kuogesha mifugo zilifanyiwa uchunguzi ambapo sampuli **71** sawa na asilimia **87** kati ya hizo zilionekana kuwa zinafaa kwa matumizi.

(x) Ujenzi wa Kliniki ya mifugo katika Wilaya ya Meatu umekamilika kwa asilimia **85**.

***106. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/2021 Wizara kupitia Wakala wa Maabara ya Veterinari itaongeza uzalishaji wa chanjo na itaanza kuzalisha wa aina tatu (**3**) mpya za chanjo ambazo ni Chanjo ya Ugonjwa wa Kichaa cha Mbwa,

Sotoka ya Mbuzi na Kondoo na Homa ya Mapafu ya Mbuzi. Pia, Wakala utaendelea kuchunguza na kutambua magonjwa ya mifugo yanayotokea nchini kwa kupima sampuli **35,000,** kufanya uchambuzi wa ubora wa vyakula kwenye sampuli **5,000** na kuchunguza nguvu za dawa za josho katika sampuli **300** kutoka maeneo yaliyoonesha usugu wa dawa za kuogeshea mifugo. Aidha, TVLA itaendelea kufanya tafiti za magonjwa ya mifugo na wadudu waenezao magonjwa hayo. Pia, TVLA itaanzisha kituo kipya cha uchunguzi na utambuzi wa magonjwa katika Mkoa wa Simiyu ili kuigawa Kanda ya Ziwa yenye mikoa sita (6) inayohudumiwa na kituo kimoja cha Mwanza.

21.5 ***Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania***

***107. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020 Wizara kupitia Taasisi ya Utafiti wa Mifugo (TALIRI) ilitekeleza miradi ya utafiti **39** katika nyanja za utafiti wa ng'ombe wa maziwa; ng'ombe wa nyama; mbuzi; kondoo; kuku; malisho; na sayansi ya jamii na uchumi. Mafanikio yaliyopatikana ni kama ifuatavyo:-

(i) Ng'ombe bora wa maziwa **119** wenye mchanganyiko wa damu za *Sahiwal* na Friesian na *Danish Red);* (*Sahiwal* na *Mpwapwa); Mpwapwa* na *Danish Red* walizalishwa.

(ii) Ng'ombe chotara wa nyama **77** wenye mchanganyiko wa damu za *Mpwapwa* na *Boran; Mpwapwa* na *Sahiwal;* na *Sahiwal, Mpwapwa* na *Boran* walizalishwa.

(iii) Ng'ombe chotara **141** wenye sifa mchanganyiko ya kuzalisha nyama na maziwa (dual purpose) walisambazwa kwa wafugaji kwa ajili ya kuboresha uzalishaji katika mikoa nane **(8)** ikiwepo Pwani; Mwanza; Simiyu; Morogoro; Tanga; Geita; Dodoma na Mbeya ikilinganishwa na ng'ombe **130** waliosambazwa katika mwaka 2018/2019.

(iv) Ziara ya mafunzo kwa wafugaji **20** kutoka Halmashauri ya Longido kwenda nchini Kenya ili kujifunza na kupata uzoefu wa umuhimu wa uhimilishaji ilifanyika. Kutokana na ziara hiyo

Ushirika wa Wafugaji wa Ng'ombe aina ya Sahiwal Longido (UWASALO) wenye wanachama **42** umeundwa kwa lengo la kuunganisha wadau na kurahisisha uratibu.

(v) Jumla ya mbuzi **1,472** wamenenepeshwa kupitia Kituo Atamizi kinachoendeshwa na TALIRI kwa ushirikiano na PASS. Aidha, ujenzi wa mabanda **10** yenye uwezo wa kunenepesha mbuzi **2,000, O**fisi **(1),** machinjio (1), maduka ya kuuzia nyama (10) na mgahawa (1) umefanyika.

(vi) Kupitia uhawilishaji kiinitete (MOET), jumla ya viinitete **34** vilivunwa na kupandikizwa kwa ng'ombe waleaji mimba **34.** Vilevile, mtambo wenye thamani ya shilingi **milioni 189** wa kuzalisha kimiminika cha hewa baridi ya Naitrojeni wenye uwezo wa kuzalisha lita **65** kwa siku umenunuliwa na kusimikwa kwenye maabara ya bayoteknolojia iliyopo Mpwapwa.

(vii) Ufuatiliaji wa mwenendo wa uzalishaji kwa kutumia Teknolojia ya TEHAMA umefanyika kwa wafugaji **19,000** ambapo ng'ombe wa maziwa **179,197** wanafuatiliwa ufanisi wao katika mikoa ya Arusha **(31,803)**; Kilimanjaro **(31,081);** Tanga (**59,589)**; Iringa **(28,458**); na Mbeya (**28,262**). Mfumo huo unawezesha wafugaji kupata ushauri wa kitaalam kulingana na hali ya ng'ombe wake.

(viii) Jumla ya vifaranga **2,400** vya kuku wa asili aina ya *Horasi* vilianguliwa kwa ajili ya tathmini ya ukuaji na uzalishaji. Utafiti huu wa kupata kuku wa asili utafanyika kwa kipindi cha miaka **5** hadi **8** kwa lengo la kupata kuku wenye wastani wa uzito wa kilo **1.5** katika umri wa wiki **16** na uwezo wa kutaga mayai **200** hadi **240** kwa mwaka.

(ix) TALIRI imesambaza kuku chotara aina ya *Sasso* **32,000** na *Kroiller* **11,000** kwa kaya za wafugaji **1,864** katika Mikoa ya Dodoma, Tanga, Mtwara, Singida, Mbeya, Simiyu na Mwanza.

(x) Ili kutekeleza utafiti wa kuku, TALIRI imenunua vifaa na mitambo mbalimbali vikiwemo; mashine ya kuangulia vifaranga (*egg incubator*) yenye uwezo wa kuatamisha

mayai **5,280,** Vizimba (cages) tisa (**9**) vyenye uwezo wa kubeba kuku **432**, Mashine ya kusaga na kuchanganya chakula cha kuku yenye uwezo wa kuchakata tani **1.0** hadi **1.5** kwa saa moja.

(xi) Wataalam **16** walipatiwa mafunzo ya uhimilishaji mbuzi ambapo mbuzi **181** wamehimilishwa kwenye Halmashauri ya Siha. Vilevile, mbuzi **134** walisambazwa kwa wafugaji katika maeneo ya Kwimba, Ulanga, Bariadi, Tanga, Pwani, Morogoro, Chato, Nyamagana, Meatu, Misungwi, Bagamoyo, Dodoma Mjini na Ilala. Aidha, mbuzi **119** aina ya *Malya, Gogo White, Sonjo Red* na *Pare White* walizalishwa.

(xii) Vitalu 90 vyenye aina sita (6) za Mikunde na nne (4) za nyasi kwa ajili ya majaribio ya urasimishaji wa mbegu za malisho vimestawishwa kwenye Vituo vya Mpwapwa, Uyole na Tanga.

***108. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TALIRI inatekeleza utafiti kwa kufuata Agenda ya Utafiti wa Mifugo nchini. Aidha, TALIRI imeanzisha kanzidata ya kitaifa ya tafiti za mifugo (*National Livestock Research Database*) ambapo jumla ya Tafiti **433** zimekusanywa kutoka Taasisi zinazofanya tafiti za mifugo nchini ambazo ni Vyuo Vikuu (**187**); Taasisi za Utafiti (**210**); Taasisi za Wizara (**27**) na Mashirika yasiyo ya Serikali (**9**). Tafiti hizo zinapatikana kupitia tovuti ya TALIRI http://research.taliri.go.tz

***109. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TALIRI imebaini aina **saba (7)** za magugu sumbufu katika maeneo ya machunga nchini yanayohitaji kupata ufumbuzi kwa haraka. Magugu hayo ni Gugu la Kongwa (Mahata); Gugu la Siam (Amachabongo), Gugu caroti; Gugu la Cordifolia, Gugu la Jaegeri, Gugu mti Prosopis (Mrashia) na Gugu Ndulele. Aidha, TALIRI kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Sokoine inafanya utafiti wa kudhibiti gugu "Mahata" kwa kutumia njia za kemikali, kibaiolojia na matumizi dawa za miti ya asili.

***110. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/2021 Wizara kupitia TALIRI itaratibu tafiti zote nchini, kutathmini na kuendeleza

utafiti wa mifugo na malisho ili kuongeza tija katika uzalishaji wa maziwa, nyama, mayai na ngozi kuchangia uchumi wa viwanda. Aidha, Taasisi itaimarisha miundombinu ya mashamba ya utafiti katika kanda saba **(7).** Pia, TALIRI kwa ushirikiano na PASS itanenepesha mbuzi **4,000** na Kuzalisha mbuzi **1,500** kwa njia ya uhimilishaji. Vilevile, TALIRI kupitia Mradi wa ADGG, itafanya maonesho ya Gwaride la pili la ng'ombe bora wa Maziwa kwa njia ya TEHAMA katika kipindi hiki cha Janga la ugonjwa wa *Corona (COVID – 19*).

21.6 ***Wakala wa Mafunzo ya Mifugo***

***111. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020 Wizara kupitia Wakala wa Mafunzo ya Mifugo (LITA) imedahili wanafunzi wa ngazi ya Astashahada na Stashahada **3,634** ukilinganisha na wanafunzi **2,536** waliodahiliwa mwaka **2018/ 2019**. Idadi hii ni ongezeko la wanafunzi **1,098,** sawa na asilimia **43.3.** Idadi ya wanafunzi wanaotarajiwa kuhitimu masomo katika mwaka 2019/2020 kutoka Vyuo vya Serikali ni **1,678** ukilinganisha na wanafunzi **1,208** waliohitimu mwaka 2018/2019, ikiwa ni ongezeko la wanafunzi **470, sawa na** asilimia **38.9**. Idadi ya wanafunzi wanaotarajiwa kuhitimu masomo kutoka vyuo binafsi ni **407**. Aidha, jumla ya wafugaji **594** wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi katika Kampasi za Wakala ukilinganisha na wafugaji **363** waliopatiwa mafunzo katika mwaka 2018/2019, ikiwa ni ongezeko la wafugaji **231** sawa na asilimia **63.6.** Pia, jumla ya wafugaji **1,468** wamefikiwa na wanachuo wakati wa mafunzo yao kwa vitendo.

***112. Mheshimiwa Spika,*** ili kukabiliana na ongezeko la wanafunzi waliodahiliwa katika mwaka huu na LITA, miundombinu mbalimbali imeboreshwa. Miundombinu iliyokarabatiwa ni pamoja na Hosteli tatu (**3**) katika Kampasi ya Tengeru; Hosteli mbili (**2**) katika Kampasi ya Buhuri; Hosteli mbili (**2**) katika Kampasi ya Temeke; Hosteli moja (**1**) katika Kampasi ya Morogoro; Hosteli mbili (**2**) katika Kampasi ya Mpwapwa; Madarasa matatu (**3**) katika Kampasi ya Morogoro; Kumbi mbili (**2**) za mihadhara katika Kampasi za Morogoro na Mpwapwa; Maabara mbili (**2**) katika Kampasi

za Tengeru na Temeke, Maktaba mbili (**2**) katika Kampasi za Madaba na Tengeru na vyoo vitano (5) katika Kampasi za Morogoro, Mabuki, Tengeru, Mpwapwa na Buhuri. Miundombinu iliyojengwa upya ni vyoo vitatu (**3**) vya wanafunzi katika Kampasi za Morogoro, Mabuki na Kikulula.

***113. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020 Wizara kupitia LITA imefanya utafiti wa ajira za wahitimu wa Vyuo vya Mifugo nchini (2014 – 2019). Katika kipindi tajwa wanafunzi **8,132** walihitimu masomo katika ngazi ya Astashahada, Stashahada na Shahada ambapo matokeo ya awali kwa wahitimu **776** sawa na asilimia **9.5** ya wahitimu wote ndio waliofanikiwa kuajiriwa katika Sekta za Umma (**651**), walioajiriwa katika Sekta Binafsi (**60**) na waliojiajiri katika Sekta Binafsi (**65**) ndani ya Sekta ya Mifugo hadi sasa na asilimia **90.5** hawajulikani kazi wanazofanya baada ya kuhitimu masomo yao. Aidha, changamoto kubwa zimeainishwa katika utafiti huu na maeneo pendekekezwa ya utatuzi yameainishwa ambapo Serikali inayafanyia kazi.

***114. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/2021 Wizara kupitia LITA itatekeleza yafuatayo:-

(i) Kudahili wanafunzi **4,000** wa ngazi ya Astashahada na Stashahada.

(ii) Kuboresha miundombinu mbalimbali ikiwemo mabweni/ hostel, madarasa, maktaba, vyoo na maabara ili kuwezesha utoaji wa mafunzo ya muda mrefu na mfupi

(iii) Kuandaa Mpango wa utoaji mafunzo ya muda mfupi kwa Wafugaji na wajasiriamali wengine ili kuongeza uzalishaji na tija katika Sekta ya Mifugo. Aidha, Mafunzo hayo yatatolewa katika miezi ya Machi, Aprili, Agosti, Septemba na Oktoba kila mwaka. Miongozo ya utekelezaji wa Mpango huu inaandaliwa kwa kushirikiana na chama cha wafugaji Tanzania ambapo katika awamu ya kwanza kaya **1,500** za wafugaji zitafikiwa. Lengo la mpango huu ni kuzifikia kaya za wafugaji **milioni 4.6** ndani ya miaka mitano ijayo.

## C SEKTA YA UVUVI (FUNGU 64) HALI YA SEKTA YA UVUVI

***115. Mheshimiwa Spika***, Sekta ya Uvuvi ni moja kati ya sekta muhimu za kiuchumi hapa nchini. Shughuli za uvuvi hapa nchini zinahusisha uvuvi kwenye maji ya asili na ukuzaji viumbe maji. Katika mwaka 2019, Sekta ya Uvuvi ilichangia asilimia **1.71** ya Pato la Taifa na imekua kwa asilimia **1.5** Aidha, Sekta ya Uvuvi huchangia katika kuwapatia wananchi uhakika wa chakula, lishe, kuongeza kipato, fedha za kigeni na kupunguza umaskini. Vilevile, inakadiriwa kuwa zaidi ya Watanzania milioni **4.5** wanategemea shughuli zinazohusiana na uvuvi.

***116. Mheshimiwa Spika***, shughuli za uvuvi kwenye maji ya asili huendeshwa na wavuvi wadogo ambao huchangia zaidi ya asilimia **95** ya samaki wote wanaozalishwa nchini na asilimia tano (**5**) iliyobaki huchangiwa na uvuvi wa kibiashara. Aidha, uvuvi wa kibiashara hufanyika katika maji ya Kitaifa kwa uvuvi wa samaki aina ya Kambamiti na kwenye Ukanda wa Uchumi wa Bahari kwa kuhusisha meli za kigeni. Katika mwaka 2019/ 2020 jumla ya wavuvi **202,053** wanaotumia vyombo vya uvuvi **58,930** walivua kiasi cha tani **392,933.0** za samaki zenye thamani ya shilingi trilioni **1.85** (**Kiambatisho Na. 28**).

***117. Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kuhamasisha shughuli za Ukuzaji Viumbe Maji ambapo kwa mwaka 2019/ 2020, jumla ya vifaranga **21,676,187** (**Kiambatisho Na. 29)** vimezalishwa kutoka katika vituo vya binafsi na Serikali ambapo uzalishaji wa mazao ya viumbe maji ulifikia tani **18,716.56**. Kati ya tani hizo, tani **17,233** ni za samaki wenye mapezi, tani **73.56** ni za Kambamiti, tani **1,410** ni za mwani pamoja na vipande **550** vya lulu kutoka kwa wakuzaji viumbe maji **28,009**.

***118. Mheshimiwa Spika,*** samaki huchangia takriban asilimia **30** ya protini inayotokana na wanyama. Ulaji wa samaki kwa mtu kwa mwaka hapa nchini umeongezeka kutoka kilo **8.2** mwaka 2018/2019 hadi kufikia kilo **8.5** mwaka 2019/2020. Aidha, kwa mujibu wa Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa wastani wa ulaji samaki duniani kote ni kilo **20.3**

kwa mtu kwa mwaka (FAO, 2018). Serikali itaendelea kuhamasisha ulaji wa samaki miongoni mwa watanzania.

***119. Mheshimiwa Spika,*** kutokana na taarifa za utafiti, wingi wa samaki katika maji yetu umeongezeka kutoka tani **2,803,000** mwaka 2018/2019 hadi kufikia tani **3,274,165** mwaka 2019/2020 sawa na ongezeko la asilimia **16.8**. (**Kiambatisho Na. 30**). Ongezeko hilo limetokana na juhudi za Serikali katika kuimarisha ulinzi na usimamizi wa rasilimali za uvuvi kupitia doria na operesheni maalum dhidi ya uvuvi na biashara haramu ya samaki na mazao yake ikiwa pamoja na kutoa elimu ya uvuvi endelevu.

***120. Mheshimiwa Spika,*** pamoja na mafanikio yaliyopatikana, Sekta ya Uvuvi imeendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo:

i. Kutokuwepo kwa Bandari ya Uvuvi na hivyo kupoteza mapato ambayo yangepatikana kutokana leseni na tozo kwa meli zinazovua katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari;

ii. Kutokuwa na meli za kutosha za kitaifa kwa ajili ya uvuvi katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari;

iii. Kuendelea kuwepo kwa uvuvi na biashara haramu ya samaki na mazao ya uvuvi;

iv. Upotevu wa mazao ya uvuvi baada ya kuvunwa unaokadiriwa kufikia asilimia 40;

v. Uhaba wa vifaranga na vyakula vya samaki vyenye ubora;

vi. Uhaba wa Maafisa Ugani wa Uvuvi ikilinganishwa na mahitaji; na

vii. Uhaba wa huduma za kifedha kwa ajili ya kuwawezesha wavuvi kukua na kutumia teknolojia za kisasa (**Kiambatisho Na. 31**).

***121. Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na changamoto hizi Wizara imeandaa na kutekeleza mikakati mbalimbali ikiwemo:

i. Kukamilisha upembuzi yakinifu wa ujenzi wa Bandari ya Uvuvi;

ii. Kukamilisha taratibu za kufufua Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO 2018) na kununua meli za uvuvi katika maji ya kitaifa, pamoja na kutoa leseni kwa meli kubwa zinazomilikiwa na Sekta Binafsi;

iii. uongeza kasi ya utekelezaji wa Mkakati wa Usimamizi na Udhibiti wa Rasilimali za Uvuvi Nchini;

iv. Kuendelea kuimarisha ushirikiano na Mamlaka za Serikali za Mitaa na Sekta Binafsi katika kujenga na kuboresha masoko, mialo na kuwekeza katika ujenzi wa viwanda vya kuongeza thamani ya mazao ya uvuvi na kutengeneza zana za uvuvi;

v. Serikali pamoja na Sekta Binafsi zitaendelea kuimarisha vituo vya kuzalisha vifaranga, kuongeza upatikanaji wa samaki wazazi na kuboresha vitotoleshi na kuhamasisha kuanzisha viwanda vya kuzalisha vyakula bora vya samaki;

vi. Kuongeza upatikanaji wa Maafisa Ugani wa Uvuvi kwa kuimarisha Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi na kuhamasisha Mamlaka za Serikali za Mitaa na SektaBinafsi kuajiri Wagani wa Uvuvi ili kukidhi mahitaji; na

vii. Kuimarisha Dawati la Sekta Binafsi la Wizara ili kuwaunganisha wavuvi na Taasisi za fedha kwa ajili ya kupata mikopo yenye masharti nafuu na kuwahamasisha wavuvi kuanzisha vyama vya ushirika ili waweze kukopesheka.


## 22.0 **MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2019/2020**

## 23.0 **Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka 2019/2020**

***122. Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka wa fedha 2019/2020, Wizara ilitarajia kukusanya kiasi cha **Shilingi 32,301,458,000** kupitia Fungu 64. Hadi kufikia tarehe **30 Aprili, 2020** kiasi cha **Shilingi 24,484,806,549.62** sawa na asilimia **75.80** ya lengo zilikuwa zimekusanywa kutoka Sekta ya Uvuvi. Hata hivyo, makusanyo hayo ni sawa na asilimia **91** ya makusanyo yaliyolengwa kukusanywa ndani ya kipindi cha miezi kumi (**10**) ambayo ni shilingi **bilioni 26.9**. (**Kiambatisho Na. 32).**

***123. Mheshimiwa Spika,*** fedha hizi zimekusanywa kutoka vyanzo vifuatavyo: leseni za kusafirisha samaki na mazao yake (*Export Licences*); leseni za uingizaji mazao ya uvuvi (*Import Licences*); ushuru wa mrabaha (*Export Royalty*); Mrabaha wa kuingiza mazao ya uvuvi nchini (*Import Royalty*), leseni za uvuvi katika Ukanda wa Uchumi wa bahari Kuu, Tozo ya Maabara; leseni za uvuvi wa kambamiti, mauzo ya vifaranga vya samaki na faini kwa makosa mbalimbali ya ukiukwaji wa sheria za uvuvi.

24.0 **Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2019/ 2020 (*Pie Chart*)**



25.0 **Makadirio ya Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka 2020/2021**

***124. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/2021, Wizara kupitia Fungu 64 inatarajia kukusanya kiasi cha Shilingi **33,000,000,000.** Vyanzo vikuu vya fedha hizo ni pamoja na; leseni za kusafirisha samaki na mazao yake (*Export Licences*); leseni za uingizaji mazao ya uvuvi (*Import Licences*); ushuru wa mrabaha (*Export Royalty*); Tozo ya Maabara; mauzo ya vifaranga vya samaki; mauzo ya mazao ya uvuvi na faini kwa makosa mbalimbali ya ukiukwaji wa sheria za uvuvi.

26.0 **Fedha Zilizoidhinishwa**

***125. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2019/2020, Wizara ya Mifugo na Uvuvi kupitia Fungu 64 ilitengewa jumla ya Shilingi **33,127,378,551.00.** Kati ya fedha hizo, Shilingi **18,432,461,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi **14,694,917,551.00** ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.

27.0 **Matumizi ya Bajeti ya Kawaida.**

***126. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2019/2020, Fungu 64 lilitengewa jumla ya Shilingi **18,432,461,000**. Kati ya fedha hizo, Shilingi **11,557,566,693** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Wizara (PE) na Shilingi **6,874,895,000** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC). Hadi kufikia tarehe **15 Aprili, 2020**, jumla ya Shilingi **12,668,326,728.20** zilikuwa zimetolewa, sawa na asilimia **68.72** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo Shilingi **7,385,963,728.20** ni fedha za mishahara ya watumishi (PE) na shilingi **5,282,363,000.00** ni fedha za matumizi mengineyo

28.0 **Matumizi ya Bajeti ya Maendeleo**

***127. Mheshimiwa Spika,*** **k**atika mwaka 2019/2020, Wizara kupitia Fungu 64 ilitengewa kiasi cha Shilingi **14,694,917,551** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ikiwa ni fedha za ndani na nje. Kati ya fedha hizo Shilingi **3,000,000,000.00** ni

fedha za ndani na Shilingi **11,694,917,551** ni fedha za nje. Hadi kufikia tarehe **30** Aprili, **2020**, jumla ya Shilingi **6,783,584,061.19** sawa na asilimia **46.16** kutoka vyanzo vya ndani na nje zilitolewa kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi **426,312,537.92** ni fedha za ndani na shilingi **6,357,271,523.27** ni fedha za nje.

## 29.0 MAENEO YA VIPAUMBELE KATIKA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2020/2021

***128. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2020/2021, Wizara kwa kushirikiana na wadau itatekeleza vipaumbele mbalimbali ili kuifikisha nchi yetu kwenye uchumi wa viwanda. Vipaumbele hivyo ni pamoja na:-

i. Kuimarisha usimamizi, udhibiti na matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi;

ii. Kuongeza na kudhibiti upotevu wa mapato ya Serikali yatokanayo na Sekta ya Uvuvi;

iii. Kuimarisha usimamizi wa rasilimali za uvuvi katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari na Bahari Kuu;

iv. Kuimarisha usimamizi na uthibiti wa ubora, usalama na viwango vya samaki na mazao ya uvuvi;

v. Kuimarisha miundombinu na kukuza biashara ya mazao ya uvuvi;

vi. Kuboresha upatikanaji wa taarifa sahihi za Uvuvi na Ukuzaji Viumbe Maji;

vii. Kuongeza upatikanaji wa vifaranga bora vya samaki; na

viii. Kuimarisha Utafiti, Huduma za Ugani na Mafunzo ya Uvuvi.

## 30.0 UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU KATIKA MWAKA 2019/2020 NA MPANGO WA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

### 31.0 Sera, Sheria na Kanuni

***129. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020 Wizara imefanya mapitio na kutunga Sera, Sheria na Kanuni mbalimbali zinazosimamia Sekta ya Uvuvi ikiwemo:

i. Kuandaa Mpango Kabambe wa Kuendeleza Sekta ya Uvuvi na kusimamia utekelezaji wake (*Tanzania Fisheries Sector Development Master Plan*).

ii. Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya Mwaka 2003 imefanyiwa mapitio na marekebisho katika kifungu cha 8, 40, na 47 ili kuwa na adhabu zinazoendana na ukubwa wa makosa;

iii. Muswada wa "Sheria ya Mamlaka ya Kusimamia na Kuendeleza Uvuvi wa Bahari Kuu – *The Deep-Sea Fisheries Management and Development Act, 2020"* umewasilishwa kwa mara ya kwanza katika Mkutano wa 17 wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Muswada huo unategemewa kuwasilishwa kwa mara ya Pili na ya Tatu katika Mkutano wa 19 wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

iv. Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya Mwaka 2003 imefumuliwa na kuandaliwa Sheria mbili zilizotenganisha masuala ya uvuvi na Ukuzaji Viumbe Maji, na pia kuondoa kasoro zilizopo ili kukidhi mahitaji ya sasa;

v. Sheria mpya ya Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu inaandaliwa ili kuongeza wigo wa maeneo ya hifadhi hadi kwenye maji baridi;

***130. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imepokea malalamiko mengi kutoka kwa wavuvi na wadau wa mazao ya uvuvi kuhusu utekelezaji wa Kanuni ya Uvuvi ya mwaka 2009, kwa kuwa Kanuni hizo zimepitwa na wakati na kwa kuwa tafiti mpya zimefanyika pamoja na mabadiliko ya sayansi na teknolojia, Wizara imezifumua Kanuni za Uvuvi za mwaka 2009 na

kuandaa Kanuni mpya za Uvuvi za mwaka 2020. Baadhi ya mabadiliko makubwa yaliyofanyika katika Kanuni mpya ni kama ifuatavyo:

i. Kuruhusu matumizi ya taa za nguvu ya jua (*solar*) katika maeneo ya mavuvi katika Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika, Ziwa Nyasa na Bahari ya Hindi;

ii. Kuruhusu matumizi ya nyavu za makila za kuunganisha kufikia ukomo wa macho 78 katika Ziwa Victoria na macho 144 katika Ziwa Tanganyika uvuvi wa samaki aina ya Sangara na Migebuka;

iii. Kuruhusu matumizi ya *ringnet* katika uvuvi wa dagaa Ziwa Tanganyika umbali mita 1,000 kutoka mwaloni, peninsula na kisiwa;

iv. Kuruhusu nyavu za makila za ukubwa wa macho ya inchi 1.5 kwa ajili ya uvuvi wa samaki aina ya vitui na mantura katika Ziwa Nyasa;

v. Kuweka na kuzingatia kipimo kisichopungua sentimita 2 kwa samaki wabichi na sentiminta 3 kwa samaki waliokaushwa kutoka katika kipimo kilichokubalika kisheria kwa samaki aina ya Sangara;

vi. Kuruhusu misimu ya uvuvi wa samaki aina ya Kambamiti katika kipindi cha kuanzia tarehe 1 Machi hadi tarehe 30 Septemba kwa Kanda ya Kaskazini na kuanzia tarehe 1 Aprili hadi tarehe 31 Agosti ya kila mwaka kwa Kanda ya Kusini;

vii. Kuruhusu uuzwaji wa Pweza wenye uzito kuanzia gramu 440 baada ya kuchakatwa;

viii. Kuruhusu uvuvi wa Kambakoche aina ya Pakupaku (Sandy lobster) kuanzia gramu 250;

ix. Kuruhusu kuvuliwa kwa samaki jamii ya Perege wenye urefu kuanzia sentimita 20 katika Ziwa Rukwa, Ziwa Tanganyika, Ziwa Nyasa, Mabwawa ya Mtera na Nyumba ya Mungu;

x. Kuruhusu samaki wasiochakatwa (*whole fish*) waliotolewa matumbo kuuzwa katika masoko ya Kikanda na Kimataifa;

xi. Kuruhusu biashara ya mabondo chini ya urefu wa sentimita 12 au uzito wa gramu 13 kwa mabondo mabichi na urefu wa sentimita 8 au uzito wa gramu 4 kwa mabondo makavu; na

xii. Kuweka miongozo ya usimamizi wa uvuvi katika maji madogo kwenye maziwa ya Eyasi, Manyara, Kitangiri, Rukwa, Singidani, Basuto, Burigi na bwawa la Bahi na mto Kilombero.

***131. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imesikia kilio cha wavuvi na kufanya maboresho ya ada mbalimbali za leseni. Mabadiliko haya yataonekana katika muswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2020/2021. Uboreshaji wa ada za leseni na tozo za uvuvi unalenga kuhamasisha uwekezaji katika Sekta ya Uvuvi na kukuza biashara ya samaki na mazao yake.

***132. Mheshimiwa Spika,*** Wizara ipo katika hatua za mwisho kutangaza Kanuni za kutekeleza Ajenda ya Taifa ya Utafiti wa Uvuvi na Ukuzaji Viumbe Maji ili kuongeza matumizi ya tafiti katika Sekta ya Uvuvi. Aidha, Wizara imeandaa na kufanya maboresho ya Kanuni za Tozo ya Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu ambazo zinatarajiwa kuanza kutumika katika mwaka wa fedha 2020/2021.

***133. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2020/2021, Wizara itakamilisha mapitio ya Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya Mwaka 2003 na kuandaa Muswada wa Sheria mpya ya Uendelezaji Ukuzaji Viumbe Maji na Sheria ya Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu. Aidha, itasimamia utekelezaji wa maboresho ya kanuni na tozo mbalimbali yaliyofanyika. Vilevile, Wizara itakamilisha kuandaa Mpango Kabambe wa Kuendeleza Sekta ya Uvuvi na kusimamia utekelezaji wake (*Tanzania Fisheries Sector Development Master Plan*).

## 32.0 **MWENENDO WA UVUNAJI WA RASILIMALI ZA UVUVI**

***134. Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kusimamia uvunaji na matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi nchini.

Katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai, 2019 hadi mwezi Machi 2020 jumla ya tani **392,933.0** za samaki wenye thamani ya shilingi **trilioni 1.85** walivunwa ikilinganishwa na tani **389,459.40** zenye thamani ya shilingi **trilioni 1.83** zilizovunwa katika kipindi kama hiki mwaka 2018/2019 ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia **0.89**. Ongezeko hilo limechangiwa na kuimarika kwa usimamizi wa Sekta ya Uvuvi uliopelekea kuongezeka kwa wingi wa samaki katika maji asili, hususan katika Ziwa Victoria.

***135. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuratibu na kusimamia biashara ya samaki na mazao ya uvuvi nje ya nchi kwa kuzingatia viwango vya kitaifa na kimataifa. Hadi kufikia mwezi Machi 2020, tani **32,388.88** za mazao ya uvuvi na samaki hai wa mapambo **102,458** wenye thamani ya shilingi **bilioni 436.96** waliuzwa nje ya nchi na kuiingizia Serikali mrabaha wa shilingi **bilioni 19.1** (**Kiambatisho Na. 33**) ikilinganishwa na tani **38,114.72** za mazao ya uvuvi na samaki hai wa mapambo **46,098** wenye thamani ya shilingi **bilioni 491.15** waliouzwa nje ya nchi na kuliingizia Taifa mrabaha wa shilingi **bilioni 15.63** katika mwaka 2018/2019 kwa kipindi kama hicho. Hata hivyo, mauzo ya mazao ya uvuvi nje ya nchi yalifikia shilingi **bilioni 691** kuishia Juni, 2019.

***136. Mheshimiwa Spika,*** sehemu kubwa ya mazao ya uvuvi yanayosafirishwa nje ya nchi ni kutoka Ziwa Victoria ambayo yamechangia tani **30,012.91** sawa na asilimia **92.66** ya mauzo yote. Mazao ya samaki aina ya Sangara yalikuwa tani **22,714.87** sawa na asilimia **70.13** ya mauzo yote yaliyosafirishwa nje ya nchi katika Mwaka 2019/2020 (**Kiambatisho Na. 34a na 34b**). Mazao mengine kutoka Ziwa Victoria yanajumuisha Dagaa na Furu. Aidha, mauzo ya mabondo yalipungua kwa asilimia **35.6** ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2020 mauzo ya mabondo nje ya nchi yalikuwa tani **569.43** zenye thamani ya shilingi **bilioni 130.05** na kuingiza mrabaha wa shilingi **bilioni 3.93** ikilinganishwa na tani **884.30** zenye thamani ya shilingi **bilioni 178.31** zilizoingiza mrabaha wa shilingi **bilioni 2.87** mwaka 2018/2019 katika kipindi husika (**Kiambatisho Na.35**).

***137. Mheshimiwa Spika,*** kushuka kwa kiasi cha mauzo ya mazao ya uvuvi nje ya nchi yakiwemo mabondo kumetokana na kuyumba kwa soko la bidhaa hizo kunakosababishwa na sababu mbalimbali zikiwemo ushindani katika soko na kwa sehemu kubwa mlipuko ***wa*** ugonjwa wa Corona. Aidha, kutokana na kuwepo kwa mlipuko wa ugonjwa wa Corona (COVID – 19)mashirika mengi ya ndege kama vile *Kenya Airways*, *Emirates*, *Qatar Airways* na *Ethiopia Airways* yaliyokuwa yakisafirisha bidhaa hizo yamesitisha safari zake. Vilevile, ndege za mizigo zimeweka masharti ya kuwepo kwa mzigo usiopungua tani nane (8) kutoka kiwanja cha ndege Mwanza na mzigo usiopungua tani **26** kutoka uwanja wa *Julius Nyerere International Airport*. Hali hiyo imesababisha kuchelewa kwa usafirishaji wa mizigo kutoka katika viwanja vya ndege hivyo. Pia, gharama ya usafirishaji wa bidhaa hizo imepanda kutoka dola za kimarekani **2.5** hadi kufikia **3.8** kwa kilo.

***138. Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia mwezi Machi mwaka 2020, jumla ya tani **8.18** za samaki wenye thamani ya shilingi **milioni 161.01** wameingizwa nchini ikilinganishwa na tani **7,760.12** zenye thamani ya shilingi **bilioni 15.31** zilizoingizwa nchini katika kipindi kama hiki mwaka 2018/2019 (**Kiambatisho Na. 36**). Uingizaji wa samaki kutoka nje umepungua kwa asilimia **99.9** kutokana na kuimarika kwa uzalishaji na upatikanaji wa samaki katika soko la ndani.

## 33.0 **USIMAMIZI NA UDHIBITI WA RASILIMALI ZA UVUVI NA MAPAMBANO DHIDI YA UVUVI HARAMU**

***139. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, Wizara imeendelea kuimarisha Kanda Kuu tatu (3) na Vituo **30** vya Usimamizi na Udhibiti wa Rasilimali za Uvuvi nchini kwa kuvipatia vitendea kazi na watumishi ili kupambana na uvuvi na biashara haramu ya mazao ya uvuvi. Aidha, Wizara imeanzisha vituo vipya vinne (**4**) vya Bwawa la Nyumba ya Mungu, Bwawa la Mtera, Ziwa Rukwa na Rorya ili kupanua wigo wa kupambana na uvuvi na biashara haramu ya mazao ya uvuvi.

***140. Mheshimiwa Spika***, Usimamizi na udhibiti wa rasilimali za uvuvi nchini ni jukumu la kila mtanzania kwa kuzingatia Katiba ya Nchi kama ilivyoainishwa katika Ibara ya 26 na 27 na kwa mujibu wa sheria zingine za nchi. Pia, jukumu hili limeainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2015- 2020. Lengo la usimamizi na udhibiti ni kuhakikisha kuwa rasilimali za uvuvi zinakuwa endelevu kwa ajili ya kizazi kilichopo na vizazi vijavyo.

***141. Mheshimiwa Spika***, kabla ya awamu ya tano kuanza uvuvi haramu katika maji yetu ulikuwa umekithiri kwa kiwango cha kutishia uwepo wa rasilimali za uvuvi. Mnamo mwezi Desemba, 2017 Wizara yangu ilifanya tathmini ya kina kuhusu Utendaji wa Sekta ya Uvuvi na kiwango cha Uvuvi haramu katika maeneo ya mavuvi na kubaini mambo yafuatayo:

i. Kukithiri kwa uvuvi na biashara haramu ya mazao ya uvuvi katika Ziwa Victoria ambalo huchangia asilimia **64** ya mavuno ya samaki nchini. Aidha, tathmini hiyo ilibaini kuwa asilimia **96.6** ya samaki aina ya Sangara waliokuwa wanavuliwa walikuwa wachanga chini ya urefu wa sm **50**. Vilevile, samaki aina ya Sangara waliokuwa wanavuliwa ambao wanakidhi viwango kisheria walikuwa wamebaki asilimia **3** tu na samaki wazazi walikuwa wamebakia asilimia **0.4** tu;

ii. Kuongezeka kwa matumizi ya zana haramu, hususan makokoro toka **1,665** mwaka 2006 hadi kufikia makokoro **3,216** mwaka 2017 sawa na ongezeko la asilimia **93;** nyavu za timba ziliongezeka toka **4,801** mwaka 2006 hadi **19,382** mwaka 2017 sawa na ongezeko la asilimia **300;**

iii. ukithiri kwa matumizi ya milipuko katika uvuvi ukanda wa bahari na uvuvi holela katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari (EEZ) na utoroshaji wa mazao ya bahari kwenda nje ya nchi;

iv. Upotevu wa mapato yatokanayo na Biashara ya mazao ya uvuvi nje ya nchi, mfano lango la Tunduma pekee tani **7,000** zilipitishwa kuelekea katika nchi jirani za Zambia na Malawi lakini ni tani **3,000** tu ndizo zilizolipiwa ushuru na kwa upande wa mpaka wa Kagera tathmini ilionesha kuwa

takriban tani **100** zinatoroshwa kila wiki kuelekea katika nchi ya Uganda;

v. Vikundi vya Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi (BMU's) kutowajibika ipasavyo; na

vi. Ushirikiano hafifu kati ya BMUs, Serikali za Vijiji, Kata na Halmashauri Ngazi ya Wilaya.

***142. Mheshimiwa Spika***, kutokana na hali hiyo, Wizara yangu iliamua kuendesha doria na operesheni dhidi ya uvuvi haramu katika Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika, Mabwawa ya Nyumba ya Mungu na Mtera na Bahari ya Hindi. Operesheni hizo zimedumu kwa kipindi chote cha miaka mitatu (2017/2018 hadi 2019/2020). Operesheni hizo ni pamoja na:

i. Operesheni Sangara 2018 iliyofanyika Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika na Mabwawa ya Nyumba ya Mungu na Mtera;

ii. Operesheni MATT iliyofanyika katika Mwambao wa Bahari ya Hindi; na

iii. Operesheni Jodari iliyofanyika katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari (EEZ).

***143. Mheshimiwa Spika,*** matokeo ya mapambano dhidi ya uhalifu huo kwa kipindi cha miaka mitatu (2017/2018, 2018/2019 na 2019/2020 ) ni pamoja na kukamatwa nyavu haramu za makila 1,162,555; makokoro 17,924; nyavu za timba 69,437; nyavu za dagaa 13,224; kamba za kokoro zenye urefu wa mita 1,893,097; ndoano 4,652,697; nyavu za *ringnet* 1,375; nyavu za tembea 6,953; samaki wachanga kilo 423,882; Kaa hai wachanga kilo 5,676; mabomu vipande 4,583; *detonator* 2,534; mbolea ya urea kilo 626; na watuhumiwa 14,384. Aidha, vifaa vingine vilivyokamatwa ni pamoja na injini za boti 2,404; magari 7,240; pikipiki 704; mitungi ya gesi 624 (Kiambatisho Na. 37).

***144. Mheshimiwa Spika,*** kwa kipindi hicho chote cha miaka mitatu mfululizo (2017/2018 hadi mwezi Machi, 2020), Wizara

imefanikiwa kudhibiti uvuvi na biashara haramu ya mazao ya uvuvi kwa asilimia zaidi ya **80** katika maji baridi na asilimia **100** kwa uvuvi wa kutumia mabomu kwa ukanda wa pwani ya bahari yetu.

***145. Mheshimiwa Spika,*** kufuatia operesheni JODARI iliyofanyika mwezi Januari hadi Februari, 2018 kwa kushirikisha Kikosi kazi cha Taifa cha Kuzuia na Kupambana na Uharibifu wa Mazingira (*National Multi-Agency Task Team - NMATT*), meli ya Buah Naga 1 ilikamatwa ikiwa na mapezi ya papa bila miili ambapo Mahakama Kuu Kanda ya Mtwara iliwahukumu mmiliki, nahodha na wakala kifungo cha miaka 20 au kulipa faini ya shilingi bilioni 1. Watuhumiwa hao walishindwa kulipa faini hiyo na wanatumikia kifungo. Aidha, meli ishirini (**20**) (**Kiambatisho Na. 39**) zenye kupeperusha bendera ya China zilikimbia bila kuhakikiwa mavuno (catch verification) na kushusha samaki wasiolengwa (*by-catch*) kabla ya kuondoka katika maji ya Tanzania kinyume na Kanuni za Uvuvi wa Bahari Kuu ya 10(1)(a) na 10(1)(c) ya Mwaka 2009 na marekebisho yake ya Mwaka 2016.

***146. Mheshimiwa Spika***, hatua mbalimbali zimefanyika kuhakikisha kuwa wamiliki wa meli hizo wanalipa faini, ikiwa ni pamoja na kuwaandikia barua wakala na wamiliki wa meli hizo kuwataka kukubali makosa na kulipa faini kwa mujibu wa sheria za Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu, kuwasilisha shauri hili katika Kamisheni ya Jodari ya Bahari ya Hindi (IOTC), na kufanya mazungumzo kati ya Ujumbe wa Tanzania na China kwenye IOTC mjini Hyderabad, India mwezi Juni 2019. Katika mazungumzo hayo ilikubalika kuwa kila upande ufanyie kazi makubaliano yaliyofikiwa kwa kuzishirikisha Serikali kwa hatua zaidi. Wizara ya Mifugo na Uvuvi kupitia Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu tayari imefanya mawasiliano na Kiongozi wa Ujumbe wa China - IOTC ili kujua msimamo wa serikali ya China wa kuwataka wamiliki wa meli hizo kulipa faini ili ya jumla ya **shilingi bilioni 20** ili kulimaliza suala hilo kabla ya Mkutano wa IOTC unaotarajiwa kufanyika mwezi Novemba, 2020.

***147. Mheshimiwa Spika,*** mapambano hayo yameleta mafanikio makubwa katika Sekta ya uvuvi na Taifa kwa ujumla. Mafanikio yaliyopatikana ni kama ifuatavyo:-

i. Kuimarika kwa usimamizi na udhibiti wa rasilimali za uvuvi nchini, uvunaji wa rasilimali za uvuvi na hivyo kusababisha samaki kuongezeka kutoka tani **387,543** waliovuliwa mwaka 2017/2018 na kufikia tani **448,467** mwaka 2019/2020.

ii. Kuongezeka kwa wingi wa samaki aina ya Sangara kutoka tani **417,936** mwaka 2016 hadi kufikia tani **553,770** mwaka 2018 na tani **816,964** mwaka 2019, ikiwa ni ongezeko la asilimia **47.5**. Aidha, dagaa waliongezeka kutoka tani **660,333** mwaka 2018 kwa ziwa lote hadi kufikia tani **936,247** mwaka 2019 ikiwa ni ongezeko la asilimia **41.8** na kwa upande wa Tanzania dagaa waliongezeka kutoka tani **340,422** mwaka 2018 hadi tani **512,840** mwaka 2019.

iii. upungua kwa samaki wachanga aina ya Sangara wenye urefu wa chini ya sentimita **50** kutoka asilimia **96.6** mwaka 2017 hadi kufikia asilimia **62.8** mwaka 2018;

iv. Kuongezeka kwa samaki aina ya Sangara wenye urefu wa kuanzia sentimita **50** hadi **85** kutoka asilimia **3.3** mwaka 2017 hadi kufikia asilimia **32.0** mwaka 2018;

v. Kuongezeka kwa samaki aina ya Sangara wenye urefu wa juu ya sentimenta **85** kutoka asilimia **0.4** mwaka 2017 hadi kufikia asilimia **5.2** mwaka 2018;

vi. Kuongezeka kwa wastani wa urefu wa Sangara kutoka sentimeta **16** mwaka 2017 hadi kufikia sentimeta **25.2** mwaka 2018; na

vii. Kupungua kwa uingizaji wa samaki kutoka nje ya nchi kutoka thamani ya shilingi bilioni **56** mwaka 2016/2017 hadi shilingi milioni **161.01** Machi, 2020 sawa na upungufu wa asilimia **99.7**. Hivyo, kusaidia kupunguza matumizi ya fedha za nje katika mwaka 2019/2020;

viii. uongezeka kwa upatikanaji wa samaki uliosababisha kushuka kwa bei ya mazao ya uvuvi katika soko la ndani toka wastani wa shilingi **9,000** kwa kilo ya samaki aina ya Sangara mwaka 2017/2018 hadi shilingi **4,500** mwaka 2019/2020. Vilevile, bei ya samaki aina ya Sato imeshuka kutoka wastani wa shilingi **9,500** mwaka hadi shilingi **7,500** mwaka 2019/2020.

***148. Mheshimiwa Spika,*** Aidha, kuimarika kwa uzalishaji wa mazao ya uvuvi, kumewahamasisha wadau wa sekta kuanzisha viwanda vya kuchakata samaki hapa nchini, katika ukanda wa Ziwa Victoria ambako kuna viwanda tisa (**9)** vinavyofanya kazi, viwanda vipya vinne (**4**) viko kwenye hatua ya ujenzi, kuongezeka kwa maghala ya ugandishaji/ kuhifadhia (*Cold rooms*) samaki na mazao ya uvuvi kutoka nane (**8)** mwaka 2017/2018 hadi **90** mwaka 2019/2020. Maghala hayo kwa sasa yanauwezo wa kuhifadhi wastani wa tani **350** kwa siku.

***149. Mheshimiwa Spika,*** mafanikio mengine yaliyopatikana ni kuimarika kwa ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali ambapo hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2019 jumla ya Shilingi Bilioni **33.796** zimekusanywa sawa na asilimia **156.94** ya lengo la kukusanya Shilingi **bilioni 21.534.** Vilevile, mauzo ya samaki nje ya nchi yameongezeka kutoka wastani wa shilingi **bilioni 379** kwa miaka miwili iliyopita na kufikia shilingi **bilioni 691.88** katika mwaka wa fedha 2018/2019 kiasi ambacho hakijafikiwa katika kipindi chochote kile.

***150. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2019/2020 pekee, Wizara imeendesha operesheni maalum na doria zenye sikukazi **7,472** kwenye maji, nchi kavu na maeneo ya mipakani ambapo zana haramu mbalimbali zilikamatwa zikiwemo; nyavu za makila **166,177**, makokoro **808**, nyavu za timba **31,671**, nyavu za dagaa **547**, kamba za kokoro zenye urefu wa mita **149,071**, ndoano **12,000**, mitumbwi **736**, boti **56**, nyavu za *ring net* **204**, vyandarua **22**, katuli **10**, injini za boti **275** na kasia **8**. Pia, magari **8**, pikipiki **36**, baiskeli **6**, samaki wachanga kilo **28,450**, kaa hai wachanga kilo **30**, kambakoche hai wachanga kilo **46**, simbi kilo **22,000**, pamoja

na watuhumiwa **2,040** walikamatwa na kufunguliwa kesi mahakamani na wengine kutozwa faini.

***151. Mheshimiwa Spika**,* Wizara kwa kushirikiana na Kikosi Kazi cha Kitaifa cha Kudhibiti Uhalifu wa Mazingira (*National Mult-Agency Task Team* - NMATT) imeendesha operesheni nne (**4**) ambapo (**3**) zilifanyika katika Ukanda wa Pwani na (1) katika Ukanda wa Ziwa Victoria. Aidha, jumla ya raia wa kigeni **25** walikamatwa katika Ukanda wa Ziwa Victoria. Pia, zana haramu mbalimbali zikiwemo; makokoro **105**, nyavu za makila **8,445**, nyavu za timba **201**, kamba za kokoro zenye urefu wa mita ***20,705***, nyavu za *ring net* **55**, mitumbwi **30**, magari **5**, mitungi ya gesi **20** na watuhumiwa **101** walikamatwa**.**

***152. Mheshimiwa Spika*,** nyavu haramu zilizokamatwa wakati wa doria na operesheni hizo ziliteketezwa kwa idhini ya Mahakama. Samaki wachanga waliokamatwa waligawiwa katika Taasisi za umma zikiwemo shule za Sekondari na kwenye vituo vya kulelea watoto na watu wenye mahitaji maalum (**Kiambatisho Na. 38)**. Pia, vifaa mbalimbali vilivyokamatwa vikiwemo magari manne (***4***), baiskeli sita (**6**), pikipiki (**36**), injini (**275**), maboti (**56**) na mitumbwi (**680**) vilikabidhiwa kwa wahusika baada ya kukidhi matakwa ya kisheria.

***153. Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2019/2020, utafiti wa kuangalia wingi na mtawanyiko wa samaki kwa kutumia njia ya mwangwi (*Acoustic Survey*) katika Ziwa Victoria ulifanyika, ambapo matokeo yanaonyesha kuwa samaki aina ya dagaa waliongezeka kutoka tani **660,333** mwaka 2018 kwa ziwa lote hadi kufikia tani **936,247** mwaka 2019 ikiwa ni ongezeko la asilimia **41.8** na kwa upande wa Tanzania dagaa waliongezeka kutoka tani **340,422** mwaka 2018 hadi tani **512,840** mwaka 2019. Aidha, samaki aina ya Sangara wameongezeka kutoka tani **553,770** mwaka 2018 hadi tani **816,694** kwa ziwa lote, mwaka 2019 ikiwa ni ongezeko la asilimia **47.5**. Kwa upande wa Tanzania, Sangara waliongezeka kutoka tani **301,460** mwaka 2018 hadi tani **422,076** mwaka 2019. Kuongezeka kwa wingi wa Sangara

kunatokana na juhudi za Serikali katika kupiga vita uvuvi haramu.

***154. Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2020/2021, Wizara kwa kushirikiana na wadau, itaendelea kuimarisha shughuli za usimamizi na ulinzi wa rasilimali za uvuvi kwa kufanya doria za kawaida zenye siku kazi **7,800**. Aidha, Wizara itafanya Operesheni Maalum kila robo mwaka na kuiwezesha NMATT kutekeleza majukumu yake kwa kufanya operesheni maalum **10**. Vilevile, Wizara itaimarisha vituo tisa (**9**) katika Ukanda wa Ziwa Victoria; Bahari ya Hindi na Mashariki; na Nyanda za Juu Kusini. Pia, itaendelea kufanya kaguzi kwenye maeneo ya bandari, mipakani, vizuizi, masoko na mialo ya kupokelea samaki.

## 34.0 **HIFADHI ZA BAHARI NA MAENEO TENGEFU**

***155. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2019/2020, Wizara kupitia Kitengo cha Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu (MPRU) iliendelea kulinda na kusimamia maeneo yaliyohifadhiwa katika Bahari ya Hindi ambayo ni Hifadhi za Bahari tatu (**3**) na Maeneo Tengefu (**15)** kwa kufanya jumla ya doria zenye sikukazi **797** hadi kufikia Machi, 2020 ikilinganishwa na doria zenye sikukazi **677** kwa kipindi kama hicho Machi 2019. Matokeo ya doria hizo ni kukamatwa kwa kilo **83** za makome, vipande **108** vya nyavu haramu, michinji **2** na fito **10** za mikoko iliyovunwa kinyume na sheria.

***156. Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia MPRU iliendelea kutoa gawio la maduhuli kwa Halmashauri na Vijiji vilivyomo ndani ya maeneo ya Hifadhi ambazo maduhuli hukusanywa. Katika mwaka 2019/2020, jumla ya **shilingi 232,968,726** zilitengwa na kutolewa kwa ajili ya kugharamia shughuli za uhifadhi na miradi ya maendeleo katika vijiji vilivyomo ndani ya Hifadhi ya Kisiwa cha Mafia.

***157. Mheshimiwa Spika***, hadi kufikia mwezi Machi, 2020 jumla ya wageni **30,412** walitembelea maeneo ya Hifadhi za Bahari ikilinganishwa na wageni **46,304** kwa mwaka 2018/2019. Kupungua kwa idadi ya watalii katika maeneo ya hifadhi

kumetokana na mlipuko wa ugonjwa wa *COVID 19* unaosababishwa na virusi vya *Corona (COVID – 19)*ambao umesababisha kusitishwa kwa safari za ndege za kimataifa na hivyo kuzuia kuja kwa watalii kutoka nje ya nchi.

***158. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2020/2021, Wizara kupitia MPRU itaendelea kulinda, kutunza na kusimamia mifumo ikolojia katika maeneo yaliyohifadhiwa kwa kufanya doria za sikukazi **800.** Aidha, MPRU itaendelea kutekeleza Mkakati wa Kujitangaza na Kuongeza Mapato kwa kutangaza maeneo yaliyohifadhiwa ikiwa pamoja na vivutio vya utalii vilivyomo. Vilevile, MPRU itaboresha miundombinu katika maeneo ya utalii wa kiikolojia (*eco tourism)* ili kuvutia watalii kutoka ndani na nje ya nchi na hivyo kuongeza mapato.

35.0 **UVUVI KATIKA BAHARI KUU**

***159. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020 juhudi za kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli kutokana na uvuvi wa Bahari Kuu zilifanyika ikiwa ni pamoja na Serikali kuondoa tozo ya Dola za Kimarekani **0.4** kwa kilo ya samaki wanaolengwa kutoka Bahari Kuu kwa kipindi cha mwaka mmoja kuanzia mwezi Novemba 2019 hadi Novemba 2020 kama ilivyoainishwa kwenye Tangazo la Serikali Na. **883** la mwaka 2019. Baada ya Serikali kuondoa tozo hiyo mashirika ya meli kutoka nchi za Ufaransa, Uhispania na Ushelisheli zilileta maombi ya leseni za uvuvi ili kufanya uvuvi katika Bahari Kuu. Hata hivyo, baada ya kutokea kwa mlipuko wa ugonjwa wa COVID 19 mashirika hayo yametoa taarifa za kusitisha nia hiyo. Aidha, Mamlaka imefanikiwa kutoa leseni za uvuvi wa Bahari Kuu kwa meli (2) zenye bendera ya Tanzania (AL-MAIDA na SEHEWA 02) na kuiingizia Mamlaka kiasi cha **Shilingi 31,920,817** zilizotokana na ada ya leseni. Vilevile, doria za anga zenye jumla ya masaa **72** zilifanyika na kuonesha kuwa hakukuwa na meli zenye kuvua katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari (EEZ) nchini kinyume cha Sheria.

***160. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, Mamlaka inafanya tafiti tatu za *Analysis of Tuna and Tuna like species,*

*Stock Structure and Genetic connectivity* na *Study on Oceanographic Factors influencing spatial distribution of Tuna and Tuna like species in Tanzania waters* katika EEZ zenye lengo la kutoa uelewa juu ya rasilimali inayopatikana na kuwezesha usimamizi endelevu. Vilevile, Mamlaka kupitia Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI) inafanya tafiti za kutambua maeneo yenye samaki wengi katika EEZ na maji ya Kitaifa nchini katika pwani ya Tanga, Wete, Nungwi, Mkinga, Pangani, Bagamoyo, Kinondoni, Mkuranga, Rufiji, Kibiti, Kilwa, Lindi, na Mtwara.

***161. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, Mamlaka imeendelea kuboresha Mfumo wa Takwimu za Uvuvi kwa kuongeza *moduli* tatu (3) za Ukaguzi wa Meli, Doria za majini, Dashboard na kuunganishwa na Mfumo wa kufuatilia mienendo ya meli (*Vessel Monitoring System* - VMS). Vilevile, Mamlaka imekamilisha mfumo wa malipo kwa njia za kielektroniki ambapo waombaji wa leseni za uvuvi watafanya malipo kwa njia ya mtandao (*online)*, malipo kwa njia ya *QR Code* na kwa njia ya kuhamisha kutoka Benki yoyote duniani. Kwa kutumia mfumo huu mapato yote yataonekana katika mfumo Mkuu wa Serikali wa kukusanya mapato (GePG) hivyo kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato.

***162. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/2021, Mamlaka itafanya tafiti nyingine tatu zenye lengo la kutoa uelewa juu ya rasilimali inayopatikana na kuwezesha usimamizi endelevu katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari. Tafiti hizo ni: *Tuna Biology*, *Economic profile* na *Pole and line fishery.* Vilevile, Mamlaka kwa kushirikiana na TAFIRI itaendelea kufanya tafiti za kutambua maeneo yenye samaki wengi katika EEZ na maji ya Kitaifa (*Potential Fishing Zones*).

***163. Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka itaendelea kusimamia ulinzi wa rasilimali za uvuvi Bahari Kuu kwa kuendesha doria za anga na majini na kuboresha Mfumo VMS. Aidha, Mamlaka itaandaa Mkakati wa kuongeza uwekezaji kwa kutoa vivutio mbalimbali kwa wawekezaji wazawa ikiwa pamoja na kuwaunganisha na masoko ya nje kwa ajili ya kuuza bidhaa zao. Vilevile, Mamlaka itandaa Mpango Biashara (*Business*

*Plan*) utakaosaidia kuongeza mapato na kuiwezesha Mamlaka kuweza kujiendesha.

36.0 **SHIRIKA LA UVUVI TANZANIA – TAFICO**

***164. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2019/2020 Serikali inaendelea na Mkakati wa kufufua Shirika la Uvuvi Tanzania (*Tanzania Fisheries Corporation-TAFICO*) ili kuiwezesha Nchi kunufaika na rasilimali za uvuvi, hususan zile zilizopo katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari na Bahari Kuu. Pamoja na mambo mengine Wizara imeendelea kuweka mipaka na alama zinazoonekana na kufanya ukarabati wa mali zilizofanyiwa tathmini yenye thamani ya **shilingi bilioni 118.**

***165. Mheshimiwa Spika***, Serikali imeandaa Mpango Biashara wa Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO *Business Plan*). Lengo la Mpango huu ni kutoa mwelekeo wa kibiashara wa Shirika kwa kipindi cha miaka 10 ambapo utafanyika kupitia Serikali na Sekta Binafsi kwa njia ya ubia. Mpango huu umeainisha miradi mikubwa mitatu kama ifuatavyo:

i. Mradiwa uvuvi utakaojumuisha Meli ya Uvuvi wa Mishipi (*Longliner*), Meli ya Uvuvi Wavu wa Kuzungusha (*Purse Seiner*), na Meli ya Uvuvi wa Maji ya Ndani (*Territorial Waters Fishing Vessel*);

ii. Mradi wa Kuchakata samaki utakaojumuisha Kiwanda cha Kuchakata samaki (*Fish Processing Plant*), Kiwanda cha Kuzalisha Barafu (*Ice Making Plant*) na Ghala la Ubaridi la Kuhifadhia Samaki (*Cold Storage Facility*); na

*iii.* Mradi wa Ukuzaji Viumbe Maji (*Aquaculture*) utakaojumuisha Ufugaji Samaki kwenye Vizimba (*Cage Fish Farming*) katika Ziwa Victoria na Bahari ya Hindi, Ufugaji Samaki kwenye Mabwawa (Pond Fish Farming), Vitotoleshi vya Kuzalishia Vifaranga vya Samaki (*Fish Hatchery*) na Kiwanda cha Vyakula vya Samaki (*Fish Feed Plant).*

***166. Mheshimiwa Spika***, Miradi hiyo mitatu (3) itatekelezwa kupitia miradi midogo kumi yenye thamani ya jumla ya **Shilingi**

**89,282,057,278.00.** Miradi hiyo inatarajiwa kuanza kutekelezwa mwanzoni mwa mwaka 2020/2021 **(Kiambatisho Na. 40).**

***167. Mheshimiwa Spika***, katika mikakati ya kuiwezesha TAFICO, Serikali kupitia Programu ya Maendeleo ya Uchumi na Jamii - Japan (*The Economic and Social Development Programme*) imepata msaada wa **shilingi bilioni 4.2** kwa ajili kutekeleza miradi mbalimbali ambapo tayari hatua za ununuzi zimeanza kama ifuatavyo:

i. Ujenzi wa meli yenye urefu wa mita 20 itakayovua katika maji ya kitaifa;

ii. Usimikaji wa mtambo wa kuzalisha barafu;

iii. Ujenzi wa ghala la baridi la kuhifadhia samaki (*Cold room*);

iv. Ukarabati wa karakana ya uhandisi; na

v. Ununuzi wa gari maalum la kusambazia samaki na barafu (*Refrigerated Truck*).

***168. Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea na Mazungumzo na Mfuko wa Maendekeo ya Kilimo Duniani (IFAD) ili kuweza kupata kiasi cha **Shilingi Bilioni 68.8** kwa ajili ya kununua meli mbili (2) za *longlinner* na *purse seiner* zitakazogharimu kiasi cha **shilingi bilioni 55.9** ili kuliwezesha Shirika la TAFICO kuvua katika Bahari Kuu. Aidha, **shilingi Bilioni 12.9** zitatumika kuwezesha mradi wa ufugaji viumbe maji. Vilevile, katika vikao vilivyofanyika tarehe 24 Februari hadi 7 Machi 2020 kati ya wajumbe kutoka IFAD na Serikali waliweka ratiba ya utekelezaji na kukubaliana kuanza utekelezaji wa mradi huo mwezi Januari, 2021 (**Kiambatisho Na. 41)**.

***169. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/2021 Serikali itanunua Meli tatu (**3)** za Uvuvi na kuanza uvuvi wa Bahari Kuu na maeneo mengine; kujenga na kuendesha viwanda vya kuchakata mazao ya uvuvi; kuendelea na ukarabati wa majengo na miundombinu ya TAFICO itakayojumuisha gati la kuegeshea Meli za Uvuvi, kusimika mitambo ya barafu,

maghala ya baridi pamoja na kuiwezesha TAFICO kuanza miradi ya ukuzaji viumbe maji.

## 37.0 UJENZI WA BANDARI YA UVUVI

***170. Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa Bandari ya Uvuvi kupitia Mtaalam Mwelekezi ambaye ni Kampuni ya M/S Sering Ingegneria ya Nchini Italia kwa gharama ya **shilingi 1,421,041,703.08.** Hadi sasa Mtaalam Mwelekezi amewasilisha Ripoti (***Interim Report***) ya kina ya ukusanyaji wa taarifa muhimu za maeneo yanayofaa kwa ajili ya ujenzi wa Bandari ya Uvuvi. Katika hatua ya ukusanyaji wa taarifa muhimu jumla ya maeneo kumi na moja (**11**) ya Mbegani-Bagamoyo, Ras Buyuni, Shangani-Mtwara, Bandari ya Lindi, Rushungi, Kilwa Masoko, Kilwa Kivinje, Moa-Tanga, Bandari ya Tanga, Mwambani-Tanga na Pangani yalifanyiwa tathmini kwa kuzingatia vigezo vya kimazingira/ikolojia.

***171. Mheshimiwa Spika,*** Baadhi ya vigezo hivyo ni uwepo wa miundombinu wezeshi kama vile barabara, upatikanaji wa eneo la kutosha, eneo kutokuwa kwenye hatari za athari za kimazingira (*exposure to extreme conditions*); matumizi ya ardhi kwenye eneo husika (*Land use*); na hali ya ikolojia ya pwani (*coastal ecology*). Aidha, vigezo vingine vilivyozingatiwa ni pamoja na ukaribu wa eneo kwenye kina kirefu cha maji; hitaji la kuwa na kinga maji (*breakwater*), kiasi cha mtaji na gharama za matengenezo; na hitaji la kuchimba ili kuongeza kina cha maji (dredging). Kwa kuzingatia vigezo hivyo, maeneo matatu (**3**) ya Mbegani-Bagamoyo, Kilwa Masoko na Bandari ya Lindi yamependekezwa. Kutokana na kazi hiyo Serikali imemlipa Mtaalam Mwelekezi asilimia **50** sawa na **shilingi 710,520,896.54** kulingana na Mkataba uliosainiwa.

***172. Mheshimiwa Spika,*** ili kuendelea na hatua inayofuata, Serikali inakamilisha taratibu za kuchagua eneo moja kati ya matatu yaliyopendekezwa. Aidha, baada ya Serikali kufanya uamuzi wa eneo linalofaa kujenga Bandari ya Uvuvi Mtaalam Mwelekezi atafanya upembuzi wa kina

(***bathymetric, topographic and geotechnical survey***) na kisha kuandaa michoro, kuainisha gharama za ujenzi na kuwasilisha taarifa ya mwisho (*Final Report*). Baada ya kuwasilisha taarifa ya mwisho Mtaalam Mwelekezi atalipwa sehemu ya mwisho ya malipo ya asilimia 50 sawa na **shilingi 710,520,896.54** kulingana na mkataba uliosainiwa.

***173. Mheshimiwa Spika,*** katika juhudi za kuwezesha ujenzi wa bandari ya uvuvi, mazungumzo yanaendelea baina ya Serikali ya Tanzania na Korea ya Kusini kwa ajili ya kupata ufadhili wa Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi katika eneo litakalopendekezwa. Aidha, Randama ya Makubaliano (Mou) kati ya nchi hizi mbili umeandaliwa na taratibu za kuusaini zinaendelea.

***174. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/2021, Serikali itakamilisha upembuzi wa kina na kuanza ujenzi wa Bandari ya Uvuvi katika eneo litakalochaguliwa. Aidha, uwepo wa Bandari ya Uvuvi utawezesha meli za uvuvi zinazovua katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari ya Tanzania na Bahari Kuu kutia nanga, kushusha mazao ya uvuvi na kupata huduma mbalimbali zikiwemo mafuta na chakula. Aidha, kuwepo kwa Bandari ya Uvuvi kutawezesha ukuaji wa biashara ya mazao ya uvuvi, kuongeza ajira, kuchochea uwekezaji na ujenzi wa viwanda, kuongeza fedha za kigeni, kuongeza mchango wa Sekta ya Uvuvi katika Pato la Taifa na hivyo kuiwezesha nchi kunufaika kikamilifu na rasilimali za uvuvi.

### 38.0 **UKUZAJI VIUMBE MAJI**

***175. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020 Wizara imeendelea kuimarisha vituo vinne (**4**) vya Kuendeleza Ukuzaji Viumbe Maji vya Kingolwira - Morogoro, Mwamapuli – Tabora, Ruhila – Ruvuma na Nyengedi – Lindi ili kuongeza uzalishaji wa samaki kwa kufanya yafuatayo:

i. Kununua samaki wazazi 27,640 na kuwagawanya katika vituo;

ii. Kusimika happa net 60 kwa ajili ya kutunzia samaki wazazi; na

iii. Kununua matanki 22 kwa ajili ya kulelea vifaranga na kukarabati mabwawa nane (8).

***176. Mheshimiwa Spika,*** maboresho hayo yamesababisha kuongezeka kwa uzalishaji vifaranga kufikia **4,146,840** kutoka vifaranga **478,300** vilivyozalishwa kutoka katika vituo vya wizara, Taasisi zilizo chini ya Wizara na Taasisi zingine za Serikali katika mwaka 2018/2019 (**Kiambatisho Na. 29)**. Aidha, vifaranga **1,500** vimepandikizwa katika bwawa linalomilikiwa na wananchi katika Wilaya ya Msalala ili kuongeza upatikanaji wa samaki katika maeneo hayo.

***177. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imefanya kaguzi mbili (**2**) zenye sikukazi **88** katika vitotoleshi, mashamba ya ufugaji wa samaki na viwanda vya kutengeneza vyakula vya samaki katika mikoa **11** nchini. Aidha, kaguzi nyingine mbili (**2**) zenye sikukazi **10** zimefanyika katika shamba la ufugaji wa kambamiti la *Alphakrust Limited* lililopo Mafia. Kaguzi hizo zilionesha kuwa wadau wa ukuzaji viumbe maji walio wengi wanafuata sheria na kanuni zilizopo.

***178. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, Wizara imeandaa miongozo saba (**7**) kuhusu: Uzalishaji Vifaranga vya Samaki; Uzalishaji Vyakula vya Samaki na Ulishaji; Ufugaji Samaki kwenye Vizimba; Ukulima wa Mwani; Ufugaji Samaki kwenye Mabwawa; Ufugaji wa Kaa na Udhibiti wa Magonjwa ya Samaki.

***179. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, Wizara imeendelea kuhamasisha jamii kuwekeza katika ukuzaji viumbe maji kwa kutoa elimu. Jumla ya wadau **7,072** walipata elimu ya mbinu bora za ufugaji wa samaki na kilimo cha mwani kupitia maonesho ya Nane Nane **(2,876),** Siku ya Chakula Duniani **(231)** na katika vituo vya Kuendeleza Ukuzaji Viumbe Maji **(3,965)** ikilinganishwa na wadau **6,695** waliopatiwa elimu kwa mwaka 2018/2019. Aidha, Wizara imeandaa na kusambaza vipeperushi **7,300** kuhusu kanuni bora za ukuzaji viumbe maji.

***180. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji katika tasnia ya Ukuzaji Viumbe Maji. Katika mwaka 2019/2020, kumekuwa na ongezeko la vizimba **23** vya kufugia samaki na kufanya idadi ya vizimba kufikia **431** ikilinganishwa na vizimba **408** vilivyokuwepo mwaka 2018/2019. Mtawanyiko wa vizimba hivyo ni: Ziwa Victoria **(370)**, Ziwa Tanganyika **(9)** na katika malambo mbalimbali nchini **(52).**

***181. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/2021, Wizara itakarabati na kujenga vituo sita **(6)** vya kuzalisha vifaranga vya samaki na kuendeleza ukuzaji viumbe maji katika maeneo ya Mwamapuli-Tabora, Ruhila-Ruvuma, Kingolwira-Morogoro, Nyengedi-Lindi, Machui-Tanga, na Rubambagwe-Geita. Aidha, vituo hivi vitazalisha vifaranga **milioni 8** na **tani 60** za samaki na pia vitakuwa mashamba darasa kwa ajili ya kutoa elimu ya ufugaji bora wa samaki. Vilevile, vitotoleshi vya sekta binafsi vitahamasishwa kuzalisha vifaranga **milioni 22** na hivyo kufikia jumla ya vifaranga **milioni 30** kwa mwaka kutoka wastani wa uzalishaji wa sasa ambao ni vifaranga milioni **22** kwa mwaka.

***182. Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea kusimamia na kuendeleza matumizi ya teknolojia mpya za kuongeza thamani katika mazao ya viumbe maji bahari hususani mwani kwa mikoa ya Lindi, Mtwara, Pwani na Tanga pamoja na kuanzisha kituo kimoja **(1)** cha Ukuzaji Viumbe Maji bahari katika ukanda wa Pwani.

***183. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuhamasisha uzalishaji wa chakula cha samaki nchini kupitia sekta binafsi ambapo tani **58.45** zenye thamani ya shilingi **175,350,000** zimezalishwa na viwanda **12** vilivyopo nchini**.** Aidha, tani **276.7** za chakula cha samaki zenye thamani ya shilingi **1,125,062,200** zimeingizwa nchini.

***184. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/2021 Wizara itaendelea kusimamia na kutoa ushauri katika vitotoleshi **21** vya sekta binafsi na mashamba **100** ya ukuzaji viumbe maji katika mikoa ya Ruvuma, Kigoma, Mwanza, Mbeya, Katavi

na Pwani. Pia, Wizara itaendelea kutoa mafunzo ya mbinu bora za ukuzaji viumbe maji na kuhamasisha uwekezaji. Aidha, Wizara itapandikiza vifaranga vya samaki katika malambo **12** yaliyoko kwenye mikoa ya Rukwa, Arusha, Mtwara, Ruvuma, Kilimanjaro, Simiyu, Dodoma, Kagera, Njombe, Shinyanga na Tabora.

***185. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/2021 Wizara itaendelea kufanya kaguzi zenye sikukazi **200** katika viwanda vya kutengeneza vyakula vya samaki, vitotoleshi vya vifaranga vya samaki, na mashamba ya ufugaji samaki katika mikoa **11** nchini (Mwanza, Mara, Geita, Morogoro, Mbeya, Pwani, Dar es Salaam, Ruvuma, Kilimanjaro, Arusha na Kagera). Aidha, Wizara itaanzisha mashamba darasa manne (**4**) katika Halmashauri za Wilaya za Njombe, Mwanga, Meatu, na Mkuranga.

## 39.0 UTHIBITI WA UBORA NA USALAMA WA MAZAO YA UVUVI

***186. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, Wizara imeendelea kuthibiti ubora na usalama wa samaki na mazao yake kwa kufanya kaguzi katika mialo, masoko, viwanda na maghala ya kuhifadhia samaki na mazao yake ili kuchochea biashara ndani na nje ya nchi. Aidha viwanda **12** vya wachakataji wakubwa na viwanda vinne (**4**) vya wachakataji wa kati vimefanyiwa ukaguzi na kukidhi viwango vya ubora na usalama wa kuchakata mazao ya uvuvi kwa ajili ya soko la Kikanda, Kimataifa likiwepo Soko la nchi za Jumuiya ya Ulaya **(Kiambatisho Na. 42).** Aidha, viwanda vidogo **33** vya uchakataji, maghala **39** ya kuhifadhi samaki wakavu na maghala **34** ya kupokelea samaki hai yamefanyiwa ukaguzi na kukidhi viwango vya ubora na usalama. Pia, jumla ya kaguzi **7,520** za mazao ya uvuvi zilifanyika katika viwanda, maeneo ya mipakani, viwanja vya ndege na bandarini.

***187. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa imefanya kaguzi za kawaida **264** katika maeneo ya wachakataji wadogo na vyombo **862** vya usafirishaji wa mazao ya uvuvi. Pia, kaguzi **158** zimefanyika

katika mialo ya Ukanda wa Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika na Pwani ya Bahari ya Hindi.

***188. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020 Wizara kupitia Maabara za Nyegezi-Mwanza na Dar es Salaam imefanya uhakiki wa ubora na usalama wa mazao ya uvuvi kwa kufanyia uchunguzi sampuli **2,848** za minofu ya samaki, dagaa, maji na udongo ili kubaini uwepo wa vimelea, kemikali na madini tembo. Matokeo ya chunguzi hizo yalibaini kuwa mazao hayo yamekidhi viwango vya usalama na ubora kwa ajili ya matumizi ya binadamu na wanyama.

***189. Mheshimiwa Spika,*** Maabara Nyegezi-Mwanza imeendelea kupata hati ya umahiri katika kiwango cha ISO/ IEC 17025:2017 kutoka Taasisi ya Ithibati ya Nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika-SADC (SADCAS). Aidha, idadi ya wataalam wa Maabara walioidhinishwa na kutambuliwa kimataifa wameongezeka kutoka **7** mwaka 2018/2019 hadi **11** mwaka 2019/2020.

***190. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2020/2021, Wizara itafanya kaguzi za kina **120** katika viwanda na kaguzi za kawaida **1,500** katika mialo, masoko, maghala, na vyombo vya usafirishaji mazao ya uvuvi; Wizara itahakiki usalama na ubora wa samaki na mazao yake kabla ya kusafirishwa ndani na nje ya nchi kwa kufanya kaguzi **8,080**. Pia, Wizara itatoa mafunzo kwa wadau **100** kuhusu teknolojia za kisasa, ufungashaji na uwekaji lebo unaozingatia uhifadhi wa mazingira, miundombinu inayohusika na upokeaji na uchakataji, utangazaji masoko na usafirishaji wa samaki na mazao ya uvuvi.

***191. Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa kukarabati mialo **20** katika Ukanda wa Ziwa Victoria (**11**), Ukanda wa Pwani (**4**), Ziwa Tanganyika (**2**), Ziwa Nyasa (**2**) na Bwawa la Nyumba ya Mungu (**1**). Pia, Wizara itafanya ukarabati wa masoko ya samaki **15** katika mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Iringa, Pwani, Ruvuma, Tanga, Kagera, Mtwara na Geita, ili

kuhakikisha kuwa mahitaji ya msingi ya kulinda afya za walaji yanazingatiwa.

***192. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/2021, Wizara itaendelea kuboresha shughuli za Maabara katika maeneo yafutayo:

i. Kuongeza idadi ya sampuli zitakazofanyiwa chunguzi kufikia **6,000** kwa minofu ya samaki, dagaa, maji na udongo ili kubaini uwepo wa vimelea, kemikali na madini tembo ikilinganishwa na sampuli **2,848** zilizochunguzwa mwaka 2019/2020.

ii. Kuboresha mifumo ya usimamizi ya maabara ili kuendelea kukidhi vigezo vya kiwango kipya cha ISO/IEC 17025:2017.

iii. Kusimamia maabara ndogo za viwanda vya kuchakata samaki na kuhakiki mifumo ya uchakataji katika viwanda hivyo.

## 40.0 **HUDUMA ZA UGANI WA UVUVI**

***193. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, Wizara imeendelea kutoa huduma za ugani nchini licha ya kuwa na Wagani 677 ukilinganisha na hitaji la sekta ya kuwa na wagani **16,000** na hivyo kuwa na upungufu wa wagani **15,323.** Aidha, Wizara imeendelea kuwasiliana na Ofisi ya Rais - TAMISEMI ili kuzielekeza Mamlaka za Serikali za Mitaa kuajiri Maafisa Ugani. Vilevile, Wizara imeendelea kuhamasisha Sekta binafsi kuwekeza katika kutoa huduma za ugani ili kuongeza upatikanaji wa huduma hizo katika maeneo mbalimbali nchini.

***194. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2019/2020, Wizara ilishiriki katika maonesho mbalimbali ya kitaifa ikiwa ni pamoja na Maonesho ya biashara ya kimataifa – Sabasaba, Nanenane, na siku ya chakula Duniani ambapo zaidi ya wadau **33,742** walitembelea mabanda ya Wizara na kupata ufahamu juu ya Sera ya Taifa ya Uvuvi ya mwaka 2015, Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya mwaka 2003 na kanuni zake na kupatiwa elimu ya Uvuvi na Ukuzaji viumbe maji kwa ujumla wake.

***195. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2019/2020, Wizara imetambua Vyama vya Ushirika vya Wavuvi **102,** kuwezesha kuanzishwa kwa vyama vipya **14** na kuwezesha upatikanaji wa mikopo kwa vyama viwili (**2**). Vilevile, vyama vitano (**5**) vimepatiwa Injini za Boti **5** na vyama **14** viko katika hatua za mwisho za kupatiwa mikopo.

***196. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2019/2020, Wizara imezindua Agenda ya Taifa ya Utafiti wa Uvuvi na Ukuzaji Viumbe Maji (*The Fisheries and Aquaculture Research Agenda* 2020 – 2025). Agenda hiyo imeainisha maeneo matano (**5**) ya vipaumbele ambavyo ni: mfumo wa ikolojia ya viumbe maji; uvuvi endelevu katika maji ya asili; Ukuaji wa tasnia ya Ukuzaji viumbe maji; Masoko na biashara ya samaki na mazao yake; na masuala mtambuka.

***197. Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliendelea kusambaza teknolojia mbalimbali za uvuvi na Ukuzaji Viumbe Maji kwa kufanya yafuatayo:

i. Kutoa mafunzo rejea kwa wadau 5,008 wa Sekta ya Uvuvi katika Halmashauri 23 nchini (Kiambatisho Na. 43) kuhusu matumizi ya zana halali za uvuvi, ukuzaji bora wa Viumbe Maji na uhifadhi bora wa mazao ya uvuvi.

ii. Kuandaa na kurusha hewani vipindi 30 vya redio, vipindi 10 na makala 22 za luninga kupitia Shirika la TBC. Vipindi hivyo vilihusu ufugaji na upatikanaji wa vifaranga bora vya samaki; uchimbaji; utunzaji wa mabwawa na upandikizaji wa vifaranga pamoja na ufugaji wa samaki katika mabwawa na vizimba. Pia, nakala 11,250 za machapisho yaliyohusu ufugaji bora wa samaki, athari za uvuvi haramu na uhifadhi bora wa mazao ya uvuvi yalichapishwa na kusambazwa kwa wadau mbalimbali.

***198. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, Wizara kupitia FETA ilifanya tathmini ya kufahamu walipo wahitimu wa kada za uvuvi kwa kufanya ufuatiliaji (*Tracer Study*) kuanzia mwaka 2010 hadi mwaka 2019 waliohitimu katika vyuo vya FETA (**Kiambatisho Na. 44**), SUA na CKD. Matokeo ya tathmini hiyo yalionesha kuwa asilimia 28 ya vijana wote

waliohitimu katika kipindi hicho hawana ajira. Aidha, Wizara inafanya mapitio ya mitaala ili kuhakikisha kuwa mafunzo yanayotolewa yanakidhi mahitaji ya soko la ajira kwa wakati uliopo na baadae.

***199. Mheshimiwa Spika,*** pia, Wizara imeelekeza vyuo vinavyotoa taaluma za Uvuvi na Ukuzaji Viumbe Maji kuweka mkazo katika mafunzo yanayohusu ujasiriamali, ubunifu na mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi waliodahiliwa katika vyuo hivyo. Vilevile, Wizara inandaa utaratibu wa kuwaunganisha wahitimu wasio na ajira na Dawati la Sekta Binafsi ili kupata mikopo yenye riba nafuu kwa ajili ya kuanzisha shughuli za ujasiliamali.

***200. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/2021, Wizara itaandaa na kurusha hewani vipindi **30** vya redio, **10** vya luninga kuhusu masuala ya Uvuvi na Ukuzaji Viumbe Maji. Aidha, Wizara itahamasisha na kutoa mafunzo rejea kwa wadau **25,000** ili kuwa na Uvuvi endelevu. Vilevile, Wizara itaendelea kusambaza matokeo ya tafiti za kiteknolojia kwa wadau mbalimbali na itawawezesha wanafunzi wa Uzamili na Uzamivu kufanya tafiti za kipaumbele zinazohusiana na masuala ya uvuvi na ukuzaji viumbe maji ili kuendeleza na kutekeleza Agenda ya Taifa ya Utafiti wa Uvuvi na Ukuzaji Viumbe Maji “2020-2025”.

***201. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/2021, Wizara itaendelea kuviwezesha vyama vya ushirika vya wavuvi na wakuzaji viumbe maji kwa kuvipatia vifaa na zana za uvuvi ili kuongeza tija katika sekta. Aidha, Wizara itaendelea kushiriki na kuhamasisha wadau kushiriki katika maonesho ya Kitaifa (Sabasaba, Nanenane, Siku ya Chakula Duniani na Mvuvi day) ili waweze kujifunza teknolojia mbalimbali za uvuvi pamoja na kubadilishana uzoefu.

## 41.0 **TAASISI YA UTAFITI WA UVUVI TANZANIA –TAFIRI**

***202. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020 Wizara kupitia Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI) imefanya

tafiti mbalimbali ambazo zimesaidia katika kusimamia na kuendeleza Sekta ya Uvuvi nchini na kuchangia katika ukuzaji wa uchumi wa wananchi na Taifa kwa ujumla. Tafiti hizo zilifanyika kwa samaki wa maji ya asili na ukuzaji viumbe maji. Tafiti zilifanyika katika maeneo mbalimbali ikiwemo maziwa makuu, bahari, na mabwawa **(Kiambatisho Na. 45)**.

***203. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TAFIRI, imeandaa Agenda ya Utafiti wa uvuvi na ukuzaji viumbe maji (*National Fisheries and Aquaculture Research Agenda*), kanuni za utafiti wa uvuvi na ukuzaji viumbe maji (*Fisheries and Aquaculture Research Regulations).* Aidha, TAFIRI imeandaa kanzidata ya tafiti za uvuvi na ukuzaji viumbe maji nchini (*National Fisheries and Aquaculture Research Database*), ambapo katika kipindi cha mwaka 2015 hadi 2020, TAFIRI imetoa machapisho **112**, na vyuo vikuu vimezalisha tasnifu za Uzamili (*Master's*) na Uzamivu (PhD) **35** katika kipindi husika. Utekelezaji wa Agenda ya Utafiti ya Taifa utaleta faida zifuatazo:

i. Kuwezesha kufungua makabati yaliyohifadhi tafiti zilizo fanyika miaka ya nyuma kutoka mwaka 2015 hadi 2020, kutafsiri matokeo na kuziorodhesha tafiti hizo pamoja na kuzifikisha kwa watumiaji;

ii. Kupanua wigo wa kufanya tafiti kwa kuzitambua na kuziorodhesha tafiti zote kwenye masuala ya Uvuvi na Ukuzaji Viumbe Maji zinazofanywa na watafiti nchini kwa kujumuisha tafiti zinazofanywa na wanafunzi wa shahada za Uzamili (Masters) na Uzamivu (PhD) wakati wa kukamilisha masomo yao;

iii. Kuweka misingi ya kisheria kwa kutoa miongozo, wajibu na majukumu kwa watafiti wote kuzingatia vipaumbele vilivyowekwa na Ajenda ya Utafiti;

iv. Kuorodhesha na kuweka tafiti zote pamoja ili kurahisisha utunzaji, usambazaji na utumiaji wa taarifa zinazotokana na tafiti husika; na

v. Kuwezesha uratibu wa shughuli za utafiti ili kupata muunganiko wa taarifa kuhusu tafiti za Uvuvi na Ukuzaji Viumbe Maji.
Taarifa zaidi za machapisho pamoja na tafiti mbalimbali za uvuvi na ukuzaji viumbe maji zinapatikana kwenye kiunganishi hiki: http://tafiri.go.tz/publications.php?id=1.

***204. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, tafiti mbalimbali zimeendelea kufanyika. Kupitia Mradi wa SWIOFish utafiti wa uvuvi wa Pweza na mazingira yake katika maeneo ya Mtwara (Msangamkuu na Mgao), Tanga (Kwale na Mtambwe), Pwani (Jojo, Jibondo na Bwejuu) na Lindi (Songosongo) unaendelea ambapo matokeo ya utafiti yatasaidia katika uhifadhi na uvuvi endelevu wa rasilimali ya pweza. Pia, utafiti huu utasaidia katika mchakato wa kulipatia zao la Pweza Nembo ya Kiikolojia (*Eco-labeling*) inayotolewa na Taasisi ya *Marine Stewardship Council*.

***205. Mheshimiwa Spika,*** Nembo ya Kiikolojia itasaidia Pweza wa Tanzania kuuzwa katika soko la Kimataifa na kuongeza thamani ya Pweza wetu katika soko la Dunia. Mpaka sasa zoezi la kupata Nembo ya Kiikolojia limefikia asilimia **79**. Kwa sasa, Wizara kupitia TAFIRI na kwa kushirikiana na WWF inaandaa mkakati wa uvunaji wa Pweza (*Octopus Harvesting Strategy*) ambao utawezesha kuongeza asilimia hadi **81** kuelekea kupata Nembo ya Kiikolojia.

***206. Mheshimiwa Spika,*** kupitia TAFIRI, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Uhifadhi wa Mazingira (*The Nature Conservancy* - TNC) imefanya utafiti ili kubaini madhara ya uvuvi wa *Ringnet* katika Ziwa Tanganyika. Matokeo ya utafiti huu yanaonyesha kuwa ringnet inaweza kutumika kuvua samaki katika Ziwa Tanganyika lakini ufanyike kuanzia umbali wa **mita 1,000** kutoka ufukweni na kwenye ***visiwa***. Ruhusa hiyo inahusu uvuvi wa usiku tu.

***207. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/2021, Wizara kupitia TAFIRI itasimamia kikamilifu utekelezaji wa Ajenda ya Taifa ya Utafiti wa Uvuvi na Ukuzaji Viumbe Maji. Pia, itaendelea kufanya tafiti za ufugaji wa samaki nchini ili kupata

mbegu bora ya samaki iliyoratibiwa kijenetiki; vyakula bora vya samaki vilivyotokana na malighafi asili inayopatikana katika eneo la wafugaji samaki; teknolojia bora na rahisi ya ufugaji samaki katika maeneo mbalimbali ya Tanzania na ufugaji wa vizimba katika Maziwa Makuu ya Victoria, Tanganyika na Nyasa.

***208. Mheshimiwa Spika,*** TAFIRI itaendelea kufanya tafiti za kuendelea kujua wingi, aina na mtawanyiko wa samaki katika Maziwa Makuu (Victoria, Tanganyika na Nyasa), Maziwa ya Kati, Maziwa Madogo, mito na mabwawa; na kuainisha rasilimali za uvuvi katika Bahari ya Hindi, hasa zile ambazo ni muhimu kwa chakula na uchumi kwa wavuvi na Taifa kwa ujumla.

***209. Mheshimiwa Spika,*** TAFIRI itafanya tafiti katika Bahari ya kitaifa (*Territorial waters*) na katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari (*Exclusive Economic Zone* - EEZ) kuchunguza bailojia, ikolojia na wingi wa makundi ya samaki aina ya jodari na jamii zake na mazingira ya bahari yanayovutia uwepo wa samaki hao wanaopatikana Bahari ya Hindi.

## 42.0 **WAKALA WA ELIMU NA MAFUNZO YA UVUVI – FETA**

***210. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020 Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi (FETA) imeendelea kutoa mafunzo mbalimbali katika Tasnia ya Uvuvi. Katika kipindi hicho FETA ilidahili jumla ya vijana **1,103** kwa masomo ya Astashahada na Stashahada katika Kampasi za Mbegani, Nyegezi na Kigoma. Aidha, Wizara iliwezesha mafunzo ya muda mfupi kwa washiriki **2,176** yaliyofanywa na FETA **(Kiambatisho Na. 46).**

***211. Mheshimiwa Spika***, FETA imetoa mafunzo kwa washiriki kutoka nchi mbalimbali zikiwemo Kenya, Uganda, Afrika ya Kusini, Namibia, Angola, Malawi, Zambia, Jamhuri ya Somalia na Madagascar. Aidha, katika kipindi cha mwaka 2018/2019 na 2019/2020, kupitia msaada kutoka Shirika la Ushirikiano wa

Kimataifa la Japan (JICA), FETA ilitoa mafunzo kwa maafisa uvuvi **45** kutoka Jamhuri ya Somalia.

***212. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, Wizara kupitia FETA ilifanya tathimini ya kufahamu waliko wahitimu wa kada za uvuvi (*Tracer Study*) waliohitimu kuanzia mwaka 2010 hadi mwaka 2019 katika kampasi za FETA, SUA na CKD. Matokeo ya tathimini kwa vyuo vyote vitatu yalionesha kuwa asilimia **61** ya wahitimu hao wameajiriwa (Serikalini asilimia **52**, sekta binafsi asilimia **9**), asilimia **3** wamejiajiri, asilimia **36** hawana ajira. Matokeo ya tathimini kwa FETA yameonyesha kuwa asilimia **49** ya wahitimu hao wameajiriwa (Serikalini asilimia **23**, sekta binafsi asilimia **26**), asilimia **6** wamejiajiri, asilimia **28** hawana ajira na asilimia **17** wanaendelea na elimu ya juu. Maoni ya waliofuatiliwa yanaonesha kuwa elimu inayotolewa na vyuo husika inakidhi mahitaji ya Sekta.

***213. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2019/2020 FETA imejenga mifumo miwili ya ututoleshaji wa vifaranga vya samaki itakayokuwa na uwezo wa kutotolesha vifaranga **500,000** kwa wiki kwenye kampasi zake za Mikindani – Mtwara na Nyegezi – Mwanza. Aidha, FETA imezalisha jumla ya vifaranga **2,767,400** katika vituo vyake vya Nyegezi – Mwanza, Mbegani – Pwani na Gabimori – Mara.

***214. Mheshimiwa Spika,*** FETA ikishirikiana na TASAC ipo katika hatua za mwisho za kuridhiwa kwa Itifaki ya *Standards of Training, Certification and Watch Keeping for fish Vessels Personel* (STCW – F). Faida zitakazopatikana baada ya Itifaki hiyo kuridhiwa ni pamoja na:-

i. Vyeti vitakavyotolewa kwa wahitimu wa vyuo vya mafunzo ya uvuvi nchini vitatambuliwa kimataifa;

ii. Kuongezeka kwa fursa za ajira za kimataifa kwa wataalam wa vyombo vya uvuvi;

iii. Uwepo wa wakaguzi na waangalizi (inspectors and observers) wenye weledi utahakikisha matumizi endelevu ya rasilimali za bahari;

iv. Kuimarika kwa vyuo vya ndani vya mafunzo ya uvuvi na kutambulika kimataifa;

v. Kuwa na viwango bora vya ufundishaji wa wanafunzi katika vyuo vya uvuvi nchini;

vi. Kuimarika kwa usalama wa wafanyakazi katika vyombo vya uvuvi hivyo kupungua kwa ajali;

vii. Kuimarika kwa ulinzi, usalama na uhifadhi wa mazingira ya bahari;

viii. Kuimarika kwa upatikanaji wa takwimu na taarifa mbalimbali za uvuvi; na

ix. Wahitimu wa mafunzo ya uendeshaji wa meli na usalama kuwa na sifa ya kufanya kazi Bahari Kuu.

***215. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/2021, Wizara itahakikisha kuwa miundombinu ya kufundishia katika vituo vya FETA vya Gabimori - Rorya na Mikindani - Mtwara inaboreshwa ili kuanza kutoa mafunzo. Kwa sehemu kubwa, vituo hivi viwili, vitajikita katika kutoa elimu ya ufugaji samaki, kuzalisha vifaranga vya samaki na kuvisambaza kwa wananchi na kutoa huduma za ushauri na ugani katika Kanda husika. Aidha, FETA itaendelea kutoa elimu na mafunzo ya uvuvi, uchakataji na ufugaji samaki kwa nadharia na vitendo ili kuongeza tija katika Sekta ya Uvuvi.

***216. Mheshimiwa Spika,*** vilevile, FETA imeandaa mpango wa kutoa mafunzo ya siku saba (**7**) kwa wadau wa Uvuvi na Ukuzaji Viumbe Maji **3,210.** Mafunzo hayo yatakuwa yakitolewa katika kipindi cha miezi minne (4) katika kampasi za FETA husuan wakati wa likizo ya wanachuo.

## 43.0 MIRADI YA MAENDELEO YA SEKTA YA UVUVI

### I Mradi wa Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi (SWIOFish)

***217. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, Wizara imeendelea kutekeleza Mradi wa Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi (SWIOFish) ambao unatekelezwa kwa kipindi cha miaka Sita (2015 hadi 2021). Mradi huo unafadhiliwa na Benki ya Dunia kwa thamani ya shilingi **39,486,528,000.00**. Lengo kuu la mradi huo ni kuimarisha usimamizi madhubuti wa uvuvi katika ngazi ya kijamii, kitaifa na kikanda. Katika mwaka 2019/2020, mradi umetenga kiasi cha shilingi: **11,094,917,551.00** kwa ajili ya utekelezaji wa kazi mbalimbali ikiwemo:

i. Kuimarisha na kuijengea uwezo Wizara ya Mifugo na Uvuvi pamoja na Taasisi zake (TAFIRI, FETA na MRPU) kwa kuwezesha mafunzo mbalimbali na vitendea kazi kwa watumishi wake;

ii. Ujenzi wa miundombinu ya kuimarisha sekta ya Uvuvi kama vile Maabara ya Utafiti wa Uvuvi Dar es Salaam, nyumba za watumishi katika Hifadhi ya Bahari ya Silikanti Tanga (TACMP) na ofisi ya Hifadhi ya Bahari ya Kisiwa cha Mafia; ukarabati wa miundombinu ya soko la Feri - Dar es Salaam; na ujenzi wa Kituo cha Ukuzaji Viumbe Maji Bahari (National Mariculture Resource Centre) Kunduchi, Dar es Salaam.

iii. Ununuzi wa Boti, vifaa vya doria, Vifaa vya utafiti – TAFIRI pamoja na kutoa mafunzo stahiki kwa walengwa;

iv. Kuwezesha mafunzo kwa Vikundi 50 vya Ulinzi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi (BMU) kuhusu masuala ya utawala bora na uongozi ikiwa pamoja na kuwanunulia vitendea kazi mbalimbali; na

v. Kuwezesha mapitio ya Sheria ya Uvuvi, kutafsiri na kuchapisha Sera ya Uvuvi katika lugha ya Kiswahili.

***218. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/2021 Wizara kupitia mradi wa SWIOFish umetenga bajeti ya **shilingi 7,082,358,000** kwa ajili ya utekelezaji wa kazi mbalimbali ikiwemo: kuiwezesha TAFIRI kufanya tafiti za mavuvi ya kipaumbele; kuimarisha ushiriki wa jamii za wavuvi katika usimamizi na ulinzi wa Rasilimali za Uvuvi; kuwezesha Doria katika ulinzi wa rasilimali za uvuvi; kuiwezesha Kitengo cha Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu (MPRU); kuimarisha Mfumo wa Taarifa zinazohusu Uvuvi kulingana na matakwa ya kikanda; na kuwezesha kurejea Mpango wa Usimamizi wa Samaki wanaopatikana katika tabaka la juu la maji.

***219. Mheshimiwa Spika***, mradi wa SWIOFish utaboresha miundombinu mbalimbali ikiwemo: kuendelea na ujenzi wa maabara ya TAFIRI; kukamilisha ujenzi wa nyumba za watumishi wa MPRU Tanga; kuendelea na ujenzi wa jengo la ofisi MPRU - Mafia; ukarabati wa miundombinu ya soko la Feri - Dar es Salaam; na ujenzi wa Kituo cha Ukuzaji Viumbe Maji Bahari (*National Mariculture Resource Centre*) Kunduchi, Dar es Salaam.

**II Mradi wa Usimamizi wa Samaki wanaopatikana katika Tabaka la Juu la Maji**

***220. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020 Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) inatekeleza Mradi wa Kuwezesha Utekelezaji wa Mpango wa Usimamizi wa Samaki wanaopatikana katika Tabaka la Juu la Maji (*Project to Support the Implementation of the Tanzania Small and Medium Pelagic Fisheries Management Plan*) katika Ukanda wa Bahari ya Hindi**.** Mradi huo utatekelezwa kwa kipindi cha miezi (18) kuanzia mwezi Agosti, 2019 kwa thamani ya shilingi 228,737,551. Lengo la Mradi huo ni kuimarisha uendelevu wa samaki wanaopatikana katika Tabaka la Juu la Maji wakiwemo dagaa ambao huchangia takribani theluthi moja ya mavuno ya samaki wanaopatikana katika Bahari ya Hindi.

***221. Mheshimiwa Spika,*** kupitia mradi huo Wizara imetekeleza kazi zifuatazo:-

i. Kutoa mafunzo kuhusu Mzunguko wa Usimamizi wa Uvuvi kwa wadau 30 wanaohusika katika kutekeleza Mpango wa Usimamizi wa Samaki wanaopatikana katika Tabaka la Juu la Maji. Mafunzo hayo yalilenga kuimarisha uwezo wadau katika kutekeleza Mpango huo.

ii. Kufanya maandalizi ya Mpango wa Mafunzo kwa kuzingatia dhana ya usimamizi wa uvuvi unaozingatia ikolojia na mazingira (Ecosystem Approach to Fisheries Management). Mpango huu utakaotumika kutoa mafunzo kwa wadau wanaohusiana na utekelezaji wa Mpango wa Usimamizi wa Samaki Wadogo na wa Kati Wanaopatikana katika Tabaka la Juu la Maji ili kuimarisha usimamizi wa rasilimali hiyo;

iii. Kufanya tathmini ya Mfumo wa Wizara wa Ukusanyaji, Uhifadhi na Uchakataji wa Takwimu za Uvuvi ili kubaini changamoto zilizopo. Kufahamika kwa changamoto hizi kutawezesha Serikali kuhuisha Mfumo uliopo na kuandaa Mkakati ya Usimamizi wa Takwimu Nchini utakayowezesha upatikanaji wa takwimu na taarifa sahihi za uvuvi kwa wakati; na

iv. Kufanya mapitio ya Mpango wa Usimamizi wa Samaki wanaopatikana katika Tabaka la Juu la Maji kwa kufanya tathmini ya hali halisi ya utekelezaji wa Mpango ili kubaini changamoto zilizojitokeza katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango tangu ulipoandaliwa Mwaka 2013 pamoja na fursa mpya zilizopo kwa sasa. Taarifa hii itaiwezesha Serikali kuandaa Mpango mpya na kuweka mikakati ya usimamizi itakayoendana na hali halisi ya rasilimali husika.

***222. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/2021, Wizara itaendelea kutekeleza Mradi huo kwa kufanya yafuatayo:-

i. Kutoa mafunzo kwa wadao 50 wakiwemo Maafisa Uvuvi Wilaya, Wakusanya Takwimu za Uvuvi na Vikundi shirikishi vya usimamizi wa rasilimali za Uvuvi (BMUs) kuhusu uvuvi endelevu; na

ii. Kufanya utafiti kuhusu madhara yatokanayo na uvuvi wa samaki wasiolengwa (Bycatch) kwa samaki wanaopatikana katika tabaka la juu la maji.

## D MASUALA MTAMBUKA KATIKA SEKTA YA MIFUGO NA UVUVI

### 44.0 **Dawati la Sekta Binafsi la Wizara**

***223. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, Wizara kupitia Dawati la Sekta Binafsi imeunganisha wadau wa sekta ya mifugo na uvuvi wanaohitaji huduma za mikopo na bima, hususan kutoka Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB). Katika mwaka 2019/2020, jumla ya Shilingi **bilioni 26.1** zimeidhinishwa na TADB ikiwa ni ongezeko la asilimia **8.7** ikilinganisha na shilingi **bilioni 17.3** zilizotolewa katika mwaka 2018/2019. Fedha zilizoidhinishwa na kutolewa katika mwaka 2019/2020 ziko katika mgawanyo ufuatao:-

i. Uzalishaji wa mifugo na usindikaji wa nyama: kampuni 10 zimeomba mkopo ambapo kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na TADB mpaka sasa ni shilingi bilioni 12.9 na shilingi bilioni 10.3 tayari zimetolewa

ii. Uzalishaji wa maziwa na usindikaji: kampuni nane (8) na Vyama vya Ushirika vya Msingi viwili (2) vimeomba mkopo ambapo shilingi bilioni 12.2 zimeidhinishwa na shilingi bilioni 1.69 tayari zimetolewa.

iii. Uvuvi na Ukuzaji Viumbe Maji: kampuni saba (7) na Vyama vya Ushirika viwili (2) vimeomba mkopo ambapo shilingi milioni 944.2 zimepitishwa na shilingi milioni 323.8 tayari zimetolewa.

***224. Mheshimiwa Spika,*** ili kuongeza upatikanaji wa mikopo kwa Sekta za Mifugo na Uvuvi, Dawati limefanikisha masuala yafuatayo:-

i. Benki ya TPB imefungua dirisha maalum la mikopo kwa wavuvi. Uzinduzi wa dirisha hilo ulifanyika tarehe 23 Septemba, 2019 Ilemela, Mwanza.

ii. Mfumo wa Utambuzi na Ufuatiliaji wa Wavuvi walio katika vyama vya ushirika unaoitwa "Uvuvi Data Base"umeandaliwa. Vyama vya Ushirika 9 na wavuvi 557 kutoka mikoa ya Mwanza, Geita na Kigoma wameingizwa katika mfumo huo utakaowezesha taasisi za fedha kuwatambua na kuwafuatilia wakopaji hivyo kuvutia utoaji wa mikopo kwa wavuvi.

iii. Shirika la Bima la Taifa (NIC) limekubali kutoa bima kwa mikopo na zana za uzalishaji katika sekta za mifugo na uvuvi.

iv. Vijarida vya mnyororo wa thamani wa mazao saba (7) ya mifugo na uvuvi vimeandaliwa kwa kushirikiana na ASPIRES-USAID ili kutambua changamoto za uzalishaji katika Sekta za Mifugo na Uvuvi.

***225. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020 Wizara kupitia Dawati la Sekta Binafsi imeshughulikia hoja za kampuni za Sekta Binafsi kwa Taasisi za Serikali ili kuharakisha upatikanaji wa huduma zinazochelewesha ufanisi. Pia, Dawati limeshiriki kwenye mijadala ya kisera iliyotoa fursa za kujengwa na upanuzi wa kiwanda cha maziwa cha *Galaxy Food and Beverages* (Arusha); kiwanda cha ngozi cha *ACE Leather Ltd* (Morogoro); kiwanda cha dawa za mifugo cha *Farm Access* (Arusha); viwanda vya nyama vya Nguru Hills (Morogoro); Tan Choice (Pwani); na Kiwanda cha Mabondo (Kagera). Vilevile, katika kipindi hiki cha Mlipuko wa CORONA (COVID – 19), Dawati limewaunganisha wasafirishaji wa mazao ya mifugo na uvuvi kusafirisha mazao nje ya nchi kupitia TAHA.

***226. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2020/2021, Wizara kupitia Dawati la Sekta Binafsi itaendelea kuainisha, kuratibu na kufuatilia changamoto na kuzitafutia ufumbuzi kwa haraka ili kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara katika Sekta za Mifugo na Uvuvi. Aidha, Dawati litaendelea kuhamasisha uwekezaji katika Sekta za Mifugo na Uvuvi ikiwemo: uwekezaji katika viwanda vya kusindika mazao ya mifugo (nyama, maziwa na ngozi), vyakula vya mifugo, ufugaji samaki katika vizimba, mabwawa, uzalishaji wa vifaranga na vyakula bora vya mifugo na samaki.

## 45.0 **Utawala Bora, Jinsia na UKIMWI**

***227. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, Wizara imehamasisha watumishi kupima afya zao kwa hiari na kuwawezesha watumishi wanaoishi na Virusi vya UKIMWI kupata huduma ya lishe. Aidha, Wizara imetekeleza Mkakati wa Kuzuia na Kuziba Mianya ya Rushwa kwa kuanzisha mfumo wa malipo kwa njia ya kielektroniki katika vituo vyake pamoja na kutoa elimu kwa watumishi na wadau wa Sekta ya Mifugo na Uvuvi.

***228. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, Wizara imeajiri watumishi wapya **52** wakiwemo Maafisa Mifugo **(25)**, Maafisa Uvuvi (**5**), Manahodha (**2**), Wateknolojia wa Maabara (**2**), Wahasibu (**2**) na watumishi wa Kada Mtambuka saba **(16).** Aidha, vikao vitatu (**3**) vya Kamati ya Ajira vimefanyika ambapo watumishi tisa **(9)** wamepandishwa vyeo, watano **(5)** wamethibitishwa kazini baada ya kumaliza vizuri muda wa majaribio. Pia, taarifa za kiutumishi na mishahara ya watumishi **465** zimehakikiwa kupitia Mfumo Shirikishi wa Taarifa za Utumishi na Mishahara (HCMIS) na watumishi **53** wamepatiwa mafunzo ya Itifaki, Sheria, Kanuni na miongozo ya kazi. Vilevile, Mfumo Shirikishi wa Taarifa za Utumishi na Mishahara (HCMIS) na Mfumo wa Malipo ya Mishahara kwa watumishi (GSPP) imeendelea kusimamiwa.

Aidha, watumishi **20** wamewezeshwa kushiriki mafunzo ya muda mrefu na watumishi **25** mafunzo ya muda mfupi.

***229. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2020/2021 Wizara itatekeleza Mkakati wa Kuzuia na Kuziba Mianya ya Rushwa na kuelimisha watumishi wote kuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo ya kazi katika Utumishi wa Umma. Pia, Mkataba wa Huduma kwa Mteja utafanyiwa mapitio na Mfumo wa Wazi wa Upimaji wa Utendaji Kazi (OPRAS) utasimamiwa. Aidha, Mfumo Shirikishi wa Taarifa za Utumishi na Mishahara (HCMIS) na Mfumo wa Malipo ya Mishahara ya watumishi (GSPP) itawezeshwa. Vilevile, michezo kwa watumishi mahali pa kazi itapewa umuhimu unaostahili.

***230. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2020/2021 Wizara itaajiri watumishi **235** wakiwemo **173** wa Sekta ya Mifugo na **62** wa Sekta ya Uvuvi, watumishi **111** wanatarajiwa kupandishwa vyeo na watumishi **23** wanatarajiwa kuthibitishwa kazini. Aidha, Wizara itafanya uhakiki wa watumishi **465**, watumishi **400** wataelimishwa kuhusu kupima afya zao kwa hiari na watumishi wanaoishi na Virusi vya UKIMWI watahudumiwa. Vilevile, vikao vinne vikiwemo viwili (**2**) vya Kamati ya Ajira na viwili (**2**) vya Baraza la Wafanyakazi vitawezeshwa, pia majukumu ya Vyama vya Wafanyakazi, michezo na mabonanza yatawezeshwa.

## 46.0 **Teknolojia ya Habari na Mawasiliano**

***231. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020 Wizara imeanzisha Mfumo wa Mawasiliano Kielektroniki (*e-office*) kwa ajili ya kuboresha utendaji kazi. Mfumo huo umewezesha kuongezeka kwa kasi ya utendaji kazi, kupunguza gharama za uendeshaji wa ofisi, kuwezesha upatikanaji wa taarifa za ofisi kwa haraka. Aidha, watumishi **99** wa Wizara wamepatiwa mafunzo ya kutumia mfumo huu.

***232. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, Wizara imeendelea kutekeleza majukumu yake hususan ya ukusanyaji wa maduhuli ya Sekta ya Mifugo na Uvuvi kwa kutumia mifumo ya TEHAMA. Katika utekelezaji huo, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeanza kukusanya maduhuli kwa njia ya kieletroniki yatokanayo na vibali vya Afya ya Wanyama (Animal Health Movement Permit) kupitia mfumo wa makusanyo wa *Local Government Revenue Collection Information System* (LGRCIS) ambao unasimamiwa na Ofisi ya Rais - TAMISEMI. Kupitia mfumo wa makusanyo wa TAMISEMI (LGRCIS) wastani wa makusanyo umeongezeka kutoka **Shilingi 1,884,822,638.55** kwa kipindi cha Julai hadi Aprili 2018/2019 hadi kufikia **Shilingi 3,795,970,430.02** kwa kipindi kama hicho 2019/2020; uwazi umeongeza kwenye makusanyo na umewezesha ufuatiliaji wa karibu wa makusanya yatokanayo na mifugo. Pia, mfumo huu umeisaidia upatikanaji wa taarifa za mifugo inayokaguliwa kwenye minada ya awali. Vibali vya Afya ya Wanyama ni

kasma inayokusanywa na Mamlaka za Serikali Mitaa (MSM) kwenye minada **504** ya awali nchini. Aidha, mafunzo kuhusu matumizi ya mfumo wa makusanyo wa LGRCIS yametolewa kwa watumishi **163** kutoka Halmashauri **117** zenye minada ya awali.

***233. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, Wizara imeendelea kukamilisha ujenzi wa mfumo wa kielektroniki (*Fisheries Licence Online Application*) utakaowezesha wafanyabiashara wa samaki na mazao yake kuomba leseni na vibali vya kusafirisha samaki na mazao yake ndani na nje ya nchi. Lengo likiwa ni kuongeza ufanisi na kurahisisha biashara ya samaki na mazao yake. Aidha, wizara imeimarisha na kusimamia Mfumo wa kukusanya maduhuli ya Serikali (*Fisheries Revenue Collection System*) ambao umeunganishwa na mfumo wa Serikali wa GePG (*Government Electronic Payment Gateway*) na Mfumo wa kielektroniki wa Kukusanya na Kutunza Takwimu za Uvuvi (*Electronic Catch Assessment Survey* - eCAS). Aidha, Wizara imesambaza mashine sita (6) za kielektroniki za kukusanyia maduhuli (*Point Of Sales* - POS) katika vituo vya kukusanyia mapato na hivyo kuwezesha idadi ya vituo vyenye POS kufikia **33**.

***234. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2020/2021, Wizara imepanga kuboresha na kusimamia utekelezaji wa majukumu yake kwa kutumia mifumo ya kieletroniki katika ukusanyaji maduhuli yatokanayo na Sekta ya Mifugo na Uvuvi kwenye minada, masoko na mialo ili kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali na kuboresha mazingira ya kufanya biashara. Pia, Wizara itaendelea kutumia mfumo wa *e-office* katika Idara na taasisi zake ili kufikia lengo la kutumia karatasi chache (*less paper*) na baadaye kutotumia karatasi (*paperless*).

47.0 **Mawasiliano Serikalini**

***235. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2019/2020 Wizara imeendelea kutoa taarifa mbalimbali kwa wadau wa mifugo na uvuvi zikiwemo taarifa za uzinduzi wa kampeni za uogeshaji

mifugo kupitia majosho, taratibu za uendeshaji wa minada ya mifugo nchini, uzinduzi wa ajenda za utafiti wa mifugo na uvuvi, uanzishwaji na uendeshaji wa mashamba darasa. Aidha, ufafanuzi wa masuala mbalimbali ya mifugo yanayopotoshwa katika jamii umetolewa ikiwemo ufafanuzi baada ya kuwepo taarifa zisizo za kweli juu ya Virusi vya Corona (COVID – 19) kuwa na uwezekano wa kusambazwa na mifugo wakiwemo kuku. Hivyo, Wizara ilitoa ufafanuzi kuwa mifugo haiwezi kusambaza virusi hivyo kwa binadamu. Vilevile, Wizara imerusha vipindi maalum 52 vya runinga kupitia Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC 1) pamoja na vipindi vya redio kupitia TBC Taifa juu ya elimu mbalimbali kuhusu Sekta za Mifugo na Uvuvi.

***236. Mheshimiwa Spika*** Wizara inavipongeza vyombo mbalimbali vya habari vikiwemo vituo vinavyorusha matangazo katika ngazi ya jamii (community radio and television stations), magazeti, redio, televisheni na mitandao ya kijamii, namna vinavyotoa ushirikiano mkubwa kwa Wizara kwa kuhabarisha umma shughuli mbalimbali zinazofanywa na Wizara kupitia njia mbalimbali yakiwemo matangazo ya moja kwa moja (mubashara), pamoja na kusambaza taarifa za Wizara zinazotolewa na kusambaza kwa umma kwa kutumia vyombo vya habari.

***237. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2020/2021 Wizara itaendelea kutoa ufafanuzi na taarifa sahihi kwa wananchi juu ya mambo mbalimbali yanayohusu Wizara na taasisi zake pamoja na kuendelea kushirikiana na vyombo vya habari katika kuutarifu umma juu ya shughuli mbalimbali za Wizara. Aidha, Wizara itaendelea kuandaa vipindi maalum vya redio na televisheni na kuvitangaza ili kuwapatia wananchi fursa ya kupata taarifa mbalimbali hususan kwa wafugaji na wavuvi ili watumie vyema Sekta za Mifugo na Uvuvi katika kukuza uchumi wao na kuongeza pato la Taifa.

### 48.0 **Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi**

***238. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kusimamia hifadhi ya Mazingira katika sekta ya mifugo na uvuvi kwa kutoa

mafunzo yanayohusu ufugaji unaohimili mabadiliko ya tabianchi kwa wawezeshaji **84** katika Halmashauri zote za Mikoa ya Dodoma na Singida. Aidha, Wizara imeendelea kushirikiana na Wizara ya Kilimo katika kutekeleza Mradi wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi katika maeneo ya vijijini *(Ecosystem Based Adaptation for Rural Resilience in Tanzania)* katika Halmashauri za Mvomero (Morogoro), Mpwapwa (Dodoma), Kishapu (Shinyanga) na Simanjiro (Manyara). Jumla ya wafugaji **1,400** wamewezeshwa kuibua shughuli zinazoweza kufanyika katika mazingira ya maeneo yao ili kuwawezesha kuwa na ufugaji unaohimili mabadiliko ya tabianchi. Pia, imepata mafanikio makubwa katika kudhibiti uvuvi wa milipuko kwa asilimia **100,** ambao huchangia kuharibu mazalia ya samaki (matumbawe) katika mwambao wa Bahari ya Hindi.

***239. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/2021 Wizara itatoa mafunzo kwa wawezeshaji katika Halmashauri 32 nchini kuhusu ufugaji unaohimili mabadiliko ya tabianchi. Pia, Wizara itaendelea kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira na Wizara ya Kilimo katika kutekeleza Mradi wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi katika maeneo ya vijijini *(Ecosystem Based Adaptation for Rural Resilience in Tanzania)* katika Halmashauri za Mvomero (Morogoro), Mpwapwa (Dodoma), Kishapu (Shinyanga) na Simanjiro (Manyara). Pia, Wizara itashirikiana na Wizara ya Maji katika utekelezaji wa Mradi wa Kukabiliana na Athari za Mabadiliko ya Tabianchi wa Mkoa wa Simiyu utakaotoa maji kutoka Ziwa Victoria kupitia Miji ya Bariadi, Mwandoya na Meatu (Simiyu). Mradi huu utasaidia kupunguza changamoto ya maji kwa ajili ya mifugo.

***240. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/2021 wizara itaendelea kufuatilia athari za mabadiliko ya Tabianchi katika maziwa makubwa na maziwa mengine. Aidha, wizara itaandaa jarida la kufundishia wavuvi na wafugaji wa samaki kuhusu utunzaji wa mazingira. Lengo ni kujenga uelewa wa masuala ya utunzaji wa mazingira kwa wavuvi na wafugaji samaki.

49.0 **Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa**

***241. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, Wizara imeendelea kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa ili kuendeleza Sekta ya Mifugo na Uvuvi. Kupitia ushirikiano huo, nchi yetu inapata fursa ya kushiriki na kutekeleza Sheria, miongozo, mikataba, itifaki na taratibu mbalimbali za kikanda na kimataifa zenye lengo la kuimarisha Sekta ya Mifugo hususan udhibiti wa magonjwa ya mifugo na biashara ya mazao ya mifugo ikiwemo nyama, ngozi na maziwa.

***242. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2019/2020, Wizara imeendelea kushiriki kwenye mikutano, makongamano na warsha mbalimbali zenye lengo la kujadili na kuweka mikakati ya pamoja ya kusimamia Sekta ya Mifugo. Miongoni mwa mikutano hiyo ni Baraza la Sekta ya Kilimo na Usalama wa Chakula ambao ulijadili maeneo ya Sumu kuvu katika mazao ya Kilimo (*Aflatoxin*); Afya ya Mimea na Mifugo (*Sanitary and Phytosanitary*); Udhibiti wa magonjwa ya mifugo yasiyo na mipaka (TADs); Taarifa ya Sera ya Uwekezaji kwa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (*EAC Investment Policy*); Mkutano wa Eneo Huru la Biashara kwa Afrika (ACfTA); Baraza la Biashara na Uwekezaji la Jumuiya ya Afrika Mashariki; na Mkutano Mkuu wa SADC kuhusu uwekezaji katika viwanda.

***243. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/2021, Wizara itaendelea kushirikiana na Taasisi za kikanda na kimataifa ili kuendeleza Sekta ya Mifugo hususan uwekezaji na biashara ya mifugo na mazao yake. Vilevile, Wizara itaendelea kushiriki katika masuala ya kikanda, kimataifa na kutekeleza mikataba na itifaki mbalimbali za kikanda na kimataifa ambazo nchi yetu ni mwanachama.

***244. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuimarisha mashirikiano ya kikanda na kimataifa ili kusimamia rasilimali za uvuvi katika maji tunayomiliki kwa pamoja na nchi nyingine. Katika mwaka 2019/2020, Wizara imeshiriki katika vikao na warsha mbalimbali kupitia Taasisi za *Lake Victoria Fisheries Organisation* (LVFO) inayosimamia Ziwa Victoria, *Lake Tanganyika Authority* (LTA) inayosimamia Ziwa Tanganyika,

pamoja na taasisi za IOTC, WIOMSA, SWIOFC, IORA zinazosimamia Ukanda wa Bahari ya Hindi.

***245. Mheshimiwa Spika***, kupitia mashirikiano hayo, Wizara inaratibu na kushiriki katika vikao vya kujadili Mkataba wa Shirika la Biashara Duniani (WTO) wa kuondoa ruzuku isiyoendana na usimamizi endelevu wa rasilimali za uvuvi. Mkataba huo unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2020. Pia, kupitia LVFO wafanyabiashara wadogo 100 kutoka nchi za Tanzania (**25**), Kenya (**25**), Uganda (**25**) na Burundi (**25**) walipewa mafunzo kuhusu uchakataji, ufungashaji na kuongeza thamani katika mazao ya uvuvi.

***246. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2019/2020, Wizara imeendelea kushiriki kwenye mikutano, makongamano na warsha mbalimbali za Kikanda na Kimataifa kwa lengo la kuweka mikakati ya kuendesha operesheni za pamoja dhidi ya Uvuvi Haramu Usioratibiwa na Usiotolewa Taarifa katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari ya Hindi, Ziwa Victoria na Ziwa Tanganyika. Aidha, Tanzania ilishiriki katika mafunzo kuhusu mfumo wa kikanda wa kutoa taarifa ya utekelezaji wa Itifaki ya Uvuvi ya Jumuiya ya Maendeleo ya nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) yaliyofanyika nchini Zimbambwe. Pia, katika Mkutano wake wa **17**, Bunge lako tukufu liliridhia Mkataba wa Kimataifa wa FAO wa kuzuia Uvuvi Haramu, Usioratibiwa na Usiotolewa Taarifa (*Port States Measures Agreement* - PSMA).

***247. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/2021, Wizara itaendelea kushirikiana na Taasisi za kikanda na kimataifa katika Sekta ya Uvuvi ili kuimarisha usimamizi endelevu wa rasilimali za uvuvi. Aidha, Wizara itaendelea kutekeleza mikataba na itifaki mbalimbali za kikanda na kimataifa ambazo nchi yetu ni mwanachama ikiwemo Itifaki ya PSMA.

50.0 **Uwekezaji na Uwezeshaji katika Sekta ya Mifugo na Uvuvi**

***248. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, Serikali kupitia Wizara imeendelea kuweka mazingira wezeshi kwa wawekezaji katika ujenzi wa viwanda vya kuchakata na

kusindika mazao ya mifugo na bidhaa zake. Kutokana na jitihada hizo mafanikio yafuatayo yamepatikana:-

i. Machinjio **21** zinazokidhi viwango vya kimataifa zenye uwezo wa kuchinja ng'ombe **3,160**, mbuzi na kondoo **5,650**, kuku **35,500**, nguruwe **90** na punda **200** kwa siku zinafanya kazi (**Kiambatisho Na. 47**).

ii. Viwanda tisa **(9)** vya kusindika nyama vyenye uwezo wa kusindika jumla ya tani **794** za nyama kwa siku vinafanya kazi (**Kiambatisho Na. 48**).

iii. Machinjio za kisasa **10** zenye uwezo wa kuchinja ng'ombe **7,000**, mbuzi/kondoo **12,610** na kuku **3,000** kwa siku zinaendelea kujengwa na kukarabatiwa (**Kiambatisho Na. 49**).

iv. Viwanda **11** visivyofanya kazi vyenye uwezo wa kuchinja ng'ombe **4,500**, mbuzi/kondoo **8,500**, kuku **5,000**, punda **200** kwa siku vimehamasishwa kuanza uzalishaji (**Kiambatisho Na. 50**).

***249. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuhamasisha ujenzi wa viwanda vya nyama ili kuzalisha nyama safi na salama kwa ajili ya soko la ndani na nje ya nchi. Katika mwaka 2019/2020 ujenzi wa kiwanda cha *Tan Choice Limited* kilichopo Kibaha Mkoa wa Pwani umekamilika kwa asilimia **98**. Kiwanda hiki kitakuwa na uwezo wa kuchinja ng'ombe **1,000** na mbuzi **4,500** kwa siku. Pia, ujenzi wa kiwanda cha *Elia Foods Overseas Ltd* kilichopo Longido Mkoa wa Arusha umekamilika kwa asilimia **97**. Kiwanda kitakuwa na uwezo wa kuchinja ng'ombe **1,000** na mbuzi **4,000** kwa siku. Vilevile, ujenzi wa kiwanda cha *Binjiang Company Ltd* kilichopo Manispaa ya Shinyanga umekamilika kwa asilimia **99**. Kiwanda kitakuwa na uwezo wa kuchinja ng'ombe **1,000** kwa siku.

***250. Mheshimiwa Spika***, Serikali kwa kushirikiana na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) inaendelea na upanuzi wa kiwanda cha kuzalisha bidhaa za ngozi cha Gereza la Karanga ambapo kwa sasa upanuzi huo umefikia

asilimia **80**. Aidha, upanuzi huo utakapokamilika utawezesha kiwanda hicho kusindika futi za mraba **12,500** za ngozi kwa siku; kuzalisha viatu vya kiraia jozi **4,000** kwa siku; kuzalisha soli za viatu **3,000** kwa siku; na kuzalisha bidhaa nyingine za ngozi zikiwemo mikanda, pochi na mabegi. Vilevile, kiwanda cha ACE Leather cha Morogoro kinapanuliwa kwa kuwekewa mtambo wa kisasa utakaowezesha kusindika ngozi kufikia hatua ya mwisho (finished leather) ambapo upanuzi huo umefikia asilimia **90.**

***251. Mheshimiwa Spika,*** ili kuwa na chanjo za magonjwa ya mifugo za kutosha kulingana na mahitaji nchini, Wizara imeendelea kuhamasisha ujenzi wa viwanda vya kuzalisha chanjo za magonjwa ya mifugo ambapo katika mwaka 2019/2020 mafanikio yafuatayo yamepatikana:-

i. Ujenzi wa jengo la kuzalishia chanjo za aina ya bakteria katika Kiwanda cha Serikali cha uzalishaji Chanjo cha Kibaha (TVI) umefikia asilimia 75. Ujenzi wa jengo hilo utakapokamilika mwezi Juni, 2020 utawezesha kiwanda kuzalisha chanjo za Magonjwa 13 ya kipaumbele zinazohitajika hapa nchini ikiwemo chanjo mpya tatu (3) za Magonjwa ya Homa ya Mapafu ya Mbuzi, Sotoka ya Mbuzi na Kondoo na Kichaa cha Mbwa.

ii. Ujenzi wa kiwanda kikubwa cha kuzalisha chanjo za mifugo cha Hester Biosciences Africa Limited cha Kibaha chenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 18 (Shilingi bilioni 41.4) unaendelea ambapo ujenzi umekamilika kwa asilimia 90. Kiwanda hicho kitakapo kamilika mwezi Juni, 2020 kitazalisha chanjo 27 zinazoagizwa kutoka nje ya nchi ambapo kwa mwaka kiwanda hiki kitaweza kuzalisha jumla ya dozi bilioni 1.5 kwa mwaka kwa ajili ya soko la ndani na soko la nje. Napenda kutumia fursa hii kuwapongeza kwa dhati wawekezaji hawa ambao wameunga mkono Serikali ya awamu ya tano katika kuwekeza kwenye Sekta ya Mifugo.

***252. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2019/2020 Wizara imetoa mafunzo kuhusu Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi kwa Vikundi **11** vya Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za

Uvuvi katika Bwawa la Mtera **(4)** na Ziwa Victoria **(7)** katika Wilaya za Ilemela na Nyamagana (Mwanza).

***253. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, Wizara imehamasisha sekta binafsi kuwekeza katika viwanda vipya vinne (**4**) ambavyo vipo katika hatua za awali za ujenzi. Viwanda hivyo ni pamoja na Supreme Perch Ltd na Lake Star vya mkoani Kagera, Abajuko Enterprise Ltd cha mkoani Pwani na Pesca Perch Ltd cha mkoani Mwanza. Vilevile, idadi ya maghala ya ugandishaji/kuhifadhia mazao ya uvuvi (*cold rooms*) imeongezeka kutoka nane (**8**) mwaka 2017/2018 hadi **90** mwaka 2019/2020 na kupelekea kuongezeka kwa usambazaji na upatikanaji wa samaki na mazao ya uvuvi nchini na nje ya nchi. Maghala hayo kwa sasa yanauwezo wa kuhifadhi wastani wa tani **350** kwa siku.

***254. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuhamasisha wavuvi na wadau wa uvuvi kujiunga pamoja na kuanzisha vyama vya ushirika ili waweze kukopesheka na kuongeza tija katika Sekta ya Uvuvi. Aidha, vyama vya ushirika vya wavuvi vimeunganishwa na taasisi za fedha ambapo mikopo iliyoombwa na kupitishwa ni shilingi **bilioni 2.6** na mikopo iliyotolewa ni **shilingi milioni 873.8**. Pia, Wizara imehamasisha Benki ya Posta Tanzania - TPB kuzindua Akaunti ya Wavuvi (*Wavuvi Account*) kwa ajili ya mikopo na bima mahususi kwa wavuvi hususan wavuvi wadogo. Juhudi hizi zinalenga kuboresha maisha ya wavuvi na kuongeza kipato ili waweze kuboresha maisha ikiwa ni pamoja na lishe.

***255. Mheshimiwa Spika,*** katika kuhamasisha uwekezaji katika tasnia ya Ukuzaji Viumbe Maji, Wizara imetoa vibali **39** bila tozo yoyote katika mwaka 2019/2020. Vibali hivyo ni kama ifuatavyo: ufugaji samaki kibiashara **(11),** kuingiza nyavu za kutengeneza vizimba **(6),** kusafirisha mwani **(4),** kusafirisha lulu **(2),** kuingiza vifaranga vya samaki **(4)**, kuingiza samaki wa mapambo **(5),** na kuingiza chakula cha samaki **(13).**

***256. Mheshimiwa Spika,*** pia, jumla ya shilingi **milioni 4** zimetolewa kwa vikundi vya wafugaji samaki katika Wilaya za Mbarali na Chato. Vilevile, jumla ya injini **13** za kupachika

za boti ambapo injini tatu (**3**) zenye uwezo wa *horsepower* **15** zimetolewa kwa vikundi vya wavuvi vya Magawa, Kisiju na Shungubweni katika wilaya ya Mkuranga. Pia injini kumi (**10**) za boti zenye uwezo wa *horsepower* 25 zimegawiwa katika kikundi cha wafugaji wa samaki Mwamapuli (**1**) kilichopo Wilaya ya Igunga, kikundi cha wavuvi Mbamba bay (**1**), kikundi cha wavuvi Kyela (**1**), Vita Fishing Group, Msangamkuu-Mtwara (1), wakulima wa mwani Kweingoma-Handeni (1), Jiwezeshe Group Naumbu - Mtwara (1), Ukerewe (1), Nyamikoma-Busega (1), Kasanga-Kalambo (1) na Kaliua-Tabora (1).

***257. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/2021 Wizara imetenga shilingi **milioni 200** kwa ajili ya kusaidia wavuvi, wakuzaji viumbe maji na wadau wengine kupitia vyama Ushirika. Aidha, Wizara itaendelea kuhamasisha wavuvi na wadau wa uvuvi kuanzisha vyama vya ushirika pamoja na kuanzisha miradi ya kuwasaidia wavuvi wadogo.

### 51.0 **Gawio la Serikali katika Sekta ya Mifugo**

***258. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2019/2020, Taasisi, Bodi na Wakala zilizopo chini ya Wizara ambazo ni NARCO, LITA, TALIRI, TVLA, Bodi ya Nyama Tanzania, Bodi ya Maziwa Tanzania, Machinjio ya Dodoma, TAFIRI, FETA na MPRU zimetoa gawio kwa Serikali lenye jumla ya shilingi **1,492,500,000** (**Kiambatisho Na. 51)** ikilinganishwa na shilingi **520,000,000 kilichotolewa** mwaka 2018/2019. Aidha, Wizara imeendelea kuhamasisha uwepo wa tija katika taasisi hizo ili kuweza kuchangia zaidi mapato katika mfuko wa Serikali.

### 52.0 **Michango katika Shughuli za Kijamii**

***259. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, Taasisi, Bodi na Wakala zilizo chini ya Wizara zimetoa mchango wa shilingi **560,971,726** (**Kiambatisho Na. 51)** ikilinganishwa na shilingi **411,793,383** zilizotolewa mwaka 2018/2019. Michango hiyo ni kwa ajili ya kuchangia shughuli za maendeleo ya jamii kwa kukarabati na kujenga miundombinu muhimu ikiwemo ukarabati wa majosho; kuchimba visima vya maji kwa

matumizi ya binadamu na mifugo; kujenga kituo cha kukusanyia maziwa; kusaidia vyama vya ushirika vya wafugaji; uhifadhi na miradi ya maendeleo katika vijiji vilivyomo ndani ya hifadhi ya kisiwa cha Mafia; kutolewa injini za boti kwa vikundi 13 vya uvuvi; na mafunzo kwa jamii kuhusiana na shughuli za uvuvi na ulinzi wa rasilimali za uvuvi.

### 53.0 **Mwenendo wa Ukusanyaji Maduhuli ya Serikali**

***260. Mheshimiwa Spika,*** mwenendo wa ukusanyaji maduhuli kwa Sekta za Mifugo na Uvuvi umekuwa ukiongezeka mwaka hadi mwaka ambapo katika mwaka wa 2019/2020 Wizara ilipangiwa kukusanya jumla ya **shilingi 82,301,458,000** hadi kufikia Aprili 2020 ilikuwa imekusanya kiasi cha **shilingi 62,985,042,833** sawa na asilimia **76.5** ya lengo. Vilevile, ukusanyaji maduhuli uliongezeka kutoka wastani wa **shilingi bilioni 21** mwaka 2015/2016 hadi **shilingi bilioni 72** mwaka 2018/2019. Aidha, mapato ya Taasisi zilizo chini ya Wizara na mapato ya Halmashauri yanayotokana na shughuli za Mifugo na Uvuvi yameongezeka kwa kasi kubwa.

## E HITIMISHO

### 54.0 **Shukrani**

***261. Mheshimiwa Spika,*** kabla ya kuhitimisha hotuba yangu, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wale wote waliochangia kwa namna moja au nyingine katika kuiwezesha Wizara kufanikisha majukumu yake. Mafanikio yaliyopatikana katika mwaka uliopita yametokana na ushirikiano na misaada ya kifedha na kiufundi kutoka kwa nchi wahisani, mashirika mbalimbali ya kitaifa na kimataifa, taasisi za fedha za kitaifa na kimataifa, taasisi za hiari zisizokuwa za kiserikali na mashirika ya kidini bila kusahau hamasa na ushiriki wa wananchi wakiongozwa na Waheshimiwa Wabunge na Madiwani.

***262. Mheshimiwa Spika,*** napenda kuchukua fursa hii kuzitambua na kuzishukuru nchi za Australia, Austria, Brazil, Canada, Jamhuri ya Czech, Hispania, Iceland, Ireland,

Japan, Israel, Korea Kusini, Jamhuri ya Watu wa China, Marekani, Misri, Norway, Poland, Sweden, Ubelgiji, Ufaransa, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani na Uswisi kwa kuchangia katika maendeleo ya Sekta za Mifugo na Uvuvi.

***263. Mheshimiwa Spika***, napenda pia kutambua na kuzishukuru jumuiya za kikanda ambazo ni Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), Umoja wa Nchi za Ulaya (EU). Aidha nashukuru taasisi za Kifedha na Wadau wa Maendeleo ambao ni Benki ya Dunia (WB), Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Shirika la Kimataifa la Ushirikiano la Jamhuri ya Korea (KOICA), Shirika la Kimataifa la Ushirikiano la Jamhuri ya Japan (JICA), Shirika la Misaada la Ireland (Irish Aid), Shirika la Misaada la Marekani (USAID), Idara ya Maendeleo ya Kimataifa ya Uingereza (DfID), Taasisi ya Rasilimali za Wanyama ya Umoja wa Afrika (AU-IBAR), Shirika la Afya ya Wanyama Duniani (OIE), Shirika la Maendeleo ya Uswisi (SDC), Shirika la Ushirikiano la Ujerumani (GIZ), United Nations University (UNU), Shirika la Maendeleo la Denmark (DANIDA), na Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Sweden (SIDA); na mashirika ya FAO, WHO, IAEA, UNICEF, UNDP, UNIDO, SIDA, ILRI, CIAT, ASARECA na CCARDESA. Pia, natoa shukrani kwa Mifuko ya Kimataifa ya GEF na IFAD kwa michango yao katika kuendeleza Sekta za Mifugo na Uvuvi.

***264. Mheshimiwa Spika***, pia, napenda kushukuru Mashirika na Taasisi za hiari za *Bill and Melinda Gates Foundation, World Wide Fund for Nature (WWF), Indian Ocean Commission (IOC), South West Indian Ocean Fisheries Commission (SWIOFC), Heifer Project Tanzania (HPT), Overseas Fisheries Cooperation Foundation of Japan (OFCF), Vetaid, Care International, OXFARM, Welcome Trust, World Vision, FARM Africa, Land O' Lakes, Building Resources Across Communities (BRAC), World Society for Protection of Animals (WSPA), Global Alliance for Livestock and Veterinary Medicine (GALVmed), Institute of Social Studies (ISS), International Land Coalition (ILC), British Gas International, Sea Sense, Indian Ocean Tuna Commission*

*(IOTC), International Whaling Commission (IWC), SmartFish, Marine Stewardship Council (MSC),* Mashirika na Taasisi mbalimbali za humu nchini zinazojihusisha na uendelezaji wa Sekta za Mifugo na Uvuvi.

***265. Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya pekee nimpongeze na kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, **Dkt. John Pombe Joseph Magufuli,** kwa namna anavyoliongoza Taifa letu na anavyotusimamia katika kutekeleza majukumu ya Serikali. Nimewahi kukutana na kufanya kazi na viongozi wengi ndani na nje ya nchi yetu lakini Mheshimiwa Rais wewe ni Kiongozi na Mwalimu bora nakushukuru sana. Umenikabidhi majukumu ambayo nimeyatekeleza kikamilifu katika Wizara yangu na kuhakikisha kuwa ahadi ulizozitoa kwa Watanzania wakati unaomba kura mwaka 2015 zimetimia na kuhakikisha kuwa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015 - 2020 imetekelezwa.

***266. Mheshimiwa Spika,*** pia nichukue nafasi hii kuwapongeza Wafugaji na Wavuvi wote nchini kwa kazi nzuri wanazofanya za kutunza, kuzalisha na kulinda rasilimali za Taifa. Kazi wanazofanya ni nzuri na za heshima na kwamba Wizara yangu itaendelea kusimamia na kuunga mkono juhudi zao. Pia, niwashukuru wafanyabiashara, wawekezaji na wadau wote wa Sekta za Mifugo na Uvuvi kwa dhamira yao njema ya kuendeleza sekta hizi muhimu.

***267. Mheshimiwa Spika,*** naomba kurejea tena kutoa shukrani zangu za dhati kwa **Mheshimiwa Abdallah Hamis Ulega,** Mbunge wa Jimbo la Mkuranga, Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi kwa msaada wake wa karibu katika kusimamia kazi za Wizara. Aidha, napenda pia nitoe shukrani zangu kwa Katibu Mkuu Uvuvi, **Dkt. Rashid Adam Tamatamah** na Katibu Mkuu Mifugo, **Prof. Elisante Ole Gabriel**, Wakurugenzi pamoja na Watendaji wote wa Wizara na Taasisi kwa kazi nzuri sana wanazofanya. Nimefurahi sana kufanya kazi nanyi na ninawapongeza kwa kukubali mabadiliko na kukubali kuchapa kazi usiku na mchana kwa kauli mbiu ya **“masaa ni namba tu”** kwa manufaa ya Taifa letu, mmejinyima mengi kufikia mafanikio haya tunayojivunia. Mwandishi wa Kitabu

cha ***How Successful People lead***, **John C. Maxwell** alisema, nakuu ***"nobody achieves anything great by giving the minimum. No teams win championship without making sacrifices and giving their best"*** namuomba Mungu aendelee kuwabariki katika utumishi wenu.

***268. Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa wananchi wa Jimbo la Kisesa ambao muda wote wameendelea kuniunga mkono katika kutekeleza majukumu yangu ya jimbo na kitaifa, nataka niwahakikishie kuwa nipo tayari kuendelea kuwatumikia kwa juhudi, bidii, maarifa na ujasiri mkubwa na wasiwe na mashaka kunitwisha tena mzigo wa kuwatumikia. Wahenga walisema mzigo mzito mtwishe mnyamwezi na mimi Luhaga Joelson Mpina, kijana wenu wana Kisesa bado niko tayari na timamu kuwa 'mnyamwezi' wenu ili niendelee kuwatumikia kwa hiyo nawaomba wananchi wa Kisesa kwenye kumbukumbu zenu muendelee kubakia na jina la Luhaga Joelson Mpina.

***269. Mheshimiwa Spika,*** wananchi wangu watakumbuka kuwa walinichagua nikiwa bado kijana mdogo hadi sasa sijawahi kuwaangusha, **JEMBE LIPO SHAMBANI,** muda ukifika niwahisheni ili tuendelee kuyasaka maendeleo ya Jimbo letu kwa udi na uvumba, tumepania na hakuna kurudi nyuma.

## F MUHTASARI WA MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

***270. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/2021, Wizara inaomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi ya jumla ya shilingi **66,817,518,000** Kati ya fedha hizo, shilingi 32,096,197,000 kwa ajili ya Sekta ya Mifugo na shilingi **34,721,321,000** kwa ajili ya Sekta ya Uvuvi. Mchanganuo wa fedha zinazoombwa kwa kila Fungu ni kama ifuatavyo:

55.0 **Fungu 99: Sekta ya Mifugo**

***271. Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaomba kutumia jumla ya shilingi **32,096,197,000** kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya

Sekta ya Mifugo. Kati ya fedha hizo, Shilingi **27,034,826,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi **5,061,371,000** ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Mgawanyo wake ni kama ifuatavyo:-

**(i) Fedha za Matumizi ya Kawaida shilingi 27,034,826,000**

- Mishahara shilingi **17,130,715,000**
- Matumizi Mengine (OC) shilingi 9,904,111,000

**(ii) Fedha za Matumizi ya Maendeleoshilingi 5,061,371,000**

- Fedha za Ndani, shilingi **5,061,371,000;** na
- Fedha za Nje shilingi - **Hakuna.**

56.0 **Fungu 64: Sekta ya Uvuvi**

***272. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/2021, Wizara inaomba jumla ya shilingi **34,721,321,000** kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya Sekta ya Uvuvi. Kati ya fedha hizo, **shilingi 21,662,107,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi **13,059,214,000** ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Mgawanyiko wake ni kama ifuatavyo:-

**(i) Fedha za Matumizi ya Kawaida shilingi 21,662,107,000.00**

- Mishahara: Shilingi **12,031,696,000.00**; na
- Matumizi Mengine (OC): **Shilingi 9,630,411,000.00.**

**(ii) Fedha za Matumizi ya Maendeleo shilingi 13,059,214,000**

- Fedha za Ndani: Shilingi **5,976,856,000.00**, na
- Fedha za Nje: **Shilingi 7,082,358,000.00**

***273. Mheshimiwa Spika,*** naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza.

Hotuba hii pia inapatikana katika Tovuti ya Wizara: www.mifugouvuvi.go.tz.

***274. Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, ahsante sana. Sasa nitamwita Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa.

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyenzi Mungu aliyenijalia afya kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha taarifa kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2019/2020 na Makadirio ya Mapato Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kamati yangu Kilimo, Mifugo na Maji napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri anayoifanya katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii nimpongeze sana Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika, Wenyeviti wetu wa Kamati wote waliokuwa waongoza Kamati hapa kwa kazi nzuri waliyoifanya katika Bunge letu. Naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, Makamu Mwenyekiti wa Kamati kwa

ushirikiano mkubwa alionipatia pamoja na Wajumbe wa Kamati tulipokuwa tunatekeleza majukumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii kuwashukuru sana wananchi wangu wa Jimbo la Mufindi Kaskazini kwa ushirikiano walikuwa wananipatia katika kuongoza Jimbo letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2019/2020, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 7(1) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 kimeipa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji pamoja na majukumu mengine jukumu la kushughulikia Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa madhumuni ya Taarifa hii, Wizara ya Mifugo na Uvuvi inajumuisha mafungu mawili ambayo ni Fungu 64 - Sekta ya Uvuvi na Fungu 99 – Sekta ya Mifugo. Taarifa hii inafafanua mambo matano ambayo yanaonekana katika Taarifa ya Kamati mliyopewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati; wakati wa kuchambua Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Kamati ilitoa maoni na ushauri kwenye maeneo tisa kama yalivyoorodheshwa katika taarifa mliyopewa, kipengele (a) mpaka (h).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kiasi kikubwa ushauri uliotolewa na Kamati umetekelezwa. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuzingatia na kutekeleza ushauri wa Kamati.

Pamoja na pongezi hizo, Kamati inaamini maeneo machache ambayo bado ushauri wake haujatekelezwa yanafanyiwa kazi na Serikali. Cha muhimu ni Watendaji kuongeza kasi ya kufanya maamuzi ili kuendana na kasi ya matarajio wa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi uliofanywa na Kamati katika Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti ya mwaka wa fedha 2019/2020 ulijikita katika kulinganisha kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge na kiasi cha fedha kilichopelekwa na kutumika hadi mwezi Februari, 2020 na eneo la ukusanyaji wa maduhuli kwa kulinganisha makadirio yaliyowekwa kwa kiasi kilichokusanywa hadi kipindi hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2019/2020 Wizara kupitia Fungu 99 iliidhinisha jumla ya shilingi bilioni 31.774. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 28.774 ni fedha kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 3,000,000,000/= ni fedha kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo kutoka fedha za ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia mwezi Februari, 2020, jumla ya shilingi bilioni 16.901 zilikuwa zimetolewa sawa na asilimia 58.7 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya shilingi bilioni 10.441 ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Wizara na shilingi bilioni 6.882 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Kwa upande wa fedha za Miradi ya Maendeleo, fedha zilizokuwa zimetolewa hadi kufikia mwezi Februari, 2020, zilikuwa shilingi milioni 204 sawa na 7% tu ya fedha za maendeleo zilizoidhinishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2019/2020, Wizara kupitia Fungu 64 – Sekta ya Uvuvi, ilitenga jumla ya shilingi bilioni 33.127. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 18.432 ni fedha za Matumizi ya Kawaida na shilingi bilioni 14.694 ni fedha kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia mwezi Machi, 2020, jumla ya shilingi 11.259 zilikuwa zimetolewa kwa ajili ya

Matumizi ya Kawaida, sawa na asilimia 61.1. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 7.053 ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi na shilingi bilioni 4.205 sawa na asilimia 30.2 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Aidha, fedha za Miradi ya Maendeleo zilizokuwa zimetolewa hadi kufikia mwezi Machi, 2020 zilikuwa shilingi bilioni 4.438. Kati ya hizo, shilingi bilioni 426.312 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 4.012 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ilipanga kukusanya jumla ya shilingi bilioni 82.301ambapo katika Sekta ya Mifugo ilipanga kukusanya shilingi bilioni 50. Hadi kufikia Februari, 2020 Sekta ya Mifugo ilikuwa imekusanya shilingi bilioni 30.147 sawa na asilimia 60 ya lengo lililowekwa na Sekta ya Uvuvi ilipanga kukusanya shilingi bilioni 32.301. Hadi kufikia Machi, 2020 Sekta ya Uvuvi ilikuwa imekusanya shilingi bilioni 21.239 sawa na asilimia 65.75 ya matarajio yaliyowekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maoni na Tathimini ya Mwenendo na Utoaji wa Fedha za Miradi ya Maendeleo na Makusanyo na Maduhuli.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi uliofanywa na Kamati umebaini kwamba kwa muda mrefu Wizara ya Mifugo na Uvuvi imekuwa ikipewa ukomo mdogo wa bajeti. Pamoja na fedha ndogo zilizotengwa kwaajili ya miradi ya maendeleo, bado fedha hizo hutolewa kwa kiasi kidogo na si kama zilivyoidhinishwa na Bunge na hivyo kuchangia kutofikia malengo yaliyopangwa. Uwekezaji mdogo unaofanywa na sekta kupitia sekta ya mifugo hauwezi kusaidia sekta hii kuchangia kikamilifu kwenye Pato la Taifa licha ya idadi kubwa ya mifugo iliyopo nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imesikitishwa na kiasi kidogo cha fedha za miradi ya maendeleo zilizotolewa katika sekta ya mifugo kwa kipindi cha mwaka wa fedhan 2019/ 2020 cha shilingi milioni 204, ambayo ni sawa na asilimia saba tu ya kiasi cha fedha kilichoidhinishwa. Kamati haijalidhishwa na kupungua kwa makusanyo na maduhuli katika sekta ya

uvuvi ikilinganishwa na makusanyo yaliyopatikana mwaka wa fedha 2018/2019 kipindi kama hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa Bajeti na Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi. Tarehe 23 mpaka tarehe Machi, 2020 Kamati ilipokea na kuchambua Mpango wa Bajeti wa Wizara ya Fedha na Uvuvi na taasisi zilizopo chini yake kwa mwaka wa fedha 2020/2021, mpango ambao umeandaliwa kwa kuzingatia miongozo stahiki. Aidha, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 maeneo ya kipaumbele ya Wizara yaliyopangwa kutekelezwa na kwa Sekta ya Mifugo na Uvuvi ni kama yalivyoainishwa katika taarifa ya Kamati mliyopewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa fedha 2020/2021. Kwa ujumla kwa mwaka wa fedha 220/2021 Wizara ya Mifugo na Uvuvi Fungu Na. 64 na Na. 69 inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 64,900,756,055 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Aidha Wizara inatarajia kukusanya maduhuli kiasi cha shilingi bilioni 82. Maelezo yafuatayo yatafafanua maombi ya fedha kwa kila kifungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu Na. 64 Sekta ya Uvuvi. Katika mwaka wa fedha 2020/2021 Wizara kupitia Fungu Na. 64 inaomba kuidhinishiwa kiasi cha shilingi bilioni 34,721,321,000. Kati ya fedha hizo shilingi bilio ishirini na moja, milioni mia sita ishirini na mbili ni kwaajili ya matumizi ya kawaida, na bilioni kumi na tatu ni kwaajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. Kati ya fedha za miradi ya maendeleo shilingi bilioni tano, milioni mia tisa sabini na sita ni fedha za ndani na shilling bilioni mia saba milioni themanini na mbili ni fedha za nje. Aidha, kwa upande wa maduhuli Wizara kupitia Fungu. Na. 64 imepanga kukusanya jumla ya shilingi bilioni 33.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu Na. 99 Sekta ya Mifugo. Aidha, katika mwaka wa fedha 2020/2021 Wizara kupitia Fungu Na. 99 inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 32. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 27 ni kwa ajili ya

matumizi ya kawaida, shilingi bilioni tano ni kwaajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. Kati ya fedha za mradi ya maendeleo shilingi bilioni tano ni fedha za ndani na hakuna fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tathimini ya Malengo ya Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2020. Kwa upande wa Sekta ya Mifugo Kamati ilipokuwa inachambua bajeti ya sekta ya mifugo ilibaini kuwa kasi ndogo katika kuainisha, kupima na kumilikisha wafugaji maeneo ya ufugaji imesababisha kuendelea kwa migogoro baina ya wagufaji na watumiaji wengine wa ardhi. Kamati ilipokuwa inatekeleza majukumu yake tumebaini kuwa pamoja na kazi nzuri iliyofanywa na Mheshimiwa Rais kwa kuunda timu ya kutatua migogoro ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi bado kuna changamoto kubwa ya migogoro baina ya wafugaji na Mamlaka ya Hifadhi za Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilipokea malalamiko na tuhuma kutoka Chama cha Wafugaji Tanzania kuwa bado kuna vitendo vya uonevu vinavyofanywa na baadhi ya watendaji wa Mamlaka ya Hifadhi za Taifa dhidi ya wafugaji. Vitendo hivyo ni pamoja na;

i. Utaifishaji wa mifugo usiozingatia sheria
ii. Mauaji ya mifugo na wafugaji
iii. Wizi wa mifugo
iv. Watendaji wa Serikali kukaidi amri za mahakama
v. Ni mifugo kuliwa na wanyama bila wafugaji kulipwa fidia
vi. Ni mifugo kufa kwa kukose huduma muhimu kama malisho, maji, matibabu na chanjo
vii. Mifugo kuingizwa kwenye hifadhi na mapori ya akiba kwa nguvu na wafugaji kudaiwa kulipa faini ili kuokoa mifugo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maoni na Mapendekezo ya Kamati. Baada ya Kamati kufanya uchambuzi katika maeneo mbalimbali ya majukumu ya Wizara ikiwa ni pamoja na maombi ya fedha kwa bajeti ya mwaka wa fedha 2020/2021 naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuongezeka kwa mazao samaki katika Ziwa Victoria ni muhimu, ongezeko hili litaleta manufaa kwa Serikali na kwa wavuvi wenyewe. Serikali imekuwa ikifanya operesheni mbalimbali za kudhibiti uvuvi haramu na matumizi ya dhana za uvuvi kwa lengo la kulinda mazao ya samai na kudhibiti uhalibifu kwa mazingira na kumaliza tatizo la kuuza samaki kwa magendo. Operesheni hizi zimekuwa na manufaa na Serikali imeweza kwa kiasi kikubwa kudhibiti uvuvi haramu na dhana za uvuvi zisizokuwa kwa mujibu wa sheria. Hatua hii imesaidia kuongezeka kwa samaki. Kamati inaipongeza Serikali kwa haya:-

i. Kamati inashauri Serikali kuwa ongezeko la samaki katika Ziwa Victoria ni lazima liendane naongezeko la kuimarika kwa kipato cha wavuvi wanaozunguka Ziwa Victoria.

ii. Changamoto za viwanda vya kuchakata mazao ya samaki kuhamishia shughuli za uzalishaji nchi jirani. Ili kuvutia wawekezaji wa ndani na wa nje ya nchi Kamati inaishauri Serikali kufanya mapitio ya Sheria ya Uvuvi ya Mwaka 2003 ambayo imepitwa na wakati na haiendane na mazingira ya sasa ya kufanya biashara ya ushindani. *(Makofi)*

iii. Athari za homa ya mapaafu. Kwa kuwa makusanyo ya maduhuli kwa sekta ya Uvuvi kwa kiasi kikubwa kutokana na mauzo ya samaki nje ya nchi, na kwa kuwa nchi za Ulaya Mashariki hususani Spain, Italy na Asia ambao ndio wateja wakubwa wa samaki wa nchi yetu, na kwa kuwa nchi hizo zimeathirika kwa kiasi kikubwa na gonjwa hili la homa ya mapafu upo uwezekano mkubwa wa mauzo yatakayotokana na samaki kupungua. Kufuatiwa changamoto hiyo Kamati inashauri Serikali kufanya upya tathimini ya maoteo ya maduhuli ili kuendana na bajeti halisi. Kamati inaamini kwa kufanya hivi Wizara inaweza kupanga na kutekeleza mipango yake ya maendeleo kulinga na na hali halisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kuendelea kwa Migogoro Kati ya Wafugaji na Mamlaka ya Hifadhi. Kufuatia malalamiko

ya wafugaji kuhusu uonevu unaofanywa na baadhi ya Askari wa Wanyamapori dhidi ya wafugaji na mifugo yao Kamati inaushauri Serikali kufanyia kazi malalamiko yaliyoainishwa katika taarifa hii; na endapo itabainika wahusika wachukuliwe hatua za kisheria na za kinidhamu. Aidha, ni muhimu kwa Serikali kudumisha utawala bora kwa kutekeleza maamuzi na hukumu zinazotolewa na mahakama mbalimbali nchini dhidi ya fidia na maamuzi yaliyotolewa kuhusu wagufaji kurudishiwa mifugo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu pia kwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi ishirikiane na Wizara ya Maliasili na Utalii kutoa elimu ya mara kwa mara kwa wafugaji na Askari na wanyamapori kuhusu umuhimu wa kuheshimu mipaka, kazi na kila upande. Ni muhimu kwa Wizara kushirikiana na halmshauri kutoa elimu za mara kwa mara kuhusu ufugi bora kwa biashara pamoja na kanuni bora za ufugaji, ni vyema halmshauri na Wilaya zikatenga maeneo kwa ajili ya malisho ili kupunguza migogoro.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Hitimisho. Napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kwa niaba ya wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji. Napenda pia kumpongeza na kumshukuru Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mheshimiwa Luhaga Mpina, Naibu wake Waziri Mheshimiwa Abdallah Ulega, Katibu Mkuu Uvuvi Dkt. Rashid Tamatama, Katibu Mkuu Profesa Elisante Gabriel, wataalam wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa ushirikiano mkubwa waliokuwa wanaipatia Kamati yangu. Kwa dhati kabisa napenda kuwashukuru wajumbe wa Kamati kwa ushikiriano na michango yao waliyoitoa kwa kipindi cha kuchambua bajeti ya Wizara pamoja na kuandaa taarifa hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho napenda kushukuru Katibu wa Bunge Ndugu Stephen Kagaigai, Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati ndugu Michael Chikokoto, Mkurugenzi Msaidizi Gerald Magili pamoja na Sekretarieti ya Kamati ambaye ni ndugu Vigili Mtui, Rachel Nyega...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa kengele ya pili imeshagonga ahsante sana.

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA - MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

## MAONI YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020 PAMOJA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

## SEHEMU YA KWANZA

---

### MAJUKUMU YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 7(1) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016 kimeipa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji pamoja na majukumu mengine jukumu la kushughulikia bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa madhumuni ya Taarifa hii, Wizara ya Mifugo na Uvuvi inajumuisha mafungu mawili (2) ambayo ni:-

a) Fungu 64- Sekta ya Uvuvi; na

b) Fungu 99 –Sekta ya Mifugo.

**Mheshimiwa Spika,** taarifa hii inafafanua mambo matano (5) kama yanavoonekana katika Taarifa ya kamati mliyopewa.

## SEHEMU YA PILI

## UCHAMBUZI WA MASWALA MBALIMBALI

### UTEKELEZAJI WA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kuchambua Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 kwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Kamati ilitoa maoni na ushauri kwenye maeneo tisa (9) kama yalivyoorodheshwa katika taarifa mliyopewa, kipengele (a) hadi (h).

**Mheshimiwa Spika,** kwa kiasi kikubwa ushauri uliotolewa na Kamati umetekelezwa, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuzingatia na kutekeleza ushauri wa Kamati. Pamoja na pongezi hizo, Kamati inaamini maeneo machache ambayo bado ushauri wake haujatekelezwa yanafanyiwa kazi na Serikali cha muhimu ni watendaji kuongeza kasi ya kufanya maamuzi ili kuendana na kasi ya matarajio wa wananchi.

### UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi uliofanywa na Kamati katika Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/ 2020 ulijikita katika kulinganisha kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge, kiasi cha fedha kilichopokelewa na kutumika hadi mwezi Februari, 2020 na eneo la ukusanyaji maduhuli kwa kulinganisha makadirio yaliyowekwa na kiasi kilichokusanywa hadi kipindi hicho.

### Kiasi cha Fedha kilichoidhinishwa na kutolewa

**a) Sekta ya Mifugo - Fungu 99**

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 Wizara kupitia Fungu 99 iliidhinishiwa jumla ya shilingi

**31,774,378,000.00**. Kati ya Fedha hizo shilingi **28,774,378,000.00** ni Fedha za Matumizi ya Kawaida na shilingi **3,000,000,000.00** ni Fedha kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo kutoka Fedha za Ndani.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia mwezi Februari 2020, jumla ya shilingi **16,901,026,353.00** zilikuwa zimetolewa sawa na **asilimia 58.7** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya hizo, shilingi **10,441,358,001.950** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Wizara na shilingi **6,822,849,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Kwa upande wa Fedha za Miradi ya Maendeleo, fedha zilizokuwa zimetolewa hadi kufikia mwezi Februari 2020, zilikuwa shilingi **204,094,833.00** sawa na **asilimia 7** tu ya Fedha za Maendeleo zilizoidhinishwa.

**b) Sekta ya Uvuvi - Fungu 64**

**Mheshimiwa Spika,** Katika Mwaka wa Fedha 2019/2020, Wizara kupitia Fungu 64 ilitengewa jumla ya shilingi **33,127,378,551:00**. Kati ya Fedha hizo, shilingi **18,432,461,000:00** ni Fedha za Matumizi ya Kawaida na shilingi **14,694,917,551** ni Fedha kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia mwezi Machi, 2020, jumla ya shilingi **11,259,129,186.43.** zilikuwa zimetolewa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, sawa na **asilimia 61.1.** Kati ya fedha hizo, shilingi **7,053,411,321.00** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi na shilingi **4,205,717,955.00** **asilimia 30.2** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Aidha, Fedha za Miradi ya Maendeleo zilizokuwa zimetolewa hadi kufikia mwezi Machi, 2020 zilikuwa shilingi **4,438,956,391.12** kati ya hizo shilingi **426, 312, 537.92** ni Fedha za Ndani na shilingi **4,012,643,853. 20** ni Fedha za Nje.

**c) Makusanyo ya Maduhuli**

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 ilipanga kukusanya jumla ya shilingi **82,301,458,000.00,** ambapo Sekta ya Mifugo ilipanga kukusanya shilingi **50,000,000,000.00,** hadi kufikia Februari, 2020 sekta ya mifugo ilikuwa imekusanya shilingi **30,147,554,831.00** sawa na **asilimia 60** ya lengo lililowekwa na Sekta ya Uvuvi ilipanga kukusanya shilingi **32,301,458,000.00 ,** hadi kufikia Machi, 2020 Sekta ya Uvuvi ilikuwa imekusanya shilingi

**21,239,585,000.57** sawa na **asilimia 65.75** ya matarajio ya lengo lililowekwa.

**2.2.2Maoni na Tathmni kuhusu Mwenendo wa Utoaji Fedha za Miradi ya Maendeleo na Makusanyo ya Maduhuli**

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi uliofanywa na Kamati umebaini kwamba kwa muda mrefu Wizara ya Mifugo na Uvuvi imekuwa ikipewa ukomo mdogo wa bajeti. Pamoja na fedha ndogo zinazotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo bado fedha hizo hutolewa kwa kiasi kidogo, na sio kama zilivyoidhinishwa na Bunge na hivyo kuchangia kutofikiwa kwa malengo yaliyopangwa.

**Mheshimiwa Spika,** uwekezaji mdogo unaofanywa na Serikali kupitia Sekta ya Mifugo hauwezi kuisaidia sekta hii kuchangia kikamilifu kwenye pato la Taifa licha ya idadi kubwa ya mifugo iliyopo nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imesikitishwa na kiasi kidogo cha Fedha za Miradi ya Maendeleo zilizotolewa kwa Sekta ya Mifugo kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2019/2020 kiasi cha shilingi **204,094,833.00** ambazo ni **asilimia 7** tu ya kiasi kilichoidhinishwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati haijaridhishwa na kupungua kwa makusanyo ya maduhuli kwa Sekta ya Uvuvi ikilinganishwa na makusanyo yaliyopatikana katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 kwa kipindi kama hiki.

**UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA 2019/2020**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati haikuweza kukagua miradi yoyote ya maendeleo iliyotengewa Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 kutokana na miradi iliyoainishwa katika bajeti husika kupelekewa fedha kidogo kwa ajili ya utekelezaji. Kwa mfano; Sekta ya Mifugo hadi mwezi Februari, 2020 ilikuwa imepokea **asilimia 7** tu ya fedha za miradi ya maendeleo zilizoidhinishwa na Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na fedha kidogo za miradi ya maendeleo zilizotengwa na kutolewa ililazimu Kamati kukagua miradi inayotekelezwa na sekta binafsi ili kutathimini ushiriki wa sekta binafsi katika kukuza uchumi kupitia uchumi wa viwanda. Kwa upande wa Sekta ya Uvuvi, Kamati ilipata fursa ya kutembelea Kiwanda cha kuchakata samaki cha *Supreme Perch Ltd* na kukagua shughuli zinazotekelezwa na kiwanda hicho.

**Mheshimiwa Spika,** aidha, kwa upande wa Sekta ya Mifugo, Kamati ilipata nafasi ya kutembelea Shamba la Serikali la Malisho la Ranchi ya Misenyi kwa lengo la kukagua utekelezaji wa maoni ya Kamati kuhusu kumega maeneo ya mashamba ya Serikali kwenye ranchi za Taifa na kuwapatia wananchi ili kupunguza migogoro baina ya Wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi pamoja na kuendeleza shughuli za ufugaji kwa kufuga kisasa bila kuhama hama kwa ajili ya kutafuta maeneo ya malisho.

### 2.3.1 Kiwanda cha kuchakata mazao ya samaki cha *Supreme Perch Limited*

**Mheshimiwa Spika,** kiwanda cha samaki *Supreme Perch Limited* shughuli zake Mwaka 2017 kilianza baada ya kukodi kilichokuwa kiwanda cha kusindika mazao ya samaki *Vicky Fish Limited*. Tangu kiwanda kilipoanza uzalishaji kiwanda kimekuwa kikilipa kodi na tozo za Serikali kwa mujibu wa sheria za nchi kama inavyoonekana katika Taarifa ya Kmati mliyopewa.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na kulipa kodi na tozo za Selikali kwa ukamilifu kiwanda hiki kimeajiri takribani **wafanyakazi 238** na kuchangia kwenye kukuza uchumi na pato la Taifa, Aidha Kamati ilielezwa kuwa, Serikali haijawahi kurudisha ***VAT Returns*** tangu kiwanda hiki kilipoanza uzalishaji, mwenendo huu hauna tija kwa kiwanda na unakatisha tamaa wawekezaji.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini pia kuwepo changamoto na malalamiko kadhaa kutoka kwa wadau kuhusu changamoto zinazopelekea viwanda vya kuchakata mazao ya samaki vilivyopo nchini kutofanyakazi kwa ufanisi na

kupelekea viwanda vingine kufungwa ukilinganisha na ongezeko kubwa la viwanda vipya vya kuchakata mazao ya samaki vinavyoendelea kufunguliwa nchini Uganda.

**Mheshimiwa Spika**, utafiti uliofanywa na Kamati umebaini kuwa, ongezeko la wawekezaji kufungua viwanda vya kuchakata mazao ya Samaki nchini Uganda unatokana na maboresho ya mazingira rafiki ya uwekezaji ambayo ni pamoja na Sera na Kanuni za biashara za kuaminika na kutabirika, ukubwa na ufanisi wa uwanja wa ndege wa kimataifa wa Entebe, tozo na kodi zenye gharama nafuu kwa ajili ya wavuvi na wawekezaji na gharama nafuu kwa malighafi zinazotumika kwenye uvuvi na viwanda vya kuchakata mazao ya samaki.

### 2.3.2 Shamba la Malisho Ranchi ya Misenyi

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imefurahishwa na kuridhika kwa namna zoezi la ukodishwaji vitalu vya ufugaji ulivyofanyika na namna wawekezaji wazawa walivyoweza kutumia vizuri vitalu walivyopewa kwa ajili ya manufaa ya mifugo yao. Pamoja na pongezi hizo, Kamati ilifahamishwa kuwepo changamoto mbalimbali, kama zilivyoainishwa katika Taarifa hii.

## 2.4 MPANGO WA BAJETI NA UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

**Mheshimiwa Spika,** tarehe 23 - 24 Machi, 2020 Kamati ilipokea na kuchambua Mpango wa Bajeti wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2020/ 2021. Mpango ambao umeandaliwa kwa kuzingatia miongozo stahiki. Aidha katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2020/2021 maeneo ya kipaumbele ya Wizara yaliyopangwa kutekelezwa kwa Sekta ya Mifugo na Uvuvi ni kama yalivyoainishwa katika taarifa ya Kamati mliyopewa.

## 2.5 MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, Wizara ya Mifugo na Uvuvi Fungu 64 na Fungu 99 inaomba kuidhinishiwa jumla ya **shilingi 64,901,756,551:00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Miradi ya maendeleo. Aidha, Wizara inatarajia kukusanya maduhuli kiasi cha **shilingi 82,301,458,400:00**. Maelezo yafuatayo yanafafanua maombi ya fedha kwa kila fungu.

### 2.5.1FUNGU 64: SEKTA YA UVUVI

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 Wizara kupitia Fungu 64 inaomba kuidhinishiwa kiasi cha shilingi **34,721,321,000:00**. Kati ya fedha hizo, **shilingi 21,662,107,000:00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi **13,059,214,000:00** ni kwa ajili ya kugharamia Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha za Miradi ya Maendeleo shilingi **5,976,856,000:00** ni Fedha za Ndani na shilingi **7,082,358,000:00** ni Fedha za Nje. Aidha, kwa upande wa maduhuli Wizara kupitia Fungu 64 imepanga kukusanya jumla ya **shilingi 33,000,000,000:00** zitakazopatikana kutokana na mapato yatokanayo na Leseni za kusafirisha samaki na mazao yake (*Export Licenses*), Leseni za uingizaji mazazo ya samaki (*Import Royalty*), Ushuru wa Mrahaba (*Export Royalty*), Tozo za Maabara na faini kwa makosa mbalimbali ya ukiukwaji wa Sheria za Uvuvi.

### 2.5.2 FUNGU 99: SEKTA YA MIFUGO

**Mheshimiwa Spika**, aidha, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 Wizara kupitia Fungu 99 inaomba kuidhinishiwa kiasi cha **shilingi 32,096,197,000:00**. Kati ya fedha hizo, **shilingi 27,034,826,000:00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **shilingi 5,061,371,000:00** ni kwa ajili ya kugharamia Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha za Miradi ya Maendeleo shilingi **5,061,371,000:00** ni Fedha za Ndani na hakuna fedha za Fedha za Nje. Aidha, kwa upande wa Maduhuli Wizara kupitia Fungu 99 imepanga kukusanya jumla ya **shilingi 50,000,000,000:00** zitakazopatikana kutokana na Leseni za kusafirisha wanyama na mazao yake nje ya nchi (*Exporty Duty License fees*), Ada

mbalimbali, Ushuru wa Soko (*Market Fee*), Mauzo ya Chanjo na Kodi za Pango la Nyumba za Serikali na Mauzo ya Zabuni.

## TATHIMINI YA MALENGO YA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

**Mheshimiwa Spika,** tathimini ya Kamati imebaini kuwa kuna ongezeko kidogo la bajeti kwa **asilimia 1.6** kwa Sekta ya Uvuvi. Aidha bajeti ya Maendeleo kutoka fedha za ndani imeongezeka kwa **asilimia 96.7** wakati bajeti ya maendeleo kutoka Fedha za Nje imeshuka kwa **asilimia 11.1.** Vile vile makadirio ya ukusanyaji wa maduhuli yameshuka kwa **asilimia 19.2** kutokana na kuondolewa kwa **Tozo ya Dola za Marekani 0.4** kwa wawekezaji katika uvuvi wa Bahari Kuu.

**Mheshimiwa Spika,** tozo ya Dola za Marekani o.4 ilipoanzishwa ilipelekea wawekezaji kwenye uvuvi wa Bahari Kuu kupungua, ili kuvutia upaya tozo hii imesamehewa kwa kipindi cha mwaka mmoja ili kutahimini mwenendo wa uwekezaji utakavyokuwa mara baada ya tozo kuondolewa.

**Mheshimiwa Spika,** tathimini ya Kamati imebaini kuwa kushuka kwa bajeti ya maendeleo kwa Fedha za Nje kumetokana na sababu kuu mbili; kwanza kuyumba kwa uchumi wa dunia hususan nchi za Ulaya Mashariki kutokana na ugonjwa wa **COVID 19**, na sababu ya pili ni ukweli kwamba ahadi zinazotolewa na wadau wa maendeleo katika kuchangia maendeleo ya Sekta ya Uvuvi zimekuwa mara nyingi hazitolewi kama zilivyoahidiwa na mara kadhaa Bunge limekuwa likiwaomba wadau wa maendeleo kutenga bajeti halisi na inayotekelezeka.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kutambua hilo ndio maana Serikali imeongeza bajeti ya maendeleo kwa takribani **asilimia 70** ili kujiletea maendeleo yake yenyewe. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hii kwani inalenga kuchochea maendeleo chanya kwenye sekta ya uvuvi.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Waziri iliieleza Kamati kuwa, wakati wa Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2019/

2020 kutokana na ukomo wa bajeti unaotolewa kwa Wizara, Wizara imeshindwa kutekeleza mipango kama ilivyoainishwa katika Taarifa mliyopewa kipengele (i) hadi (viii)

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Sekta ya Mifugo, Kamati ilipokuwa inachambua bajeti ya Sekta ya Mifugo ilibaini kuwa kasi ndogo katika kuainisha, kupima na kumilikisha wafugaji maeneo ya ufugaji imesababisha kuendelea kwa migogoro baina ya Wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokuwa inatekeleza majukumu yake imebaini kuwa pamoja na kazi nzuri iliyofanywa na Mheshimiwa Rais ya kuunda timu ya kutatua migogoro ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi, bado kuna changamoto kubwa ya migogoro baina ya Wafugaji na Mamlaka ya Hifadhi za Taifa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imepokea malalamiko na tuhuma kutoka Chama cha Wafugaji Tanzania (CCWT) kuwa bado kuna vitendo vya uonevu vinavyofanywa na baadhi ya Wtendaji wa Mamlaka za Hifadhi za Taifa dhidi ya Wafugaji. Vitendo hivyo ni pamoja na: -

a) Utaifishaji wa mifugo usiozingatia sharia

b) Mauaji ya Mifugo na Wafugaji

c) Wizi wa Mifugo

d) Watendaji wa Serikali kukaidi amri za Mahakama

e) Mifugo kuliwa na Wanyamapori bila Wafugaji kulipwa fidia

f) Mifugo kufa kwa kukosa huduma muhimu kama malisho, maji, matibabu na chanjo.

g) Mifugo kuingizwa kwenye hifadhi na mapori ya akiba kwa nguvu na Wafugaji kudaiwa kulipa faini ili kuokoa mifugo yao.

## SEHEMU YA TATU

---

### MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** baada ya Kamati kufanya uchambuzi katika maeneo mbalimbali ya majukumu ya Wizara ikiwa ni pamoja na Maombi ya Fedha kwa Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2020/2021, naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kama ifuatavyo: -

**1. Kuongezeka kwa Mazao ya Samaki Katika Ziwa Victoria ni muhimu ongezeko hili likaleta manufaa kwa Serikali na kwa wavuvi wenyewe.**

**Mheshimiwa Spika,** Serikali imekuwa ikifanya operesheni mbalimbali za kudhibiti uvuvi haramu na matumizi ya dhana za uvuvi kwa lengo la kulinda mazalia ya samaki na kudhibiti uharibifu wa mazingira na kumaliza tatizo la kuuza samaki kwa magendo**.**

**Mheshimiwa Spika,** operesheni hizi zimekuwa za manufaa kwani Serikali imeweza kwa kiasi kikubwa kudhibiti uvuvi haramu na dhana za uvuvi zisizokubalika kwa mujibu wa sheria, hatua hii imesaidia kuongezeka kwa samaki hususan katika Ziwa Victoria.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa manufaa haya, pamoja na pongezi hizo, Kamati inaishauri Serikali kuwa, ongezeko la samaki katika Ziwa Victoria ni lazima liendane na kuongezeka na kuimarika kwa kipato cha wavuvi wanaozunguka Ziwa Victroria, kuongezeka kwa viwanda vya kuchakata samaki pamoja na kupungua kwa bei ya samaki ili wananchi wa kawaida waweze kumudu kula samaki kutokana na virutubisho muhimu vilivyoko kwenye samaki kwa faida kwa mwili wa binadamu.

**2. Changamoto ya Viwanda vya Kuchakata Mazao ya Samaki kuhamishia shughuli za uzalishaji nchi jirani kutokana na mazingira mazuri ya kuvutia wawekezaji kwenye nchi hizo.**

**Mheshimiwa Spika,** ili kuvutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi, Kamati inaishauri Serikali kufanya mapitio ya Sheria ya

Uvuvi ya Mwaka 2003 ambayo imepitwa na wakati na haiendani na mazingra ya sasa ya kufanya biashara kwa ushindani.

**Mheshimiwa Spika,** kuendelea kutumika kwa Sheria hii kumepelekea nchi yetu kushindwa kuenenda kiushindani kwani tumeshuhudia viwanda vya kusindika mazao ya uvuvi kufungwa na viwanda hivyo hivyo kwenda kufunguliwa nchi jirani na hivyo kuikosesha nchi mapato yatokanayo na kodi na fursa za ajira kwa Watanzania na hasa vijana.

**3. Athari za Ugonjwa wa Homa ya Mapafu (COVID 19) kwa Sekta ya Uvuvi**

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa makusanyo ya maduhuli kwa sekta ya uvuvi kwa kiasi kikubwa hutokana na mauzo ya samaki nje ya nchi na kwa kuwa nchi za Ulaya Mashariki hususan Spain na Italia na Asia ambao ndio wateja wakubwa wa samaki wa nchi yetu na kwa kuwa nchi hizo zimeathirika kwa kiasi kikubwa na Ugonjwa wa Homa ya Mapafu, upo uwezekano mkubwa wa mauzo yatokanayo na samaki kupungua. Kufuatia changamoto hiyo, Kamati inaishauri Serikali kufanya upya tathimini ya maoteo ya maduhuli ili kuwa na bajeti yenye uhalisia. Kamati inaamini kwa kufanya hivi Wizara itaweza kupanga na kutekeleza mipango yake ya maendeleo kulingana na hali halisi.

**Mheshimiwa Spika,** ni ukweli usiopingika kuwa bajeti za maendeleo kwa kiasi kikubwa huchangiwa na wadau wa maendeleo. Kutokana na nchi nyingi za Ulaya na Marekani kuathirika na ugonjwa wa **COVID- 19** na kupelekea uchumi wa nchi hizo na uchumi wa dunia kuyumba, Kamati inaishauri Serikali kupanga mipango ya maendeleo huku ikizingatia athari za ugonjwa wa corona kiuchumi. Hatua hii itasaidia kupanga mipango inayotekelezeka.

**4. Kuendelea kwa Migogoro kati ya Wafugaji na Mamlaka za Hifadhi za Taifa**

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia malalamiko ya Wafugaji kuhusu uonevu unaofanywa na baadhi ya Askari wa Wanyamapori dhidi ya Wafugaji na mifugo yao, Kamati inaishauri Serikali

kufanyia kazi malalamiko yalioainishwa katika taarifa hii, na endapo itabainika wahusika wachukuliwe hatua za kisheria na kinidhamu. Aidha, ni muhimu kwa Serikali kudumisha Utawala Bora kwa kutekeleza maamuzi na hukumu zilizotolewa na Mahakama mbalimbali nchini dhidi ya fidia na maamuzi yaliyotolewa kuhusu Wafugaji kurudishiwa mifugo yao.

**Mheshimiwa Spika**, ni muhimu pia kwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi ishirikiane na Wizara ya Maliasili na Utalii kutoa elimu ya mara kwa mara kwa Wafugaji na Askari wa Wanyamapori kuhusu umuhimu wa kuheshimu mipaka na kazi za kila upande.

**Mheshimiwa Spika,** vilevile ni muhimu kwa Wizara kushirikiana na Halmashauri kutoa elimu za mara kwa mara kuhusu ufugaji bora na wa kibiashara pamoja na kanuni bora za ufugaji. Aidha ni vyema Halmashauri za Wilaya zikatenga maeneo kwa ajili ya malisho ili kupunguza migogoro.

## SEHEMU YA NNE

### HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Maoni na Ushauri wa Kamati kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

**Mheshimiwa Spika,** napenda pia kumpongeza na kumshukuru Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Luhaga Jolsen Mpina, (Mb), na Naibu Waziri Mhe. Abdallah Hamis Ulega (Mb), Katibu Mkuu – Uvuvi Dkt. Rashid Tamatamah na Katibu Mkuu - Mifugo Prof. Elisante Ole Gabriel pamoja na Wataalamu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa ushirikiano walioipa Kamati wakati Kamati ikichambua na kujadili Bajeti ya Wizara hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa dhati kabisa napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na michango yao

waliyoitoa wakati wa kupitia na kuchambua bajeti ya Wizara pamoja na kuandaa taarifa hii hadi kukamilika kwake. Naomba kuwatambua kwa kuwataja majina kama ilivyoainishwa katika Tartifa ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** mwisho napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Stephen Kagaigai, Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Michael Chikokoto, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Gerald Magili pamoja na Sekreterieti ya Kamati ambao ni Ndg. Virgil Mtui, Ndg. Rachel Nyega na Ndg Jane Ndulesi kwa kuihudumia Kamati pamoja na kukamilisha taarifa hii kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, naliomba sasa Bunge lako lipokee, lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 kama yalivyowasilishwa na Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Mahmoud Hassan Mgimwa, (Mb)
**MWENYEKITI,**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO,**
**MIFUGO NA MAJI**
14 MEI, 2020

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge sitamuita Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa sababu taarifa yake haikuwekwa mezani. Ninayo majina hapa ya Waheshimiwa Wabunge mbalimbali kupitia vyama vyao ambao wameomba kuchangia, tutaanza na Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula, atafuatiwa na Mheshimiwa James Kinyasi Milya, Mheshimiwa Ahmed Ally Salum ajiandae lakini pia niwataje Waheshimiwa Wabunge watakaochangia kutokea Msekwa. Mheshimiwa James Kinyasi Millya, Mheshimiwa

Emmanuel Papian John, Mheshimiwa Oscar Rwegasira Mukasa, Mheshimiwa Jitu Soni, Mheshimiwa Anna Gidarya, Mheshimiwa Rose Sukum Kamili, Mheshimiwa Mussa Bakar Mbarouk na Mheshimiwa Vedasto Edgar Ngombale watachangia kutokea Msekwa. Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na mimi kwa kunipa nafasi walau ya...

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kila Mbunge anayeitwa anachangia dakika tano, Mheshimiwa Stanslaus Mabula.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na kwa msingi huo kwa kupata nafasi ya kuchangia. Mimi ningependa kidogo niguse kwenye hii Wizara ya Sekta ya Uvuvi na Mifugo na hasa kwenye eneo la Uvuvi kwenye Sekta ya Uvuvi na Viwanda. Ni kweli kwamba Wizara imefanya kazi kubwa sana katika kudhibiti na kulinda rasilimali za Ziwa Victoria hususani Samaki, lakini nikiungana na Mwenyekiti wa Kamati pale alipishia mafanikio haya ya udhibiti wa mazao ya Ziwa Victoria, kwa maana ya samaki, ni lazima yaendane na matokeo halisi kwa wananchi wanaofanya shughuli za uvuvi kwenye Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Naibu Spika, utakumbuka kwamba operesheni zote zilizopita kwa namna moja ama nyingine zitakuwa zimeathiri watu wengi sana, lakini tunapozungumza habari ya biashara ya samaki na Mwenyekiti wa Kamati amesema vizuri vizuri ni lazima iendane sambamba na watu wanaohusika kwenye *chain* nzima. Hapa tunawazungumzia wavuvi, tunazungumza wachuuzi wakubwa na tunazungumza wenye viwanda. Mimi ambaye ninatoka Mwanza pale katika ya Mji na wavuvi wote wanaofanya biashara za samaki wanazokuja Mwanza; ni lazima Wizara na Mheshimiwa Waziri na najua anafahamu vizuri biashara inayotokana ni Ziwa Victoria *source* yake kwa maana ya chanzo kinachotoa samaki ni kimoja lakini soko wanapopelekwa samaki hawa ni moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi na Uganda ndio washindani kwenye sekta hii kwa sababu ukubwa wa Ziwa Victoria sehemu ya Uganda ni *square* kilomita isizopungua 31,000 wakati sisi kama Tanzania tuna *square* kilomita 33,700. Unaweza kuona ni kwa namna gani tunashindana kwa ukaribu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vilivyokuwa vinachakata samaki Mwanza; kutokana na tozo nyingi ambazo kiukweli zimerudisha maisha ya watu nyuma, watu wamelazimika kuhamisha viwanda vyote kwenda Uganda. Nitakupa mfano Mheshimiwa Waziri utakubaliana na mimi toka mwaka 2015 mpaka 2017 Mwanza ilikuwa na viwanda takribani 7 mpaka 9 vya uchakataji wa samaki, wakati huo Uganda walikuwa na viwanda 6 peke yake leo Uganda wanazungumzia viwanda 13 na wavuvi wetu wakubwa wote wamehamia huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa hiyo mimi ninachotaka kumwomba Mheshimiwa Waziri kwa maana ya kuokoa muda hembu tuangalie tozo tunazozitoa na hii mirabaha mikubwa ambayo haiendani kabisa. Mfano mzuri tu tunaambiwa kilo moja ya samaki kwa kule Uganda inalipishwa mrabaha wa senti tano, sisi Tanzania senti 24, unaweza kuona tofuati hii kubwa; hatuwezi kuwasaidia. Hata hawa watu wenye viwanda leo wanapolalamika ni kwa sababu mtu wa kwanza anayeumia, na si kwamba wao wanaweza kuwa wanapata faida kubwa sana, lakini yule mtu ambaye ni mvuvi ambaye hatumuangalii kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata sheria tuliyopitisha hapa juzi Waheshimiwa Wabunge walipiga kelele sana lakini leo tunapoweka wigo wa faini kutoka milioni moja labda mpaka milioni 50 hapa katikati Mheshimiwa Waziri nataka nikuhakikishie, inawezekana umefanya kwa nia njema lakini umetengeneza kichaka ambacho kinakwenda kuumiza sana wavuvi wadogo hawatapa faida kupitia hapa. Ni kweli kwamba lazima sasa tuone kazi nzuri hii mliyoifanya ya udhibiti ya uimarishaji inakwenda kuwasidia wavuvi hawa wadogo ambao ni *chain* inayoungisha na wanunuzi inakwenda moja

kwa moja sambamba kwenye viwanda. Mimi naamini lazima tupitie kwenye moto ili tufike pale sehemu inapokwenda kuwa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo Mheshimiwa Mpina nategemea sana bajeti hii inakwenda sasa kuamsha hali ya wavuvi, inakwenda kuamsha hali ya wanunuzi, inakwenda kuamsha hali na mchango wa viwanda vyetu vikafanye kazi na tuweze kuongeza ajira ya kutosha ili watu wetu, vijana wetu ambao wamekimbilia kwenye biashara huria za umachinga na nyingine warudi kwenye kazi zao nyingine walizokuwa wanazifanya. Hii ndio kazi ya Serikali Awamu ya Tano kila siku tunasema. Tulikuwa tunarekebisha tunatengeneza njia sasa twende kwenye sehemu ambayo watu wetu wanakwenda kupata faida na kuona umuhimu wa Serikali hii ambayo imewatengenezea mazingira yanayokwenda kuwatoa walipo na kuwavusha kwenda sehemu nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua yako mengo lakini naomba niunge mkono hoja asilimia 100 na niipongeze sana Wizara na Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kuendelea kusimamia misingi na kulinda rasilimali za taifa. Hongereni sana na Mungu aendelee kutubariki ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa James Kinyasi Milya atachangia kutokea Msekwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Ahmed Ally Salum, Mheshimiwa Anna Gidarya ajiandae.

**MHE. JAMES K. MILLYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi nishukuru kama ambavyo wenzangu wameshukuru. Kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri, jana tumekesha naye karibu siku nzima kwa ajili ya kesi ya wale wafugaji wakiwemo akina Lenina na akina Isaya wanaotaka Pori la Swagaswaga. Tumekaa naye mpaka usiku saa mbili usiku pamoja na timu yake. Nimshukuru kipekee pia Naibu Waziri wa Maliasili ndugu yangu Mheshimiwa Kanyasu kwa sababu ya msaada mkubwa kama huo; wafugaji hakika kwa namna

ya pekee Serikali ya Mheshimiwa John Pombe Joseph Magufuli inawasaidia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kama Mbunge ninayetokana na wafugaji, letu kwa baada ya miaka mitano ya kufanya tathimini ni kumshukuru kabisa Mheshimiwa Rais kwa kuwa amesaidia wafugaji kupita kiasi. Baada ya tathimini ya miaka mitano Mheshimiwa Rais ameunda timu ya Mawaziri nane kuzunguka nchi nzima ili kuwasaidia wafugaji. Vilevile kama haitoshi ametoa mapori takriban 12, akaondoa misitu saba kwa ajili ya kuwasaidia wafugaji. Kwa ripoti ya Mheshimiwa Waziri hata mapori 14 mengine yatafutwa baada ya muda mfupi ili kuwasaidia wafugaji nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi langu kama mfugaji na Mbunge ninayewawakilisha wafugaji nikushukuru nakumuomba Mheshimiwa Rais Mungu aendelee kumjalia sana. Wafugaji wema huo hatutasahau hata siku moja Mungu aendelee kukulinda huko; ulipo wafugaji wanafurahi sana. Sisi tunataka tu 2020 kwa kweli utaona shukrani zetu kama wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna machache ambayo ningeomba Wizara hii iyasimamie. Moja ni kulinda maeneo ya wafugaji. Mfano kule kwetu Simbanjiro kuna watu wanaomba kabisa kugombea nafasi za Uenyekiti na Udiwani kwa sababu tu ya kuuza maeneo ya wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niombe Mheshimiwa Waziri wewe ni mchapa kazi na mimi nakukubali sana niombe; natoa mfano mmoja tu; kuna shamba la muwekezaji mmoja anaitwa Geri Hukus, alikuja takriban miaka ya 70 akaomba kwa mfugani mmoja wa Kimasai eneo la hekari 2500. Yule mzungu baada ya kuona hili pori lipo kubwa sana akaongeza na maeneo karibu heka 8500 sasa hivi. Hajapewa na mtu yoyote anamiliki mwenyewe na anaanza kwa sasa hivi kuuza kwa wageni wengine. Mimi niombe Mheshimiwa Waziri kwa sababu wewe unasimamia eneo hili la mifugo ni vyema kulinda maeneo ya wafugaji. Niombe tusaidiane wote ili kusaidia wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto nyingine Mheshimiwa Waziri ni hili na akina Lenina; tumesimamia jana, juzi, tumemuona Mzee wa kifugaji. Ni mfano mmoja tu, wako akina Isaya wanaotoka Kondoa, Mheshimiwa Sannda ameongea sana. Tunaomba muwasaidie sana na ikiwezekana Wizara hizi nane zikutane mara moja kama ambavyo wameonyesha ishara ya kusaidia. Haiwezekani wanakamata mifugo ya wafugaji, wanawakabidhi watu ambao ni wanyamapori, hawana uwezo wowote wa kufunga, kwa nini wasipeleke kwenye *Ranch* za Taifa ili ng'ombe wale wafugwe, mwisho wa siku kesi zitakapokwisha wafugaji wakute wana mifugo yao, hawajakufa, wameongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mahakama imetoa hukumu bado wanaendelea kushikilia mifugo yao, hiyo siyo sahihi. Sisi kama wafugaji hatukubaliani na hilo, halikubaliki popote, naomba tufanye kama ni *compromise,* sisi hatutaki kujua wale waliokosea sheria kama ni wahifadhi, tunaomba watusaidie jambo moja; kwa mfano, Mheshimiwa Mbunge wa Chemba, ndugu yangu amesaidia pia sana katika mambo haya. Na mimi niseme tu kitu kimoja; wale ambao ni wahifadhi watusaidie, kama wanataka kufanya compromise kama ambayo walifanya Rwanda kwenye *Gachacha court* baada ya mauaji yale ya kimbari, watupe mifugo yetu, hatutaki kujua wale waliokosea ni akina nani, lakini haiwezekani mfugaji wakampa mifugo 163 wakati wamekamata mifugo 300, wanampa 160 wakati wamekamata 300, miaka mitatu walikuwa wawe mifugo karibu 900. Sisi tunasema hivi, watukabidhi mifugo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine kwa kumalizia tu, nikuombe nimesikia kuna fununu kule Ngorongoro...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. JAMES K. MILLYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa haya machache niombe wafugaji walindwe, nami niunge

mkono hoja kwa asilimia mia moja, wafugaji wanafaa sana na Serikali hii...

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. JAMES K. MILLYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, shukurani, shukurani. Mheshimiwa Ahmed Ally Salum atafuatiwa na Mheshimiwa Anna Gidarya, Mheshimiwa Edwin Sannda ajiandae.

**MHE. AHMED A. SALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia Wizara hii ya mdogo wangu, Mheshimiwa Mpina, Waziri wa Mifugo pamoja na Naibu wake. Wote kwa pamoja nawapongeza sana kwa kazi kubwa sana wanayofanya, kwa kweli Wizara sasa inaonekana kuelekea vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio mara nyingi kunakuwepo na changamoto ndogo ndogo. Tanzania tuna mifugo; tuna ng'ombe zaidi ya milioni 33.4, tuna mbuzi milioni 21.9, tuna kondoo milioni 5.3, lakini bado hatujafaidika sana na biashara hii ya kuuza nyama nchi za nje. Katika kazi au mafanikio mazuri kutokana na mahusiano mazuri ambayo mara nyingi huwa tunakutana nchi za nje, mimi pamoja na baadhi ya wafanyabiashara katika nchi za Kiarabu tulikuwa tukiongea mambo mengi sana hasa nyama ndani ya Tanzania. Wakasema Tanzania mna nyama nzuri sana na mnaweza mkanufaika sana na biashara ya nyama nje ya nchi na wakanieleza mambo ambayo nilikuwa hata sikuyaelewa. Wakaniambia kwamba Kenya wana viwanda vinne, wanauza kwao na hawana nyama za kutosha, nyama zenyewe wanazinunua Tanzania, ninyi kwa nini msifanye kazi kama hiyo? Nikawaambia mbona hiyo kazi ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekuja hapa nimeongea na Mheshimiwa Waziri, katika mahusiano yale nimejaribu sana nimeweza sana, kwanza na-*declare interest* mimi ni mfanyabiashara lakini siyo biashara za nyama. Nimeweza

kuwaleta hawa wafanyabiashara na muda siyo mrefu tutaanza biashara kubwa mno hii ya nyama katika Jamhuri yetu ya Muungano wa Tanzania. Mheshimiwa Waziri anajua nimemweleza haya kwa urefu na hapa tulipo ukingoni labda asilimia 95. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kazi kubwa ambayo naiomba kwa Wizara ni kujipanga tu. Ni kujipanga ili tuiweze na tuiweze kweli kweli yaani, kwa maana kwamba rasilimali hizi za mifugo tunazo sisi. Shinyanga peke yake mimi nina kama ng'ombe milioni mbili. Kwa maana hiyo, tunapoleta biashara maslahi yake ni mapana sana, yanakwenda kwenye kodi za nchi, yanakwenda kwenye ajira, yanakwenda mpaka kwa wafugaji kule chini. Sasa kwa *order* tu ambayo wameitaka sasa hivi, Nchi za Kiarabu ambao sasa hivi tunafanya mawasiliano nao ni milioni 16.5 *kilograms* kwa kila miezi mitatu. Utaona sasa namna gani hapo tunatakiwa tujipange hasa kufanya biashara ya namna hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikwambie, mimi ni Mbunge, ni Mtanzania na inaniuma sana kuona kwamba Wakenya wananufaika sana kwa mifugo yetu na wanapunguza sana urasimu uliokuwa ambao wanauona labda sisi kwa namna moja ama nyingine unakuwa na ukakasi fulani katika *export* ya nyama katika Nchi yao ya Kenya. Wananunua Kenya ng'ombe wasiopungua 10,000 kila mwezi ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Wananunua 10,000 ng'ombe Wakenya, wananunua wale ng'ombe, wanawa-*process,* halafu wao wana-*export* kama ng'ombe wao wakati ng'ombe ni wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niseme tu kwa hili nitasimama vizuri. Mheshimiwa Waziri Mpina nakuhakikishia kabisa tutasimama vizuri tutakapoipata hii kazi usimame ili sasa tufungue ukurasa mpya kabisa wa mifugo katika Jamhuri yetu ya Muungano wa Tanzania. Wameni-*promise* kwamba, kama nyama itakuwa nzuri, kama *service* itakuwa nzuri, wataongeza mpaka kilo milioni 12 kwa mwaka. Utaona namna gani tunakwenda kunufaika kabisa na zaidi ya milioni 100 mpaka milioni *120 dollars per year.* Hiyo inakwenda

kunufaisha Watanzania na wafugaji wote walioko Tanzania na kwa kweli itakuwa ni jambo jema sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri, Katibu Mkuu, Naibu Waziri kwa kazi...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Kengele imeshagonga, Mheshimiwa ahsante sana.

**MHE. AHMED A. SALUM:** ...Mheshimiwa Waziri tuko pamoja sana...

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Anna Gidarya atachangia kutokea Msekwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Edwin Sannda na Mheshimiwa Julius Kalanga Laizer ajiandae.

Mheshimiwa Anna Gidarya kutokea Msekwa. Hayupo, Mheshimiwa Edwin Sannda atafuatiwa na Mheshimiwa Julius Kalanga Laizer na Mheshimiwa Maftah Abdallah Nachuma ajiandae.

**MHE. EDWIN M. SANNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Nitumie fursa hii adhimu kabisa kupongeza Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri Makatibu Wakuu na timu nzima kwa hotuba yao nzuri, hotuba ambayo inatia matumaini, lakini pia na kwa kazi nzuri ambayo wameendelea kuifanya pamoja na Serikali nzima ya Awamu ya Tano chini ya Dkt. John Pombe Magufuli, nawapongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo pamoja na pongezi ambazo nimewapa Wizara nataka niwaulize maswali mahususi sana. La kwanza; hivi ni nini nafasi yao na wajibu

wao katika kulinda na kusimamia haki za wafugaji na mifugo? Nauliza hivi kwa kulingania nini? Wiki iliyopita kwenye Wizara ya Maliasili nilizungumza kuhusu wafugaji wa Kondoa, Chemba na Kiteto ambapo huwa wanapata adha kutokea kwenye hifadhi, leo sitazungumzia upande huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Mifugo ipo, mifugo inanyanyasika, najua sasa hivi tunalifanyia kazi lakini kuna kesi mahususi kabisa za wafugaji wetu ambao ndiyo wanyonge wa Tanzania, ambapo siku zote Rais wetu mpendwa anasimama na kusema ni mtetezi wa wanyonge na hawa ndiyo wasaidizi wake Rais huyu. Tuna kesi hizi kama zile za Kondoa pale maeneo yanayopakana na Pori la Akiba ya Swagaswaga, Pori la Akiba la Mkungunero, watu wetu wa Kondoa, watu wetu wa Chemba, watu wetu wa Kiteto na maeneo mengine hawa ni wawakilishi tu wa wafugaji wengi wa Tanzania ambao wanapata adha na mateso ya namna hii. Kwa niaba ya wafugaji wote, hebu watuambie wanafanya nini kuhakikisha watu hawa wanapata haki zao za mifugo? Anakamatwa mtu kama juzi...

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Edwin Sannda kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Joseph Raman Selasini

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimpe taarifa pia kwamba zipo kesi nyingi sana za wafugaji wakidhulumiwa mifugo yao zilizoamuliwa na Mahakama zetu, Mahakama Kuu mpaka Mahakama ya Rufaa, lakini kwa bahati mbaya sana na sijui ni kwa sababu gani hawapewi mifugo yao au hawapewi ile haki ambayo imeamuliwa na Mahakama.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. EDWIN M. SANNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea taarifa hiyo kwa mikono miwili, namshukuru sana

kaka yangu Selasini kwa kuunga yale ambayo nataka kuyazungumza.

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa niliowataja wachache tu kama wawakilishi wa wafugaji nchi nzima wameenda Mahakamani, wameshinda ngazi zote za Wilaya, wameshinda Mkoa Makao Makuu, lakini kati ya mifugo 600 mtu anapewa mifugo 100. Kwa mfano, yule Mzee Lenina wa Kiteto; mfano, Isaya wa Serya pale Kondoa, kati ya mifugo 145 anapewa mifugo 21; yuko Bibi yule ana mifugo 22 hapewi au anapewa mifugo mitatu. Hivi hawa kama Wizara ya Mifugo wanawasaidiaje hawa na maelezo mifugo imekufa.

Ninachotaka kusikia kutoka kwa Mheshimiwa Waziri pamoja na sifa nyingi nilizompa, hawa watu lini watapata mifugo yao? Wakati anakuja kutupa mrejesho atuambie ni lini watu hawa watu watapata mifugo yao. Najua wamekaa na Waziri wa Katiba na Sheria na Waziri wa Maliasili, najua watakaa kama alivyoelezea kwenye taarifa yake, watakaa na Wizara zote nane zinazohusiana ili waweze kutatua migongano ya kisheria ambayo inaingilia sana maslahi ya mifugo, maslahi ya wahifadhi, ya kilimo na kadhalika, watupe majibu hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nataka kuelewa, hivi inapofika hatua ambapo *DPP* ndiyo wa Serikali, huku kwenye wahifadhi yupo lakini hata kwenye mifugo yupo; anakata rufaa kwenye ngazi ya Wilaya; mfugaji anashinda, anakwenda Mahakama Kuu, *DPP* anakata rufaa, nini hasa *interest* yake? Unajua hiki kitu kinanifanya natafakari sana, najiuliza ana maslahi gani? *DPP* yeye ni mwakilishi wa wote, lakini anakata rufaa, inatupa masala mengi ya kujiuliza, huenda, yaani tuna maswali mengi kuliko majibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe Mheshimiwa Waziri, nafahamu uchapakazi wake, nafahamu dhamira yake njema sambamba na dhamira ya Serikali yetu na Awamu ya Tano. Tunataka wanyonge hawa wafugaji wa Tanzania, wafugaji wa Kondoa, wafugaji wa Chemba wapate haki zao na atuambie kama Wizara yake wanasimama vipi katika hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru na naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Julius Kalanga Laizer atafuatiwa na Mheshimiwa Maftah Abdallah Nachuma na Mheshimiwa Rose Kamili Sukum ajiandae.

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia jioni ya leo katika Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Kwanza nitumie nafasi hii kumpongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uamuzi wake wa dhati wa kurejesha baadhi ya mapori tengefu kwa maslahi mapana ya wafugaji na wakulima wa nchi hii. Tunamshukuru sana na tunampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze pia Wizara ya mifugo; kama ambavyo nimesema miaka miwili iliyopita katika Bunge hili bada ya Waziri Mpina kupewa Wizara hii ndiyo tunaanza kusikia Wizara ikitoa sauti ikiwatetea wafugaji na tunaowawakilisha. Tunawashukuru, tunawapongeza sana, wasonge mbele, sisi tunawaombea dua Mungu aendelee kuwapigania.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nina mambo mawili. Jambo la kwanza, ni kumwomba Mheshimiwa Rais; kwa kuwa alionesha nia ya kukutana na wafugaji baada ya janga hili la *corona,* Rais akutane na wafugaji kama dhamira yake ilivyomtuma, kwa sababu yako mengi tunatamani kumwambia Rais ambapo pengine wasaidizi wake hawamfikishii matatizo tunayokutana nayo kama wafugaji wa nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kusema kwa nini wafugaji hawarudishiwi ng'ombe wao? Naomba Serikali na Bunge lako lisikie hili; tunataka Serikali ifanye tathmini ya *auditing* ya miaka mitano ya ng'ombe wanaokamatwa kwenye mapori tengefu na ambayo yametaifishwa. Kama kiwango cha ng'ombe waliokamatwa na kiwango cha fedha kinachoingia Serikalini kama kinafanana. Ni mara

nyingi unakuta ng'ombe wanakamatwa 500 lakini ng'ombe wanaokuja kuuzwa wakaipatia Serikali fedha hawazidi 200. Sababu unazopewa ng'ombe wamekufa, ng'ombe wanakufa katika hifadhi ambayo kuna majani, kuna maji wakati huko ambako hakuna majani kule kwa wafugaji hawafi, kinatokea nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, namwambia Mheshimiwa Waziri, huu ni wizi unaofanywa makusudi na Maafisa wa Maliasili katika nchi yetu. Ukifanyika ukaguzi, watajua madudu yanayofanyika, kwa nini ng'ombe hawarudishwi? Ng'ombe hawarudishwi kwa sababu wanapokamatwa, kesi ikiisha, ukienda kutafuta hawa ng'ombe hawapo sasa watarudisha nini? Ndiyo maana wanakata rufaa kila siku kwa sababu wameshawauza. Tunakutana na ng'ombe hata juzi Jumanne kule Monduli tulikutana na ng'ombe 20 wa huyo mtu anaitwa Lenina wakiuzwa ambao wameuzwa na watu wa hifadhi. Kwa hiyo hawataki kurejesha ng'ombe kwa sababu hawapo, wameshakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila siku wakikamata ng'ombe wanaanza kuuza siku ya kwanza huku wanasema wapo hifadhini mpaka wakati ule wakati kesi inafika mwisho, lakini sisi twende kwa nani? Kwa nini watulazimishe kila jambo twende kwa Rais? Mheshimiwa Waziri yupo Rais amemwamini, nini sauti yake dhidi ya hili jambo, kwa sababu yeye ndiye mwenye dhamana tunamkimbilia, kwa nini Wizara nyingine iwanyanyase watu anaowasimamia yeye, uwakilishi wake ambao tunauona hapa, tunaomba kauli ya Serikali kwa kitu ambacho Mahakama imeamua. Tunakuwa watu wa ajabu ambao hatuheshimu hata Mahakama zetu. Serikali ni ya kwetu, Mahakama ni za kwetu, *DPP* hakati rufaa anasema tu ng'ombe hawatoki na wote tumekaa kimya, hapana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niombe jambo lingine moja Mheshimiwa Waziri, Wizara yake iweze kutusaidia; najua iko sheria ya usimamizi wa nyama ambayo inataka machinjio ya *standards* yawepo katika maeneo yetu, lakini katika uhalisia wa mazingira yetu tunaoishi kijijini huwezi kuchukua ng'ombe au mbuzi mmoja kwenda kuchinja

kilometa 80 na kurudisha kwenye kilometa 80, huwezi kufanya hiyo biashara. Naomba Wizara kama ni sheria ipitie upya namna gani tunaweza tukawasaidia wafugaji kuhusu sera hii na sheria hii ya machinjio ambayo wafugaji wamenyimwa kuchinja kwenye maeneo yao kwa sababu tu ya kuagizwa kwamba ili uwe na machinjio ya kisasa lazima uwe na hekari 10, kwa sasa ardhi imekuwa ndogo, hizo hekari 10 zinapatikana wapi na kwa nini msingi wa ile sheria haukusimamiwa tangu mwanzo? Naomba wapitie jambo hili ili wafugaji hawa waache kupata shida kwa sababu katika maeneo yetu tunapata shida.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Maftah Abdallah Nachuma atafuatiwa na Mheshimiwa Rose Kamili Sukum na Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate ajiandae.

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nami nizungumze kwa dakika hizi chache juu ya Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza; katika Jimbo langu, Jimbo la Mtwara Mjini, wananchi wa Mitaa ya Mikindani, Kiangu, maeneo ya Kianga, Mtepwezi kwa kiasi kikubwa shughuli zao za uchumi ni uvuvi na nimezungumza na Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri muda mrefu sana kwa sababu Serikali ilikuwa na mkakati wa kuhakikisha kwamba wavuvi wanaingia kwenye vikundi mbalimbali. Mtwara mimi kama Mbunge niliwahamasisha wavuvi wangu wa maeneo ya Mikindani, Mtepwezi, Kiangu, Miseti wote waingie kwenye vikundi waweze kujisajili na mwisho wa siku Serikali kama ilivyoahidi ndani ya Bunge katika Bajeti zake zote tatu nimekuwa nazipitia na kuzisikiliza, kwamba wavuvi hawa waingie kwenye vikundi wapewe vifaa vya kuvulia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimemwendea Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri mara nyingi akaniahidi kwamba atawapatia wavuvi wa Manispaa ya Mtwara

Mikindani vifaa vya kuvulia ikiwemo maboti ya kisasa kwa ajili ya kuvulia samaki waweze kuvua uvuvi wenye tija. Mpaka leo ninavyozungumza hii ni Bajeti yangu ya mwisho kuchangia Wizara hii, bado Wizara haijawafanyia vya kutosha wavuvi wa Manispaa ya Mtwara-Mikindani. Kwa hiyo, niiombe sana Wizara hii, nimwombe Mheshimiwa Waziri vile vikundi ambavyo wamekuwa wakivipatia basi na Mtwara Mjini safari hii naomba wavuvi wangu hawa waangaliwe, waweze kukopeshwa vile vifaa vya uvuvi zikiwemo Boti za kisasa za kuvulia kwa sababu wametoa katika maeneo mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili sambamba na hilo, kuna Chuo cha Uvuvi pale Mtwara-Mikindani ambacho kimefunguliwa hivi karibuni tu, lakini bado kile chuo hakina vifaa vya kuvulia vya kutosha, vifaa vya kufanyia utafiti na vifaa vya kusomea kwa sababu vile vifaa vinapaswa viwe vinakwenda bahari kuu, wawe na maboti ya kisasa kwenda kufanya uchunguzi kule juu, lakini nimeenda kuangalia kile chuo bado vifaa havipo vya kutosha. Niiombe Serikali na Wizara kwamba bajeti hii kwa sababu ni bajeti ya mwisho ya mwaka 2020 waweze kutoa vifaa kwa ajili ya chuo kile cha Mikindani ili wanafunzi waweze kujifunza sawasawa kwa vitendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe Serikali niombe wizara kwamba bajeti hii kwasababu ni bajeti ya mwisho ya mwaka 2020 waweze kutoa vifaa kwa ajili ya chuo kile cha mikindani ili wanafunzi waweze kujifunza sawa sawa kwa vitendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo jingine tumekuwa tunazungumza kwa muda mrefu kwamba ili wavuvi waweze kuvua uvuvi wenye tija na samaki wao wakiuza waweze kuondokana na umasikini lazima kuwe na bandari ya uvuvi na Mheshimiwa waziri amegusia kidogo kwamba kuna mchakato wa kwenda kwenye bandari ya uvuvi sasa haijaelezwa kwamba bandari hii itajengwa wapi. Lakini ushauri wangu kwa Serikali kwa kuwa *strip* ya bahari ni kubwa kutoka mtwara mpaka kule tanga mpaka kule zanzibar ni vema basi hizi bandari za uvuvi zikawa kila Mkoa yaani pale

Mtwara kuwe na bandari ya uvuvi kwasababu mvuvi au mnunuzi aweze kutoka Mtwara akaenda kununua *let say* bandari iko bangamoyo huko atoke Mtwara aende kununua samaki bagamoyo*. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashauri Serikali kwamba kila Mkoa kuwe na bandari ya uvuvi, Mtwara kuwe na bandari ya uvuvi, Lindi kuwe na bandari ya uvuvi, lakini kule Tanga kuwe na bandari ya uvuvi, Bagamoyo, Dar es Salaam, tunaamini kwamba wakifanya hivyo wavuvi wetu watavua uvuvi wenye tija na samaki wao kuweza kupata masoko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo jingine tulikuwa tunazungumza hapa kwamba kwa sababu watu wamekaa maeneo ya Pwani tunategemea sana kwa kiasi kikubwa shughuli zetu za uchumi ni kuvua samaki. Lakini sasa kwasababu hatuna vifaa vyenye tija tulikuwa tunaomba Serikali iweze kununua meli kubwa ya uvuvi tumeona kila siku Serikali inajitahidi wizara inajitahidi inakamata meli za nchi nyingine na wanaziona mifano na hapa nimeangalia kwenye hotuba hii nimeweza kuona waziri akionyesha meli ambayo wameikamata imekuja kuvua kwenye bahari kuu bila kupata vibali vya watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niombe wizara inunue meli kubwa kwa ajili ya wavuvi nimekuwa nazungumza natolea mfano mwaka 2008 tulikula samaki wa Magufuli sana pale Chuo kikuu baada ya kwamba amekamata ile meli ya wachina waliweza kuvuliwa samaki wengi sana ambao tulikula wanafunzi wa vyuo vyote Dar es Salaam, lakini hatukuwamaliza mpaka tukakawachoka. Wanunue meli ya uvuvi kwa ajili ya kuwasaidia wavuvi wetu waweze kuingia kwenye vikundi ili waweze kuvua uvuvi wenye tija, uvuvi ambao utawaletea manufaa na kuweza kupata faida ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Rose Sukumu Kamili kutoka Msekwa atafuatiwa na Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate na Mheshimiwa Moshi Seleman Kakoso

ajiandae. Mheshimiwa Rose Kamili kutoka Msekwa, Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate atafuatiwa na Mheshimiwa Moshi Seleman Kakoso, Mheshimiwa Mussa Bakari Mbarouk ajiandae.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kunipa nafasi kuchangia nafasi hii muhimu awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenipa nguvu na afya kuendelea kuwatumikia wananchi wangu wa Jimbo la Kyerwa. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa waziri kwa kazi nzuri ambazo unafanya kwa kweli mawaziri hawa vijana kwa kweli wanachapa kazi nzuri na hawajamangusha Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe sana kuongelea kwenye maeneo ambayo yalitengwa kwa ajili ya wafugaji, tumesikia migogoro mingi ambayo imetokea maeneo mbalimbali migogoro hii imesababishwa na kutokuwa na usimamizi wa maeneo ambayo yametengwa kwa ajili ya wafugaji. Nitoe mfano kama kule kwangu Kyerwa kuna maeneo ambayo yalitengwa na yakapewa *GN* lakini maeneo hayo yalikuja kutumika kinyume na ule utaratibu uliokusudiwa tangu mwanzo na viongozi wa Serikali walikuwepo. Maeneo haya imefika wakati mpaka wamegawiwa watu wengine kinyume na utaratibu na imeleta mtafaruku mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimuombe mheshimiwa waziri umefika Kyerwa umejionea wewe mwenyewe umeona wananchi jinsi ambavyo wameteseka muda mrefu na wamenyanyaswa kupitia haya maeneo, niombe sana mheshimiwa waziri jambo hili ulisimamie ili haya maeneo yaweze kubainishwa na lile ambalo walikusudia tangu mwanzo liweze kusimamiwa vizuri ili kuondoa ugomvi ambao unaweza ukajitokeza kati ya wakulima na wafugaji na niombe sana Mheshimiwa waziri unapohitimiza utueleze kwasababu ulishaunda tume kwa ajili ya Kyerwa utueleze ni lini utamaliza mgogoro huu ili hawa wafugaji ambao wamenyanyasika muda mrefu waweze kufuga kwa uhuru bila shida yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo jingine Mheshimiwa Naibu waziri baada ya kutoka Kyerwa kumekuwa kama namna fulani ya kuwakomoa wafugaji, baada ya wewe kutoka kwanza kule hakuna maeneo ambayo ni rafiki majosho hakuna kitu chochote ambacho huyu mfugaji anaweza akajivunia Serikali imekifanya. Lakini wewe baada ya kutoka wafugaji hawa wameanza kutozwa shilingi 5,000 kila ng'ombe, baraza la madiwani halijawahi kukaa lakini maamuzi yamefanyika huko bila kufuata utaratibu kamati imekaa na kuamuru kila mfugaji ng'ombe mmoja au anatozwa shilingi 5,000 niombe Mheshimiwa waziri uingilie kati ili jambo halikubaliki na nikinyume na utaratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo jingine wabunge wameeleza suala la ng'ombe ambao wanakamatwa, maeneo mengine ng'ombe wanapokamatwa wanapopelekwa kwenye hifadhi, akikaribia tu kidogo na ile hifadhi ng'ombe hao wanakamatwa na kusagwa na kupelekwa kwenye hifadhi na mwisho wa siku ng'ombe hao wengi wanakufa na wafugaji wanatozwa pesa nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe sana hawa wafugaji pamoja na wale wahifadhi waweze kuwa karibu waweze kuwa na urafiki ili kuweza kulinda haya maeneo ambayo yameifadhiwa kuliko kama tunakomoana, tunaviziana hili jambo naona halijakaa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nikupongeze sana Mheshimiwa Naibu Spika na wengine wote kwa kazi nzuri mnazo zifanya Mungu awabariki na muendelee kumtumainia Mungu katika kipindi hiki kigumu cha janga la corona tunaamini Mungu wetu ni mwaminifu atatuvusha na tutavuka salama ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa bilakwate, Mheshimiwa Moshi Seleman Kakoso atafuatiwa na Mheshimiwa Mussa Bakari Mbarouk, Mheshimiwa Qambalo Willy Qulwi ajiandae.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nishukuru sana kunipa nafasi hii, niishukuru sana wizara kwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo, nimshukuru waziri Naibu Waziri, katibu Mkuu kwa jitihada ambazo alizifanya za kutatua migogoro ya wavuvi kwenye Ziwa Tanganyika tunawapongeza kwa dhati Ziwa Tanganyika ni miongoni mwa maziwa ambayo hayatowa fursa nzuri kwa wavuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wavuvi wetu wamekuwa wakivua kwenye ziwa Tanganyika lakini kuna misukosuko mikubwa sana ambayo imekuwa ikijitokeza ya hapa na pale hasa kwa wale watumishi ambao wanafanya kazi kwenye maeneo hayo ya mwambao wa Ziwa Tanganyika. Tunamshukuru waziri alisaidia sana mgogoro wa nyavu ambazo zilionekana kwamba zimekiukwa kisheria wakati zilikuwa sahihi, niombe wizara iendelee kufanya kazi kwa mazingira ambayo yatawasaidia wavuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala ambalo Mheshimiwa Rais alituahidi kiwanda cha kuchakata samaki eneo la Mkoa wa Katavi na waziri alikuwepo wakati ahadi hiyo inatolewa ningependa nijuwe ni jitihada zipi zimefanywa na wizara juu wa mchakato wa kiwanda cha kuchakata samaki eneo la Ziwa Tanganyika Tarafa ya Karema.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la mifugo, Mkoa wa Katavi unaidadi ya mifugo mingi. kwa bahati mbaya sana bado hakujakuwa na eneo la malisho ambayo yangesaidia wafugaji waweze kupeleka Ng'ombe zao wakapata malisho ya kutosha. Niiombe sana wizara ikishirikiana na TAMISEMI watenge maeneo ambayo yatasaidia kupeleka wafugaji wawe na maeneo yao na kuepusha migogoro ya mara kwa mara kati ya wakulima na wafugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo hili ni ishauri Serikali yangu, Serikali ni lazima ije na mpango mkakati wa kuwezesha *ranch* za Taifa, *ranch* zetu za Taifa ni nyingi lakini hazijawekewa fedha za kutosha ili tuweze kuwasaidia

wafugaji *ranch* ni lazima zipewe fedha ambazo zitakuwa na uwezo wa kununua mifugo kutoka kwa wafugaji wadogo wadogo na wao wakanenepesha na zinaponenepeshwa zipelekwe kwenye masoko ya kimataifa hili halijafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kipindi kirefu Serikali tumekuwa tukiishauri lakini bado uwekezaji mdogo ambao upo unafanya sekta hii ya mifugo iwe inapato dogo la Taifa kwa mchango wa kwake. Niombe angalau katika kila *ranch* tutenge shilingi bilioni tano ambazo zitaweza kuwasaidia hawa wanaosimamia hizi *ranch* na kusaidia wafugaji ambao watakuwa na uwezo sasa wa kupeleka kwenye hizo *ranch*, na hizo mifugo zitatoka kwa wafugaji wadogo wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudi tena kwenye eneo la uvuvi, ziwa Tanganyika tumepakana na nchi ya Burundi, Kongo, Zambia wenzetu wamekuwa wakinufaika sana suala zima la uvuvi na kwa bahati mbaya sana nchi ya Burundi wana nyavu haramu zile za filam yaya naomba hili mkalishughulikie kwenye eneo la ziwa Tanganyika zile nyavu ni mbaya ambazo zikidondoka zitaendelea kuuwa kizazi hadi kizazi kinachokuwepo kwenye eneo la uvuvi. Kwa hiyo, naomba hili mlishughulikie na mlifanyie kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niishukuru sana nafasi hii kwa kunipatia na nikuombee wewe katika shughuli zote za mchakato wa Bunge ili uweze kupata nafasi kwenye mchakato wa Jimbo jipya tunakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Amen amen, amen. Waheshimiwa nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Mussa Bakari mbarouk atakayechangia kutokea Msekwa atafuatiwa na Mheshimiwa Qambalo Willy Qulwi, Mheshimiwa Dkt. Balozi Kamala ajiandae.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema kwa kutuwezesha kukutana tena katika shughuli zetu za bunge tukiwa wenye afya nje. Lakini pia, niwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo langu la Tanga Mjini ambao

katika kipindi chote cha miaka mitano hii wamekuwa wakinipa ushirikiano wa kutosha na tumekuwa tuko karibu katika shida na raha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kuchangia katika sekta ya uvuvi na nianze tu kwa kusema kwamba sekta hii ya uvuvi imekuwa na changamoto nyingi lakini miongoni mwa changamoto ambazo zilikuwa ni kero kubwa ni katika suala zima la nyavu na nianze na kwenye suala zima la nyavu za milimita 16. Mji wa Tanga au Jimbo la Tanga…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mussa Bakari Mbarouk, huku bungeni husikiki kabisa sijui kama ni *microphone* imezima ghafla au ni wataalam wetu wa mitambo. Mheshimiwa Mussa Bakari Mbarouk!

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Naibu Spika, naam! Nakuja, nakuja nakuja!

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri sasa unanisikia, naanza upya. Nianze kwa kusema kwamba namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha wote kukutana tena katika shughuli zetu bunge tukiwa wenye afya njema. Lakini pia sitoacha kuwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Tanga kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakinipa katika kipindi chote cha miaka mitano, tumekuwa tuko karibu katika shida na raha, furaha na huzuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nitoe pole kwa wale ambao wamepoteza ndugu zao katika gonjwa hili la Corona ambalo limekuwa nalo ni tishio katika dunia nzima hii na sisi Tanzania tukiwemo niwaombe Mwenyezi Mungu waliotangulia mbele ya haki awasamehe makosa yao awaweke mahala pema peponi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kuchangia kwenye sekta ya uvuvi, Tanga ni miongoni mwa miji ambayo iko pembezoni mwa Bahari ya Hindi. Na shughuli kubwa miongoni mwa shughuli za wakazi wa Tanga ni pamoja na uvuvi lakini tumekuwa na changamoto kwenye suala zima la nyavu. Kwa

mfano kwenye nyavu za milimita 16 Tanga wavuvi wanapozitumia hizi hadi leo imekuwa ni tatizo kubwa na kero wanakamatwa na kudhalilishwa. Sasa nataka kujua tu, inakuwaje nyavu za milimita 16 zinatumika mpaka sasa Dar es Salaam, Kilwa, Mafia, Bagamoyo, Lindi na Mtwara lakini kwa Tanga zinaambiwa bali ni haramu na wavuvi wanasumbuliwa, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa hili nalo alitolee ufafanuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo lakini mambo lingine ni uvuvi wa *ring net*, wavuvi wa Tanga nao wamekuwa hawaruhusiwi pia kuvua uono au dagaa mchele kama tunavyoita kwa kutumia *ring net* na hususan wakati wa mchana. Na wanapovua hata ndoo moja basi inakuwa kosa la kukamatwa na kufikishwa katika vyombo vya kisheria hususan wale watu wa *Coast Zone* ndiyo wanaofanya shughuli hizo, sasa nalo hili pia Mheshimiwa Waziri alitolee ufafanuzi.

Pia kwenye suala la mitungu ya gesi ile mitungi ya *oxygen,* ninavyoijua mitungi ile ya *oxygen* inawasaidia wavuvi wetu kwenda *deep* baharini ili kuangalia samaki na baadaye alete ripoti kwa nahodha ili watu waanze kumwaga nyavu na kuvua samaki. Lakini sasa mitungi ile ambayo pamoja na shughuli hizo za kiuokozi na kuwasaidia kwenda *deep* bado pia kwa Tanga hairuhusiwi na wavuvi wamekuwa wakinipigia simu mara kwa mara kuniuliza. Je, Mheshimiwa Mkoa watu wa Tanga una sheria tofauti zinazotumika nchini Tanzania? Au sisi tunaonekana tuko Kenya? Na wanahoji hivyo kwasababu wamekuwa anasumbuliwa, na Mheshimiwa Waziri ni shahidi, mara kwa mara nimekuwa nikimfuata kujaribu kutafuta suluhu ya matatizo ya wavuvi wetu wa baharini. Kwa hiyo, hilo naomba nalo Mheshimiwa atakapokuja masuala yote hayo ayafanyie upembuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile pia Mheshimiwa niguse kidogo kwenye suala zima...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa usianze jambo jipya kengele imeshagonga. *(Kicheko)*

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Naibu Spika, basi naomba nimalizie kwenye hili la uvuvi kwamba…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Naibu Spika, pia Mheshimiwa Waziri alivyokuja alisikia kilio cha wavuvu. Kuna maeneo ya *Deep Sea* na maeneo ya Kasera kunahitajika masoko ya kisasa ya samaki, hiyo iliyozungumzwa bandari za uvuvi ningeomba Tanga nao ijumuishwe lakini ….

**NAIBU SPIKA:** Sawa Mheshimiwa.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tatizo kubwa ni barabara kutoka katika eneo kubwa la barabara zetu hizi mijini kwenda…. *(Kicheko)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, ahsante sana Mheshimiwa Mussa Bakari Mbarouk, Mheshimiwa Qambalo Willy Qulwi atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Balozi Diodorus Buberwa Kamala, Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi ajiandae.

**MHE. WILLY Q. QAMBALO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi hii ili niweze kutoa ya kwangu machache katika sekta hii ya mifugo ambayo inategemewa karibu na kila mtu. Nianze na eneo la takwimu, ukiangalia katika hotuba zote za Wizara hii kwa miaka ya nyuma hadi leo kumekuwa ongezeko la mifugo kwa aina zote jambo ambalo linanipa wasiwasi kidogo. Nikichukulia mfano wa ng'ombe, ng'ombe mwaka huu tumeambiwa wanakadiriwa

kuwa 33.4 milioni, mwaka jana tuliambiwa 32.5, mwaka juzi 30.5, kwa hiyo, kumekuwa na ongezeko la ng'ombe karibia ng'ombe milioni mbili kila mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni mfugaji sikumbuki mara ya mwisho sensa ya mifugo hawa ya uhakika ilifanyika lini, nina wasi wasi kama takwimu hizo tunazopewa kweli ziko sahihi kiasi hiki? Lakini kama ziko sahihi Wizara imejiandaa kwa kiasi gani ili kuhakikisha ongezeko hili la kila mwaka la karibu ng'ombe milioni 2 linakabiliwa ili baadaye isije ikawa tuna ng'ombe wengi kuliko ambavyo tunatarajia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kuna aina imeathirika zaidi na imepungua sana ni hawa wanyama wanaitwa Punda. Hivi sasa hata ukitaka punda wa kwenda kuchukua mzigo wako hata kwa jirani haumpati kwasababu hapa nyumba kulikuwa na biashara nzuri sana ya kupeleka pundu kwenye masoko ambayo yameibuka na punda wamepungua sana lakini takwimu za Wizara zinasema punda nao wanaongezeka. Kwa hiyo, hizi takwimu naomba ziangaliwe vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ni migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi, niungane na wale wote ambao wameeleza kwa hisia kali kwamba wafugaji wa nchi hii tunawaona kama wakorofi, tunawaona kama wao ndiyo wachokozi kila mara. Lakini wakati mwingine wanalazimika kufanya hivyo kwa sababu ardhi yao yote imechukuliwa, tumewasukuma wafugaji katika maeneo ambayo hata hayatoshi kwa ajili ya mifugo yao. Mheshimiwa Waziri amesema ili kumaliza tatizo hili ni suala la kupima, kupanga na kumilikisha ardhi kwa ajili ya wafugaji. Sijui hii ardhi iko maeneo gani lakini katika eneo ninalotoka hakuna ardhi mpya ambayo inaweza ikatengwa kwa ajili ya wafugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye eneo la biashara ya mifugo minadani. Sisi wafugaji tunapouza, tunauza tu kwa makubaliano, kwamba mtu anakuja anasema nitakupa shilingi 500,000/= au shilingi 1,000,000/=,

lakini kesho asubuhi ng'ombe huyo huyo ambaye amechukuliwa tu kwa makubaliano bila kupimwa uzito wake, akienda kwenye bucha anauzwa kwa kilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nadhani hebu Wizara itusaidie hivi haiwezekani nasi wafugaji tukauza ng'ombe wetu kwa kupimwa kwenye mizani ili nipewe kile kitu ambacho ninastahili. Wafugaji wamekuwa wakipunjwa sana na wafanyabiashara wa mifugo kwa sababu ya makisio yale. Nadhani haishindikani kufanya ubunifu kwenye Wizara hii kuja na mizani ambayo inaweza ikampima ng'ombe wa mfugaji akapata kile ambacho anastahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye eneo la uvuvi. Mimi natokea Karatu na utashangaa kwa nini naongelea uvuvi, kwa sababu sisi kule kwetu ni milimani na hatuna maziwa makubwa na pia hatupakani na bahari. Ziwa Eyasi ni ziwa la maji ya chumvi na ni ziwa ambalo samaki wanapatikana, lakini bahati mbaya sana samaki wetu wa Ziwa Eyasi ambao pia kwa kuwatumia ni wazuri sana, hawawezi kukua kufikia umri ule wa kuvuliwa kwa nyavu za nchi tatu kwa sababu ziwa linakauka kabla ya samaki hawajafikia umri huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tumekuwa tukipata hasara kubwa na wavuvi wale wamekuwa wakiingia kwenye matatizo ya kukamatwa kwa sababu wanavua samaki wale chini ya umri wa nyavu za nchi tatu, lakini tukiwaacha ziwani wanakufa na watakuwa hawana matumizi tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sisi wa Halmashauri ya Karatu tulikuwa tunaomba; na kwa sababu chanzo hiki tunadhani kitakuwa ni chanzo muhimu kwenye kuongeza mapato yetu ya ndani turuhusiwe kuvua samaki wa Ziwa Eyasi kwa kutumia nyavu za nchi mbili kwa sababu hatuwezi kusubiri tutumie nchi tatu, kwa sababu kiangazi kitakuwa kimefika na wale samaki watakufa, Serikali haipati kodi, wananchi hawapati kitoweo na Halmashauri haipati kodi yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tulikuwa tunaomba hebu jambo hili liangaliwe kwa sababu tuko ndani kabisa kwenye bonde la ufa, hawa samaki turuhusiwe kuwavua kwa nyavu za nchi mbili badala ya nchi tatu ili wavuvi wafanye hiyo biashara, nadhani inawezekana. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. WILLY Q. QAMBALO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Dkt. Balozi Diodorus Buberwa Kamala, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi na Mheshimiwa Hasna Sudi Mwilima, ajiandae.

**MHE. BALOZI DKT. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Naib Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii muhimu ya kuchangia machache kwenye bajeti hii. Naomba kwanza nianze kwa kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kazi kubwa liyoifanya ya kuwezesha kumaliza mgogoro uliochukua zaidi ya miaka 18 kati ya Kata Kakunyu na vijiji vinavyozunguka Kata hiyo. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na salamu hizo, nitakuwa mkosefu wa fadhila nisingemshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa vile alivyoitikia wito wangu na akaenda akafanya ziara katika Kata Kakunyu, akapokea changamoto ya mgogoro huo na hatimaye akafikisha mgogoro huo kwa Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru pia Mheshimiwa Waziri kwa jinsi ambavyo aliwasilisha tamko la Mheshimiwa Rais na maamuzi yake kwa Wana-Kakunyu na aliona alivyopokelewa. Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kufikisha maelekezo ya Mheshimiwa Rais bila kuyapindisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie kwa ufupi masuala machache ninayofikiri ni ya msingi katika kusaidia Sekta ya Uvuvi. Jambo la kwanza nashukuru katika kiambatisho Na. 35 cha Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, amebainisha kwamba kuanzia leo hii ametoa ruhusa kwa nyavu za macho 78 kuanza kuvua sangara katika Ziwa Victoria. Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ni muhimu, naomba tuone tunavyoweza kulitekeleza, ni kuruhusu uvuvi katika Ziwa Victoria kutumia nyavu za milimita sita katika kuvua dagaa. Ziko sababu nyingi, lakini leo kwa sababu ya muda, nitaeleza sababu tatu. Sababu ya kwanza ni kwamba dagaa katika Ziwa Victoria ni wadogo, kwa hiyo, ukitumia nyavu za milimita nane maana yake hutakaa uwapate dagaa hao hata siku moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu ya pili ni kwamba hizi nyavu za milimita nane unapozitumia, ukae ukijua kwamba utaendelea kuwakosa hao dagaa lakini dagaa wao wanaishi siyo zaidi ya siku 315. Kwa hiyo, hata kama ukiwa hujawavua baada ya siku 315 hao dagaa wanachukua nafasi yake. Pia sababu ya tatu ambayo ningependa kuitumia hapa, uelewe kwamba ndani ya Ziwa Victoria mle, dagaa wenyewe wanatembea tu, usipowavua wewe wataenda Uganda watavuliwa kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia jambo ambalo ningependa kulisema ni kwamba jirani zetu waliotuzunguka wao wanatumia nyavu za milimita nane, kwa hiyo, usipofanya hivyo, unawasaidia wale wachukue dagaa wako.

Mheshimiwa Niabu Spika, jambo lingine ambalo nafikiri ni muhimu sana tulizingatie ni kwamba wakati umefika na tunatambua kwamba mabondo ya samaki za sangara thamani yake ni kubwa kuliko sangara wenyewe. Kama hivyo ndivyo ilivyo, ukiangalia katika kiambatisho Na. 35 inaonekana kwamba mrahaba tuliopokea kutokana na mabondo ni shilingi bilioni tatu, lakini kwa miezi nane kama kiambatanisho kinavyoonyesha, kama umekusanya tu shilingi

bilioni tatu kwa miezi nane maana yake kuna fedha nyingi sana umezipoteza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulitembelea viwanda vingi sana vya samaki na kila ukivitembelea, wanapokueleza changamoto hawakuelezi kabisa kuhusu mabondo; wanafanya hivyo kwa sababu wanajua mabondo ni dhahabu, hawataki kukuamsha ujue, wanakuacha uendelee kusinzia nao waendelee kuvuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda, naomba niseme kwamba naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa. Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, atafuatiwa na Mheshimiwa Hasna Sudi Mwilima na Mheshimiwa Vedasto Edger Ngombale, ajiandae.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa fursa hii niweze kutoa mchango wangu kwenye Bajeti ya Wizara ya Uvuvi. Nitumie fursa hii kwanza kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, lakini niwapongeze Waziri, Naibu, Makatibu Wakuu na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi kubwa wanayoifanya. Nitumie fursa hii kutoa pole kwa wavuvi wote wa visiwa vya Ukerewe kwa sababu kutokana na ongezeko la maji, mazingira yao ya makazi ambayo wamekuwa wanayatumia kwa ajili ya shughuli zao za uvuvi, yameathiriwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi mimi pamoja na Wabunge wenzangu tulikabidhiwa injini ambazo zimetolewa kwenye vikundi vya Ushirika vya Wavuvi kwa ajili ya kuzipeleka kwenye Majimbo yetu. Kwa hatua hiyo naipongeza sana Wizara. Kimsingi hili ni jambo linaloonyesha wananchi kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi inasema na inatenda kwa sababu kupitia Ilani ya Uchaguzi chama kimeelekeza Serikali kuwawezesha wavuvi kupitia Vyama vyao vya Ushirika na ndicho ambacho Wizara inakifanya. Hongereni sana Mawaziri na Watendaji wote wa Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Uvuvi imefanya mambo mengi na kupitia bajeti hii waliyoiwasilisha, ukiangalia kwa mfano ukurasa wa 94 imeongelea habari ya Marekebisho ya Sheria ya Uvuvi ambayo kimsingi ilikuwa ni msingi wa malalamiko mengi sana ya wavuvi. Tukienda kwenye ukurasa 131 Wizara inaeleza namna ambavyo imetoa mafunzo kwa wavuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo makubwa haya yanayofanyika kwenye Wizara hii ya uvuvi hayatakuwa na tija kama wananchi ambao ni wadau wa uvuvi hawatafaidika na mabadiliko haya. Wadau hawa ni akina mama wanaoenda kununua samaki, wanakaanga, wanapeleka sokoni kuuza na wavuvi wadogo wadogo. Kwa sababu katika wavuvi tulionao, zaidi ya asilimia 90 ni wavuvi wadogo wadogo. Kwa hiyo, ni lazima wafaidike na sekta hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukurasa wa 131 Wizara imesema imetoa mafunzo kwa wadau 5,008. Kwangu ni idadi ndogo sana. Napenda kutumia fursa hii kuishauri Wizara, ili wavuvi hawa wafaidike na elimu hii, kwa sababu matatizo mengi tunayokutana nayo kwenye jamii inawezekana ni kwa sababu wadau wa uvuvi hawana elimu ya kutosha juu ya uvuvi endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili elimu iweze kuwafikia vizuri, Wizara kwa sababu ina watumishi wachache, ni lazima ishirikiane na Halmashauri zetu ili kwa kutumia wataalamu walioko kwenye Halmashauri kutoka Idara za Uvuvi, wawe na uelewa mzuri na uwezo wa kifedha kuwafikia wadau wa uvuvi kuwapa elimu kila wakati na kwa vipindi vingi kadri inavyowezekana. Kwa sababu jukumu hili likibaki kwenye Wizara, ina watumishi wachache, matokeo yake ni nini? Wanawafikia mara moja moja sana wadau wetu wa uvuvi, kitu ambacho kinawafanya wasipate hii elimu kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkutano wa Bunge uliopita, tulipitisha marekebisho ya Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya mwaka

2003 na kanuni zake. Kifungu cha 8, 40, 47 ndivyo vilivyofanyiwa marekebisho. Binafsi nilipiga sana kelele hapa kutaka maboresho kwenye eneo hili, lakini hoja yangu hasa ilikuwa ni kutaka ufafanuzi uweze kutolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa sababu gani? Sheria hizi zimekuwa zinatumika vibaya na baadhi ya Watendaji na matokeo yake wadau wetu wa uvuvi kule chini ambao ni wananchi, wananyanyaswa sana kwa sababu ya sheria hizi. Kwa sababu ya uelewa mdogo wananchi wetu kutozijua sheria hizi wanakuwa waoga, wanashindwa kujitetea na matokeo yake wanadhulumiwa, wananyanyaswa na kufanyiwa mambo mengine ambayo kimsingi wananchi wanatukanishwa na Serikali yao kitu ambacho siyo ambacho Serikali inawatuma watumishi hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nashauri Wizara katika utekelezaji wa sheria hii, basi kuwe na miongozo ambayo itafanya watumishi wanaoenda kwenye maeneo ya chini kule, badala ya wananchi kunyanyasika; Askari anajisikia tu, anaenda mahali anaomba pesa, anawasumbua wananchi; shughuli yoyote ile itakayokuwa inafanyika kwa ajili ya kuzuia uvuvi haramu, kuwe na wataalamu wa uvuvi ambao wataelimisha wananchi, wanajua taratibu na sheria za uvuvi badala ya mtu yeyote kwenda mahali popote; sokoni akina mama wanauza samaki, anaenda mtu anawabughudhi akina mama pale, anawanyanyasa, kitu ambacho kimsingi kinatukanisha Serikali na wananchi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya yanafanyika na watumishi wachache kwenye Wizara hii ya Uvuvi. Kwa maana hiyo, kama nilivyoshauri, Wizara wakati wa utekelezaji wa sheria hii ihakikishe kwamba katika *operation* zozote katika matukio yoyote yatakuwa yanafanyika katika kuzuia uvuvi haramu, basi kuwe na wataalamu wa uvuvi ambao watasaidia kuelimisha wananchi juu ya mambo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mwingine inatokea *operation* inafanyika; *fine,* ni jambo jema, lakini unapoenda

kumkamata mvuvi kwamba ana nyavu zisizostahili, yule mvuvi amenunua kutoka dukani, anapaswa akamatwe yule mwenye duka badala ya huyu mvuvi ambaye amenunua kutoka kwenye duka na mwenye duka amemwelimisha kwamba ni nyavu sahihi. Unakuwa umtendei haki mvuvi huyu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda, naunga mkono hoja. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Hasna Sudi Mwilima atafuatiwa na Mheshimiwa Vedasto Edgar Ngombale na Mheshimiwa Sixtus Raphael Mapunda ajiandae.

**MHE. HASNA S. K. MWILIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru nami kwa kupata nafasi ya kuchangia Wizara hii muhimu sana ya uvuvi na mifugo.

Nianze kwanza kwa kumpongeza Waziri pamoja na Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanazozifanya. Kwa namna ambavyo wamewasikiliza wavuvi na wafugaji kwa kweli binafsi niseme nawashukuru sana Waziri, Naibu Waziri, Mkurugenzi, Katibu Mkuu Uvuvi na Katibu Mkuu anayeshughulikia masuala ya mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nianze kwanza na suala moja; nitoe shukrani kwa Mheshimiwa Waziri kwenye ukurasa wa 67 *NARCO;* suala lile la Uvinza kwenye eneo la Mwanduubantu nimeona umelizungumzia humu, kwamba mnajipanga kwenda kuweka mipaka; vigingi vile, mimi niseme Mheshimiwa Waziri tunakushukuru sana kwa niaba ya wafugaji wote wa maeneo hayo. Tunachoomba, ile timu yako ya tathmini iliyofanya, tunasubiria ile ripoti ya tathmini pamoja na maelekezo ya Wizara ili basi Mkurugenzi na Watendaji waweze kuendelea na mchakato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya shukrani hizo, nitoe pia shukrani kwenye Sekta ya Uvuvi. Nitoe shukrani kwa Waziri na Naibu wake pamoja na Mkurugenzi na Katibu Mkuu

wa Uvuvi kwa kilio cha wavuvi waliokamatiwa nyavu zao 43, mkaweza kurudisha nyavu 27 kwenye ziwa upande wa Katavi, nyavu 13 Kigoma na nyavu tatu Rukwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wavuvi wanasema wanawashukuru sana, sana, sana, kwani kitendo kilichofanya wao wakamatiwe zile nyavu ni vipimo kutofautiana. Wale watu wanaoshughulikia masuala ya uvuvi kwenye nyavu kwa maana ya *ringnet,* vipimo vyao vimeonekana haviko sawa, lakini Wizara mlipotembelea mliona kwamba kuna upungufu umefanyika na hatimaye kipimo chenu kikaweza kufanya wavuvi hawa warejeshewe nyavu zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachoomba tu kushauri ni kwamba sasa tuwe na kipimo kimoja; Halmashauri, Mkoa Afisa Uvuvi tuwe na kipimo kimoja na Wizara ili kuwaondolea usumbufu wavuvi na pia hasara walizopata kwa namna ambavyo walivyokamatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe pia shukrani za dhati kabisa kwa namna ambavyo Wizara imeweza kutoa leseni moja ya uvuvi kwenye ziwa Tanganyika na leseni moja ya uvuvi kwenye Ziwa Victoria kwa sababu mwanzo kila Halmashauri ilikuwa ina leseni yake, lakini sasa hivi mvuvi aliyeko Katavi anaweza akavua Uvinza, anaweza akavua Kigoma Mjini anaweza akavua Rukwa. Kwa kweli tunawashukuru sana. Kwa niaba ya wavuvi tunatoa shukrani za dhati kabisa Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri baada ya kusema hayo, niweze pia kuzungumzia katika ile *operation* iliyofanyika, ziko mashine ambazo zilikamatwa. Mashine hizi siyo za mitumbwi ya uvuvi, ni mashine za boti za abiria na zile mashine hazikukamatwa ziwani, zilikamatwa kwenye nyumba za watu. Sasa niko hapa kwa niaba ya wananchi wangu wa Uvinza, wanadai karibu mashine 25, lakini na wenzao pia wa Katavi wana mashine kama nane ambazo wanaziomba kwa vile siyo za uvuvi ni za abiria, mweze kuwarejeshea ili waweze kujikimu na hasa katika hili janga la *Corona* ambapo uchumi unakwenda unapotea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu moja kwa Waziri na Naibu Waziri, kwenye urudishaji wa zile nyavu kuna mvuvi mmoja kutoka Mgambo, Ndugu Omary Kitatile, hamkurejesha nyavu zake. Sasa amebaki anaona wenzake wamepewa 42, imebaki nyavu moja. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri baada ya hapa uone ni namna gani unaweza ukamsaidia huyo mvuvi mmoja naye kupata nyavu.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. HASNA S. K. MWILIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, niende haraka haraka nizungumzie suala la tozo, leseni. Najua kwamba kuna marekebisho...

**NAIBU SPIKA:** Kengele imegonga Mheshimiwa.

**MHE. HASNA S. K. MWILIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe shukrani ya dhati kwa Mheshimiwa mmoja tu; nitoe shukrani za dhati kabisa kwenye ukurasa wa 95 kwenye marekebisho ya kanuni Waziri na Naibu Waziri Mungu awabariki sana, mmeweza kubadilisha uvuvi wa kutumia taa ya *solar,* mmewaruhusu wavuvi kwenye Ziwa Tanganyika kutumia *ringnet.* Tunawashukuru kutumia mita 1,000 kuvua dagaa kwa kutumia *ringnet,* tunawashukuru sana, Mungu awabariki, mkashinde kwenye Majimbo yenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa. Nina uhakika nao wanakuombea. *(Kicheko)*

Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Vedasto Edgar Ngombale ambaye atachanga kutokea Msekwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Sixtus Raphael Mapunda na Mheshimiwa Oscar Rwegasira Mukasa ajiandae.

**MHE. VEDASTO E. NGOMBALE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza nitumie nafasi hii kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Kilwa Kaskazini ambao

Kwa kipindi cha miaka mitano wametoa ushirikiano nami katika kutekeleza majukumu yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini muhimu nizungumzie suala zima la migogoro ya wakulima na wafugaji. Ukiangalia kwa nini migogoro inatokea, ni kama tu kwamba watendaji wa Serikali hawatekelezi majukumu yao. Kwa mfano kwangu Kilwa ambako hatukuwa na wafugaji, maana yake tulikuwa tuna eneo la kutosha kwa ajili ya ufuugaji, na taratibu zilifuatwa ikiwepo pamoja na mpango wa matumizi bora ya ardhi ambao unaelekeza wapi wafugaji wakae na wapi wafugaji wasikae.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika hali ya kushangaza sasa hivi wafugaji wanakuja na wanapelekwa katika Kijiji ambacho hakina utaratbu wa kupokea wafugaji katika mpango wa matumizi ya ardhi na matokeo yake ni mgogoro, ni mapigano; hivi karibuni kulikuwa kuna mapgano kule katika Kata ya Kandawale, pasipokuwa na sababu yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nimuombe Mheshimiwa Waziri afuatilie hili, tuna uwezo wa kuepuka hii migogoro. Kwa sababu kwa mfano Kilwa tuna ardhi ya kutosha tu, sasa kama wafugaji watakaa maeneo yao kama mpango unavyosema basi hayo hayawezi kutokea. Vinginevyo hili linasababishwa sana na viongozi wenye tamaa na wapenda rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la ujenzi wa miundombinu kwa ajili ya wafugaji. Tumewapeleka wafugaji katika maeneo ambayo hakukuwa na mifugo, lakini ni kama tumewa-*dump* tu, tumewaacha wanahangaika. Hakuna majosho, hakuna mabwawa, hakuna rambo, hakuna chochote kinachohusiana na wafugaji, matokeo yake ni kero kwa wafugaji. Mifugo inapata shida; katika mwaka wa ukame mifugo mingi inakufa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi niseme tu Wizara ijitahidi ijenge miundombinu kwa ajili ya wafugaji kwa

maeneo ya Kilwa, tuwasaidie wafugaji, tusiwatupe tu. Wana haki zao, na wanyama pia wana haki zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ninapenda kulizungumzia leo ni kwamba nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa nia njema aliyoonesha ya kujenga bandari ya uvuvi. Ni jambo jema, jambo ambalo linaweza likatuongezea kipato chetu na uchumi wetu ukaendelea kukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, yameorodheshwa maeneo ambayo hiyo bandari itajengwa, maeneo mengi. Mimi nishauri tu bandari hii ikajengwe Kilwa, nashauri sana Bandari hii ikajengwe Kilwa. Na ni vizuri pia Serikali ikafanya haraka kueleza wapi bandari inajengwa, kusiwe na kigugumizi; kwa sababu kama tunakaa tu kwa muda mrefu bandari ya uvuvi na tayari tunaona wakandarasi wameanza pale lakini hatujui itakwenda kujengwa wapi, nalo mimi nafikiri siyo jambo jema.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukieleza mapema kwamba bandari inakwenda kujengwa wapi basi hii itasababisha na wadau wengine wa mambo ya uvuvi kujiandaa ili kuipokea hiyo bandari ya uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vinginevyo nikushukuru, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Sixtus Raphael Mapunda, atafuatiwa na Mheshimiwa Oscar Rwegasira Mukasa, Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla ajiadae.

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na mimi kupata nafasi ya kuchangia kwenye Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niungane na wenzangu wote waliompongeza Waziri na Naibu Waziri kwa kazi kubwa waliyoifanya katika kipindi cha muda mfupi. Mimi kwa namna ya pekee niwapongeze kwenye kutatua migogoro kati ya

wakulima na wafugaji, kwa hili mmefanya kazi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda niwaombe kwenye kitu kimoja; kwa muda wote tukiangalia kazi yenu katika *management* ya Wizara, *management* ya mifugo, *management* ya uvuvi, mmefanya kazi vizuri sana. Lakini kuna kitu kimoja mimi najiuliza, *what do you want to achieve;* je tunataka tufanye *management,* na je, *management* ndiyo *primary objective* ya Wizara? Mimi nadhani kuna kitu kimoja kikubwa sana Wizara hamjaangalia; asipokuwepo ng'ombe hakuna Wizara, wasipokuepo samaki hakuna Wizara.

Kwa hiyo katika nguvu ileile mliyotumia katika *management* mjitahidi sana kuwasaidia wakulima na wafugaji kwenye ustawi wa mifugo yao. Ndiyo hapo yanapokuja matatizo, kwenye hatua ya *mindset;* Wizara sasa tubadilike tuitazame hii mifugo kama fursa ya kutupatia pesa nyingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama unamkuta mkulima mwenye ng'ombe 600, ameingiza ng'ombe 600 kwenye hifadhi baadaye amekamatwa, baada ya miezi mitatu kuna ng'ombe 100. Hapa aliyepata ni nani; Serikali haijapata na mkulima hajapata.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna jambo moja mimi linanipa shida kulielewa. Hivi kitu gani, falsafa gani au *logic* gani ilitumika kuweza kumfanya Mmasai, ng'ombe, twiga, faru na Simba wakakaa Ngorongoro *Crater,* halafu ng'ombe haohao wakashindwa kukaa kwenye msitu wa hifadhi? Nadhani kuna kitu tufikiri kwa mapana.

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzetu Kenya wamezidi kwenye hilo. Kipindi ambacho chakula kinapatikana cha kutosha wafugaji hawana shida. Na wafugaji wanaingia kwenye haya maeneo kipindi ambacho hakuna nyasi, kipindi cha kiangazi. Msitu una miti na lengo la kuutunza msitu

kwenye ikolojia, utuletee hali ya hewa nzuri mvua ipatikane. Lakini ng'ombe hali miti, ng'ombe anakula nyasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini tusitengeneze utaratibu maalum inapofika wafugaji wanapata shida kwa utaratibu maalum walipie, na kuwe usimamizi maalum waingie ng'ombe kwa muda mfupi halafu watoke. Kwanza watasaidia hata kuleta mbolea kwenye miti ili miti istawi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini moja la mwisho; kuna *demand* kubwa sana ya nyama Oman, Egypt na Dubai, na wanahitaji kilo nyingi sana za nyama. Hatutagombana na wafugaji kama ranchi zetu za kitaifa zitabadili mtazamo zikafanya kazi ya kushirikiana na wafugaji ambao kwa hiyari yao wanataka ng'ombe wao wanenepe wauzwe nje, muwasaidie kwenye *markets* kwa sababu ranchi zetu za taifa zina *standards* zote za kimataifa. Ukisema ng'ombe huyu ametoka Kongwa, Oman atauzika, Dubai atauzika.

Sasa hivi ninavyoona mimi ranchi zetu zinafanya kazi chini ya kiwango. Tuwasaidie tuondokane na hii dhana ya kwamba mfugaji anajua kila kitu; anajua kufuga, anajua *market,* anajua kuchinja, anajua mahitaji, hii hapa ifike sasa *role* ya Wizara kufanya ng'ombe wote watuletee fedha za kigeni, Mheshimiwa Mpina ukiingia hapa nina uhakika Wizara yako itakuwa inafika *over fourty percent* ya bajeti yetu ya mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Oscar Rwegasira Mukasa atachangia kutokea Msekwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla, Mheshimiwa Dkt. Immaculate Sware Semesi ajiandae.

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi ya kusema leo kwenye Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote shukrani kwa Mwenyezi Mungu kwa kutupa afya wote hapa. Lakini ntasema pongezi kwa ufupi kwa sababu ya muda; Mheshimiwa Rais, namshukuru sana, nampongeza kwa uongozi na viongozi wenzake wa juu; Mheshimiwa Makamu wa Rais na Waziri Mkuu. Lakini Mheshimiwa Mpina, Waziri, Naibu Waziri Mheshimiwa Ulega na timu yenu nzima, tunawapongeza kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa sababu ya muda nitakwenda kasi kidogo. Biharamulo wafugaji wanalalamika sana, kuna kampuni inasambaza dawa ukanda wetu kule ikiwepo Biharamulo, dawa za *antibiotics* na dawa za kuosha hazifanyi kazi kwa mujibu wa matarajio. Ziko chini ya kiwango, wanalalamika kila kinachofanyika hakiendi, mpaka kwenye kuosha wanalazimika kuchanganya dawa mbili tatu na inashusha ubora.

Na kwa sababu wao wenyewe walionituma hapa wameitaja kampuni, na mimi ntaitaja, inaiwa *Bajuta Company;* na tunaambiwa, wanavyoniambia wao, kwamba kampuni hii imewahi kupigwa faini na Wizara miaka kama siyo mmoja ni miwili iliyopita, kwa matatizo kama haya. Wanalalamika sana inaharibu mzunguko mzima. Na kwa bahati mbaya ndio wame-*dominate* soko la madawa hayo ukanda wetu. Naomba Waziri aangalie.

Mheshimiwa Naibu Spika, watumishi wetu wa mifugo huko wilayani, wako ambao masomo yao ni ya *animal production* na wengine masomo yao ni ya *animal health.* Sasa sheria inawazuia wale waliosoma *animal production* kufanya shughuli za kupima nyama na kutibu ambazo ndizo huduma ambazo kwa wingi wananchi wanazihitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hawa kwa mfano kwa Biharamulo tuna watu hawa 13 katika kata 13 kati ya kata 17, kwa hiyo tuna watu jumla asilimia 76 ukichanganya wa *animal health* na *animal production* lakini wanane ndiyo wa *animal health.* Kwa hiyo hawa saba ambao wako kwenye kata lakini hawawezi kufanya huduma ya kutibu na kupima

nyama wanakuwa kwa maana ya huduma ambazo wananchi wanazihitaji hawana tija. Kwa hiyo wanalazimika kufanya shughuli zao kwa kujifichaficha kwa sababu sheria inazuia.

Naambiwa ni Sheria ya Mifugo ya Mwaka 2003. Sasa ni muhimu tukatazama lile jambo, si tu kupeleka watu kule vijijini, tupeleke watu ambao kisheria na kiutendaji wanaweza kweli wakafanya zile kazi ambazo zinahitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ni ngumu sana Mbunge au Waziri ukaenda kumwambia mwananchi wa Kijiji cha Kalenge kule kwamba huyu hapimi nyama yako kwa sababu amesoma *animal production,* haelewi hata unasema nini, yeye anaona mtu amekuja pale anapaswa amhudumie.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nataka niongelee pia suala la Corona niunganishe na hii Sekta yetu ya Mifugo na Uvuvi. Baada ya Corona kuwa imeipiga dunia sasa *story* yoyote duniani habari ni ile *resilience,* yaani uwezo wa kulichodondoka kurudi kwenye hali ya kawaida. Kwa hiyo watu wanajadili nchi zitarudije kwenye hali ya kawaida baada ya hili pigo kubwa la kiuchumi, lakini na sekta zitarudi vipi kwenye hali ya kawaida kwenye kila sekta kutokana na pigo la Corona.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesoma utafiti mmoja uliofanywa mwaka 2015. Wamezipanga nchi za Afrika, *Sub-Saharan Africa,* uwezo wake wa kuhimili *shock, resilience,* kwa sababu *shocks* zimeshatokea huko nyuma za kiuchumi mbali na Corona, utafiti wa 2015 unaiweka Tanzania nafasi ya 13 kwenye nchi za *Sub-Saharan Africa* ambayo ni ya tatu kwenye huu Ukanda wa *East Africa.* Lakini unaiweka Tanzania kwenye nafasi ya tano kwenye nchi za *SADC,* kwamba kwa sababu ya rasilimali, uwezo wake wa ku-*resilient,* kurudi kwenye hali ya kawaida uko nafasi si mbaya sana, japo siyo nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tumemsikia Waziri wa Fedha anaongelea namna ambavyo ameunda tume ya

kutazama athari za kiuchumi. Sasa mimi nahani ni vizuri kila sekta, mbali ya kutazama athari, sasa sekta *specific* watazame *resilience* yao. Na *resilience* ya sekta inatokana na namna gani utatumia fursa. Sasa kuna mifano.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ziwa Victoria, asilimia 51 ya eneo la ziwa ni Tanzania na 50, 49 wanagawana Kenya na Uganda, lakini *market share* ya mazao yanayotoka kwenye ziwa kwenda nje inaongoza Uganda, inafuata Kenya, inafuata Tanzania. Na sababu ziko nyingi tu, amesema Mheshimiwa Mabula, nimemsikia na Mheshimiwa Sixtus. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kodi; *items* za kodi sisi kwenye mambo ya uvuvi kwenye Ziwa Victoria ziko 15 ilhali kwa Kenya na Uganda ni tano kila mmoja. Lakini nichukue mfano mmoja tu minofu asilimia 79. Kwa hiyo Wizara inapaswa kuangalia *resilience* yake, inaweza ikafanyaje kutumia hizo fursa ikarudi.

Sasa hivi wavuvi wa Kagera wanauza Uganda na Kenya kwa sababu ya mambo kama hayo. Sasa turekebishe ili kuwezesha hiyo *resilience* ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kurudi kwa kasi kwa sababu dunia imepigwa na Corona na tunakwenda kuona matokeo ya kiuchumi ya Corona hivi karibuni. Kwa hiyo *resilience* ndiyo *story* ya sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri ungeambiwa kwa kawaida lakini unaambiwa kwa uzito kwa sababu inahitajika...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mukasa, kengele imeshagonga; ahsante sana, shukrani.

Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Immaculate Sware Semesi, Mheshimiwa Ritta Enespher Kabati ajiandae.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Naomba nitumie nafasi hii ya mwanzo kabisa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa ajili ya zawadi ya uzima na kuweza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa vile nasimama kwa mara ya kwanza naomba pia niwashukuru sana wanawake wa Mkoa wa Manyara kwa imani yao kubwa kwangu, na mimi nataka niwaambie kwamba wema hulipwa kwa wema.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli nisiposema haya sitakaa vizuri; naomba kwa namna ya kipekee nimshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. John Pombe Magufuli, kwa kazi kubwa anayoifanyia nchi yetu kwa ajili ya maendeleo ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge, mtakubaliana na mimi kwamba sisi Wabunge wote, wa majimbo na wa viti maalum, wote kwa ujumla wetu, wa Chama Cha Mapinduzi, tunakwenda vifua mbele kwa ajili ya kazi kubwa na ubunifu mkubwa wa Mheshimiwa Rais wetu alioufanya kwa ajili ya sisi wote na kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nije kwenye mifugo. Sekta hii imelegalega kwa muda mrefu sana; lakini tunaishukuru Serikali ya Awamu ya Tano kwa sababu ndani ya muda mfupi ambao utawala wa Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli umekuwepo madarakani tumeona mapinduzi makubwa sana katika Sekta hii ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumesikiliza taarifa ya Kamati ya Mifugo, Kilimo na Maji; wafugaji wanalalamika sana kufuatana na hali halisi iliyoko katika *field,* hasa katika Sekta ya Maliasili. Mimi naiomba Serikali, kwa sababu muda ni mfupi sana, Wizara ya Mifugo iweze kushirikiana na Wizara ya Maliasili ione ni namna gani itatatua migogoro hii iliyopo

baina ya wananchi, hasa wafugaji na watendaji wasio waaminifu wa Wizara ya Maliasili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilio hicho sio cha leo kusema kweli. Na kama ambavyo alieleza Mwenyekiti wa Kamati, mimi pia ninatokana na jamii ya wafugaji na tumeweza kukutana na uongozi wa wafugaji, malalamiko haya ni ya kweli. Kwa hiyo ninaomba Serikali ifike mahali sasa iweze kuangalia ni namna gani italeta utulivu kwa ajili ya wafugaji wetu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nieleze kwamba wafugaji mpaka sasa hivi wanamshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli kwa sababu, kwanza kabisa sasa hivi wafugaji wanapata dawa za ruzuku kwa ajili ya upatikanaji wa kuogesha mifugo yao na pia kuweza kuleta bei elekezi kwa ajili ya chanjo ya mifugo, kitu ambacho huko nyuma kilikuwa kilio kikubwa sana kwa wafugaji na imeweza ku-*encourage* masuala ya rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais wetu pia ameunda timu ya kutatua migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi. Kwa hiyo haya ni maeneo makubwa sana ambayo yanawafurahisha sana wananchi, hasa wafugaji, kwa ajili ya matatizo ambayo si ya lazima kwa kweli ambavyo yanaweza kutatulika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona kwamba kuna uboreshaji wa sheria na kanuni ambazo zinasimamia mifugo. Tunaiomba Serikali iweze kuiangalia kwa undani zaidi kuhakikisha kwamba haya maboresho yanazingatiwa na yanaweza kwenda kuhakikisha kwamba unaleta utulivu kwa ajili ya wafugaji wote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na juhudi hizo za Rais wetu na Wizara kwa ujumla, bado kuna matatizo makubwa sana katika sekta hii. Ni matarajio kwamba wafugaji wataweza kutatuliwa matatizo yao kulingana na jinsi ambavyo kilio chao kimeweza kufikishwa Wizarani, jinsi ambavyo tumeskia Mwenyekiti wa Kamati, sina haja ya

kurudia. Lakini tujue kwamba sekta hizi zinategemeana na kwa hiyo tunaomba migogoro hii iweze kumalizwa. Na yameshaelezwa sana kwa hiyo kwa ajili ya muda sitaki kuyarudia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka kuzungumzia kidogo kuhusu tozo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Muda umekwisha Mheshimiwa Umbulla; dakika moja.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona kwamba kusema kweli Sekta hii ya Mifugo bado ina matatizo kwa ajili ya tozo mbalimbali kiasi kwamba tozo hizi ambazo zinakwenda sambamba na uagizaji wa vifaa nje ya nchi kwa wawekezaji wazawa kidogo inawaletea shida kwa sababu mazao kama *milk products* ambazo zinaletwa Tanzania hazina kodi, na *VATs* mbalimbali ambazo zinachajiwa kwenye masuala ya ngozi kwa mfano kama ngozi ya punda ambayo ina gharama kubwa duniani, ninaomba hizi tozo ziangaliwe upya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Immaculate Sware Semesi, atafuatiwa na Mheshimiwa Ritta Enespher Kabati, Mheshimiwa Mbaraka Kitwana Dau ajiandae.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi nami nitoe mawazo yangu katika Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ya kwanza kabisa ninapenda kuongelea suala la madhara ya mlipuko huu wa Ugonjwa wa Virusi vya Corona katika Sekta hii ya Mifugo na

Uvuvi. Ni dhahiri kwamba mlipuko wa ugonjwa huu umeathiri sekta hii pia, *especially* katika Sekta ya Uvuvi kwa hali hii. Mazao ya uvuvi nchini yana upungufu wake, yaani hayajitoshelezi, na tumekuwa tukiagiza kutoka nje, *especially* China, ili kuweza kufanya *market* ikapata bidhaa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa wakati huu duniani usafirishaji wa bidhaa hii na *demand* ya bidhaa hii kutoka nchi za nje umepungua sana na umeathirika sana na kujikuta kwamba, sisi tunategemea rasilimali zile za uvuvi tunazozizalisha hapa nchini. Kwa hiyo, soko la ndani limekua, ndio, lakini ni la muda mfupi kwa sababu, uzalishaji wetu wa rasilimali hii bado haukidhi tunachokihitaji. Kwa hiyo, naomba Serikali imuangalie mlaji pamoja na mzalishaji hapo mbele bei zitakuja kuwa juu na watu wengine, *especialy* wenye kipato cha chini, watakuwa hawana *access* na bidhaa hii au bei itakuwa iko juu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine naomba iangalie, chini ya Wizara hii kuna *MPRU,* wahifadhi hawa wa bahari na sekta ya utalii imeathirika sana katika maeneo haya. Kwa hiyo, wangalie pia upatikanaji wa hela au fedha kutoka kwenye *MPRU* kupitia shughuli za utalii zitakuwa zimeathirika sana. Serikali pia, naomba izingatie kwamba, wawezeshe wavuvi wakaangalie masuala ya *credit programs* na misamaha ya mikopo kwa wafanyabiashara mbalimbali katika *chain* nzima ya shughuli za uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho kabisa nataka pia, wawazingatie wafugaji wetu nchini kwa sababu, wengi wao si wafugaji kama wafugaji, bali ni wachungaji. Kuna *a lot of migrations,* lazima kutakuwa kuna *effect* kubwa ya ugonjwa huu kwa wanyama wenyewe na hao wanaowafuga au wanaokuwa na shughuli hizo za ufugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo nataka niligusie ni suala la *blue economy* au uchumi unaotegemewa na bahari, maji na maziwa makuu. Kwa kuangalia tu bahari kwa nini nasema tujiangalie na nataka niiulize Serikali imejipangaje ku-*focus* sasa kuendeleza au kukuza uchumi

wa nchi kwa kuangalia *blue economy,* uchumi ambao tunautoa *especialy* kwenye bahari na maziwa makuu?

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia tu bahari ime-*cover* dunia kwa 72% kwa hiyo, uso wa dunia 72% ni maji. Sasa tunatumiaje rasilimali hii ya maji katika shughuli za usafirishaji, shughuli za uvuvi, mambo ya *waste management,* mambo ya uvunaji wa mafuta na gesi ambayo ina-*contribute 30%* kwa ujumla wake na kadhalika. Sasa Serikali imejipangaje kutukwamua kiuchumi badala ya kuangalia rasilimali ambazo ziko katika ardhi bali iangalie rasilimali ambazo ziko kwenye maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu nataka niligusie ni suala la Taasisi ya Utafiti kwenye Masuala ya Uvuvi *(TAFIRI).* Ni mwaka unaenda sasa wa nne, muda sasa taasisi hii imekosa Bodi ya Wakurugenzi na taasisi bila bodi ni ngumu kujiendeleza. Sasa Serikali ilikuwa imeji-*commit* kwamba, bodi hii itaanzishwa kabla ya mwaka huu wa fedha kwisha, lakini naona suala hili halijagusiwa. Kuendesha bodi ni gharama, lakini hata bajeti yake haijawa *reflected* kwa mnachoki-*propose* kwa mwaka huu wa fedha unaokuja. Kwa hiyo, naomba taasisi hii sasa iangaliwe ipatiwe bodi ya kuweza kuiendeleza. Taasisi hii pia kwa bahati mbaya ambayo sasa ndio kama *machinery* fulani inayofanya utafiti shughuli za mambo ya kwenye maji, baharini, maziwa, mito na kadhalika iweze kupatiwa fedha za maendeleo pamoja na vifaa vya utafiti husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dakika nne, naomba pia, bajeti izingatiwe, bajeti ya maendeleo; bila kuwekeza huwezi kupata faida yoyote. Sasa sekta hizi mbili uvuvi na mifugo ina *potential* ya kututoa katika huu uchumi tulionao na kwenda huo uchumi wa viwanda na huo uchumi wa kati. Naomba bajeti ya maendeleo iongezwe kwa sababu, wamepewa chini ya milioni 200, huwezi kuendeleza sekta muhimu namna hii bila fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, atafuatiwa na Mheshimiwa Mbaraka Kitwana Dau na Mheshimiwa Mwita Boniphace Getere ajiandae.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia katika Wizara hii ya Mifugo. Naomba nimtangulize Mwenyezi Mungu katika mchango wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee sana kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu ambaye kwa kweli, amefanya mambo makubwa sana katika Wizara hii na kutekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi. Naamini kabisa wananchi wote watamchagua kwa kura nyingi sana za kishindo kwa sababu, amefanya makubwa sana kuhakikisha Wizara hii inafanya mabadiliko makubwa. Pia niendelee kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wetu wa Mifugo ambaye ni shemeji yangu na Mheshimiwa Naibu Waziri, Makatibu wote wa Wizara na Watendaji wote wamefanya kazi kubwa sana, mpaka Wizara hii sasa hivi imeongeza mapato kwa kiasi kikubwa kitu ambacho hatujawahi kukiona.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa niendelee kuipongeza Serikali kwa kuanza kusafirisha minofu ya samaki. Tumeona juzi ndege inasafirisha minofu ya samaki kupitia Mwanza, hayo ni mapinduzi makubwa na changamoto kubwa ya viwanda wawekezaji ilikuwa ni usafirishaji wa hii minofu ya samaki, walikuwa wanakwenda mpaka huko Uganda. Kwa hiyo, nasema kwamba, siku moja Mheshimiwa Rais atafanya jambo kubwa kuhakikisha tunapata ndege yetu kama ambavyo ndege zilizopo, ili tusafirishe mpaka na mazao ya mbogamboga na matunda.

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea kumpongeza, kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Iringa ambao wanampongeza sana Mheshimiwa Rais, lakini wanampongeza sana Mheshimiwa Waziri, kwa kweli ametupatia pesa katika machinjio ya kisasa ya Iringa, Manispaa, bilioni 1.1 sio jambo dogo. Toka mwaka 2008

machinjio ile ilikuwa haiishi, lakini mwaka huu Mheshimiwa Waziri nimemwambia tu akaniambia waite watendaji wako, walipokuja tumepewa hiyo pesa na sasa hivi tunategemea ajira nyingi sana pale Iringa machinjio itakapokwisha, hivyo tutapata pato kubwa, karibu ajira 250 tutaajiri pale Iringa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vikundi vile vidogo vidogo vya usindikaji wa ngozi, vya wafugaji karibu 2,000 watapata ajira kupitia machinjio ya kisasa na tutakuwa na machinjio ya kuku wa kisasa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri Mwenyezi Mungu awabariki, mrudi tena na muwe Mawaziri kwenye Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi kubwa pia kwa Serikali na naomba iendelee kuongeza ushuru, *excise duty* kwa *product* ya maziwa ya kutoka nje, kwa sababu inapoongeza huo ushuru ni kwamba, tunalinda viwanda vyetu vya ndani. Viwanda vyetu vya ndani vimekuwa vikitupa manufaa makubwa sana hapa nchini, tukitoa mfano tu Mkoa wetu wa Iringa tuna kiwanda kile cha *ASAS,* kiwanda kile kimekuwa ni mfano wa kuigwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ajira nyingi sana karibu 2,300 zinatoka katika kile kiwanda, lakini pia tumekuwa tukipata lishe. Katibu Mkuu alikuja Iringa akaona watoto wote wa shule wamekusanyika wanapata maziwa kupitia kile kiwanda na utapia mlo sasa utaondoka.

Vilevile kimekuwa kikiwaajiri hata watu wenye ulemavu, ni jambo zuri na viwanda vingine viige mfano kama wa *ASAS.* Niwapongeze *ATCL* kwamba, sasa hivi wanatumia *products* ya kwetu hapa nyumbani ya *ASAS,* kwa hiyo, zamani tulikuwa tunaona *products* za nje ndio zinatumika. Kwa hiyo, ni mapinduzi makubwa sana katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali pia iondoe kodi kwenye vifungashio na pia kuharakisha kutekeleza *blue print* ili kuleta nafuu ya udhibiti kwenye tozo kwenye viwanda vyetu, ili viwanda vyetu viendelee kufanya vizuri kabisa hapa

Tanzania kwani tunategemea viwanda ndio vitaleta mapinduzi makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile tulipokwenda katika ziara kulikuwa kuna changamoto kubwa sana, wafugaji na wakulima, walikuwa wanasema kwamba, wanaona kama hawana benki ya kukopa. Kwa hiyo, wapatiwe elimu ili wajue kwamba, benki ya kilimo pia inakopesha hata wafugaji na wavuvi ili waone kwamba, Serikali yao inawajali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, naomba nikushukuru sana na nimshukuru sana Mwenyezi Mungu na niombe kupitia Chama Cha Mapinduzi, wananchi wa Iringa waendelee kuniamini na kunichagua tena, lakini pia wamchague sana Mheshimiwa kwa kura nyingi. Jimbo la Iringa Mjini sasa, hatuna mwakilishi kwa sababu anakimbia *corona* badala ya kuwawakilisha wananchi, hivyo naomba watoe kura nyingi sana kwa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbaraka Kitwana Dau, atafuatiwa na Mheshimiwa Mwita Boniphace Getere na Mheshimiwa Jitu Vrajilal Soni ajiandae.

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa fursa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema aliyetuwezesha kukutana leo na kujadili masuala yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya kipekee kabisa naomba uniruhusu nianze kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi Mawasiliano na Uchukuzi kwa kutupatia kibali kwa meli yetu ile ya Mafia ambayo imeshaanza kazi na ile shida imekwisha. Wananchi kwa niaba yao wamenituma nije kutoa salaam; nimemwona Ndugu yangu Mheshimiwa Kwandikwa, Waziri hayupo, basi naomba amfikishie salaam Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumshukuru pia mtoa hoja na kumpongeza sana Mheshimiwa Mpina, Ndugu yangu Mheshimiwa Ulega, kwa kweli wanafanya kazi nzuri sana. Binafsi kwa maana ya Wilaya ya Mafia wamenitendea haki sana, wote wawili kwa nyakati tofauti zaidi ya mara mbili wamefanya ziara katika Kisiwa cha Mafia. Kwangu mimi hiyo ni heshima kubwa sana na nawashukuru na nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nianze kuchangia hoja. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri ameelezea namna gani hii Sheria Namba 22 ya Mwaka 2003 na Kanuni zake za 2009 na alielezea hapa na ameielezea vizuri sana hapa Ndugu yangu Mheshimiwa Mkundi. Maboresho makubwa sana yamefanyika, lakini mimi *in particular* nina tatizo kwenye kifungu cha 66(r) ambacho kinasema, kwenye maji ya chumvi samaki anaweza akavuliwa kwa nyavu ya nchi moja unusu na chini ya hapo itakuwa ni dagaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria hiyo hiyo na kanuni zake hizohizo, Kifungu cha 66 hichohicho, lakini (f) wanasema kwamba, kwa upande wa samaki wa maji baridi ni nchi tatu. Sasa kule *site* sasa katika kutekeleza haya kunakuwa na mikanganyiko. Pia Mheshimiwa Waziri amezungumzia kuhusu Sheria ile ya Hifadhi ya Bahari na yenyewe nayo pia, wanaifanyia marekebisho makubwa na yenyewe kule inasema, samaki atavuliwa kwa nchi mbili na nusu. Sasa watekelezaji kule *site* wanawakamata wavuvi wetu, wanakamata nyavu, wanachoma, wanakwambia kwamba, sheria inasema ni nchi tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwenye sheria hiyohiyo tena kuna sehemu nyingine nchi moja unusu, ukienda kwenye hifadhi ya bahari mbili na nusu. Ndio maana tuliomba haya maboresho wajaribu kuyatenga, samaki wa maji baridi anakuwa kwa haraka kwa hiyo, inawezekana aina ya nyavu inaweza ikawa ni tofauti, lakini samaki wa kwenye bahari huku ukuaji wao ni mdogomdogo na kuna wengine wadogo sana. Kwa hiyo, waangalie namna gani ya ku-*harmonise* sheria

badala ya kuweka tu *blanket,* inatusumbua sana kule *site* kwenye utekelezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, kuhusu wakuu wa idara. Hii Wizara ina mifugo na ina uvuvi, sasa wakuu wa idara hususan kule kwangu mimi na maeneo yale ambayo yana uvuvi sana utakuta pale Mkuu wa Idara ni mtu ambaye *profession* yake ni mifugo, kwa hiyo, inakuwa shida sasa. Kwa maeneo haya ya wavuvi tungeomba sana basi Mkuu wa Idara awe mtu ambaye *profession* yake ni uvuvi kwa sababu, eneo la uvuvi; kwa mfano kama Mafia, Mkuu wa Idara ni mtu ambaye *profession* yake ni mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mtu wa mifugo kule Mafia ni kama hakuna, kuna ng'ombe wachache sana na mbuzi wachache sana, lakini kwa kiasi kikubwa sana watu wanashughulika na masuala ya uvuvi. Kwa hiyo, tungependa sana na pengine wangetusaidia ili mtu mwenye *profession* ya uvuvi awe na *qualifications* za aina gani, ili aweze kuwa Mkuu wa Idara katika maeneo haya ya uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho ni Kisiwa cha Nyololo. Namwomba Mheshimiwa Waziri kwa namna ya kipekee kabisa aje Mafia tuna mgogoro wavuvi wa Kisiwa cha Nyololo wanaondolewa pale na yeye visiwa vile ni vya kwake, kwa sababu viko chini ya *marine park.* Tunaambiwa tu kwamba kuna matatizo ya *corona*, Rais ameshasema Wananchi wachape kazi kwa sababu, tunataka kuondolewa katika kisiwa kile eti kwa sababu, kuna *corona*, wengine wanasema masuala ya usalama; kuna sintofahamu kubwa sana.

Namwomba Mheshimiwa Waziri mwenyewe sasa au hata Naibu wake kwa sababu na yeye kule ni mdau mkubwa tu, waje watuwekee sawa hili tatizo la wavuvi wa Nyololo wanaondolewa katika kile kisiwa kwa sababu, tu wanaambiwa kuna matatizo ya masuala ya *corona*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mwita Boniphace Getere, atafuatiwa na Mheshimiwa Jitu Vrajlal Soni na Mheshimiwa Aysharose Ndogoli Matembe ajiandae.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, na nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Niwapongeze tu viongozi wote kuanzia Waziri na nimpongeze kwa sababu, wakati mwingine humu ndani hawajui historia, katika Bunge hili tuna Watendaji wa Kata wawili tu ambao ni Mheshimiwa Mpina na mimi Mheshimiwa Boniphace hapa. Kwa hiyo, Watendaji wa Kata nchi nzima mjue mnaweza mkatoka hapo mlipo mkafika kwenye uwaziri. Tuliachana katika hali hiyo, mimi nikatoka nikawa Rais wa Chuo cha Mipango na badaye nikawa Mjumbe wa *NEC* na leo niko kwenye ubunge na mwenzangu akatoka akawa mpaka kwenye uwaziri, kwa hiyo, nampongeza sana. Niwapongeze watendaji wa Wizara wakiongozwa na Profesa Elisante, wanafanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye eneo moja tu. Ukienda kwenye Kipengele cha 67, kipengele cha 2, wamempongeza Mheshimiwa Rais kwa kuchukua hatua za kuchukua mapori tengefu 12; mapori tengefu na misitu mingine amechukua ekari nyingi tu, sabini na mia saba na kitu, lakini Wizara ya Waziri wa Mifugo pale kwangu kwenye Jimbo la Bunda kuna eneo moja linaitwa Kabimita, lina ekari 2000. Lilikuwepo enzi hizo wakati wa Mwalimu Nyerere mwaka 1983 wanatunzia ng'ombe baadaye wakaliacha kwenye vijiji likawa mali ya kijiji. Pale kuna mifugo, kuna wafugaji, kuna shule za msingi, kuna nini, lakini ukisoma kwenye vitabu vyao bado wanalihesabu kama eneo la Wizara ya Mifugo. Naomba wapitie maeneo yote katika nchi hii ambayo yako kwenye maeneo ya wafugaji, waweze kuyaondoa kwenye orodha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri aliyekuwepo enzi hizo, Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, alienda mpaka kwenye eneo hilo akawaambia jamani, fanyeni kazi msibabaishwe. Endeleeni ardhi ni ya kwenu kwa sababu, pale kuna shule

kuna kila kitu. Naomba eneo hilo nalo walichukue, sasa watu wanaenda pale kuwababaisha wanakijiji, wa Mekomariro na Nyasirori wala eneo sio lao wala nini kumbe ni eneo lao. Kama Rais anawachukua wajibu wa kutoa mapori kwa ajili ya wafugaji, leo Wizara wanashindwaje kutoa ekari 2,000 kwa wafugaji ambao eneo ni la kwao wako pale, hakuna hati ya kijiji, hakuna hati ya kilimo, hakuna hati ya ardhi ya sehemu yoyote ile. Kwa hiyo, naomba eneo hilo nalo Waziri alichukue na alifanyie kazi, najua nilishamweleza na atalichukulia hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo natakiwa kulieleza ni Mto Rubana ambao kuna mgogoro kati ya wanakijiji na Pori Tengefu la Grunet. Mheshimiwa mmoja amezungumza hapa, tumsaidie Mheshimiwa Rais; wakati fulani huwa najiuliza yani kila kitu sasa, hivi kama mpaka kati ya kijiji na pori ni mto. Mwaka 1994 mpaka ule ulihamishwa kutoka kilometa 350 ukasogea karibu na eneo la kijiji na mbaya zaidi katikati ya mto ndio wakaweka mpaka. Ukienda kunywesha ng'ombe mpaka upeleke watu watano uende upande wa pili wawarudishe. Ng'ombe wakishavuka wameenda kwenye pori lao, Mheshimiwa Waziri namshukuru sana amekuja pale wanakijiji wamemweleza na amesema atalichukulia hatua na leo nimeona anazungumzia, nimpongeze kwa kusema kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, huwa najiuliza hivi Waziri wa Mifugo ni nani na anafanya kazi ipi? Kama wakulima na wafugaji wananyanyasika, hasa wafugaji, wanapata shida maeneo mengi Waziri hawasemei kwa nini? Sasa nimshukuru sana Ndugu yangu anafanya kazi nzuri, wanawasemea sasa wafugaji, wamefurahi. Sasa hivi wanaona kwamba, wana Waziri wao na kile Chama cha Wafugaji Mheshimiwa Waziri akisimamie ili watu wafanye uchaguzi wapate chama kizuri chenye kuwasimamia. Kwa hiyo, eneo lile ambalo lina mpaka ule tuweke *buffer zone* mita 500 kwenda kwenye mapori na mita 500 kuja kwa wananchi; sasa mtu anashindwaje, ukivuka ukienda kwenye mto, ng'ombe akivuka hatua moja tu ameingia porini? Kwa hiyo, hilo nalo nafikiri Waziri atalifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ni ahadi ambazo Waziri aliwaahidi watu wale wa kwake kwenye Vijiji vya Maliwanda, Vijiji vya Unyali, Salakwa na Kihumbu. Zile mbegu bora za madume za kwenda kuhamilisha ambazo tumewapa zile 1,000, watu wamejitayarisha sana kuzipokea. Yale madume mawili yale ya *borana* wanahitaji kwenda kuyapokea. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri kwamba, tukitoka hapa, nadhani watu wake alishawapanga, waende wakafanye kazi, lakini vinginevyo anafanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwanzoni hatukukuelewa na hasa kwenye suala la uvuvi lakini kumbe ulikuwa umelenga. Nchi hii ilikuwa inaagiza samaki kutoka japana, kutoka hata Shelisheli wakati tuna maziwa ya kutosha na bahari ya kutosha. Lakini leo watu wamekuelewa wanavyokula samaki. Samaki wakubwa wanapatikana sasa hivi, lakini sasa ubadilishe *style.* Naomba ubadilishe *style* sasa, badala ya kwenda kuwapiga *fine* wale watu na kuwaacha maskini, waende sasa na makontena ya vifaa vya wavuvi, uende ukimpiga *fine mtu,* unaichukua nyavu mbovu, unampa nyavu halali. Unachukua mtumbwi mbovu, unampa mtumbwi halali. Kwa hiyo, utembee na makontena, ukipiga *fine* unawaachia watu faida, sio unawafilisi tena! Kwa hiyo, nadhani hilo ni jambo zuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Getere. Mheshimiwa Jitu Vrajlal Soni, atachangia kutoka Msekwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Aisharose Ndogholi Matembe, Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay ajiandae.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuchangia siku ya leo. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa siku ya leo kwa kunipa afya na fursa ya kuchangia. Lakini pia nichukue fursa hii ya kipekee kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu mpendwa Mheshimiwa John Joseph Pombe Magufuli kwa kazi kubwa

na nzuri anayofanya na hasa katika jambo la kuunda timu ya Mawaziri nane kwenda kutatua migogoro mbalimbali katika watumiaji wa ardhi maeneo mbalimbali ambayo itawapa unafuu sana wafugaji wa nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Babati, wamenituma kutuma salamu hizo pamoja na Mawaziri wote nane waliofanya kazi kubwa na nzuri na timu zao, wanasubiria sasa matokeo ya ile ripoti. Lakini pia ningependa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mpina, Naibu wake Mheshimiwa Ulega, Katibu Mkuu Ole Gabriel pamoja na Tamtam kwa kazi kubwa na nzuri wanayofanya pamoja na wenzano wote. Sasa Wizara hii imeanza kuonesha dira na mafanikio makubwa na tunaamini kwamba katika mafanikio yoyote lazima uanze na hatua moja na sasa tunaelekea huko kwa mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiangalia baada ya wizara ya Maliasili katika utalii, Wizara ya Mifugo inaweza kuwa ya pili katika kuchangia Pato la Taifa kama ikisimamiwa vizuri na kusimamiwa vizuri na kuweka sera nzuri lakini pia pamoja na kuweka uwekezaji wa kutosha ili Sekta hii sasa iwe rasmi na maeneo yote yale ambapo wanahitaji kutumia teknolojia basi waweze kutumia teknolojia na sekta hii sasa iweze kuipatia nchi yetu mapato ya kutosha na kuchangia Pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mengi tukiona kwamba tumechangia kiasi gani katika Pato hili la Taifa watu wengi huwa wanapiga hesabu ya zile bidhaa ambazo zinapelekwa nje ya nchi lakini hakuna mtu huwa anaangalia takwimu ya kila siku ya Mungu kwamba ni bidhaa ambayo inatokana na mifugo, iwe ni nyama, iwe ni maziwa, iwe ni kuku, bidhaa zote hizo za mifugo ni kiasi gani kinatumika kila siku hapa nchini na thamani yake ni nini. Tungeweza kuelewa hiyo basi umuhimu wa Wizara hii ungejulikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze Wizara kwa kazi nzuri wanayofanya na kupokea maoni mbalimbali ya kamati lakini pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Katibu

Mkuu wa Mifugo kwa ahadi yao sisi kule Babati tayari tumeanza mpango wa kuhimilisha ng'ombe. Sisi tulichangia kulipia ng'ombe 1,000 kwa kupitia Mfuko wa Jimbo lakini pia na Waziri ametuahidi na yeye atachangia ng'ombe 1,000. Kwa hiyo, tunasubiri baada ya bajeti hii tayari tumeshajiandaa kwenda kuanza huo mpango kabambe wa kuhimilisha ng'ombe katika viji vyote 102 ili tuanze kubadilisha mifugo yetu na kuwa na mifugo bora zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu ni moja kwamba Serikali iangalie namna ya kuwekeza katika utafiti kwa upande wa TARIRI upande wa mifugo, lakini upande wa TAFIRI kwa upande wa samaki. Tukiwekeza kwenye utafiti tutaweza kupata manufaa makubwa zaidi na badala ya kwenda kuchunga, tutakuwa tunafuga na tutakuwa tunapata faida kubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu moja kwamba kwenye sekta nzima hii kuna changamoto kubwa ambayo inatokana na vifaa vyote ambavyo tunaagiza kutoka nje ya nchi, vyote vinatozwa kodi. Sasa tumeshapeleka kwenye Kamati ya Bajeti kwa kupitia Kamati yetu ya Kilimo, Maji na Mifugo pia mapendekezo mbalimbali. Lakini kama Makamu Mwenyekiti wa Baraza la Kilimo la Taifa, pia tumepeleka kwenye *task force* maoni mbalimbali kwamba tasnia mbalimbali kwa mfano ya kuku, chakula cha mifugo, na tasnia ya maziwa. Hao wote, changamoto mbalimbali zilizopo lakini pia na tasnia mpya hii ya ukuaji wa viumbe hai *(Aquaculture)* pia na wao vifaa vingi vinavyoletwa vinatozwa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili mifugo iende vizuri sawa na tulivyopendekeza kwenye upande wa kilimo, tungependekeza kwamba mitambo ya kuchimba maji, mabwawa na malambo pia yangesamehewa kodi ili tuweze kutengeneza mabwawa mengi zaidi, tuweze kuchimba maji. Mifugo inahamahama kutokana na kutafuta lishe na kuhitaji maji. Sasa tukiweza kuwasaidia kwenye hilo pakawa na mitambo ya kutosha na vifaa hivyo hivyo pia vitatumika

kwenye kilimo lakini pia vitatumika kwenye kutengeneza mabwawa ya samaki. Itatusaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia suala la *pump* za umwagiliaji.... Ahsante sana naunga hoja kwa asilimia 100. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Aisharose Ndogholi Matembe, atafuatiwa na Mheshimia Zacharia Paulo Issaay, tutamalizia na Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga.

**MHE. AISHAROSE N. MATEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima, si kwa ujanja wetu, bali ni kwa rehema na huruma yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikupongeze wewe, Mheshimiwa Spika na timu yako kwa namna mnavyoliongoza Bunge letu kwa weledi mkubwa, nawapongeza sana. Nimpongeze sana Waziri wa Kilimo na Uvuvi, Naibu wake, Makatibu wote wawili, Profesa Ole na Dkt. Rashid kwa kazi nzuri wanayoifanya kaztika Wizara hii. Nawapongeza sana pamoja na watendaji wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru sana wananchi wa Mkoa wa Singida hususan wanawake na vijana kwa ushirikiano, miongozo na ushauri wanaonipa kwa kipindi chote cha muda wa miaka mitano nilipokuwa hapa Bungeni. Ninawaomba ushirikiano huo uendelee kwa kipindi kijacho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee nimpongeze sana Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri anayoifanya ya kuwaletea maendeleo wananchi wa Tanzania. Wananchi wa Mkoa wa Singida wamenituma nitoe salamu za pongezi na shukrani kwa Mheshimiwa Rais, wanampongeza sana na wanamtakia maisha marefu, afya njema na Baraka tele na watahakikisha kwamba 2020 watasimama pamoja naye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze sana Serikali kwa kupunguza migogoro ya wakulima na wafugaji. Niishauri Serikali iendelee kutenga maeneo na kutunga sheria ili sasa maeneo hayo yaweze kutumika kwa malisho na kuepusha au kumaliza kabisa migogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niishauri Serikali iweke mkakati maalum wa kuhakikisha viwanda vyetu vinatumia mazao na malighafi ya mifugo yetu na kuepuka kuagiza mazao hayo kutoka nchi za nje. Kwa kufanya hivyo, wataongeza kipato kwa wafugaji wetu lakini pia vile vile wataongeza ajira na kuongeza mapato katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Mkoa wa Singida ni wafugaji wazuri. Wanafuga ng'ombe, mbuzi na kuku lakini jambo la kushangaza hatuna kiwanda, hatuna machinjio, na soko la uhakika kwa ajili ya mifugo hiyo. Natambua kwamba Manispaa ya Singida tayari eneo limetengwa kwa ajili ya machinjio. Nimuombe sana Mheshimiwa Waziri basi katika kipindi hiki itengwe fedha ya kutosha ili sasa ujenzi wa machinjio hiyo ya kisasa uanze.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Singida una upungufu mkubwa sana wa Maafisa Mifugo, tunao 100 tu na wanatakiwa 522. Ninaomba Serikali yangu sikivu tupelekewe Maafisa Mifugo wa kutosha ili waweze kutoa huduma zinazotakiwa kwa wafugaji wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ningependa kushauri kupitia dawati la Sekta Binafasi katika Wizara ya Mifugo na Kilimo kutumia zile fursa zilizopo kubadilisha iel mikopo ya asilimia 10 kwa mfano kutoa miradi kwa vile vikundi vya wanawake vijana na kuona kwamba wale wanawake katika Halmashauri na vikundi vile vinanufaika kutokana na Dawati la Sekta Binafsi katika Wizara ya Kilimo. Lakini pia niendelee kutaka Serikali kupitia kwa Maafisa Mifugo, waendelee kutoa elimu kwa wafugaji wetu kwani hawa wafugaji bado wanafuga kwa zile njia za kiasili. Nina imani kubwa kabisa

kama iwapo wataendelea kutoa elimu basi hao wafugaji wetu wataweza kufuga ufugaji wa tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkoa wetu wa Singida hatuna vituo...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa kengele imegonga.

**MHE. AISHAROSE N. MATEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia. Hatuna vituo vya kutosha, vituo vile vinavyosaidia kugundua magonjwa ya haraka na kutoa huduma sahihi kwa wafugaji wetu. Nakushukuru saba, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, atafuatiwa na Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga. Mheshimiwa Profesa Adelardus Kilangi ajiandae.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Kwanza niseme marekebisho madogo kwenye jina kwa sabbau majina ya kwetu huwa yanahitaji *tuition.* Jina langu ni Zacharia Paulo Issaay, tunaitwa Massay mdogo na Massay mkubwa kwasababu ya kufanana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kwanza kuipongeza Serikali kwa kazi kubwa inayofanya katika nchi yetu kwa ujumla na wakati huu wa Serikali hii ya Awamu ya Tano kwa Wizara mbalimbali. Nichukue pia nafasi hii kupongeza uongozi wa Bunge na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, tuendelee kuiombea nchi yetu kwasababu ya janga hili la corona. Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema aweze kuliondoa katika Taifa letu. Nimpongeze sana Mheshimiwa Rais lakini pia tuendelee kuiombea nchi yetu na tumuombee Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeshatoa mchango wangu kwa njia ya mtandao. Naomba nichangia jambo moja tu dogo. Katika Serikali ya Awamu ya Nne tulianzisha *program* ya mnyororo wa thamani kwenye Sekta ya Kilimo na Mifugo. Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu iliyokuwa wakati

huo ilijenga vituo vya ushauri wa kitaalam kwa maafisa ughani. Kwa sasa tuna changamoto mbili, moja ni usimamizi wa vile vituo ili viweze kuutoa ushauri na mafunzo kwa wafugaji lakini pia hatuna wataalam. Nimuombe Waziri aweze kuona utaratibu kama nilivyomwandikia dokezo mwaka jana baada ya kushauriana naye apelike wataalam kule Mbulu ili tuone namna ambavyo vituo hivi vitatoa huduma stahiki na kuleta tija zaidi kwa maksudi yaliyoanzishwa toka mwanzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niseme tu kwamba wako maafisa mifugo, Serikali ione umuhimu mkubwa sana wa kutazama namna ambavyo walau hata kila kata kuwa na Afisa Mifugo, tuweze kuwaajiri hao vijana ili waweze kutoa mchango wao kwa Taifa. Pia niseme majosho, Mheshimiwa Waziri utakumbuka tulijadiliana nawe pale Ofisini baadae hapa Bungeni ukaahidi katika bajeti hii inayoisha kwamba ungetenga fedha kwa ajili ya ukarabati wa majosho pia na ujenzi wa majosho kwenye ngazi za kata. Kwasabbau ya hali hii ambayo sasa hivi tunaizungumzia kwamba pengine mtikisiko wa *Corona* na mambo mengine nimeiona kwenye Mpango wa Wizara hata kwa sasa, naomba uendelee kulitazama jambo hili ni kwa namna gani tunaweza tukatatua tatizo hili la ukarabati wa miundombinu na namna mbalimbali ambavyo wakulima na wafugaji na wadau wengine watapata huduma kulingana na Wizara yako.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa barua ile haikujibiwa kwa kuwa ulitoa wewe maelekezo wakati ule wa majadiliano, naomba ofisi yako iendelee kuifuatilia na kuweza kutoa mwelekeo ambao utatuweka katika mazingira mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Serikali, ni mchakato tunapokezana kijiti. Kwa kuwa mpango huu wa mnyororo wa thamani ulianzishwa na Serikali ya Awamu ya Nne na kwa kuwa sasa kazi yetu kubwa ni kuendeleza yale yaliyoanzishwa ili yaweze kutoa tija basi niitake Wizara waone namna ambavyo mpango/programu hii ya mnyororo wa thamani kupitia Sekta ya Mifugo unaboreshwa kwasababu lengo letu ni kwenda kwenye ufugaji wa kisasa na ufugaji wenye tija ili

kuweza kumfanya mfugaji aweze kunufaika na ufugaji anaoufanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwenye jambo hili wizara ninaamini wameisikia wataifanyia kazi na kwa jinsi ambavyo nimetoa taarifa kwa njia ya mtandao ni imani yangu hoja zote zilizotolewa au zilizotoka kwangu zitafanyiwa kazi na kupata mrejesho.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho tuna ziwa dogo kule Mbulu linaweza likapoteza samaki tulionao pale. Lile ziwa linahitaji majadiliano kwa kuwa hamashauri hatuna wataalam wa uvuvi, basi wataalam wa huku wa uvuvi waende ili waone namna ambavyo lile ziwa linaendeleza rasilimali samaki, perege na sato ili wananchi wa Mbulu waweze kupata huduma hiyo kwa ukaribu lakini pia katika namna ambavyo ustawi wa mazao haya unapatikana kwenye Ziwa Quri kule Halmashauri ya Mji wa Mbulu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nimtakie Waziri mafanikio mema, uchaguzi mwema, tunakwenda kwa wananchi, tutakutana mwakani, Mwenyezi Mungu awajaalie Waheshimiwa Wabunge wote waweze kurudi tuweze kulitumikia Taifa letu na kwa ujumla Mwenyezi Mungu ni mwingi wa rehema, atatupa nafasi ya mafanikio. Ahsante sana, nakushukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Adelardus Kilangi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Mheshimiwa Abdallah Hamis Ulega ajiandae.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumshukuru Mungu na nimshukuru sana Waziri, Naibu Waziri pamoja na Katibu Mkuu na wasaidizi wake katika Wizara hii ya mifugo kwa kazi nzuri sana walizozifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, mwanzo hatukumuelewa kumbe alikuwa na nia nje. Wanasema

ukisema kumtibu vizuri mgonjwa kamua jipu litoke vizuri ili aweze kupona. Kwa hiyo, Waziri mwanzo hatukukuelewa sasa tumekuelewa, kazi unafanya nzuri na samaki sasa wanapatikana. Ombi langu Mheshimiwa Waziri, kule Njombe tunapenda sana kula samaki, pale kuna Bwawa la Muhaji, pale Muhaji kuna magugu mengi sana kwa hiyo, samaki hawapo kutokana na magugu. Tunaomba katika bajeti yako, fedha zilizotengwa za maendeleo gawa fedha kiasi zikatengeneze bwawa lile ili na Njombe tuweze kupata samaki kwa wingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nizungumzie Jimbo la Makambako, napenda niwape habari njema wananchi wangu wa Makambako kwa mambo yale yalikuwa yamekwama sasa tumekwenda vizuri. Kwa mfano, wananchi wangu wa kule Kata ya Mahongole, kulikuwa na tatizo la umeme pale Mlucha Mkolango, niwape habari njema kwamba sasa nimeongea na Waziri, *transformer* watapata ili kusudi shughuli waliyokuwa wanategemea iweze kwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile wananchi wa Mtanga nguzo zitapelekwa kwa ajili ya kupelekewa umeme pale Mtanga na Kifumbe. Vile vile niwape habari njema ya miradi ya maji, vijiji vingi wako wakandarasi wanaendelea lakini mradi ule mkubwa wa fedha za India ambao ndiyo tegemeo kubwa la sisi wa Makambako, Waziri alituambia kwamba mwezi wa saba mkandarasi atakuwa *site* kwa ajili ya kutekeleza mradi huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile niwape habari njema ndugu zangu Makambako, tulikuwa hatuna wodi ya wanaume katika kituo cha afya cha Makambako, niwape habari njema kwamba Waziri wa TAMISEMI pamoja na Katibu wake na Naibu Waziri, tutapata fedha kwa ajili ya wodi ya wanaume, hatukuwa na wodi ya wanaume pale makambako. Vile vile katika Wizara hiyo hiyo ya Afya, Waziri Ummy na Naibu wake watatupa *x-ray* iko kwenye mpango, tutapata hivi sasa *x-ray.* Kwa hiyo, nampongeza sana Waziri Ummy tunakupongeza kwa kazi mbalimbali; nenda pale

Jimbo la Tanga Mungu akubariki upite bila kupingwa. Ninyi wana Tanga Mheshimiwa Ummy anafanya kazi nzuri sana na Naibu Waziri wake kule Kigamboni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwape habari njema nyingine kuhusu barabara zilizoharibika. Ndugu zangu wa Makambako, tumepata fedha, barabara zote zilizoharibika zitatengenezwa. Kwa hiyo, kuna barabara ya kutoka Makambako kwenda Mahongole kwenda Kifumbe Tanga, barabara hii tayari. Vilevile, kuna fedha ambazo zahanati ya Ibatu, Utengule, Mtanga na Ngamanga zitafunguliwa mwaka huu. Kwa hiyo, niwape habari njema zitafunguliwa mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ndugu zangu, Mheshimiwa Rais kutokana na kazi nzuri anazozifanya za nchi na Jimbo la Makambako nasi Wana-Makambako Madiwani wangu pamoja na wananchi, nami mwenyewe nimeunga mkono kwa miaka minne shilingi milioni 647 katika Jimbo la Makambako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Waziri wa Ardhi, ndugu yangu Mheshimiwa Lukuvi na Waziri wa Nishati, mkutane kwa ajili ya umeme wa upepo pale Makambako ili mtatue tatizo la wananchi hawa kupata fidia zao kwa sababu wamekaa muda mrefu. Waziri Lukuvi nilimpongeza juzi kwa wananchi wale wa Magongo kuwaambia wale watu 108 wasihame, Mungu akubariki sana kwa kazi nzuri unayoifanya na Naibu Waziri wako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, ndugu zangu Wabunge wenzangu na hasa ninyi wa Makambako, pale Makambako kuna mtu anapitapita anasema ametumwa na Rais, mwongo, hakuna mtu aliyemtuma, achaneni naye. Mwongo kabisa! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, mikopo. Wewe Waziri wa Fedha, mikopo ambayo wananchi wamekopa katika taasisi mbalimbali za fedha, kutokana na tatizo la *Corona*, tunaomba vyombo vya fedha

vione namna ya kuwasiliana na wakopaji badala ya kuuza mali zao, siyo jambo jema sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, mawili, (a) na (b). Kwanza, wale watu wa Mbeya ili mpate maendeleo, hivi Naibu Spika anataka sasa hivi angekuwa Mbunge aanze kuwaletea maendeleo; mpeni kura zote ili mpate maendeleo ninyi watu wa Mbeya. Msihangaike na mtu mwingine, Naibu Spika yuko hapa, watu wa Mbeya mpeni kura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimewahi kusema hapa kwamba Rais kutokana na kazi mbalimbali anazofanya kama mnakumbuka, nikasema China wao walisema Rais wao awe wa kudumu. Nasi Mheshimiwa Dkt. Magufuli awe Rais wa kudumu kutokana na kazi jamani! Kama siyo hivyo, kutokana na mipango mizuri anayoifanya, basi kipindi kinachokuja tubadilishe Katiba tumwongezee hata miaka mitano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, Mawaziri wote nawatakia kila la heri, mmekimbizana na kauli mbiu ya Rais kwa kazi anazofanya. Kwa kweli mmemuunga mkono Manaibu Waziri na Makatibu Wakuu, hongereni sana na Mungu awabariki mrudi tena. Nami wananchi wa Makambako niwaombe mnirudishe ili niweze kufanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga. Sasa nilikuwa najiuliza, jamani wale Wabunge ambao hawajatajwa wasijisikie vibaya, wao nitawaombea mimi. *(Makofi/Kicheko)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano

wa Tanzania; Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Waziri, Naibu Waziri na viongozi wote wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, kwa uongozi wao na utendaji uliotukuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na uongozi wote wa Bunge kwa uongozi wenu mahiri na wenye ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza Mhimili wa Bunge hasa katika kipindi hiki tunapopambana na janga la Covid-19.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha miaka minne iliopita, Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi imetekeleza miradi mingi na pia kusimamia kwa ufanisi sekta ya mifugo na uvuvi. Zoezi la kusajili mifugo lilifanyika vizuri na linatakiwa liwe endelevu na kuhakikisha usajili wa ki-TEHAMA kwa wafugaji na wavuvi wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza Serikali iangalia kwa umakini biashara ya ngozi kuhakikisha ubora na kupunguza changamoto za kikodi. Mfumo wa kodi kwenye biashara ya ngozi ujielekeze kutoa motisha kwa wafugaji ili kuwepo na ubora wa ngozi kwa soko la ndani na soko la nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi hiki tunapopambana na janga la corona virus (Covid-19), tumejifunza umuhimu wa kuwepo kwa mikakati mbadala kama vile kufanya kazi kwa kutumia TEHAMA. Kutokana na changamoto za Covid-19, kuna fursa za biashara ya mifugo na samaki kwenye soko la nje, napendekeza Serikali iweke mkakati wa ubora wa bidhaa zetu. Serikali iongeze uwekezaji kwenye mabwawa kwa ajili ya mifugo na hata ufugaji wa samaki. Nashauri Serikali ijenge mabwawa katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya kwenye vijiji vya Mjele, Ipwizi na Chang'ombe Kata ya Mjele na pia vijiji vya Mshewe, Njelenje na Mapogolo kata ya Mshewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. BERNADETHA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Makatibu Wakuu kwa kazi nzuri sana na uboreshaji uliofanyika katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mifugo ni kitu cha thamani sana Tanzania na inachangia ukuaji wa pato la Taifa. Ili kuongeza ubora wa mifugo inabidi tufanye yafuatayo:-

Mosi, kuboresha ng'ombe kwa kutafuta mbegu bora na kusambaza kwa wakulima.

Pili, kwa kutumia *artificial insemination,* kubadili kizazi hiki cha ng'ombe tuliokuwa nao mfano Mkoani Kagera, kuwafanyia *artificial insemination* ili tuweze kupata kizazi kipya cha ng'ombe, wakubwa, wenye minofu mingi na wenye uwezo wa kutoa maziwa mengi. Tusiendedelee kufuga kama tulivyozoea, tubadilike, ili ufugaji huu uache kuwa wa kuchunga bali ng'ombe wapate malisho yanayofaa. Kwa kufanya hivyo, ufugaji huu endelevu utamnufaisha mkulima mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu ya uvuvi usio endelevu na ongezeko la watu wanaoishi kwa kutegemea uvuvi wa samaki, inachangia kwa kiasi kikubwa kupungua kwa samaki kwenye Ziwa Victoria. Naipongeza Wizara kwani *operation* mlizofanya za kudhibiti uvuvi haramu, zimesaidia siku hizi tunapata samaki wakubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuongeza samaki watu wengi wameanza kufuga samaki kwenye mabwawa na kwenye vizimba *(cage).* Tatizo wafugaji wa samaki wameshindwa kupata mbegu/vifaranga vizuri wa sato wanaoweza kukua na kunenepa vya kutosha katika kipindi cha miezi nane hadi kumi. Je, Wizara wana mpango gani wa kuwapatia wafugaji wa samaki mbegu/vifaranga bora vitakavyonenepa vya sato?

Je, mchakato wa *tender* iliyotangazwa ya ugawaji wa vitalu vya ufugaji Mkoani Kagera umefikia wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. LUCIA M. MLOWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia katika hoja hii kama ifuatavyo; kwa kuwa kuna hitaji kubwa la samaki naomba Serikali itoe elimu kwa wananchi juu ya ufugaji wa samaki hasa maeneo ambayo yako mbali na maziwa. Iwapeleke wataalam maeneo mbalimbali ili watoe mafunzo ya namna ya uchimbaji wa mabwawa na upandaji wa samaki katika mabwawa hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa bado kuna mifugo mingi iko mijini mfano hapa Dodoma kuna mifugo mitaani, naomba Wizara ifuatilie kwenye Halmashauri ili wenye mifugo hao watozwe kodi kubwa ili walazimike kuhamisha mifugo yao. Naomba kuwasilisha.

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii ya kutoa mchango wangu katika Wizara hii muhimu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wake wote kuwa kutayarisha na hatimaye kuiwasilisha katika Bunge lako tukufu kwa ufasaha mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuchangia hotuba hii napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo; mosi ni elimu kwa wavuvi wadogo wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wavuvi ni miongoni mwa jamii kubwa katika nchi yetu. Jamii hii ya wavuvi wadogo inafanya kazi zake kimazoea kiasi ambacho maendeleo katika sekta hii ni madogo sana. Hii inatokana na Wizara kujiweka mbali kidogo na sekta hii. Naipongeza Serikali yetu kwa kuanza kuwa karibu na wavuvi hawa.

Ushauri wangu kuwa Serikali ni kuwapatia elimu pamoja na vitendea kazi ili waweze kumudu kazi zao za kuwapatia na kupata mapato wanayotarajia na kuwapunguzia makali ya maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, migogoro kati ya wakulima na uvuvi katika nchi yetu inazidi kukua kila siku. Hii inatokana na pamoja na mambo mengine ni uaminifu mdogo wa baadhi ya viongozi katika vijiji. Baadhi ya viongozi wa maeneo husika wanauza maeneo ya wafugaji kwa matajiri hivyo kuwapa taabu wafugaji kupata maeneo ya kufuga.

Ushauri wangu katika jambo hili kwa Serikali ni kuwadhibiti hawa viongozi ambao si waaminifu kwa kuwatungia sheria ambazo zitawabana kisheria kuliko kuwaacha wanaendelea na udhalimu huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. STEPHEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia kwa maandishi hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Mifugo kwa kuwasilisha hoja kuhusu wafugaji wa *West Kilimanjaro* ambao kwa miaka mingi sasa wamekuwa wakiililia Serikali bila mafanikio kuhusu kurejeshewa ardhi yao ya asili ya malisho iliyotwaliwa na kupewa wawekezaji ambao baadhi yao hawaitumii na yamebaki kama mashamba pori. Hoja hii niliizungumzia pia Bunge la bajeti la mwaka 2018/2019 lakini mpaka sasa Serikali haijatoa jibu lolote.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafugaji walikuwepo *West Kilimanjaro* kabla ya Bara la Afrika kugawanywa na wakoloni mwaka 1884. Wajerumani ndio wakoloni wa kwanza kuitawala Tanganyika na ndio waliowatoa wafugaji kutoka katika nyanda za juu zenye rutuba, mvua za uhakika, malisho na maji kwenda katika maeneo ya mbugani ambayo ni makavu na yasiyo na maji wanapoishi hadi leo.

Baada ya Vita Kuu ya Pili ya Dunia mwaka 1945, Serikali ya Uingereza baada ya kukabidhiwa koloni la

Tanganyika na Umoja wa Mataifa wakati huo ukiitwa *The League of Nations,* waliwazawadia wanajeshi waliopigana Vita vya Pili vya Dunia yale maeneo na wafugaji wakaendelea kubaki bila ardhi yenye maji na malisho ya mifugo yao nyakati za kiangazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 1968 baada ya Serikali kutangaza Azimio la Arusha na kutaifisha yale mashamba, Rais wa Tanzania, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere (Mungu ampe heri ya milele) alipotembelea Wilaya ya Maasai kama ilivyojulikana wakati huo alisikitika alipobaini kuwa wafugaji hawana ardhi inayofaa kwa malisho na maji ya mifugo yao nyakati za kiangazi. Akaagiza wapewe ekari 5,500 kwa ajili ya malisho ya mifugo yao. Tarehe 13/3/1973 Bunge liliridhia wafugaji kurudishiwa hizo ekari 5,500. Tarehe 16/3/1973 Serikali ilitenga rasmi ekari 5,500 za malisho kupitia GN No. 59.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TANAPA* ilipopitisha *operation* ya kubaini na kuweka alama mipaka ya Hifadhi ya Mlima Kilimanjaro miaka ya karibuni, eneo hilo lilijumuishwa katika Hifadhi ya *KINAPA (Kilimanjaro National Park).*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuishauri na kuiomba Serikali iwape wafugaji hawa ardhi mbadala katika mashamba pori ya *NDC; NARCO* na *NAFCO* yaliyoko katika ukanda huo wa *West Kilimanjaro.*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha kuna shamba moja ambalo matumizi yake yamekuwa yasiyo na tija, hususan Endarakwai Ranchi yenye ekari 11,000 ambazo mwekezaji mmoja wa kiingereza, Peter Jones analitumia kufugia wanyamapori na mifugo hawarusiwi kuingia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 1982 Rais wa Awamu ya Kwanza, Hayati Mwalimu Nyerere alimwagiza aliyekuwa Waziri Mkuu wakati huo, Hayati Edward Moringe Sokoine (apumzike kwa amani) kuanzisha Ranchi ya Jamii ya Larkarian. Ardhi husika iliainishwa, Mbunge na Waziri Mkuu wa wakati huo, Hayati Sokoine aliwahamasisha wafugaji

wakachanga mitamba 1,500. Lakini baada ya kifo chake, Mradi wa Ranchi ya Jamii nao ukafa. Baada ya Hayati Sokoine na Mradi wa Ranchi ya Jamii kufa, wawekezaji wakapewa ardhi hiyo ambayo inajumuisha mashamba nane yafuatayo; *Ndarakwai Ranch, Roselyn Farm, Tilonga Farm, Simba Farm, Mountain Side Farm, Engushai Farm, Mawenzi Farm* na *Leghumushira Farm.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa baadhi ya mashamba haya yamekuwa mashamba pori. Kwa hiyo, naomba kuishauri na kuiomba Serikali iwarejeshee wafugaji wa Kanda ya *West Kilimanjaro* ardhi hiyo au wapewe mbadala kwa ajili ya shughuli zao za ufuaji na hata kufufua Mradi wa Ranchi ya Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Ndarakwai Ranch* yenye ukubwa wa ekari 11,000 ilikuwa ni mojawapo ya maeneo muhimu ya jamii ya Kimasai ya kulisha mifugo yao hadi wakoloni walipojimilikisha. Ni baada ya Azimio la Arusha mwaka 1967 ndio Serikali ilitaifisha shamba hili na kulikabidhi *TBL.*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 1992 *TBL* ilibinafsisha shamba la Endarakwai kwa Kampuni ya *Tanganyika Film and Safari Outfitters* inayomilikiwa na Bwana Peter Jones, raia wa Uingereza. Mwekezaji huyu aligeuza shamba hili kuwa pori la kufugia wanyamapori na amekuwa na ugomvi mkubwa na wafugaji wanapojaribu kwenda kilisha katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafugaji wa *West Kilimanjaro* wanaiomba Serikali iwarejeshee ardhi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuhitimisha kwa kutoa kilio cha wafugaji; wafugaji wana matatizo mengi lakini kubwa zaidi ni la kupoteza ardhi yao ya asili katika sehemu mbalimbali za nchi yetu ikiwemo eneo hili la *West Kilimanjaro* nililojadili, Serengeti, Tarangire, Mkungunero na maeneo mengine mengi ndani ya nchi yetu. Maeneo haya yalibadilishwa kuwa ya matumizi mengine yenye maslahi mapana kwa Taifa lakini tatizo ni pale wenyeji wanapoachwa

bila ardhi inayofaa ya mbadala kwa malisho na maji ya mifugo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara ya Mifugo na Uvuvi ichukue hatua za kizalendo na watatue migogoro ya ardhi ya wazawa iliyotwaliwa kwa jina la uwekezaji na ambayo sasa yamegeuka kuwa mashamba pori yasiyo na faida kwa Serikali wala wananchi na badala yake yamekuwa chanzo cha ufilisi kwa wafugaji maskini ambao kila wanapokanyaga mashamba pori hayo wakitafuta malisho na maji wakati wa kiangazi wanakamatwa, wanapigwa na kutozwa faini kubwa zinazozidi kuwakandamiza kiuchumi na kuwaacha katika umaskini mkubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi kwa Waziri, Naibu wake na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri na kuboresha sekta ya mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na sekta ya mifugo kuchangia pato la Taifa bado Serikali haijawekeza nguvu ya kutosha kusaidia kuboresha wafugaji na mifugo hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini Serikali haitoi ruzuku ya madawa ya mifugo ili kusaidia kupunguza mzigo kwa wafugaji na kuondoa magonjwa ya mifugo yanayosumbua kila siku? Kuhusu masoko ya mifugo na mazao yake hapa nchini ni tatizo kubwa sana. Mifugo wengi wanapelekwa Kenya, kila siku pale mpaka wa Namanga malori zaidi ya kumi mpaka kumi matano yanabeba ng'ombe, mbuzi, kondoo kupeleka Kenya. Nini mkakati wa Serikali kujenga viwanda vya kuchakata mifugo na mazao yake hapa nchini?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilianzisha ujenzi wa machinjio ya kisasa pale Ruvu Darajani tangu mwaka 2012. Hatua gani imefikia kukamilisha machinjio hayo?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeweka mpango gani wa matumizi ya fedha inayokusanywa na Halmashauri ya Wilaya kwa kuweka mifugo alama?

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Kaliua ilikusanya milioni 130 mwaka 2018 kwa wafugaji kwa kuweka alama. Hakuna hata josho moja lililojengwa au kukarabatiwa kuendeleza mifugo, pesa yote wanagawana watendaji na baadhi ya viongozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Ardhi Namba 5 ya mwaka 1999 inaelekeza kutengwa kwa maeneo ya malisho ya mifugo na kulindwa. Maeneo yaliyotengwa ni machache sana na hayalingani na idadi ya mifugo tuliyonayo. Nini mpango wa haraka kutenga maeneo ya malisho ya mifugo ya kutosha ili kuondoa migogoro ya wakulima na wafugaji maeneo ya hifadhi?

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshauri Bandari ya Uvuvi kujengwa ili Taifa tunufaike na uvuvi wa bahari kuu na kuuza mafuta ya meli za uvuvi wa bahari. Ujenzi umefikia wapi na wapi? Ahsante.

**MHE. SILAFU J. MAUFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani kwa Rais wetu ni kubwa sana kwa kila Wizara na kila sekta hapa nchini, hakika zimetukuka kwa huyu mzalendo wa kujivunia. Mungu ampe maisha marefu. Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashukuru sana kwa kazi waifanyao hadi sasa katika halingumu sana ambayo kwa namna moja au nyingine na bado wananchi wanaendelea kuwalaumu ndani ya utekelezaji wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna taarifa ya makusanyo ya fedha kwa mifugo inayokamatwa kwenye hifadhi zetu, kwani zoezi hili kwa eneo kubwa linawanyanyasa wafugaji hasa. Wahusika na zoezi wanawadhulumu mifugo ya wafugaji na kuwarudisha nyuma kiuchumi na tunakoendelea wafugaji watatoweka au kutokuwa na imani na Serikali yao na kumpa kazi kubwa Rais

wetu. Hizi shilingi 7,032,625,639 za mwaka 2018/2019 zinawasaidia vipi wafugaji wenyewe kwa maendeleo yao, zinawarudia?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara kujenga mazingira bora ya kuendeleza sekta ya wafugaji kuwa endelevu, kuliko inavyoonekana hata watoto wa wafugaji kukatishwa tamaa ya kurithi. Kutokana na jinsi wazazi wao wanavyonyanyasika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema Wizara ikawa inatoa na idadi ya majosho yanayotakiwa kufuata na idadi ya mifugo iliyopo kwenye eneo husika. Tupate kuufahamu wigo wa zoezi lenyewe kwa tija ya wafugaji. Tuweze kulinganisha na ukarabati unaofanyika, upungufu uliopo na ujenzi wa majosho mapya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kiambatanisho kilichopo ukurasa wa 230 wa hotuba ya Waziri, kwani mifugo ni mingi ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano, Mkoa wa Rukwa ndani ya ukurasa wa 217 wanakarabatiwa majosho saba yaliyoorodheshwa, lakini ukurasa wa 230 inasomeka majosho 15 kukarabatiwa na josho moja kujengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. ABDALLAH HAJI ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyeizi Mungu muweza mambo yote. Aidha nakupongeza kwa utendaji wako wa kazi hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uvuvi wa samaki katika bahari kuu, samaki ni chakula na ni biashara ambayo unaweza kuuza popote duniani. Nchi yetu imebarikiwa kuwa na eneo kubwa la ukanda wa bahari, bahari ambayo ni mfano wa shamba ambalo limesheheni mazao mengi mazuri

ya kila aina. Shamba ambalo halitaki mbolea, madawa wala pembejeo yoyote bali linataka kuvunwa tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika kwamba nchi yetu bado hatujaweza kuitumia bahari yetu ipasavyo ili iweze kutoa faida stahiki kwa ustawi wa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa taarifa ya kitaalamu ni kwamba bahari yetu ina samaki wengi mno ambao kama tukiweza kuwavua wanaweza kutuongezea poto kubwa kwa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali kuiona bahari ni sehemu mbadala wa kukuza uchumi wa nchi, kwa hiyo, naiomba Serikali kuyafanya yale yote yaliyopangwa kwa muda mrefu sasa ambayo yakipangwa na kutekelezwa tunaweza kupiga hatua kubwa kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina uwezo mkubwa katika kutafuta wawekezaji wenye uwezo na kuja kuwekeza hapa nchini katika suala kubwa la uvuvi, jambo ambalo lingeweza kutusaidia sana hata katika kuajiri watu wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni ujenzi wa bandari za uvuvi katika mwambao wa Bahari ya Hindi jambo ambalo linalalamikiwa sana kwa muda mrefu sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uvuvi wa bahari kuu na upatikanaji wa samaki unakwenda sambamba na mahitaji ya kuwepo kwa viwanda hivyo, naishauri Serikali kutokulifumbia macho suala la ujenzi wa viwanda vya kuchakata na kusindika samaki. Aidha, Serikali itilie maanani suala la ujenzi wa vyuo vya uvuvi ili kuwapatia mafunzo stahiki ya uvuvi vijana wazalendo ili waweze kuyatumia mafunzo hayo katika kuokoa rasilimali yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na uwepo wa samaki wengi katika bahari yetu kumekuwa na taarifa ya wizi wa samaki unaofanywa na wavuvi kutoka nchi za nje. Naishauri Serikali kuimarisha ulinzi juu ya maeneo yetu kuzuia

wizi huu. Naiomba Serikali kuzingatia haya na mengine zaidi kwa maslahi ya nchi yetu. Ahsante sana.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Naibu Spika, madhara ya mlipuko wa ugonjwa wa Corona katika sekta ya mifugo na uvuvi; kupungua kwa *demand* kutoka wanunuzi wakubwa kutoka hoteli na migahawa wa bidhaa za uvuvi; kufungwa kwa usafirishaji mkubwa hususan kutoka Bara la Asia (hususan China) wa bidhaa za uvuvi; kumekuwa na upungufu wa bidhaa za uvuvi ambazo ni adimu na za bei kubwa (kamba, kamba kochi, kaa); hali hii imesababisha kupungua kwa bidhaa za samaki kutoka nje, hivyo kusababisha kupanda kwa *demand* ya samaki wanaozalishwa ndani. Angalizo, hali hii ni ya muda mfupi kwani kinachozalishwa ndani hakijitoshelezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi, kupungua kwa zao la samaki na kuongezeka kwa bei ya zao hili madhara yake yatakuwa zaidi kwa wenye kipato kidogo na kuathiri hali ya lishe. Serikali izingatie jinsi ya kumsaidia mvuvi kwa kuwawezesha kupata/kuboresha *credit programs* na msamaha wa mikopo kwa wafanyabiashara katika sekta hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Serikali ijikite katika kuimarisha ufuatiliaji *(remote monitoring)* na ufuatiliaji wa shughuli za uvuvi *(surveillance of fishing activities).*

Kuhusu mlipuko wa ugonjwa huu pia umeathiri shughuli za kiutalii katika maeneo ya mwambao ya pwani na baharini na *sports fishing,* hali hii inaathiri mapato kwa Kitengo cha *MPRU.* Nashauri Wizara ije na mipango mikakati ya kujinasua katika hali hii. Pia Serikali iangalie madhara ya ugonjwa huu pia kwa wafugaji nchini ambao wengi wao ni wachungaji/*migratory* na si wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa *TAFIRI;* taasisi haina Bodi ya Wakurugenzi; taasisi bila bodi ni ngumu kuiendesha; taasisi haina fedha za maendeleo kutoka vyanzo vya ndani kwa muda mrefu, hivyo tafiti zimebaki kutekelezwa kwa kutegemea fedha za nje (zaidi ya 80%). Ni vyema taasisi

ikapatiwa *research vessel* kwa baharini, ambacho ni kitendea kazi muhimu sana katika shughuli za tafiti na kuna upungufu mkubwa wa watumishi, japo Serikali ilitoa vipaumbele vyake ambavyo haviwapi nafasi *TAFIRI* kuajiri *core research staff* isipokuwa watu wa *IT* tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, *blue economy*/uchumi wa bahari, mito na maziwa; ni nini mkakati wa Serikali wa kujikita katika kuwekeza na kuimarisha shughuli za kiuchumi katika eneo hili? Kuna faida kubwa sana katika utumiaji endelevu wa rasilimali za bahari kwa ukuaji wa uchumi, kuboresha maisha, kutengeneza ajira wakati pia kuhifadhi afya ya mazingira ya bahari. *Blue Economy* italeta mabadiliko makubwa na chanya katika miundombinu ya kiuchumi *(structural transformation),* maendeleo ya kiuchumi na maendeleo ya jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ya kiuchumi ndani ya *blue economy* yanajumuisha;

(a) Nishati endelevu;

(b) Usafiri na uchukuzi *(means of transport for 80% of global trade);*

(c) Utalii;

(d) *Waste management*; na

(e) Mafuta na gesi (30% huchangiwa kutoka baharini).

Mheshimiwa Naibu Spika, angalizo; bahari inachukua 72% ya dunia *(area coverage),* bahari inatupa uhai kwa kuzalisha hewa *(oxygen)* na huchukua hewa ukaa *(CO2)* na hivyo hupunguza/*regulate* mabadiliko ya tabia nchi na hali ya hewa kwa ujumla. Bahari hutupatia 15% ya mahitaji ya protini duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mgawanyo wa bajeti ni mdogo sana katika sekta hii ambayo ni muhimu sana

katika kukuza uchumi wa nchi, uchache wa bajeti katika sekta hii huathiri mchango wake kwa ustawi wa uchumi wa nchi na pato la Taifa. Kuna uhusiano chanya kati ya ongezeko la bajeti kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na mchango wa sekta kwenye pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ilitengewa fedha katika Fungu 99-Mifugo (Maendeleo) shilingi bilioni 3.0 lakini mpaka kufikia Februari, 2020 Wizara iligaiwa shilingi milioni 154 tu, na Fungu 64 - Uvuvi (Maendeleo) ilitengewa shilingi bilioni 14 (fedha za nje) na shilingi bilioni 3.0 (fedha za ndani), lakini mpaka Machi, 2020 fedha zilizotolewa ilikuwa ni shilingi bilioni 4 (fedha za nje) na shilingi milioni 426 tu.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kuungana na viongozi wote wa Taifa letu, kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kuijalia nchi yetu mafanikio ya ustawi wa kijamii, kisiasa, kiuchumi, kidplomasia na huduma bora kwa wananchi. Nikianzia kwa Mheshimiwa John Joseph Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kwa pamoja tunasema ahsante sana Mwenyezi Mungu sisi sote tu waja wako, Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaasa Watanzania wote kuungana katika kuliombea Taifa letu kwa Mwenyezi Mungu kuhusu janga hili la Corona linalohatarisha ustawi wa jamii kwa Taifa na dunia nzima hakika ugonjwa huu ni hatari sana. Hivyo basi sote tuungane kwa kupambana na ugonjwa huu kwa kuzingatia maelekezo, kanuni ya Wizara ya Afya nyakati zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mbulu Mjini nachukua nafasi hii kuipongeza sana Serikali ya Awamu ya Tano kwa jinsi ilivyotekeleza Ilani ya CCM ywa mwaka 2015-2020. “Hakika tuko kidedea kuelekea uchaguzi mwezi Oktoba, 2020.”

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nitoe mchango wangu wa kuishauri Serikali kupitia Wizara hii kama

ifuatavyo; Serikali ya Awamu ya Nne ilianzisha programu ya mnyororo wa thamani katika sekta za kilimo na mifugo kwa kujenga vituo vya huduma za mifugo na mafunzo kwa wafugaji na zana za kilimo, pembejeo na samani za ofisi kwa Jimbo la Mbulu kulijengwa vituo vine kwenye kata za wafugaji hadi sasa hakuna kituo kilichoanza kutoa huduma hivyo basi Wizara ifanye mapitio kwenye mradi huu ili mradi huu utoe huduma.

Suala la kuajiri Maafisa Ugani kwa sekta hii muhimu ya mifugo ni la muhimu sana walau kwa ngazi za Kata kote nchini ili kupeleka huduma bora za kitaalam kwa wafugaji. Katika Hamashauri ya Mji wa Mbulu kwenye mnada wa mifugo wa Endagikort Serikali ilijenga mizani ya mifugo mwaka 2003 hadi sasa mizani hiyo haijatumika kwa sababu ya ukosefu wa wataalam wa kusimamia kupima mifugo. Hivyo basi Serikali itume wataalam kwenda Halmashauri ya Mji wa Mbulu, ila kuna namna sahihi ya mizani hiyo.

Kwa kuwa mwaka 2019 nilimwandika Mheshimiwa Waziri kuhusu mpango wa kukarabati majosho katika Kata za Tlawi, Gehandu, Murray, Gunyoda, Kainam, Nambis na hadi sasa hakuna majibu ya maombi hayo Serikali kupitia bajeti ya mwaka 2020/2021 iweze kutafuta fedha za kutatua hilo na kutoa huduma bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iwe na mpango wa kuhamasisha uanzishwaji wa mazao ya mifugo kwenye maeneo ya mikoa ya ufugaji. Halmashauri ya Mji wa Mbulu ina Ziwa dogo la Tlawi Kwaanseri ambalo hutoa samaki aina ya sato na perege; hata hivyo wavuvi hutumia nyavu inchi 1.5. Hata hivyo upatikanaji wa samaki uko hatarini kutoweka. Hivyo timu ya wataalam ifanye ziara ya kwenda Mbulu ili kuwa mkakati wa kutatua changamoto hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga hoja 100% na naomba kuwasilisha.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu

Waziri, viongozi wa Wizara kwa kazi nzuri, Waziri Mheshimiwa Mpina ahsante sana kwa kututembelea katika Mkoa wetu wa Lindi, kuja kujionea maendeleo na changamoto zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mambo mawili kwa Waziri; mosi ni kuhusu machinjio yetu ambayo ni bora na ya kisasa. Tayari imejengwa kwa utaalam mkubwa na imemalizika na thamani ya fedha inaonekana. Kwa kuwa bajeti ya mashine haikuwepo na hili jambo unalifahamu, tulikuambia na umekubali kutusaidia. Je, ni lini utekelezaji wake utafanyika ukizingatia hii ni bajeti ya mwisho?

Mheshimiwa Naibu Spika, pili nakushukuru sana, nakumbushia boti ambayo uliahidi kunipatia mbele ya Bunge letu tukufu mwezi tano, mwaka 2020.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Prof. Adelardus Kilangi atafuatiwa na Mheshimiwa Abdallah Hamis Ulega na mtoa hoja ajiandae.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia katika mjadala huu tunapohitimisha. Nami nitajielekeza zaidi kwenye suala linalohusiana na ukamataji wa mifugo na mwenendo mzima wa kesi zinazohusiana na suala hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la nitakayoyazungumza ni kutoa ufafanuzi kidogo, japokuwa kwa upande mmoja nakubali kwamba kwa sababu ofisi yetu imeshahusika mara kadhaa kwamba zipo changamoto kadhaa zinazohitaji kufanyiwa kazi, lakini pia ni muhimu kuendelea kufafanua na kuelezea msimamo sahihi wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikilizungumzia jambo hili la kuwakamata ng'ombe katika ujumla wake pamoja na utaratibu mzima unaohusiana na kesi zinazohusiana na ukamataji huo, nianze kwa kusema kwamba linafanyika kwa mujibu wa sheria na sheria yenyewe tumeitunga wenyewe hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaloweza kusema ni kwamba mara nyingi katika utekelezaji wa sheria hizi, changamoto huwa zinajitokeza. Itoshe tu kusema kwamba katika Sekta ya Sheria, najua Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria ataliongelea pia kidogo, tumeshaona baadhi ya changamoto hizi na hatua stahiki zinachukuliwa kuziondoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kutoa wito kwamba pamoja na yote haya, wakati mwingine changamoto zinatokea kwa sababu ya kutofuata sheria. Ninaposema kutokufuata sharia, ninagusa pande zote; ninagusa upande wa wale wanaotakiwa kusimamia sheria hizo wanatakiwa wazisimamie kwa mujibu wa sheria na pia kwa upande wa wa ndugu zetu wafugaji nao vile vile tunawapa wito wa kufuata na kuzingatia sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na suala mahususi lililojitokeza kwamba Mahakama inatoa hukumu, lakini mifugo hairudishwi, inaendelea kushikiliwa. Kwa bahati mbaya kidogo, katika masuala haya kuna ukweli mwingi ambao haufahamiki, kuna mambo yanayofahamika na yasiyofahamika; na mara nyingine wanaotoa taarifa hawatoi ama taarifa zote au zinakuwa na ukweli kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe tu mfano wa hii *clip* ambayo imekuwa inazunguka iliyokuwa inaeleza kwamba Mahakama imeshatoa hukumu lakini mifugo haijarejeshwa. Kitu kimoja kwa mfano katika *clip* ile ambacho hakikuzungumzwa ni kwamba kumekatwa rufaa na kukikatwa rufaa, basi hukumu ya Mahakama ile ya chini haiwezi kutekelezwa kwanza mpaka ile rufaa inapokuwa imekamilika; na hii ni kesi ya jinai. Ingekuwa kesi ya madai, wakati mwingine hukumu inaweza kutekelezwa katika mazingira fulani fulani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, kama nilivyosema hapo awali, hii haimaanishi kwamba kunaweza kuwa na tatizo mahali fulani, inawezekana katika baadhi ya hizi kesi lipo tatizo mahali fulani la msingi. Nami niseme tu tena

hapa bila kuzungumza mambo mengi kwamba tunafuatilia kwa karibu kabisa hizi kesi zote na tujue kwenye kesi ipi mfugaji alitakiwa kurudishiwa mifugo yake kihalali na kwenye kesi ipi kesi ile bado haijaisha na kwa hiyo, bado mfugaji hawezi kurudishiwa mifugo yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu lilihusu suala la *DPP* kukata rufaa. Ninaelewa kwa kweli *concerns* za Waheshimiwa Wabunge wanaposhangaa kwamba kwa nini Mheshimiwa *DPP* anaendelea kukata rufaa hata anapokuwa ameshindwa kwa mfano kwenye Mahakama ya Awali, akaenda Mahakama Kuu bado akashindwa, kwa nini anaendelea kukata rufaa?

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu hapa kwamba kwamba kwa kuanzia majukumu ya *DPP* yapo Kikatiba na kwa kweli hayaingiliwi na mtu yeyote, lakini siku zote tunaamini kwamba anatekeleza wajibu wake kwa kufuata sharia. Kwa vyovyote vile, anakuwa ana sababu anapoamua kukata rufaa, lazima zipo sababu za msingi. Pia siyo kila wakati *DPP* anapokata rufaa ni kwa sababu hakuridhika na uamuzi uliotolewa katika jambo lile, lakini mara nyingine na hasa anapokata rufaa kwenda Mahakama ya Rufaa kunaweza kuwa na tafsiri isiyo sahihi ya sheria na mahali pekee unapoweza kupata tafsiri sahihi ya sheria ni kwenda katika Mahakama ya Rufaa.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa dakika moja, kwa ruhusa yako.

Mheshimiwa Naibu Spika, palikuwa pia na suala la uhusika wa wadau mbalimbali, sasa Wizara ya Mifugo ina nafasi gani? Katika jambo hili, zipo Wizara mbalimbali zinahusika; Mifugo yenyewe, Wizara ya Maliasili na Utalii, Ofisi ya Taifa ya Mashitaka na pia kuna mhimili wa Mahakama pia. Sasa huu ni mchanganyiko wa wadau wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda niseme tu kwamba tunaloliangalia la muhimu ni kuwa na mfumo mzuri wa uratibu wa hawa wahusika wote katika suala hili. Ila kwa kweli kila taasisi ina sheria na taratibu zake na unapoingiza hata Mahakama basi huu ni mhimili ambao hata huwezi ukausukuma. Ni kwamba tu tunafanya *appeal* kwa mhimili wa Mahakama kwamba kama zipo kesi basi zimalizwe kwa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nami naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mwigulu Nchemba.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii nami niweze kuchangia kidogo kwenye hoja iliyopo Mezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais. Kwa Wabunge ambao hii ni awamu yetu ya pili mtakumbuka kwamba ilipokuwa ikifika Wizara ya Mifugo kulikuwa na vilio vingi sana. Mheshimiwa Rais pamoja na wasaidizi wake katika Wizara hii kwa kweli wamejitahidi sana kuhakikisha kwamba vile vilio vilivyokuwa vinaikumba Wizara hii vimepungua kwa kiwango kikubwa japo kama ambavyo tumesikia kutoka kwa baadhi ya Wabunge zimebakia dosari dosari ambazo na zenyewe zinaendelea kushughulikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu Mwanasheria Mkuu wa Serikali ameshapita kwenye yale mambo mahususi, niseme tu kwa niaba ya Wizara kwamba tutaendelea kushirikiana na Wizara nyingine kama ambavyo unaona Mheshimiwa Rais alishatoa maelekezo ya kutengeneza jopo la Wizara nane kushughulikia dosari ambazo zinaendelea kujitokeza. Hii imekuwa kawaida ya Mheshimiwa Rais kwamba pale ambapo kuna sheria ambazo zinaonekana kukwaza shughuli za kila siku za wananchi wetu katika

kujiletea maendeleo, amekuwa akitengeneza mapendekezo ambayo yanapitishwa na Bunge lako Tukufu kurekebisha hizo sheria ili wananchi wetu waweze kujiletea maendeleo bila vikwazo vyovyote. Imefanyika hivyo kwenye kutengeneza mazingira bora ya biashara, Wizara ya Madini na masuala ya manunuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hata haya ambayo Waheshimiwa Wabunge wameyaongelea kama sehemu ya maeneo ambayo bado yanakwamisha Wizara husika. Sisi kama Wizara wezeshi inayoshughulika na masuala ya sheria kama ambavyo Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ameweza kusema, tutashirikiana na Wizara hizo ili tuweze kutengeneza hayo mazingira bora mahususi ya upande wa kisheria ambayo yatawezesha wenzetu waweze kutekeleza majukumu yao vizuri ili wafugaji pamoja na maeneo mengine waweze kutimiza majukumu yao ya kujiletea maendeleo mahususi bila kupata vikwazo vya kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu lingine moja, kama ambavyo kuna baadhi ya Wabunge wamegusia suala la *Corona*, niseme kwamba tumpongeze sana Mheshimiwa Rais aliona mbali sana kwenye jambo hili. Watanzania wameitikia vizuri sana. Juzi juzi nilipata taarifa kwamba mpaka vijijini wameitikia maelekezo ya Mheshimiwa Rais pamoja na maelekezo ya wataalamu wetu. Vile vile wameitikia vizuri sana kuondoa taharuki. Siyo hilo tu, wameendelea kuliombea Taifa letu. Kwenye majanga hatuwezi kujiokoa kwa ujuzi wetu wenyewe, ndiyo maana unaweza ukaona kila eneo msisitizo ni huo huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kauli na rai yangu kwa Watanzania baadhi yetu ambao wanafanya kazi ya kupiga ramli, utasikia, Tanzania tutatengwa. Ukisoma ndani yake unaona ni kama vile wanataka kujituhumu kama Watanzania kuhusu jitihada ambazo zinachukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili jambo ni la dunia nzima; na kila Taifa wanaendelea kuhangaika. Hakuna Taifa ambalo limeshakuja na mbinu au njia muafaka waseme kwamba njia

yao wanayotumia ndiyo mia kwa mia inaweza kulikoa Taifa hilo katika eneo hilo. Kila Taifa linahangaika! Hata sisi tumeshafanya jitihada kubwa na utaweza kuona kwamba hata yale Mataifa ambayo wametumia mbinu nyingine mbadala wameweza tu kuzalisha matatizo mengine. Wale ambao walisema waweke *lock down,* tumeona *cases* zinaendelea kuongezeka na wamezalisha na matatizo mengine. Wale ambao viongozi wao walikuwa wanatokea kuhutubia asubuhi, mchana na jioni na wenyewe *cases* zimeendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wale Watanzania ambao wanajipa kazi ya kupiga ramli, tunawaomba wawe na upendo na Taifa lao wenyewe ambalo ndiyo Taifa letu. Kama wenzetu wana hati mbili mbili, wana na Mataifa mengine, basi watuachie sisi ambao Taifa letu ni hili hili. Wasilipake Taifa matope kwa jambo ambalo ni janga la dunia. Wewe angalia *Corona* imebisha hodi mpaka Ikulu ya Marekani, Ikulu ya Uingereza na kila eneo, lakini utasikia madereva, madereva; Tanzania, Tanzania; wanazalisha taarifa. Bahati nzuri sana Waziri wa Mambo ya Nje jana ameweka vizuri sana, hakuna Taifa ambalo limetoa kauli ya aina hiyo ya kuisukuma Tanzania, lakini Watanzania wenzetu wao wapo *busy* kulipaka matope Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitamwomba Mwanasheria Mkuu wa Serikali aangalie vipengele vya mtu akilihujumu Taifa inaangukia kwenye vipengele gani? Kwa sababu tunajua ile ya kuhujumu uchumi ipo wazi, lakini hii ya mtu kupaka Taifa matope akilengesha watu walione Taifa letu kama kuna mahali ambapo hatufanyi vizuri, hii haijakaa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania tuendelee kumwombea Mheshimiwa Rais, aliongelea vile vitendea kazi vinavyotoa majibu ya ovyo, wiki moja baadaye India na Mataifa mengine wakasema hivyo hivyo. Hata yale aliyosema tuangalie namna, huenda hili gonjwa tukaendelea kuishi nalo; nimeona taarifa hata Shirika la Afya Duniani limesema linakisia hili jambo linaweza likaenda muda mrefu,

tuangalie namna ambavyo tunaweza tukaendelea kujihami na huenda likawa nasi kwa muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niliona niongelee na hili ili watu wetu waendelee kuona kwamba tunahitaji sana uzalendo katika jambo hili linaloikumba dunia na nchi yetu kwa ujumla. Wale wanasiasa wanaodhani na hii ni ajenda, niseme, wangezaliwa enzi ya kupigania uhuru huenda Taifa letu lingechelewa sana kupata uhuru kwa sababu ya usaliti wa aina hii. Ni dhahiri kwamba wangekuwa na wale ambao walikuwa wanatunyonya. Kwa hiyo, kwa wakati huu, wajue kwamba hili jambo siyo la nchi moja, ni jambo la dunia nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasisitiza yale yaliyokuja yanayohusu Wizara yangu, tutashirikiana na Wizara nyingine pamoja na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na taasisi nyingine ili tusimkwamishe Mheshimiwa Rais kwenye nia yake ya kuwasaidia Watanzania wanyonge kupata haki yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Namwita sasa Mheshimiwa Abdallah Hamis Ulega almaarufu Baba Tulia. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami niungane na wenzangu wengine wote kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Sub-hanah-Wataala kwa kunijaalia rehema na kuweza kuwa ni miongoni mwa wazungumzaji jioni hii ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nichukue fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Mtume wa Mwenyezi Mungu Muhammad Sallallahu Alaih Wasallam katika hadithi Sahihi anasema, *Laayashkurinnasa, Laayashkuri-llah.* Kama huwezi kuwashukuru wanadamu wenzio, basi huwezi kumshukuru Mwenyezi Mungu vilevile. Kwa maneno hayo, namshukuru

sana Mheshimiwa Rais kwa kuniamini kuweza kumsaidia kazi katika Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi kama Naibu Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo humu Waheshimiwa Wabunge wengi wametupa pongezi nyingi sana. Kusema ukweli kwa uzoefu wangu wa miaka hii miwili, mitatu nimeona leo kwa mara ya kwanza Wabunge wameishangilia na kuipigia makofi na wamekiri ya kwamba tumefanya vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nimesikia humu Waheshimiwa Wabunge wengi wametupa pongezi nyingi sana kwa kusema ukweli kwa uzoefu wangu wa miaka hii miwili mitatu nimeona leo kwa mara ya kwanza Wabunge wameishangilia na kuipigia makofi na wamekiri ya kwamba tumefanya vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ninaomba nichukue fursa hii kuwashukuru sana wapiga kura wangu wa Jimbo la Mkuranga Mkoani Pwani kwa mapenzi na mahaba yao makubwa sana kwangu, na mimi nataka niwahakikishie ya kwamba nitaendelea kuwatumikia kwa uadilifu na kwa unyenyekevu uliokuwa mkubwa. Kazi ambayo tumeshaanza kuifanya katika Jimbo letu la Mkuranga ni kubwa na hivyo tunahitaji kuendelea kuhakikisha Mkuranga inaendelea kupaa; Mkuranga tuliyoikuta mwaka 2015/2016 siyo Mkuranga tuliyonayo leo. Mkuranga iliyokuwa na viwanda 20 leo ina viwanda 86, Mkuranga ambayo imerekebisha vituo vya afya, Mkuranga ambayo imerekebisha hospitali ya wilaya, Mkuranga ambayo imejenga miundombinu ya madaraja na matuta ya kupita maji na watu kuepuka adha za mvua.

Mheshimiwa Naibu Spika, miongoni mwa viwanda vilivyojengwa ni vile vya mifano. Mkuranga leo ina viwanda vya korosho ambavyo vimewezesha mwaka huu kuchukua hata korosho za wakulima na kuzibangua na kuongeza thamani. Mkuranga leo hii ina kiwanda kikubwa cha *tiles* Afrika ya Mashariki yote; Mkuranga ambayo ina kiwanda

kikubwa cha *gypsum* kinachokwenda kujengwa pale kinachotumia *German technology,* hakuna katika Afrika ya Mashariki. Mkuranga ambayo ina viwanda vya mabati na nondo, Mkuranga ya mfano, Mkuranga hii ya Ulega na Magufuli Mkuranga hoye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema haya naomba nielekee kidogo katika muktadha wa jambo ambalo linaendelea duniani kote. Nachukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, na ninukuu *suratul al Imran* aya ya 159 mwenyezi mungu *subhanahu wa taala* anasema katika suratul al *Imran Bismilahi Rahman Rahim faidha adhamta fatawakkal alallah innallah yuhibu mutawakiliyn.* Nini anasema hapa mwenyezi Mungu? Anawatia nguvu wale watu ambao wanamtumainia yeye na anawaambia kwa wale wote wenye kumtumainia mwenyezi Mungu, hakika Mwenyezi Mungu anawapenda sana ndiyo ile kusema *innallah yuhibul mutawakiliyn* hakika ya Mwenyezi Mungu anawapenda watu wanaomtumainia.

Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli amelionesha hilo kwa uwazi kabisa; ya kwamba yeye anamtumainia Mwenyezi Mungu na ametutaka sisi Watanzania tumtumainie Mwenyezi Mungu huku tukichukua tahadhari ya ugonjwa wa Corona. Inashangaza sana wale watu ambao wakati fulani pale nyuma nilipokuwa *back bencher* niliwaita popo; wametusaliti tena wakati huu katika jambo ambalo ilipaswa tuungane. Dunia leo maono ya Mheshimiwa Rais yako wazi. Tazama ametoka kusema hapa Waziri wa Sheria na Katiba sasa hivi ya kwamba *WHO* Mkurugenzi anayehusika na masuala ya *program* za afya na *program* za *emergency* Dkt. Maik Riyan jana ame-*declare* yeye mwenyewe ya kwamba corona virus haiwezi kuendelea kuwa ni *pandemic it is going to be endemic* tutaishi nayo kama vile tunavyoishi na maradhi ya Ukimwi na maradhi mengine. Kwa hiyo wewe leo ukichukua *option* ya kujifungia ndani wengine walijifungia ndani miezi mitatu wametoka wamepata tena hayo maradhi. China mlipuko umeanza tena upya katika baadhi ya miji. Kwa kweli kama kuna kiongozi

tumempata katika taifa letu mwenye maono ni Dkt John Pombe Joseph Magufuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo ni katika *scenario* hii ya ugonjwa wa corona ukichukua katika mipango ya kimaendeleo. Ukiangalia SGR, mimi siamini kwamba SGR hii ni kwa ajili ya kizazi cha leo tu. *SGR* hii ni kwa ajili ya kizazi kinachokuja na kinachokuja tena miaka 50, 100 ijayo. Ukiangalia mradi wa Nyerere si wa miaka hii. Haya maono ni maono kama vile ya Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alipojenga Chuo Kikuu cha Dar es Salaam miaka ya 60 na 70 hata wanafunzi 1000 walikuwa hawafiki; kumbe alikuwa anawatazama akina Abdallah Hamis Ulega watakaokuja miaka 50 baadaye. Tumekwenda, tumenufaika na sisi leo tunajenga taifa letu mungu ambariki sana Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikienda katika baadhi ya zile hoja zilizozungumzwa, kwa mfano *blue economy;* tumeulizwa ni namna gani tumejipanga sisi Serikalini ili ku-*trap opportunity* hii ya *blue economy;* Serikali imejipanga vyema.

Mheshimiwa Naibu Spika, *blue economy* ni *concept* pana inayohusisha mambo mengi. *Gas industry* inahusika, mambo ya *tourism* yanahusika, mambo ya *fisheries* ni *subset,* ni eneo dogo katika *blue economy. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiitazama Serikali imeshafanya kazi hiyo, na ndiyo maana Mheshimiwa Rais ametoa bilioni 5.2 kule Lindi kwa ajili ya kulipia mradi wa *LNG;* ile ni gesi ambayo iko katika upande wa baharini, hiyo ni *blue economy*. Ukiona tumesisitiza sana juu ya utalii wa *eco-tourism* hiyo ni *blue economy*. Sisi wa *fisheries* tumejipanga vyema; Ibara ya 27(a) ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi inatuelekeza kuhakikisha kwamba tunaunda vikundi vya wafugaji na wakulima na tumeunda hivyo vikundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, na nikupe habari njema, kwa mara ya kwanza katika historia ya taifa letu haijawahi kupata kutokea sekta za mifugo na uvuvi ziende kukopa benki

bilioni 100 na kutengewa bilioni 26; na hapa tunapozungumza tayari wafugaji na wavuvi wameshapewa bilioni 11/bilioni 10 zimeenda katika upande wa wafugaji na bilioni moja imekwenda katika upande wa wavuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, na basi habari njema zaidi ni kwamba hizi bilioni 10 unazozizungumzia hazikwenda kwa wafugaji wakubwa tu peke yake zimekwenda pia kwa wafugaji walio kwenye vyama vya ushirika. Kwa mfano Chama cha Ushirika cha Chawamu na Uwamwa vya ng'ombe wa maziwa kule Tanga *(TDCU)* wamepata pesa kutoka benki yetu ya kilimo kwa ajili ya kulisha kiwanda chetu cha *Tanga Fresh haya* ni mafanikio makubwa ambayo sisi tumeyapiga.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile vyama vya ushirika vya wavuvi pale Ukerewe Bukasiga kwa Mheshimiwa Michael Mkundi wamepata pesa lakini vilevile chama cha ushirika cha kule Buchosa, panaitwa Zilagula, kitapata pesa; hivi vyote vinapata kutoka katika benki yetu ya kilimo. Nini kilichofanyika, ni kuweka imani mpango mkakati mzuri wa Serikali ya Awamu ya Tano wa kuhakikisha kwamba tunalinda rasilimali zetu lakini vile vile tunaonesha njia na kuwadhamini wafugaji na wakulima wetu ndiyo maana hata benki leo zinakuwa na imani na wafugaji na wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia kabisa naomba niseme tu natoa shukrani nyingi sana kwa Waheshimiwa Wabunge wote waliotupongeza sana mimi na Mheshimiwa Waziri wangu; na mimi kwa namna ya kipekee na kwa umuhimu naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Luhaga Joelson Mpina.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hakika kabisa nilalo jambo nililojifunza kutoka kwa Mheshimiwa Waziri Luhaga Joelson Mpina. Katika miaka hii miwili mitatu nimejua ni kwanini tunasema kwamba mzigo mzito mpe Msukuma. Huyu jamaa anajua kuchapa kazi; wala sijasema mnyamwezi nimesema mpe Msukumu; anajua kuchapa kazi kama liko

jambo ambalo nimejifunza kwake ni kutumia maarifa na nguvu zake zote katika uchapaji kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamtakia kila la heri na yeye na nina amini kabisa wananchi wa Jimboni kwake Kisesa watamchagua tena kwa mara nyingine kwa kishindo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mungu awabariki Waheshimiwa Wabunge wote awabariki na aibariki taifa letu ambariki Mheshimiwa Rais Dkt John Pombe Joseph Magufuli nashukuru sana, naomba kuunga mkono hoja asilimia 100 ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina Waziri wa Uvuvi na Mifugo uhitimishe hoja yako.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii uliyonipa ili niweze kuhitimisha hotuba yangu; lakini pia niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao mizuri sana walioitoa na maswali mengi sana waliyoyauliza na mambo mengi waliyouliza wakitaka ufafanuzi na kutaka hata msimamo wa Serikali katika baadhi ya maeneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachoweza kusema tu Waheshimiwa hawa wamechangia kwa kuandika wengi sana, wameongea hapa na wametoa hoja nyingi sana ambao kwa muda huu hazitaweza kujibiwa kwa hizi dakika 15 lakini tunaahidi kabisa kwamba majibu yote yatapatikana na Waheshimiwa Wabunge watayapata majibu yao ya kila swali walililoliuliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo furaha sana leo, tangu niwe Waziri wa Mifugo na Uvuvi hii ni hotuba yangu ya tatu kuwasilisha hapa kwenye Bunge lako; na nifurahi kwamba leo nimepigiwa makofi mimi na Wizara yangu. Wizara yangu ilikuwa kila siku ilikuwa mshike mshike mkubwa sana hapa Bungeni lakini niliwaahidi Waheshimiwa Wabunge niliwaahidi wananchi wa Tanzania ya kwamba ipo siku Wizara hii itawasilisha taarifa yake na itashangiliwa kwa makofi; na

leo nifurahi sana kwamba Waheshimiwa Wabunge wametuunga mkono katika shughuli ambazo tunazifanya na majukumu tunayoyatekeleza na hatimaye mafanikio mengi yamepatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu tunajitahidi sana, na leo hii tumeleta hii bajeti *the pro-poor* bajeti kwa ajili ya masikini. Ukisoma randama yetu hii utashindwa kuelewa bajeti ya maendeleo na bajeti ya matumizi ya kawaida ikoje kwasababu ni yote maendeleo. Hizi fedha ndogo mipango mizuri ya fedha ndogo zinazopangwa kwa wananchi Watanzania maskini zinaenda kutumika kwa Watanzania wenyewe. Kwahiyo Waheshimiwa Wabunge mtapata nafasi nzuri ya kusoma landama na mtapata nafasi nzuri ya kusoma hotuba ambayo nayo ina kurasa nyingi mtayaona hayo ninayoyazungumza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikianzia na suala hili la marekebisho ya sheria ambalo Wabunge wengi sana wamelizungumza; nataka tu niwaambie Waheshimiwa Wabunge, ni kwamba safari ya mageuzi ya sekta yameanzia sana katika hili eneo la marekebisho ya sera, sheria na kanuni. Kwenye sheria tu za mifugo zenyewe tumerekebisha kanuni 20 zimetungwa kanuni 20. Haijawahi kutokea katika historia ya nchi yetu kutungwa kanuni 20 kwa mara moja na kwa wakati mmoja; na kanuni hizi katika sekta ya mifugo zinaenda sasa kwenda kuleta mageuzi ya kweli katika sekta yenyewe. Mtaona kuna ya chanjo *(vaccine and vaccination regulation 2020).*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inaenda kutoa ulinzi wa kutosha kuhakikisha kwamba mifugo ya Watanzania yote inakingwa kwa magonjwa, inalindwa kwa magonjwa, inalindwa kwa kupewa dawa feki, inalindwa kwa nguvu zote. Na katika kufanya hivyo mifugo ya Watanzania wote watakingwa na magonjwa na hawata kufa kwa magonjwa; na kwa maana hiyo tutahakikisha kwamba masoko tuliyoyakosa tutayapata sasa kwasababu si Tanzania hiyo tena ambayo mifugo ilikuwa ikifa kwa magonjwa kila mwaka.

Kwa hiyo kanuni hiyo imetungwa leo mmeona kanuni ya uvuvi ya mwaka 2009 ambayo na yenyewe tuliifumua. Baada ya kuifumua tumeweka baadhi tu ya vipengele kwenye kanuni hiyo, tumeweka baadhi ya vipengele kwenye hotuba ya sheria kwenye hotuba yetu hii ya bajeti tumejaribu kuweka baadhi ya vipengele. Hata hivyo hayo tuliyoyaweka si yote ambayo tumefanya mabadiliko katika hiyo kanuni. Ile kanuni tumebadilisha vitu vingi, tumeweka vitu vingi ambavyo vinaenda kuleta mageuzi ya kweli kwa wavuvi wetu na nataka niwatakie kila la kheri wavuvi Watanzania ambao watanufaika na hayo mageuzi makubwa ambayo tuliyoyafanya na mmoja tumesema pale. Kwa mfano suala la kuunganisha nyavu liliombwa muda mrefu sana. Tumefanya utafiti tumefuatilia na tumeona turidhie kibali cha kuruhusu matumizi ya nyavu zilizoungwanishwa zenye macho 78 ambayo ilikuwa ndilo ombi kubwa la muda mrefu la wavuvi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia ukiweka na hizi faida nyingine tulizoziweka katika kufumua hii kanuni tumeweza kuruhusu matumizi ya watu wafanyabiashara wa mabondo na wafanyabiashara wa samaki; walivyokuwa wakisema bwana samaki akipungua tu sentimita moja tayari umekamatwa tumeruhusu leo kwamba kutoka sentimita 50 sasa mvuvi anaweza kuruhusiwa mpaka sentimita 48 kwa maana ya kwamba ile *level standard era* ya tume-*establish standard era* ya hasi mbili ambayo wavuvi wetu hawataingia tena kwenye mtego huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia samaki waliokaushwa tume-*establish standard era* ya hasi tatu tumeenda kuruhusu uvuvi mpaka wa vitui ulioshindikana katika Ziwa Nyasa kwa kaka yangu Mwakyembe. Kwahiyo mambo haya mengi yamefanyika na vile vile tumeweza pia kuruhusu kwamba watu katika kukata leseni kwamba kuanzia tarehe moja mpaka mwezi wa tatu hakuna kutozwa faini na mtu atozwe alipe muda huo bila kutozwa faini yoyote na aruhusiwe kurejea leseni yake mpya bila kuzuiliwa kufanya shughuli za uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, muda ni mfupi kweli kweli. Niseme, kuna hili suala la *TAFICO* au Serikali sasa kuanza uvuvi wa bahari kuu. Nataka niwaambie, hili jambo limezungumzwa muda mrefu Serikali hii ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Dkt. John Pombe Joseph Magufuli imedhamiria kwa dhati kuhakikisha kwamba sasa taifa letu litanufaika na *blue economy* kwa kuhakikisha shirika letu linafufuliwa; na shirika letu sasa hivi limeshasimama. Tayari tumepata bilioni 4.2 ambazo hizi tayari tunanunua meli ya kwanza kwa ajili ya uvuvi wa maji ya kawaida tunakarabati maghala yetu kwa ajili ya kuhifadhi samaki, tunanunua magari kwa ajili ya kubebea barafu na samaki tunakarabati majengo ya *TAFICO* na *TAFICO* itasimama.

Mheshimiwa Naibu Spika, siku zingine watu waliongea tu, sasa *TAFICO* na meli za Watanzania ambazo zimeahidiwa muda mrefu; *business plan* ya *TAFICO* hii hapa; Kitabu hiki ambacho kimejaa mipango mizuri kwa ajili ya kuhakikisha kwamba meli za Watanzania za kwenda kuvua uvuvi wa Bahari Kuu sasa inawezekana. Fedha za kununua meli nazo tumeshazipata na lililobaki ni suala tunategemea kufikia mwaka 2021 Januari tayari tutakuwa tumefikia kwenye hatua za manunuzi kwa ajili ya kununua meli na kuanza uvuvi wa Bahari Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, luhusu ujenzi wa bandari Waheshimiwa Wabunge hapa wametushauri vizuri juu ya kuanza ujenzi wa bandari ya uvuvi na sisi mipango yetu imekamilika, tunahitimisha suala la upembuzi yakinifu, Baada ya upembuzi yakinifu tu kukamilika tayari ujenzi wa bandari utaanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhusu Migogoro ya Wafugaji. Mwanasheria Mkuu wa Serikali ametoa maelezo hapa na Waheshimiwa Wabunge wameuliza *role* ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi iko wapi katika hili eneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge mimi na Wizara yangu katika muda mfupi tumefanya ziara katika halmashauri zote 152 zenye

mifugo na kuwasikiliza wafugaji eneo kwa eneo, mikutano kwa mikutano, usiku na mchana kama tulivyofanya vilevile kwa wavuvi. Tumewasikiliza wafugaji wetu tumesikiliza migogoro yao kama nilivyoiainisha kwenye hotuba. Migogoro ya wakulima na wafugaji, wafugaji pamoja na wahifadhi ukweli ni mikubwa na inahitaji kutafutiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme, tumeshafanya tathmini tumeshafanya upembuzi, tumesha ainisha changamoto zote, tumesha ainisha migogoro yote kama sawa sawa na majawabu ambayo yametolewa na Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali; kwamba sasa kwasababu majukumu yote hayo yameshabainishwa na tunapitia *case by cases* matatizo haya ya wafugaji, mifugo yao kukamatwa na kama ilivyoorodheshwa yatashughulikiwa kikamilifu na Wizara, na mimi Wizara yangu itasimamia kikamilifu. Ninachotaka niwaambie tu wafugaji na Watanzania wote ni kwamba suala la haki ya Watanzania limeainishwa kwa mujibu wa katiba. Kwa hiyo, hakuna *compromise* mwenye haki atapewa haki ambaye hatakuwa na haki hatapewa haki hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwahiyo nataka niwaambie kwamba wafugaji wakae wakijua Wizara iko usiku na mchana katika kusimamia majukumu yao na ndiyo maana mnatukuta mpaka saa nyingine saa saba za usiku tuko ofisini hii Wizara yangu nafanyakazi. Kwahiyo yote haya nikuhakikisha kwamba matatizo ya wananchi haya yanaweza kutatuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni suala hili la biashara ya mazao ya mifugo pamoja na mazao ya uvuvi. Kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Ahmed Salum kwa biashara kubwa aliyotuletea ya nyama, na sisi tumeipokea na kwamba vikwazo vyote vinavyoweza kusababisha asiweze kuhudumia soko alilolipata la Uarabuni kwa ajili ya kupeleka nyama tani kwa matani; mimi na Wizara yangu tunasimamia vizuri kuhakikisha kwamba mkataba huu unasimamiwa kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala ya tozo za *royalty* Wabunge hapa wamezungumzia kuhusu *royalty,* kuwa ni nyingi na ni kubwa; lakini Waheshimiwa Wabunge si lazima kila kitu tujilinganishe na Uganda ama na Wakenya, zipo *factor* na *parameters* nyingi. Ninachoweza kuzungumza katika hili eneo ni kimoja tu, kwamba sisi tumewasikiliza wavuvi wetu, tumewasikiliza wadau wetu. Tunachokifanya ni *adjustment* katika tozo zetu tunazotoza ili kuweza kupunguza kama zilikuwa zimezidi sana. Kwa hiyo, tumefanya *adjustment* na hizo *adjustment* kama nilivyosema Waziri wa Fedha atakapokuja hapa atatoa maelezo ya kina juu ya Serikali imeamua nini katika kupunguza baadhi mizigo kwa wananchi wake ili waweze kupata manufaa makubwa katika biashara wanazozifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Getere Mtendaji wa Kata mwenzangu, mimi nilikuwa Kata ya Ng'oboko nampongeza sana tupo pamoja na maombi yake aliyoyaleta tutaendelea kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwamba ukweli kabisa, ukweli wa moyo wangu, nataka nirejee tena kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri wa Tanzania kwa jinsi ambapo analitumikia Taifa hili na watu wengi wamejaribu kutukatisha tamaa katika safari hii, lakini wameshindwa. Mheshimiwa Rais toka alipoamua kuinyanyua ilani ya Chama cha Mapinduzi na akakabidhi wasaidizi wake tumsaidie pamoja na ninyi Waheshimiwa Wabunge, watu wote wanaotutakia mabaya wameshindwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namtakia kila kheri Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa sana aliyoifanya, Wizara yangu alituagiza, alisema kwamba, nendeni mkafute machozi ya Watanzania, siwezi kuongoza Taifa lenye machozi. Wizara yangu imefanya kazi usiku na mchana kuhakikisha kwamba machozi ya Watanzania yanakwisha na vilio vyote vinakwisha. Tumekuta Wizara hapa watu wanachinjana; wafugaji na wakulima wanachinjana usiku na mchana, utaona ng'ombe kwenye *TV* amekatwa

mapanga, utaona wananchi wameuana, leo mauaji hayo yamepungua na karibu kama yamekwisha kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna haya mengine madogo madogo ya kuhusu wahifadhi na mifugo, ambayo nayo tumeweka misingi mizuri na sheria hizi ambazo tumezitunga, zingine zimeenda kuweka ugumu sana haitakuwa rahisi kihivyo mtu kukamata mifugo, kila mtu anayetaka tu awe anaweza kukamata mifugo. Kanuni hizi zingine tulizozitunga hapa zinaenda kuweka zuio kubwa sana. Watu wengine wapo hapa, kwa kweli tumefanya kazi kubwa, nimeingia mwaka 2005, nilikuwa mmoja wa Waheshimiwa Wabunge wachache sana vijana, tena wadogo zaidi tulikuwa mimi na Mheshimiwa Zitto Kabwe, lakini nashangaa Mheshimiwa Zitto Kabwe kila leo akisimama ni kutoa majibu ya kashfa dhidi ya Mheshimiwa Rais sijui ni kwa jambo gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme, uwezo wa Mheshimwa Zitto Kabwe umeshuka sana na Zitto Kabwe, *size* yake ni yule Samson Yanga, yule *DC* wa Kigoma na wala asipoteze muda mkubwa kuhangaika na huyu Mkuu wa nchi, Mheshimiwa Rais huyu aliyevunja *record* ya dunia katika kuhakikisha maendeleo ya Watanzania yanapatikana, nani asiyejua leo hii Waheshimiwa Wabunge tunakaa hapa tunapanga mipango kwa fedha zetu. Tulikuwa tukiletewa ulaghai hapa, mnapanga fedha, mnaweka kwenye mipango fedha haziji, za kutegemea kutoka nje. Leo tumejenga miradi mikubwa na tunatekeleza miradi mikubwa kwa fedha yetu, nani asiyemjua Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli katika mageuzi yake mpaka ajilinganishe na yeye Mheshimiwa Zitto Kabwe?

Mheshimiwa Naibu Spika, nani asiyemjua Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kazi kubwa aliyoifanya na *sacrifices* kubwa kwa Taifa lake, toka alivyokuwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi na Waziri wa Ujenzi? Nani asiyejua *transformation* tunazozipata leo? Nani asiyejua miradi mikubwa hii tunayoitekeleza kwa fedha zetu? Nani asiyejua mambo ya *illicit financial flows* yaliyakuwa yakikausha fedha zetu? Nani asiyejua mambo ya *transfer pricing* yalivyokuwa

yakikausha fedha za nchi yetu? Nani asiyejua namna ya usimamizi wa fedha ndogo kuweza kuwahudumia Watanzania?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli ameyaweza haya katika muda mfupi. Sasa mambo mengine Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli achape kazi za Watanzania, hawa wote wanaojaribu kumkatisha tamaa na hawa wote wanaojaribu kuwa sehemu ya kutuhujumu jitihada zetu mwenyenzi Mungu atashughulika nao. Nimhakikishie pia Mheshimiwa Rais kwamba sisi vijana wake tupo katika kuhakikisha majukumu ya Watanzania yanatekelezwa kikamilifu na hatutashindwa lolote katika hili na ndiyo maana tumeendelea kutekeleza majukumu hayo kikamilifu kuhakikisha kwamba Watanzania wananufaika na rasilimali yao, wavuvi wananufaika na rasilimali zao na wafugaji wananufaika na rasilimali zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwamba najua sasa hivi tunaenda kwenye uchaguzi, naomba tutakapokuwa tunaendelea na uchaguzi wetu, watu wasitumie rasilimali za kitaifa kujitafutia umaarufu wa kisiasa. Tunaendelea kuzisimamia hizi rasilimali mpaka siku ya mwisho. Mimi na Wizara yangu nitakuwa kazini mpaka siku atakapoteuliwa Waziri mwingine na kwamba misimamo yote ya Serikali kuhakikisha kwamba rasilimali zinalindwa itaendelea, mpaka dakika ya mwisho atakapopatikana Waziri mwingine wa Mifugo na Uvuvi na mpaka dakika ya mwisho atakapopatika Naibu mwingine wa Mifugo na Uvuvi yawezekana wakawa hao hao labda Waziri mwingine mpya kwa sababu kila mtu akapoteuliwa atakuwa mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwahakikishie wavuvi wote nchini, wapo kwenye mikono salama changamoto zao zote zitakwisha, nikihakikishie Chama change cha Mapinduzi na Wizara yangu katika utekelezaji wangu wa majukumu haya Chama changu cha Mapinduzi maeneo yote nitapokelewa na wavuvi kwa shangwe nitapokelewa na wafugaji kwa shangwe. Ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA**: Ahsante sana, Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kama ulivyo utaratibu wetu nilikuwa naangalia kura zilizopigwa hapa. Katika kura zilizopigwa kwa Wabunge wote walioko humu ndani na wengine waliopo Msekwa na vyumba vingine. Wabunge walio wengi wamepiga kura ya Ndiyo. Kwa sababu hiyo maana yake ni kwamba Bunge limekubali na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021. *(Makofi)*

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 yalipitishwa na Bunge kama ifuatavyo:-**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

Fungu 64 – Sekta ya Uvuvi................................Sh.21,662,107,000
Fungu 99 – Sekta ya Mifugo............................Sh. 27,034,826,000

**MIPANGO YA MAENDELEO**

Fungu 64 – Sekta ya Uvuvi..................................Sh.13,059,214,000
Fungu 99 – Sekta ya Mifugo.................................Sh.5,061,371,000

**NAIBU SPIKA:** Nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri na Watendaji wenu waliopo hapa, Wataalam hongereni sana na nadhani mmeshuhudia Kamati pia imewapongeza na Wabunge wote wamewapongeza, kwa hiyo tunawapongeza kwa kazi nzuri sana mliyoifanya na kwa kweli mmepunguza changamoto nyingi. Kwa hiyo maana yake mmesaidia sana kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi, lakini pia kutimiza ahadi ambazo Mheshimiwa Rais

alikuwa amezitoa kwa wananchi ambao alikuwa anawaona wana unyonge na sasa wanaweza kufanya kazi zao vizuri, maana yake wanaondokana na huo unyonge sasa. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa niaba yenu, niwashukuru sana Kamati kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kushirikiana na Serikali. Pia kwa ushauri wao, naamini yale yote yaliyokuwa yanazungumzwa miaka ya nyuma humu ndani yaliendelea kwenye Kamati na ndio maana wenzetu wameweza kuyafanyia kazi hayo na sasa tunaona mabadiliko, badala ya Wabunge kulalamika sasa wanapongeza. Kwa hiyo Kamati yetu tunaipongeza sana kwa kazi nzuri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge ambao wamepata fursa ya kuchangia, tunawashukuru kwa mawazo mliyoyatoa, tunaamini wamewasikia na kama wao walivyoahidi ufafanuzi wataleta kwa maandishi, lakini kimsingi kila Mbunge aliyezungumza naamini ushauri wake wameuchukua na yumkini tutakuja kuusikia hapo baadaye wamesonga kiasi gani kwa fedha hizi ambazo Bunge limeidhinisha. Kwa hiyo, tunawashukuru Wabunge wote kwa namna mlivyoshiriki katika mjadala huu.

Waheshimiwa Wabunge, nina ombi moja tu upande wa Serikali, wakati bado tupo kwenye hili zoezi la *corona* msichoke kutoa elimu kwa sababu huko tunakopita tunaona mambo mengi yanayoendelea hasa ya uvaaji wa barakoa. Kila mtu anavaa aonavyo inafaa.

Kwa hiyo Serikali msichoke kuendelea kutuelimisha sisi wananchi ili tusije tukapata sasa madhara mengine ya kuvaa barakoa isivyofaa. Maana nimeona kuna wengine wanavaa vile vizuia sumu, sasa kama amevaa kuanzia asubuhi mpaka jioni, sijajua kiafya atakuwa na hali gani. Kwa hiyo ni vizuri muendelee kutoa ushauri na muendelee kutoa elimu ili tusije tukapata madhara mengine wakati tukijinga na *corona*. Kwa hiyo kuna watu wanavaa majitu ya *plastic* hivi mazito kabisa, sasa sijui kiafya yanatakiwa kuvaliwa kwa muda gani kama mtu anavaa kwa siku.

Mheshimiwa Mpina nae alikuwa ameonesha mfano, kuna miwani fulani hivi alikuwa anavaa sasa sijui labda mwenzetu amepata elimu. Kwa kweli kazi nzuri imefanyika hata kwenye hili janga, lakini niwaombe upande wa Serikali msichoke kutoa maelekezo na kutoa elimu, itatusaidia sana kuepuka madhara mengine ambayo tunaweza kuyapata kwa matumizi ya hivi vifaa kama tukitumia vile ambavyo haipaswi.

Kwa hivyo baada ya kusema hayo, Waheshimiwa Wabunge naahirisha Shughuli za Bunge mpaka kesho saa nane kamili mchana.

*(Saa 11.50 Jioni Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Ijumaa, Tarehe 15 Mei, 2020, Saa Nane Mchana)*